

## KIBONG'OTO

Hospitali ya Taifa iliyopania kupaa kimataifa

Uk 32-34



## MSD

Yajivunia mafanikio ya Rais Samia

Uk 55-57

## MANYARA



Utoaji wa huduma za afya waing'arisha

Uk 13-16

## TABORA



Hopitali ya rufaa kitete yachanja mbuga

Uk 21-24

**TOLEO MAALUMU LA MIAKA MITATU YA RAIS DK. SAMIA NA UBORESHAJI SEKTA YA AFYA NCHINI**


# UHURU

*ya kijani*

ISSN 0876 - 3896 Na. 0042
Jumanne Machi 19, 2024

@UhuruOnline


## SHINYANGA



Hospitali ya rufaa iliyoleta matumaini na faraja kwa wananchi Kanda ya Ziwa


Uk 29-31

### MIAKA MITATU YA DK. SAMIA

# MAGEUZI MAKUBWA AFYA



Rais Dk. Samia Suluhu Hassan




### HUDUMA

Katika kuimarisha huduma za uchunguzi wa mionzi kwa wagonjwa, Serikali imenunua vifaa Tiba vya Uchunguzi na matibabu ya wagonjwa vyenye thamani ya shilingi bilioni 290.9, vinapatikana kuanzia ngazi ya Hospitali za Taifa hadi Hospitali za Rufaa za Mikoa na Halmashauri.



Waziri wa Afya Ummy Mwalimu

## Madaktari bingwa waguswa utoaji, uboreshaji wa huduma za kitabibu

>>UK.4

## Wananchi waipongeza serikali kupunguza vifo vya wajawazito na watoto wachanga nchini

>>UK.12

# Mafanikio sekta ya afya

Na HAMIS SHIMYE

WIZARA ya Afya ina dhamana ya kusimamia utoaji wa huduma za afya kwa wananchi wote ili kuwa na Jamii yenye afya bora na Ustawi, ambayo itachangia kikamilifu katika maendeleo ya mtu binafsi na Maendeleo ya nchi kwa ujumla.

Katika kufikia azma hiyo, Wizara imeendelea kuandaa mipango na bajeti zake kwa kuzingatia Dira ya Taifa ya Maendeleo (2025), Sera ya Afya ya mwaka 2007, Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi (CCM) ya mwaka 2020-2025.

Pia, inatekeleza kwa kuutazama Mpango Mkakati wa Tano wa Sekta ya Afya (2021/22 -2025/26) pamoja na makubaliano ya Kimataifa na Kikanda yenye lengo la kuimarisha utoaji wa huduma bora za afya kwa wananchi.

Katika kipindi cha Miaka mitatu ya Uongozi wa Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, Wizara ya Afya imetekeleza kwa mafanikio majukumu yake, ikijikita katika maeneo makuu mbalimbali.

Maeneo hayo ni pamoja na Ujenzi wa Miundombinu ya Kutolea Huduma za Afya nchini, kuimarisha upatikanaji wa dawa na bidhaa nyingine za afya, Upatikanaji wa Huduma za Ubingwa na ubingwa Bobezi nchini.

Pia, kuimarisha huduma za Uchunguzi wa magonjwa ikiwemo huduma za Mionzi, kuimarisha Huduma za Afya ya Uzazi, Mama na Mtoto, kudhibiti maambukizi ya UKIMWI, Kifua KIkuu.

Mafanikio mengine ni mapambano ya ugonjwa wa Malaria na Magonjwa ya mlipuko, Ajira kwa Watumishi na Ufadhili wa Wanafunzi katika ngazi na fani mbalimbali pamoja na kupitishwa kwa Sheria ya Bima ya Afya kwa wote.

## UJENZI WA MIUNDOMBINU YA KUTOLEA HUDUMA ZA AFYA NCHINI

Katika kipindi cha Serikali ya Awamu ya Sita (6) umefanyika uwekezaji mkubwa katika miundombinu ya kutolea huduma za afya ambapo vituo vya kutolea huduma za afya vimeongezeka kutoka vituo 8,549 mwaka 2021 hadi kufikia vituo 9,610 Machi 2024. Hii ni sawa na ongezeko la vituo 1,061.

Mgawanyo wa vituo vya kutoa huduma za afya hadi kufikia Machi 2024 ni Zahanati – 7,999 (83.2%), Vituo vya Afya – 1,170 (12.2%), Hospitali za Halmashauri – 172 (1.8%), Hospitali zenye hadhi ya Wilaya -181 (1.9%), Hospitali za Rufaa za Mikoa – 28 (0.3%).

Pia, Hospitali zenye hadhi ya Mkoa 36 (0.4%), Hospitali za Rufaa za Kanda – 5 (0.05%), Hospitali zenye hadhi ya kanda-12 (0.1%), Hospitali Maalumu – 6 (0.1%), Hospitali ya Taifa – 1 (0.01%).

Ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya kutolea huduma za afya

Serikali ya Awamu ya Sita (6) imejenga na kufanya maboresho ya miundombinu ya kutolea huduma za afya ikiwa ni pamoja na ujenzi wa maengo mapya, ukarabati na kukamilisha ujenzi wa hospitali mpya katika mikoa mipya mitano.

Maboresho hayo yamegharimu jumla ya sh. Trilioni 1.02 na yalifanyika katika maeneo mbalimbali ikiwemo kukamilisha awamu ya kwanza ya ujenzi wa hospitali ya Rufaa ya Kanda ya Kusini Mtwara na kukamilisha awamu ya pili ya ujenzi wa Hospitali ya Rufaa ya Kanda Chato.

Kukamilisha ujenzi wa Hospitali mpya za Rufaa za Mikoa mitano (5) ambayo ni Katavi, Njombe, Songwe, Simiyu na Geita pamoja na kuhamisha Hospitali tano (5) kutoka majengo yake ya zamani kwa kujenga Hospitali mpya katika maeneo mapya, Hospitali hizo ni Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Ruvuma, Shinyanga, Singida, Mara na Lindi.

Kukarabati na kujenga majengo mapya ya kutolea huduma za afya katika Hospitali za Rufaa za Mikoa ya Ligula (Mtwara), Sekoutoure (Mwanza), Maweni (Kigoma), Sumbawanga (Rukwa) na Kitete (Tabora).

Kujenga na kukarabati miundombinu ya kutolea huduma za Afya ngazi ya msingi ambapo Hospitali mpya za Halmashauri 127 zimejengwa (Hospitali 95 zimeanza kutoa huduma kwa wagonjwa wa nje na Hospitali 32 zipo katika hatua mbalimbali za ujenzi).

Pia, miaka mitatu katika sekta ya afya imesaidia kufanya ukarabati wa Hospitali Kongwe 50 za Halmashauri ambapo ujenzi umefanyika, Ujenzi wa Vituo vya Afya vipya 367 na ukamilishaji wa maboma ya Zahanati 980, Ujenzi wa Nyumba za Watumishi 270 katika Hospitali mbalimbali nchini.

Mafanikio mengine ni ujenzi wa mitambo 21 ya kuzalisha hewa tiba ya oksijeni kwa ajili ya wagonjwa mahututi na Wagonjwa wa dharura

**UJUMBE MAHUSUSI:** Ongezeko la vituo vya kutoa huduma za afya nchini na maboresho ya miundombinu yaliyofanyika yametuwezesha kusogeza huduma za afya karibu zaidi na wananchi kama tunavyoelekezwa na Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2020 - 2025. Hivi sasa asilimia 80 ya wananchi wanapata huduma za afya ndani ya kilometa 5 ya maeneo yao wanayoishi. Lengo ni kufikia asilimia 95 ifikapo mwaka 2030.



## KUIMARISHA HUDUMA ZA UCHUNGUZI WA MAGONJWA

Katika kuimarisha huduma za uchunguzi wa magonjwa, Serikali ya Rais Dkt Samia imenunua vifaa Tiba vya Uchunguzi na matibabu ya wagonjwa vyenye thamani ya shilingi bilioni 290.9 ambavyo vinapatikana ngazi ya Hospitali ya Taifa hadi Hospitali za Rufaa za Mikoa (RRHs) na Halmashauri.

Mchanganuo wa vifaa vilivyonunuliwa na Serikali ya awamu ya sita ikiwemo MRI ambapo awali zilikuwepo saba, mpya zimenunuliwa saba na kufikisha jumla zimekuwa 13, CT Scan zilizokuwepo 13 huku shule mpya 32 na kufanya jumla 45.

Huduma za kipimo cha CT Scan sasa zinapatikana katika Hospitali 27 kati ya Hospitalii 28 za rufaa za Mikoa nchini. Hadi kufikia Machi 2024 jumla ya wagonjwa 15,386 walipatiwa huduma za kipimo cha CT Scan katika Hospitali za Rufaa za Mikoa ambapo huduma hizo zilikuwa hazitolewi katika hospitali za Rufaa za Mikoa hapo awali.

## VITANDA VYA KULAZA WAGONJWA VYAONGEZEKA

Idadi ya vitanda vya wagonjwa katika vituo vya kutolea huduma za afya nchini imeongezeka kutoka vitanda 86,131 mwaka 2021 hadi vitanda 126,209 Machi 2024. Ongezeko la vitanda vya wagonjwa limesaidia kuongeza ubora na ufanisi wa huduma za afya hususani huduma za afya ya mama na mtoto.

Serikali imekamilisha ujenzi wa wodi 45 za wagonjwa mahututi (ICU) katika hospitali ngazi ya Taifa, Maalum, Kanda na Mkoa na kuziwekea vifaa na vifaa tiba. Pia Serikali inaendelea na ujenzi wa ICU 28 katika ngazi ya Halmashauri ambapo 27 kati ya hizo zimekamilika na moja (1) iko hatua ya ukamilishaji. Hatua hii imeongeza idadi ya vitanda kwa ajili ya wagonjwa mahututi (ICU) katika vituo vya umma kutoka vitanda 258 vya mwaka 2021 hadi kufikia vitanda 1,362 mwaka 2023.

MATOKEO: Ongezeko la vitanda vya wagonjwa mahututi (ICU) katika Hospitali za umma linalenga kusogeza huduma karibu na wananchi, kupunguza rufaa za wagonjwa wanaohitaji huduma za ICU kwenda katika Hospitali za Rufaa za Mikoa na Taifa na hivyo kupunguza msongamano wa wagonjwa sambamba na kupunguza vifo vinavyotokea ndani ya hospitali ambavyo vinaweza kuzuilika kati ya asilimia 20 hadi 30.

## KUIMARISHA UPATIKANAJI WA DAWA NA BIDHAA ZA AFYA

Serikali ya awamu ya sita imeendelea kuimarisha hali ya upatikanaji wa dawa na bidhaa za afya ambapo, katika kipindi cha miaka mitatu, wastani wa Shilingi Bilioni 20 zimekuwa zikitolewa kila mwezi.

Upatikanaji wa fedha hizo umewezesha kuimarika kwa upatikanaji wa dawa muhimu na bidhaa nyingine za afya (aina 290) katika vituo vya kutolea huduma za afya vya umma kufikia asilimia 84 mwaka 2023 ikilinganishwa na asilimia 58 mwaka 2022.

Aidha, hali ya upatikanaji wa bidhaa za afya kwa ngazi za vituo vya kutolea huduma za afya hadi kufikia mwezi Desemba 2023 ni kama ifuatavyo ikiwemo Zahanati- asilimia 75 Vituo vya afya – asilimia 69, Hospitali za Wilaya – asilimia 82, Hospitali za Rufaa za Mikoa asilimia 93, Hospitali za Taifa, Kanda na Maalum – asilimia 99.

Ujumbe: Upatikanaji wa dawa, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi umehakikisha kila mwananchi anapata mahitaji yote muhimu ya msingi ya kimatibabu pale anapoenda kupata huduma katika vituo vya kutolea huduma za afya

## KUIMARISHA HUDUMA ZA AFYA YA UZAZI, MAMA NA MTOTO

Katika kipindi cha mwaka 2021 hadi Machi 2024, Serikali ya Awamu ya Sita imeendelea kuwekeza katika huduma za afya ya Uzazi, Mama na Mtoto. Uwekezaji huo umefanyika katika maeneo mbalimbali.

Kukamilisha ujenzi wa jengo la kutoa huduma za afya ya Mama na Mtoto Meta iliyopo katika Jiji la Mbeya ambayo tayari inatumika na imegharimu shilingi bilioni 13.2.

Kuendelea na ujenzi wa majengo ya huduma za Mama na Mtoto (Maternity Blocks) kwenye Hospitali za Rufaa za Mikoa ambazo ni Sekou Toure (Mwanza), Geita, Simiyu, Mawenzi, Njombe na Songwe ambazo zimegharimu kiasi cha shilingi bilioni 71.1.

Rais Dk. Samia ameimarisha huduma za Upasuaji wa Wajawazito kwa Kuongeza vituo vyenye uwezo wa kutoa huduma za upasuaji wa dharura wa kumtoa mtoto tumboni (CEMoNC) kutoka vituo 340 mwaka 2021 hadi kufikia vituo 523 mwaka 2023.

Kuanzisha wodi maalum kwa ajili ya huduma za watoto wachanga wagonjwa (Neonatal Care Units - NCU), ambapo hadi kufikia desemba 2023 jumla ya Hospitali 189 zinatoa huduma za NCU ikilinganishwa na Hospitali 165 mwaka 2022 na Hospitali 14 tu mwaka 2018.

Kuimarisha upatikanaji wa bidhaa za Afya ya Uzazi, Mama na Mtoto ambapo upatikanaji wake katika

# MIAKA MITATU YA MAGEUZI MAKUBWA SEKTA YA AFYA



la kutoa huduma za afya ya Mama na Mtoto Meta iliyopo katika Jiji la Mbeya ambayo tayari inatumika na imegharimu shilingi bilioni 13.2.

Kuendelea na ujenzi wa majengo ya huduma za Mama na Mtoto (Maternity Blocks) kwenye Hospitali za Rufaa za Mikoa ambazo ni Sekou Toure (Mwanza), Geita, Simiyu, Mawenzi, Njombe na Songwe ambazo zimegharimu kiasi cha shilingi bilioni 71.1.

Rais Dk. Samia ameimarisha huduma za Upasuaji wa Wajawazito kwa Kuongeza vituo vyenye uwezo wa kutoa huduma za upasuaji wa dharura wa kumtoa mtoto tumboni (CEMoNC) kutoka vituo 340 mwaka 2021 hadi kufikia vituo 523 mwaka 2023.

Kuanzisha wodi maalum kwa ajili ya huduma za watoto wachanga wagonjwa (Neonatal Care Units - NCU), ambapo hadi kufikia desemba 2023 jumla ya Hospitali 189 zinatoa huduma za NCU ikilinganishwa na Hospitali 165 mwaka 2022 na Hospitali 14 tu mwaka 2018.

Kuimarisha upatikanaji wa bidhaa za Afya ya Uzazi, Mama na Mtoto ambapo upatikanaji wake katika Vituo vinavyomilikiwa na Serikali umeongezeka kutoka asilimia 82.5 mwaka 2021 hadi asilimia 88.2 mwaka 2023.

Kuimarisha huduma za Saratani ya mlango wa kizazi, ambapo jumla ya mashine 140 (Thermalcoagulator) za uchunguzi wa Saratani zimenunuliwa na kusambazwa kwenye vituo 140 vya kutolea huduma za afya katika Halmashauri 104 katika Mikoa 26. Vifaa hivi vina thamani ya jumla ya shilingi Bilioni 1.1

Mfumo wa M-mama - Serikali ya Awamu ya Sita imeanzisha mfumo wa kieletroniki wa M-mama unaoratibu rufaa, kwa kusafirisha akina mama wajawazito na watoto wachanga wanaohitaji huduma za dharura kutoka ngazi ya jamii hadi vituo vya kutolea huduma za afya au kutoka katika kituo cha kutolea huduma cha ngazi ya chini kwenda kituo cha ngazi ya juu.

Kwa kipindi cha mwaka 2022 hadi mwaka 2023 mfumo huu umendelea kufanya kazi katika Mikoa yote 31 Tanzania Bara na Zanzibar, jumla ya wateja 46,941 wamenufaika na huduma za dharura za rufaa, kati ya hao kina mama walikuwa 38,560 sawa asilimia 82, watoto wachanga walikuwa 8,273 sawa na asilmia 17 na mama pamoja na mtoto kwa pamoja walikuwa 108 sawa na asilimia moja (1).

Wateja wote wa m-mama wanahudumiwa na Watoa huduma waliopo katika vituo vyote vya kutolea huduma za afya vya Serikali nchini. Mfumo huu umerahisisha utoaji wa huduma za dharura kwa wakati kwa kuwafikisha wateja katika vituo sahihi vya matibabu.

**MATOKEO:** Kutokana na. uwekezaji mkubwa uliofanywa na Rais Samia Suluhu Hasssan katika kuimarisha ubora wa huduma za afya ya uzazi, mama na mtoto ambapo kupitia Viashiria vikuu vinavyotumika kupima mwenendo wa ubora wa huduma kwa nchini Wanachama wa Shirika la Afya Duniani imejidhihirisha wazi kuwa nchi yetu mefanya vizuri sana katika kuimarisha huduma za afya ya uzazi, mama na mtoto katika kipindi cha miaka mitatu (3).

Matokeo ya baadhi ya viashiria hivyo ni pamoja na Ongezeko la Wajawazito waliojifungulia kwenye vituo vya kutolea huduma za afya.

Idadi ya wajawazito wanaojifungulia katika vituo vya kutolea huduma za afya Nchini imeendelea kuongezeka kutoka asilimia 63 mwaka 2021 hadi asilimia 85 mwaka 2023. Lengo la nchi ni kufikia asilimia 95 ya wanaojifungulia kwenye vituo vya kutolea huduma za afya ifikapo mwaka 2030.

Vifo vya wanawake wajawazito kwa asilimia 80 - Kuimarika kwa huduma za uzazi, mama na mtoto kumepelekea kupunguza vifo vya wajawazito vitokanavyo na uzazi kutoka vifo 556 kwa kila vizazi hai 100,000 mwaka 2016 hadi kufikia vifo 104 kwa kila vizazi hai 100,000 kwa sasa .

Vifo vya watoto umri chini ya miaka mitano vimepungua kutoka vifo 67 kwa kila vizazi hai 1,000 mwaka 2016 hadi kufikia vifo 43 kwa kila vizazi hai 1,000 mwaka 2022.

Vifo vya watoto umri chini ya mwaka mmoja vimepungua kutoka vifo 43 kwa kila vizazi hai 1,000 mwaka 2016 hadi kufikia vifo 33 kwa kila vizazi hai 1,000 hadi sasa,

Vifo vya watoto wachanga (wenye umri wa chini ya siku 28) vimepungua kutoka 25 kwa kila vizazi hai 1,000 mwaka 2016 hadi vifo 24 kwa kila vizazi hai 1,000 hadi sasa

> Kuweka puto tumboni wagonjwa 166 wamepata huduma hiyo tangu kuanzishwa kwake mwaka 2021 na Huduma hizi ziliolewa katika Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI); Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), Taasisi ya Mifupa (MOI); Taasisi ya Saratani ya Ocean Road, Hospitali ya Benjamin Mkapa Dodoma na Hospitali nyingine za Rufaa za Kanda na Mikoa.



**KUIMARISHA UPATIKANAJI WA HUDUMA ZA UBINGWA NA UBINGWA BOBEZI NCHINI.**

Rais Dk. Samia ameimarisha upatikanaji wa huduma za matibabu ya ubingwa na ubingwa bobezi (Specialized and Super Specialized) ikiwemo huduma za Upasuaji mgumu wa moyo bila kufungua kifua (Cathetarization procedure).

Upasuaji wa moyo kwa njia ya tundu dogo; upandikizaji Figo (Kidney Transplant), Upandikizaji Uloto (Bonne Marrow Transplant); Upandikizaji wa Vifaa vya Usikivu kwa watoto (Cochlea implants), kuweka puto tumboni na upasuaji mgumu wa mifupa na mishipa ya fahamu.

Katika kipindi cha miaka mitatu, Huduma za Ubingwa Bobezi zilizotolewa zilikuwa ni pamoja na upandikizaji vifaa vya usikivu kwa watoto ambapo jumla ya watoto 25 waliowekewa kati ya hao watoto 11 wamewekewa vifaa hivyo mwaka 2023/24.

Upandikizaji wa figo ulifanyika kwa wagonjwa 27, kati yao wagonjwa 16 wamefanyiwa katika kipindi cha mwaka 2023/24, Upandikizaji uloto wagonjwa15 tangu ilipoanzishwa mwaka 2021.

Upasuaji wa Moyo kwa njia ya Tundu dogo wagonjwa 5,954 kati yao wagonjwa 2,289 wamefanyiwa katika kipindi cha mwaka 2023/24, Kuweka Goti Bandia wagonjwa 662, kati yao wagonjwa 385 wamefanyiwa katika kipindi cha mwaka 2023/24.

Kuweka puto tumboni wagonjwa 166 wamepata huduma hiyo tangu kuanzishwa kwake mwaka 2021 na Huduma hizi ziliolewa katika Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI); Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), Taasisi ya Mifupa (MOI); Taasisi ya Saratani ya Ocean Road, Hospitali ya Benjamin Mkapa Dodoma na Hospitali nyingine za Rufaa za Kanda na Mikoa.

MATOKEO: Uwekezaji mkubwa uliofanywa na Rais Dkt Samia Suluhu Hassan katika kuimarisha huduma ubingwa na ubingwa bobezi umewezesha wananchi wengi kupata huduma hizi ndani ya nchi kwa gharama nafuu badala ya kuzitafuta nje ya nchi. Aidha uwekezaji huu umeweza kuvutia wagonjwa mbalimbali kutoka nje ya nchi na hivyo kuifanya nchi yetu kuwa Kituo cha Tiba Utalii kwa ukanda wa nchi za afrika mashariki na kusini mwa afrika.

Tiba Utalii nchini inakuwa, tunashuhudia ongezeko la Raia wa kigeni kuja Tanzania kwa ajili ya matibabu.

Kutokana na uwekezaji mkubwa uliofanyika katika kuboresha huduma za kibingwa na bobezi, nchi yetu imeweza kuvutia wagonjwa mbalimbali kutoka nje ya nchi.

Kwa mwaka 2023, idadi ya wagonjwa kutoka nje ya nchi wa Tiba Utalii waliokuja kutibiwa nchini ilikuwa 6,931 ikilinganishwa na wagonjwa 3,957 mwaka 2022 na wagonjwa 75 mwaka 2021. Wagonjwa hawa wanatoka katika



# Miaka mitatu ya mageuzi makubwa Sekta ya afya

Motokeo: Jitihada hizi zitasaidia kupata wataalam wa afya kwenye fani za kibingwa na bobezi watakaotumika kujenga uwezo wa wataalam wetu wa afya katika vyuo vya mafunzo ya afya nchini. Vilevile jitihada hizo zitaimarisha upatikanaji wa huduma hizo za kibingwa bobezi ambazo zitawezesha nchi kunufaika na tiba utalii. Hadi sasa Taasisi zetu zimeweza kutoa tiba utalii kutoka nchi za Comoro, Burundi, Malawi, Kenya, Congo DRC, Uganda na Zambia.

nchi za Comoro, Malawi, Burundi, Zambia, Congo DRC, Uganda, Zimbabwe na Kenya.

Wagonjwa hawa walihudumiwa katika Hospitali 6 ambazo ni Hospitali ya Taifa Muhimbili, Taasisi ya Saratani ya Ocean road, Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete, Taasisi ya Mifupa (MOI) na Hospitali binafsi za Aga khan na Saifee.

Serikali ya Rais Samia kupitia Wizara ya Afya imejipanga kuendelea kutoa huduma za ubingwa na ubingwa bobezi karibu zaidi na wananchi.

Kupitia Mafunzo elekezi kutoka kwa wataalam bingwa (Mentorship Program) kutasaidia kuleta chachu ya mabadiliko ya utoaji huduma za afya kuweza hudumia vema wananchi katika kupata huduma bora za kibingwa

**KUIMARISHA HUDUMA ZA DHARURA NA AJALI**

Serikali ya Awamu ya Sita imekamilisha ujenzi wa majengo 23 ya kutoa huduma za dharura (EMD) katika hospitali Maalum, Kanda na Mikoa na kuziwekea vifaa na vifaa tiba. Aidha kwa upande wa ngazi ya msingi, ujenzi wa EMD 82 katika ngazi za Halmashauri unaendelea, ambapo EMD 66 zimekamilika na zinatoa huduma na nyingine 16 ziko kwenye hatua ya ukamilishaji.

Miaka mitatu ya Rais Samia imewezesha kuanzishwa kwa majengo mahusus ya huduma za dharura na ajali (EMDs) 105 kutoka EMD 7 zilizokuwepo mwaka 2020, , hadi sasa jumla ya wateja 262,260 wamenufaika na huduma za dharura nchini.

Kukamilika kwa ujenzi wa EMD kutapunguza vifo na kuokoa maisha kwa wagonjwa wa dharura na wa ajali kwa asilimia kati ya 40-50 kwa mujibu wa tafiti za kitaalam.

**MATOKEO:** Kukamilika kwa ujenzi wa EMD kumeongeza idadi ya Hospitali za Rufaa za Mikoa, maalumu, na kanda zinazotoa huduma hiyo kutoka 7 mwaka 2020 na kufikia 116 Desemba 2023.

Yote haya yamepatikana ndani ya miaka mitatu ya Uongozi wa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan. Matokeo ya uwezekaji huu kutapunguza vifo ndani ya hospitali kwa asilimia 40 na kuokoa maisha ya wananchi wanaohitaji huduma za dharura na ajali.

Magari ya kubebea wagonjwa yanunuliwa na kusambazwa kila kona Pia, Serikali imenunua jumla ya magari ya kubebea wagonjwa 727 ambapo hadi sasa jumla ya 327 yamepokelewa na kusambazwa katika vituo vya kutolea huduma za afya nchini. Ambulance hizi zinakwenda kusaidia kusafirisha wagonjwa wakiwemo akinamama wenye changamoto za uzazi kwa haraka na kuwafikisha katika huduma za rufaa na hivyo kupunguza adha kwa wananchi na kupunguza vifo vinavyoweza kuzuilika.

**RASILIMALI WATU KATIKA SEKTA YA AFYA**

Serikali ya Awamu ya sita imeendelea kufanya uwekezaji katika eneo la rasilimali watu katika afya ikiwemo kuajiri watumishi wapya wa Sekta ya Afya na kusomesha wataalamu wa afya katika fani mbalimbali za ubingwa na ubobezi.

**KUONGEZA IDADI YA WATUMISHI WA AFYA**

Serikali imeendelea kuajiri wataalam katika Sekta ya Afya ambapo jumla ya wataalam 35,450 wa kada mbalimbali wameajiriwa na kusambazwa katika vituo vya kutolea huduma za afya nchini katika kipindi cha kuanzia mwaka 2021 hadi 2023. Aidha, jumla ya ajira za mikataba kwa watumishi wa Afya 2,836 kupitia miradi mbalimbali ya Serikali zilitolewa.

Ongezeko la Madaktari bingwa na bobezi

Jumla ya madaktari bingwa nchini hadi kufikia mwaka 2023 wamefikia 2,464 ukilinganisha na madaktari Bingwa 805 mwaka 2020.

Uendelezaji wa Rasilimali Watu katika Afya

Serikali ya Awamu ya Sita imeendelea kuimarisha upatikanaji wa wataalam wabobezi kwa ajili ya utoaji wa huduma za Kibingwa na Ubingwa Bobezi, kwa kuanzisha Dk. Samia Super Specilized Scholarships ambapo hadi sasa.

Jumla ya wataalam 1,211 wamepata mafunzo mbalimbali ya kibingwa na bobezi na hivyo kuongeza idadi ya wataalam wa mafunzo ya kibingwa na bobezi kutoka 535 mwaka 2021 hadi 1,211 hadi kufikia sasa. Aidha, kiasi cha shilingi bilioni 22 kimetumika kugharamia mafunzo haya.

Motokeo: Jitihada hizi zitasaidia kupata wataalam wa afya kwenye fani za kibingwa na bobezi watakaotumika kujenga uwezo wa wataalam wetu wa afya katika vyuo vya mafunzo ya afya nchini. Vilevile jitihada hizo zitaimarisha upatikanaji wa huduma hizo za kibingwa bobezi ambazo zitawezesha nchi kunufaika na tiba utalii. Hadi sasa Taasisi zetu zimeweza kutoa tiba utalii kutoka nchi za Comoro, Burundi, Malawi, Kenya, Congo DRC, Uganda na Zambia.

**MAPAMBANO DHIDI YA VIRUSI VYA UKIMWI, MALARIA NA KIFUA KIKUU**

Kwa upande wa ugonjwa wa UKIMWI, Serikali imeendelea kudhibiti maambukizi ya ugonjwa wa UKIMWI ambapo katika mwaka 2023 jumla ya watu 8,145,576 walipima Virusi vya UKIMWI (VVU) kulinganisha na watu 6,930,758 mwaka 2022 na watu 6,493,583 mwaka 2021 (Taarifa kutoka Mfumo wa DHIS2 2023).

Kati ya watu waliopima mwaka 2023, watu 163,131 walingundulika kuwa na maambukizi ya VVU ukilinganisha na watu 182,095 mwaka 2022 na watu 198,042 mwaka 2021 (DHIS2 2023).

Waliokuwa wanatumia dawa za kufubaza virusi vya VVU walikuwa 1,663,651 Desemba 2023 kulinganisha na watu 1,612,512 Desemba 2022 na watu 1,520,589 mwaka 2021. Mwaka 2023, Vifo vitokanavyo na UKIMWI vilikuwa 22,000 kulinganisha na vifo 29,000 mwaka 2022 na vifo 25,000 mwaka 2021 (Spectrum 2022).

Katika kuhakikisha kuwa huduma kwa WAVIU zinasogezwa karibu zaidi na jamii, Wizara ya Afya kwa kushirikiana na Wadau mbalimbali wa maendeleo imekuwa ikifanya jitihada za makusudi kabisa za kuhakikisha kila kituo cha afya nchini kinakuwa na uwezo wa kutoa huduma kwa waathirika wa UKIMWI.

Hadi kufikia Mwezi Desemba 2023, Idadi ya vituo vinavyotoa huduma ya Tiba na Matunzo vimefikia vituo 7,396 kutoka vituo 7,072 mwaka 2021 na kati ya hivyo CTC kamili ni 3,572 na vituo vya huduma ya mama na mtoto (RCHS) vinavyotoa huduma ya kutoa dawa ya kufubaza Virusi vya UKIMWI vipo 3,824.

Kwa upande wa ugonjwa wa MALARIA, Serikali imeendelea kudhibiti maambukizi ya Ugonjwa wa Malaria ambapo katika mwaka 2023 jumla ya watu milioni 19.8 walipima ugonjwa wa Malaria kati yao watu milioni 3.46 walikutwa na Malaria kulinganisha na watu milioni 18.6 walipima mwaka 2022 na kati yao milioni 3.52 walikutwa na ugonjwa na watu Milioni 20,241,982, waliopimwa mwaka 2021 na kati yao Milioni 4,443,946 walikutwa na maambukizi. Vifo vitokanavyo na Malaria vilikuwa 1,540 mwaka 2023 ukilinganisha na vifo 1,735 mwaka 2022 na vifo 1,882 mwaka 2021.

Kwa upande wa ugonjwa wa kifua kikuu, Serikali iliendelea kudhibiti maambukizi ya ugonjwa huu ambapo katika mwaka 2023 jumla ya watu 440,988 walipima ugonjwa wa TB kulinganisha na watu 398,676 mwaka 2022 na watu 354,324 mwaka 2021. Waliogundulika kuwa na TB mwaka 2023 ni 90,585 kulinganisha na watu 100,984 mwaka 2022 na watu 60,068 mwaka 2021. Mwaka 2023, Vifo vitokanavyo na TB vilikuwa 18,100 kulinganisha na vifo 25,800 mwaka 2022 na vifo 26,800 mwaka 2021.

**UDHIBITI WA MAGONJWA YA MLIPUKO KWA MUDA MFUPI**

Mwaka 2023, visa vya viwili vya ugonjwa wa Marburg vilipatikana, ambapo Serikali iliweza kudhibiti kabisa kusambaa kwa ugonjwa hatari wa Marburg kwa kupitia uwekezaji wa miundombinu ya maabara ya kisasa Mkoani Kagera, nchi yetu iliweza kupambana na janga la Marburg kwa kugundua mapema na kuudhibiti ndani ya siku 69 hii ikiwa ni historia ukilinganisha na nchi za jirani kama Uganda iliyotumia siku 113 na Equtorial Guinea siku 122.

**SHERIA YA BIMA YA AFYA KWA WOTE YAPITISHWA BUNGENI**

Serikali ya Awamu ya Sita imefanikisha kutungwa kwa Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote Na. 13 ya mwaka 2023 Novemba 19, 2023 iliwekwa saini na Rais Dkt. Samia ambapo malengo makuu ya Sheria ya bima ya afya kwa wote ni kuwawezesha wananchi wote kuwa na uhakika wa kupata huduma za afya wakati wote bila kikwazo cha fedha hususan kwa kaya masikini.

Mafanikio ya kutungwa kwa Sheria hiyo pia ni kuanzishwa kwa mfuko wa kugharamia bima ya afya kwa kuwa na vyanzo mahususi vya fedha. Mfuko huo utawezesha wananchi wasio na uwezo kunufaika na huduma za afya kwa uhakika ikilinganishwa na hali ilivyo hivi sasa.

Kutekelezwa kwa Sheria hiyo kutawezesha vituo vya kutolea huduma za afya kuwa na mapato ya uhakika na hivyo kuboresha huduma za afya zitolewazo kwa wananchi.

**MWELEKEO WA SEKTA YA AFYA KWA MWAKA 2024**

Wizara ipo katika mapitio ya Sera ya Afya ya mwaka 2007 ili kuimarisha utoaji wa huduma za afya. Sera inayoandaliwa ina dira ya kuwa na jamii yenye afya bora na ustawi inayochangia kikamilifu katika maendeleo binafsi na ya nchi.

# Madaktari bingwa waguswa utoaji, uboreshaji wa huduma za kitabibu

**IRENE MWASOMOLA na Ashura Assed**

BAADHI ya madaktari bingwa nchini wameeleza mafanikio yaliyoletwa na Rais Dk.Samia Suluhu Hassan, katika sekta ya afya,kipindi cha miaka mitatu madarakani, ikiwemo kuweka vifaa tiba vya kisasa hadi ngazi ya vituo vya afya.

Wametaja baadhi ya mafanikio mengine ni kutoa ufadhili wa masomo kwa madaktari kupitia fedha zilizotolewa na serikali, na kuifanya Tanzania kuwa kitovu cha utalii tiba Afrika.

Akizungumza na gazeti hili Daktari Bingwa wa magonjwa ya moyo kutoka Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete Dk. Angellah Muhozya alisema, katika miaka mitatu ya uongozi wa Rais Dk.Samia, amefanya uwekezaji mkubwa katika magonjwa ya dharula, amejenga Vyumba vya Wagonjwa Mahututi (ICU) kila mkoa.

Dk Angellah alimshukuru Rais Dk. Samia kwa uwekezaji huo mkubwa aliyoufanya, kwasababu kwa muda mrefu kitengo cha magonjwa ya dharula kilisahaulika kufanyiwa uwekezaji na maboresho.

"Nampongeza Mheshimiwa Rais kwa uwekezaji mkubwa aliyoufanya katika sekta ya afya, ununuzi wa vifaa tiba vya kisasa, MRI, ujenzi wa ICU na kutoa magari ya kubebea wagonjwa hospitali zote,"alisema.

Aidha, Dk. Angellah alisema, Rais Dk. Samia amewezesha hospitali ya JKCI kufanya tiba utalii kwa kufanya kambi katika nchi za matibabu Comoro, Malawi, Zambia.

Alisema madaktari wa wamefanikiwa kuweka kambi katika nchi hizo ambazo wananchi wake walikua hawapati huduma hizo katika mataifa hayo.

Rais wa Chama Cha Madaktari Tanzania (MAT) Dk. Deus Ndilanha, alisema katika kipindi cha miaka mitatu ya uongozi wa Rais Dk.Samia, amefanya mageuzi makubwa ikiwemo kushughulikia swala la bima ya afya kwa wote,muswada ambao ulikwama Wizarani kwa miaka 20.

Dk.Ndilahnta, alimshukuru Rais Dk.Samia kwa kuweka vifaa tiba vya kisasa katika hospitali zote kuanzia vituo vya afya,ikiwemo mashine za MRI Ctscan, na X ray.

Alisema maboresho hayo yaliyofanyika yamesaidia wananchi wa mikoani kutosafiri kwenda kupata matibabu nje na mikoa yao na kuokoa gharama za kusafiri nje ya nchi.

Aidha Raisi huyo alisema, katika miaka mitatu ya uongozi wa Rais Dk.Samia,amefanikiwa kutoa ufadhiri wa masomo kwa madaktari bigwa bobezi.

Dk.Ndilahnta,alimshukuru Rais Dk.Samia kwa kufanya Tanzania kuwa sehemu ya utalii tiba kutokana na huduma bora na maboresho yaliyofanywa na serikali.

"Nchi kuwa sehemu ya taifa la utalii tiba Afrika, imepiga hatua sana, kuwa kitovu cha kutoa huduma Afrika hii yote ni jitihada za Rais Dk.Samia, katika sekta hii ametutendea haki ndani ya miaka mitatu sekta ya afya kuna mapinduzi makubwa,"alisema.

Kwa mujibu wa Dk.Ndilahnta, mageuzi yaliyofanywa na Rais Dk.Samia, katika sekta ya afya, madaktari hawakuwahi kuwaza kama yatatokea katika kipindi cha muda mfupi wa uongozi wake.

"Rais Dk.Samia amefanya mageuzi makubwa katika sekta ya afya,hatukuwahi kuwaza kama itatokea ndani ya muda mfupi wa uongozi wake, ununuzi wa vifaa tiba vya kisasa MRI, X ray C tscan, kuweka kuanzia ngazi ya vituo cha afya ni jambo la kushukuru na Rais amefanya kazi kubwa,"alisema

Rais wa Chama cha Madaktari Tanzania (MAT), alisema kumekuwa na mafanikio makubwa ambayo yamepunguza changamoto kwa wananchi.

Alisema maeneo hayo ni pamoja na ujenzi wa miundombinu ya huduma za afya nchini, kuimarisha upatikanaji wa dawa na bidhaa nyingine za afya na upatikanaji wa huduma za kibingwa na ubingwa bobezi nchini.

Ndilanha alisema kwa upande wa ajira amefanikiwa kwa kutoa ajira nyingi katika sekta hiyo, sambamba na kutoa ufadhili wa kimasomo kwa madaktari bingwa kuongeza ujuzi kwa lengo la kupunguza gharama za matibabu ya nje.

Kipindi hiki cha miaka mitatu, kumefanyika uwekezaji mkubwa, katika huduma za afya kwa kuongezeka vituo vya kutolea huduma hiyo kutoka vituo 8,549 mwaka 2021 hadi kufikia vituo 9,610 Machi 2024.

Alisema hali hiyo ina wawezesha wananchi kupata huduma kwa urahisi na uhakika ni sawa na ongezeko la vituo 1,061.

Kwa mujibu wa Rais wa MAT, Rais Dk. Samia alisema imeboresha huduma za kipimo cha CT Scan, sasa zinapatikana katika hospitali 27 kati ya hospitalii 28 za rufaa za mikoa nchini.

Alisema katika suala la vifaa tiba baada ya kukumbwa na janga la Uviko- 19 kulikuwa na taharuki kwa mashirika ya fedha na wadau nwengine walikuwa wanatoa misaada katika nchi tofauti tofauti, Tanzania nayo iliopata fedha za Uviko – 19.

Alisema fedha hizo zilitakiwa kununua barakoa na vitakasa mikono kwa ajili ya kujikinga na ugonjwa huo, kupitia busara za mama aliamua kuchukua fedha hizo na kuziwekeza katika kununua vifaa tiba kama CT Scan.

"Vifaa hivyo vimesambazwa katika hospitali zote za mikoa nchini kitu ambacho hakijawahi kutokea tangu tupate Uhuru. Hospitali za kanda zote zinakuwa na MRI na kupeleka X-ray hadi ngazi ya hospitali za wilaya" alisema

Aliongeza; "Mafanikio yaliopo sasa hatukuwahi kuyaona kipindi cha nyuma ni mapinduzi makubwa sana katika sekta ya afya"

"Unapopeleka CT scan katika ngazi ya mkoa, ni kitu muhimu sana kwa sababu waghonjwa waliokuwa wanasafiri kufuata huduma hiyo inakuwa imesogea karibu na kuokoa muda,"alisema.

Alisema hadi sasa wagonjwa zaidi ya 15,386 walipatiwa huduma za kipimo cha CT Scan katika Hospitali za Rufaa za Mikoa,kipindi cha nyuma huduma hizo zilikuwa hazitolewi katika hospitali za Rufaa za Mikoa.

Kwa upande wa vitanda vya wagonjwa katika vituo vya kutolea huduma za afya nchini, imeongezeka kutoka vitanda 86,131 mwaka 2021 hadi vitanda 126,209 Machi 2024.

Alisema ongezeko hilo la vitanda vya wagonjwa limesaidia kuongeza ubora na ufanisi wa huduma za afya hususani huduma za afya ya mama na mtoto.

Serikali ya awamu ya sita inaendelea kuimarisha hali ya upatikanaji wa dawa na bidhaa za afya katika utawala wake kwa kutoa huduma ya dawa za malaria bure sambamba na upatikanaji wa dawa kuanzia ngazi ya vituo vya afya.

Hali hiyo imewezesha kuimarika kwa upatikanaji wa dawa muhimu na bidhaa nyingine za afya katika vituo vya kutolea huduma za afya vya umma kufikia na asilimia 84 mwaka 2023 ikilinganishwa na asilimia 58 mwaka 2022.

'Hali ya upatikanaji wa huduma za afya katika ngazi za vituo vya kutolea huduma kwa kipindi cha miaka mitatu ni asilimia 75 kwa Zahanati, Vituo vya afya ni asilimia 69, Hospitali za Wilaya asilimia 82" alisema

Hali ya kuongezeka kwa vituo vya afya kila kata ni hatua nzuri kwa serikali kwa sababu wagonjwa wengi wanatokea katika ngazi za chini.

Dk. Ndilanha alisema Serikali ya Awamu ya Sita imeanzisha mfumo wa kieletroniki wa mama na mtoto unaoratibu rufaa, kwa kusafirisha kina mama wajawazito na watoto wachanga wanaohitaji huduma za dharura kutoka ngazi ya jamii hadi katika vituo vya kutolea huduma za afya ngazi ya juu.

Mfumo huo ulianza mwaka 2022 hadi mwaka 2023 mfumo huo umeendelea kufanya kazi katika mikoa yote 31 Tanzania Bara na Zanzibar.

Alifafanua kuwa jumla ya watu 46,941 wamenufaika na huduma za dharura za rufaa, kati ya hao akina mama ni 38,560 sawa asilimia 82, watoto wachanga ni 8,273 sawa na asilimia 17.

Alisema kina mama wanahudumiwa na watoa huduma waliopo katika vituo vyote vya kutolea huduma za afya vya serikali nchini. mfumo huo umerahisisha utoaji wa huduma za dharura kwa kuwafikisha katika vituo sahihi vya matibabu.

Hata hivyo Serikali ya Awamu ya Sita imeimarisha upatikanaji wa huduma za matibabu ya kibingwa na ubingwa kibobezi, kama vile pasuaji wa moyo kwa njia ya tundu dogo, upandikizaji figo na Uloto katika hospitali za hapa nchini hali hii inasaidia kuondoa gharama za matibabu ya nje ya nchi.

Kutokana na uwekezaji mkubwa uliofanyika katika kuboresha huduma za kibingwa na bobezi, nchi yetu imeweza kuvutia wagonjwa mbalimbali kutoka nje ya nchi.

Alisema Rais Dk. Samia anataka kuibadilisha sekta ya afya na iwe ni kitovu cha utalii kwa nchi za Afrika Mashariki na Kati na hilo linaonekana kutoka na huduma zinazotolewa katika hospitali zetu kuwa za kibingwa na kibobezi.

Miaka mitatu ya Rais Dk. Samia imewezesha tiba za nchini kuwa tiba za kiutalii kwa sababu ya kuongezeka kwa idadi ya wagonjwa kutoka nje ya nchi wanaokuja kutibiwa ilikuwa 6,931 ikilinganishwa na wagonjwa 3,957 mwaka 2022.

Alifafanua kuwa wagonjwa hao, wanatoka katika nchi za Comoro, Malawi, Burundi, Zambia, Congo DRC, Uganda, Zimbabwe na Kenya.

Dk. Ndilanha alisema wagonjwa hao wanapata matibabu katika Hospitali ya Taifa Muhimbili, Taasisi ya Saratani ya Ocean road, Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete, Taasisi ya Mifupa (MOI).

Miaka mitatu ya Rais Dk. Samia katika sekta ya afya amefanya vizuri eneo la ajira kila mara inaonekana ajira za sekta hiyo zinavyotoka hali hiyo haionekani kwa sekta nyingine na kuona kada ya afya tumependelewa sana.

"Serikali ya Rais Dk.Samia inaendelea kufanya uwekezaji katika eneo la rasilimali watu katika afya ikiwemo kuajiri watumishi wapya wa Sekta ya Afya na kusomesha wataalamu wa afya katika fani mbalimbali za ubingwa na ubobezi" alisema.

Alisema pamoja na kufanya marekebisho katika vifaa tiba pia anafanya maboresho ya kuongeza ujuzi kwa wafanyakazi wa sekta hiyo kuweza kuimarika na kuwa ya mfano kwa mataifa mbalimbali.

"Ufadhili wa mama Samia alioutoa kwa wanafunzi wa masomo ya sayansi pamoja na madaktari wabobezi katika fani mbalimbali unasaidia kuongeza ujuzi kwa madaktari wabobezi na kupunguza changamoto za kiafya,"alisema.

Kuongeza idadi ya watumishi wa afya Serikali imeendelea kuajiri wataalam katika Sekta ya Afya ambapo jumla ya wataalamu 35,450 wa kada mbalimbali wameajiriwa na kusambazwa katika vituo vya kutolea huduma za afya nchini.

Katika kipindi cha kuanzia mwaka 2021 hadi 2024, jumla ya ajira za mikataba kwa watumishi wa Afya 2,836 kupitia miradi mbalimbali ya Serikali zilitolewa.

Ongezeko la Madaktari bingwa na bobezi jumla ya madaktari bingwa nchini, hadi kufikia mwaka jana wamefikia 2,464 ukilinganisha na madaktari Bingwa 805 mwaka 2020.

Naye Daktari Bingwa wa Magonjwa ya Afya ya Akili kutoka Hospitali ya Kanda ya Mbeya Dk.Raymond Mgeni alisema katika miaka mitatu ya uongozi wa Rais Dk.Samia, amesaidia magonjwa ya afya ya akili kupewa kipaumbele na kufanyika mdahalo mkubwa wa kitaifa wa kujadili suala hilo.

"Miaka mitatu ya uongozi wa Rais Dk.Samia tumeweza kuona hatua kubwa katika sekta ya afya kupitia Wizara ya Afya hasa katika wigo wa afya ya akili. Kwa kipindi cha uongozi wake ilikuwa mara ya kwanza kwa Tanzania kufanya mdahalo wa kitaifa kuhusu afya ya akili Oktoba 2022,"alisema

Aidha Dk.Mgeni alisema, katika uongozi wa Rais Dk.Samia serikali iliweka kipaumbele kada ya afya ya akili kwa kuongeza bajeti na kutanua huduma hiyo.

Alisema kwa kipindi cha muda mrefu kabla ya uongozi wa Rais Dk.Samia, magonjwa ya afya ya akili yalikua hayapewi uzito, lakini baada ya kuingia madarakani kukawa na mabadiliko makubwa.

Rais Dk.Samia aliingia madarakani Machi 19 mwaka 2021 baada ya aliapishwa na Jaji Mkuu wa Tanzania Profesa Ibrahim Juma katika Ikulu ya Magogoni Jijini Dar es Salaam.

Rais Dk.Samia alichukua nafasi ya Hayati Dk.John Magufuli ambaye alifariki dunia Machi 17 katika Hospitali ya Mzena Dar es Salaam alipokua akipatiwa matibabu ya ugonjwa wa moyo.



Muonekano wa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Songwe

"Katika kuimarisha huduma za uchunguzi wa mionzi kwa wagonjwa, Serikali imenunua vifaa Tiba vya Uchunguzi na matibabu ya wagonjwa vyenye thamani ya shilingi bilioni 290.9, vinapatikana kuanzia ngazi ya Hospitali za Taifa hadi Hospitali za Rufaa za Mikoa na Halmashauri.

"Tumekamilisha ufungaji wa mashine ya uchunguzi na matibabu ya mishipa ya damu (Angio Suite) kwenye Taasisi ya Tiba ya Mifupa Muhimbili (MOI) kwa ajili ya kufanya upasuaji wa ubongo bila kufungua kichwa uliogharimu shilingi bilioni 7.9"

"Katika kipindi cha mwaka 2021 hadi Machi 2024, Serikali ya Awamu ya Sita imeendelea kuwekeza katika huduma za afya ya Uzazi, Mama na Mtoto

"Serikali imeendelea kuajiri wataalam katika Sekta ya Afya ambapo jumla ya wataalam 35,450 wa kada mbalimbali wameajiriwa na kusambazwa katika vituo vya kutolea huduma za afya nchini katika kipindi cha kuanzia mwaka 2021 hadi 2023.




UHURU ya Kijani

MAONI YA MHARIRI

# Miaka mitatu ya mafanikio ya sekta ya afya nchini

AFYA ni moja ya nyenzo muhimu katika maisha ya binadamu, kutokana na hilo serikali imekuwa ikitilia mkazo suala hilo kwa kuwa taifa lenye nguvu ni lile lenye rasiliamali watu wenye afya bora.

Kwa kutambua hilo, serikali ya Tanzania katika awamu zote za utawala imekuwa ikitoa kipaumbele katika suala la afya ya wananchi wake, kupitia programu na mikakati mbalimbali ya kuhakikisha afya za wananchi zinalindwa kwa gharama yoyote.

Katika kipindi cha miaka mitatu ya serikali ya awamu ya sita, inayoongozwa na Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, tumeshuhudia mageuzi makubwa katika sekta ya afya.

Mageuzi hayo ni kupitia uboreshaji mkubwa wa miundombinu, upatikanaji wa dawa, damu salama na huduma za mama na mtoto.

Lengo ni kuhakikisha kila Mtanzania anafikiwa na huduma za afya, zikiwemo za kibingwa kwa urahisi na kwa gharama nafuu katika kila pembe ya Tanzania.

Katika kipindi cha miaka mitatu ya Serikali ya Awamu ya sita inayoongozwa Rais Dk. Samia imeendelea kuwekeza katika kuboresha miundombinu, upatikanaji wa dawa, damu salama na huduma za afya ya uzazi mama na mtoto.

Kwa upande wa miundombinu, Serikali imekamilisha ujenzi wa Hospitali ya Mama na Mtoto Meta iliyopo katika Jiji la Mbeya ambayo hadi sasa imegharimu shilingi bilioni 13.2, sanjari na ujenzi wa majengo ya huduma za Mama na Mtoto kwenye Hospitali za Rufaa za Mikoa ambazo ni Sekou Toure (Mwanza), Geita, Simiyu, Mawenzi, Njombe na Songwe ambazo zimegharimu shilingi bilioni 71.1.

Kukamilika kwa ujenzi wa majengo hayo kumepunguza mlundikano wa kina mama wajawazito ikiwemo kulala zaidi ya mtu mmoja kitanda kimoja, au kulala chini, na kutoa huduma yenye staha.

Aidha, imeendelea kuboresha huduma za uzazi kwa kuweka miundombinu stahiki na vifaa tiba katika vituo vya afya ili kuviwezesha kutoa huduma za uzazi na dharura ikiwemo upasuaji wa kumtoa mtoto tumboni.

Pia vituo vya afya 92 vilipata mafunzo na hivyo kuongeza idadi ya vituo vya afya vyenye uwezo wa kutoa huduma hizo kutoka 329 mwaka 2020 kufikia 421 hadi sasa, hivyo kufikia lengo la kitaifa la angalau asilimia 50 ya vituo vya afya nchini viweze kutoa huduma hiyo.

Serikali ya Rais Dk. Samia kupitia Wizara ya Afya imeendeelea kuwajengea uwezo wakunga na wauguzi ili kuimarisha utoaji wa huduma za uzazi ambapo Wizara kwa kushirikiana na Hospitali za Taifa na Kanda ilipeleka madaktari bingwa wa magonjwa ya uzazi na kina mama (20), madaktari bingwa wa huduma za usingizi na ganzi (20), watalaamu wa vyumba vya upasuaji, 20, wauguzi na wakunga (20) kwenye mikoa ya Singida, Shinyanga, Njombe na Tanga. Jumla ya watumishi 185 walijengewa uwezo katika vituo vya kutolea huduma kwenye mikoa hiyo.

Kimsingi uwekezaji uliofanywa ndani kipindi cha miaka mitatu ni mkubwa na hivyo kuwawezesha wananchi kupata huduma bora za afya na kibingwa ikiwemo upatikanaji wa vipimo sahihi kwa muda mfupi.

Uwekezaji huo umeifanya Tanzania kuvutia watu kutoka mataifa jirani kupata huduma za tiba za kibingwa na wakati huo huo kupunguza idadi ya Watanzania waliokuwa wakitibiwa nje ya nchi.

Pia umeipunguzia serikali mzigo wa kutumia fedha za kigeni kwa ajili ya kusafirisha wagonjwa nje ya nchi kwa ajili ya matibabu ya kibingwa ikiwemo uchunguzi wa afya.

Hivyo ndani ya miaka mitatu ya Rais Dk. Samia madarakani, sekta ya afya ina mengi ya kujivunia mbele ya wananchi kutokana na uwekezaji mkubwa uliofanywa kuongeza tija katika utoaji wa huduma za afya nchini.

## ENZI HIZO

KATIBU Mkuu wa TANU, Meja Hashim Mbita, akipokea hundi ya ya sh.100,000 kutoka kwa Mwenyekiti wa Umoja wa Wanawake Tanzania (UWT) Bi Sofia Kawawa kwa ajili ya ujenzi wa Makao Makuu ya TANU Dar es Salaam. Hiyo ilikuwa mwaka 1971.



**Uhuru Publications Limited (UPL)**
S.L.P. 9221, Dar es Salaam
Makao Mkuu: Mtaa wa Lumumba Mkabala na Shule ya Msingi Mnazi Mmoja
**Chumba cha Habari:**
+255-739 957 882/FAX: 2183780
email: uhurunews@yahoo.com
uhuruadvert@gmail.com
uhurumakala@gmail.com

**Mkurugenzi Mtendaji Mkuu:** ____________________ 0655 - 355810
**Naibu Mhariri Mtendaji:**________________________ 0784 - 599717
**Mhariri wa Habari:** _____________________________ 0714 - 140524

IDARA YA BIASHARA
**Meneja Biashara UPL:**___________________________ 0683 - 378522
**Meneja Matangazo:** ______________________________0765 - 142207
**Meneja Mauzo na Usambazaji:** __________________0683 - 378522

UHURU FM (PMCL)



Mheshimiwa Rais Dk. Samia Suluhu Hassan akimjulia hali mtoto aliyepandikizwa uloto katika Hospitali ya Benjamin Mkapa jijini Dodoma.

# MAFANIKIO BMH

**Daktari** Bingwa Kelvin Masava asema fedha alizowekeza Rais Samia zimewezesha Watanzania zaidi ya 1,400, raia wa kigeni kutibiwa moyo kwa msaada wa mtambo wa Catheterization.



Madaktari wakiendelea na upasuaji wa moyo.

**Katika** mwaka mmoja tangu kuanzishwa huduma, watoto wanane wapona ugonjwa wa selimundu

**Daktari** Bingwa Stella Malangahe amshukuru Rais Samia kuwapa bilioni 2.7/- zilizoleta mafanikio hayo




Mheshimiwa Waziri Mkuu Kassim Majaliwa akikata utepe kuzindua huduma za upandikizaji uloto katika hospitali ya Benjamin Mkapa.

**MAWASILIANO**
Hospitali ya Benjamin Mkapa
SLP 11088, Dodoma-Tanzania
Simu : +255-262963710
Barua pepe : info@bmh.or.tz
Tovuti : www.bmh.or.tz

## HOSPITALI YA BENJAMIN MKAPA Inavyotekeleza Ilani kwa kishindo

**MAFANIKIO MAKUBWA YAPATIKANA TIBA UPANDAKIZAJI ULOTO**



MHESHIMIWA Rais Dk. Samia Suluhu Hassan akisikiliza maelezo kutoka kwa Dkt. Bingwa Stella Malangahe kuhusu maendeleo ya mtoto aliyepandikizwa uloto Hospitali ya Benjamin Mkapa jijini Dodoma.

# Mafanikio makubwa upandikizaji uloto Hospitali ya Benjamin Mkapa

>>**Katika** mwaka mmoja tangu kuanzishwa huduma, watoto nane wapona ugonjwa wa selimundu

>>**Daktari** Bingwa Stella Malangahe amshukuru Rais Samia kuwapa bilioni 2.7/- zilizoleta mafanikio hayo

**Na FRED MAJALIWA**

SERIKALI imezidi kupiga hatua kubwa katika sekta ya afya kwa kuboresha huduma za matibabu ya kibingwa na bobezi ambazo baadhi hazikuwepo nchini kwa takriban miaka 40.

Miongoni mwa huduma hizo ni upandikizaji uloto kwa wagonjwa wa selimundu, ambao matibabu yake yalianza kutolewa nchini mwaka mmoja uliopita katika Hospitali ya Benjamin Mkapa (BMH) iliyoko mkoani Dodoma.

Kwa mujibu wa Mkurugenzi Msaidizi Idara ya Magonjwa ya Saratani na Damu Hospitali ya Benjamin Mkapa, Dkt Stella Malangahe, huduma ya kupandikiza uloto nchini ni ngeni, miaka 40 iliyopita ilikuwa ikitolewa kwa nchi zilizoendelea mfano barani Ulaya, Amerika au Asia, ingawa idadi ya wanaougua ugonjwa huo ni kubwa nchini na Afrika kwa ujumla.

Jumla ya watu 1,000 huzaliwa na ugonjwa wa selimundu kila siku duniani huku Tanzania 11,000 wakikadiriwa kuzaliwa na ugonjwa huo kila mwaka.

Tanzania ni nchi ya tano duniani kuwa na idadi ya wagonjwa wengi wenye selimundu na inashika nafasi ya nne barani Afrika, hali inayopaswa kutiliwa mkazo kuuthibiti ugonjwa huo. Nchi zenye wagonjwa wengi ni Nigeria, India, Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo (DRC) na Angola.

Dkt Stella alisema ugonjwa huo husababisha athari katika ini, figo, mapafu na kupooza ikiwemo vifo vya mapema huku akibainisha asilimia 80 ya watu wanaougua ugonjwa huo ni kutoka katika nchi za Jangwa la Sahara.

**UWEKEZAJI WA SERIKALI**

Dkt Stella alisema serikali inastahili pongezi kwa kuwekeza fedha nyingi katika hospitali hiyo kiasi cha kufanikisha kuanzishwa huduma ya matibabu ya kibingwa na bobezi ya upandikizaji uloto katika Hospitali ya Benjamin Mkapa na magonjwa mengine.

Stella ambaye ni Daktari Bingwa wa Magonjwa ya Damu na Mkuu wa Kitengo cha Upandikizaji Uloto katika hospitali hiyo ya kanda, alisema tangu kuanzishwa huduma hiyo wamefanikiwa kuwapandikiza uloto watoto nane.

"Serikali iliposikia mafanikio tuliyopata kwa kupandikiza wagonjwa wa kwanza, ikaja ikasema wagonjwa 20 wa kwanza watakaopandikizwa mwaka huu wa fedha, itagharamia na hadi hivi sasa wagonjwa nane tuliowapandikiza hakuna aliyetoa fedha zake mfukoni," alisema.

**SH. MILIONI 65 AU 75**

**ya kumpandikiza uloto mtoto ni gharama nafuu kuliko muda mrefu kutumia dawa za kupunguza makali, kukinga maambukizi ya bakteria, kuugua kila mara na mzazi kupoteza muda hospitali sababu ya kuugua.**



**Mkurugenzi Mtendaji wa Hospitali ya Kanda ya Benjamin Mkapa, Dkt. Alphonce Chandika.**

Alieleza serikali imetoa sh. bilioni 2.7 kufanikisha maandalizi yaliyochukua takribani miaka mitano hadi kuweza kuanzishwa huduma ya upandikizaji uloto katika Hospitali ya Benjamin Mkapa.

Fedha hizo zimegharamia ujenzi wa wodi, kutoa mafunzo ndani na nje ya nchi kwa watalaamu, ununuzi wa vifaatiba na huduma za maabara na damu salama.

Dkt Stella alisema serikali imewekeza kiasi hicho kikubwa cha fedha kupunguza gharama za matibabu kutokana na wagonjwa kusafirishwa nje ya nchi.

Alisema tangu serikali ilitangaza kuwasaidia wagonjwa 20 wa mwanzo na hospitali kutoa msamaha, mwitikio umekuwa mkubwa kwa wenye kadi za bima na wasio na bima kujitokeza kufuata huduma hiyo ya kupandikizwa uloto na hivi sasa miongoni mwa wagonjwa hao wapo katika foleni kusubiri tiba.

"Kiuhalisia mafanikio ambayo tumeyapata chini ya uongozi wa Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, kwanza kabisa kupitia Hospitali ya Benjamin Mkapa ni kupata ushirikiano mkubwa wa kufanikisha kuzindua huduma ya upandikizaji uloto kwa watoto wenye changamoto ya selimundu," alisema.

**GHARAMA ZA MATIBABU**

Akieleza kuhusu gharama za matibabu, Dkt Stella alisema kwa wastani mgonjwa mmoja inakadiriwa anatibiwa kwa sh. milioni 75 hadi 80. Gharama hiyo kabla inahusisha maandalizi na baadaye matibabu.

"Kuna gharama za awali kwa mgonjwa na mtu anayemchangia uloto, halafu kuna gharama kwa upandikizaji uloto ambayo ni sh. milioni 55 hadi 65," alifafanua.

Dkt. Stella pia alisema katika maandalizi, gharama kubwa ya vipimo inafanywa kwa ushirikiano kati ya Hospitali ya Benjamin Mkapa na maabara ya genetics iliyoko nchini Ujerumani.

**FEDHA ZILIZOOKOLEWA**

Dkt Stella alisema kuanzishwa huduma za upandikizaji uloto katika Hospitali ya Benjamin Mkapa, kumeokoa fedha nyingi za serikali ambazo zingetumika nje ya nchi kutibu watoto wanane.

"Kwahiyo, wagonjwa nane waliotibiwa nchini tumeokoa fedha nyingi. Pia muda wa mzazi au ndugu kumuhudumia mgonjwa umepungua," alisema.

Hata hivyo, Dkt Stella alibainisha malipo ya sh. milioni 65, 70 au 80 ya kumpandikiza uloto mtoto ni gharama nafuu kuliko kutumia dawa za kupunguza makali, kukinga maambukizi ya bakteria, kuugua mara kwa mara na mzazi kupoteza muda mwingi hospitali sababu ya kuuguza.

"Hizo gharama zote zinalinganishwa na kumtibia mtoto kwa staili hiyo kati ya miaka sita hadi nane. Pia akifikisha miaka 16 gharama zinaongezeka mara mbili yake wakati ukimpandikiza uloto, ugonjwa inakuwa umeishia hapo," alisema.

Dkt Stella alisema huduma hiyo hufanyika kwa muda wa miezi sita na mgonjwa anakuwa ameondokana na tatizo kabisa.

Alisisitiza licha ya ukubwa wa gharama kwa miaka yote ya kuuguza, pia uwezekano wa mtoto kupoteza maisha unaendelea kuwa mkubwa, kwani huduma ya sasa ya kupunguza makali haitoi suluhisho la kudumu kwa mgonjwa.

"Kwa hiyo gharama ya kupandikiza uloto kwa mara moja (sh. milioni 70 au 80) inalinganishwa na gharama ya kumuuguza mgonjwa kwa miaka sita hadi nane."

Alisema ukubwa huo wa gharama unachangiwa na vifaatiba kuagizwa kutoka nje ya nchi, kwani kuna dawa zinazouzwa sh. milioni moja badala ya

# Watoto nane wapona selimundu baada ya kupandikizwa uloto

sh. 400,000 au 500,000 kutokana na kuwa hazitoki ndani ya nchi.

Dkt Stella akitaja gharama za matibabu kwa nje ya nchi, alisema mgonjwa anayepatiwa matibabu hukadiriwa kutumia sh. milioni 100 hadi 150 kwa matibabu, wakati Ulaya na Marekani ni sh. milioni 250 mpaka 300.

Kuhusu bei kubwa ya vifaatiba, daktari huyo alisema matumaini yaliyopo huduma ikiendelea kupanuka, wazabuni wanaoagiza vifaa kutoka nje ya nchi watapunguza bei kwa wahitaji ambao watakuwa ni wengi kutofautisha na sasa wapo wachache.

**MAFANIKIO, MATARAJIO**

Dkt Stella alisema uongozi wa Hospitali ya Benjamin Mkapa unatarajia kukuza huduma kwa kuwafikia watu wengine wenye changamoto ya mfumo wa damu zikiwemo saratani na magonjwa ya kurithi mfano selimundu.

"Kwa hivyo kuzungumzia moja kwa moja mafanikio makubwa ambayo tumeyapata ni kupandikiza uloto katika kipindi cha mwaka mmoja wa huduma hiyo," aliongeza.

Alisema baada ya kuwapandikiza uloto watoto wanane waliokuwa wakiugua selimundu tayari wanafurahia matokeo ya kupona kwao, hivyo aliutaka umma kujitokeza kuchangamkia huduma hiyo katika Hospitali ya Benjamin Mkapa.

Aliiomba serikali kuwaongezea uwezo kwani hivi sasa wodi yao ya kutolea huduma inamudu kuchukua wagonjwa wanne kwa mara moja na mgonjwa akishahudumiwa hubaki kwa uangalizi muda wa mwezi mmoja.

"Uwezo wa wodi ni wagonjwa wanne ambao wanapishana ndani ya mwezi mmoja au mwezi mmoja na nusu anakuwa tayari kutoka nje, ndipo mwingine anaingia.

**SELIMUNDU INARITHIWA**

Dk. Stella alisema selimundu ni ugonjwa wa kurithi kutoka kwa wazazi wote wawili, lakini lazima mgonjwa awe amepata kopi zote mbili kutoka kwa baba na mama yake, kwani anayepata kopi moja hawezi kuugua.



***Kiuhalisia mafanikio ambayo tumeyapata chini ya uongozi wa Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, kwanza kabisa kupitia Hospitali ya Benjamin Mkapa ni kufanikisha kuzindua huduma ya upandikizaji uloto kwa watoto wenye selimundu.***
**Dkt. Stella Malangahe.**

Hivyo, alitahadharisha umuhimu wa kuzingatia kupima selimundu kabla ya kufunga ndoa kuepuka kuzaa watoto wenye kinasaba cha ugonjwa huo.

"Katika Watanzania milioni 60, kati yao asilimia 29 wanabeba kopi moja mbovu ya kinasaba japokuwa hawaugui, hivyo kuna haja ya kumpima mwenza wako kabla ya kuanzisha naye uhusiano kuepuka hilo tatizo kuendelea kwa watoto baadaye," alitahadharisha.

**MAFUNZO NA UPANDIKIZAJI**

Dkt Stella alitaja mchakato wa matibabu kwa mgonjwa wa selimundu, kwanza analazimika kuwa na ndugu wa kuzaliwa tumbo moja ambao hutolewa chembechembe ambazo hupimwa kuangalia ufanano na mgonjwa na ikithibitika vipo sawa, ndipo hatua ya upandikizaji inafuata.

"Mtu mmoja anaweza kuwa na wachangiaji watano au mmoja na kutokana na wingi huo, uwezekano wa kufanana kinasaba inakuwa ni mkubwa," alieleza.

Aliongeza: "Kinasaba lazima kipatikane kupitia ndugu uliyezaliwa naye tumbo moja. Lakini huenda usifikie kiwango cha kinasaba hata kama mnafanana sura kwa asilimia 99.9."

Dkt Stella alisema kwa mujibu wa utafiti uliofanywa duniani, asilimia 20 hadi 30 kati ya watu wanaopimwa vinasaba, ndiyo huwa na uwezekano wa kufanana.

"Tunatathmini protini sita, tukipata tatu kutoka kwa ndugu wa mgonjwa, zinatosha kumpandikiza selimundu na kikubwa tunazingatia tukipandikiza uloto mwilini kusitokee tatizo maana kuna baadhi ya protini nyeti sana tukizigusa inakuwa hatari sana kwa mgonjwa kwa kusababisha vurugu kubwa mwilini."

Alisema mgonjwa akishapandikizwa uloto, unapaswa kuota ndani ya wiki mbili hadi tatu, lakini kabla ya kufanyiwa huduma hiyo hulazimika kulazwa siku 10 katika chumba cha upasuaji na kupewa 'chemotherapy' kuondoa uloto uliomo mwilini.

Daktari huyo bingwa akieleza mchakato wa kupata uloto kutoka kwa ndugu wa mgonjwa jinsi unavyokuwa, alisema hatua zinazofanyika ni kupimwa afya yake kujiridhisha iwapo atahimili misukosuko katika chumba cha upasuaji kwa kuwa ni lazima kuzingatia usalama wa mchangiaji.

"Chembechembe mama ziko ndani ya mifupa kama nyumba na ili tuweze kupata kirahisi tunaangalia katika mifupa mipana mfano kifua au kalio. Tunaingia ndani ya mfupa kwa kutoboa, tunavuna hizo chembechembe mama. Ni ndani ya saa moja hadi mawili tunakuwa tumeshavuna uloto," alieleza.

Alisema timu ya wataalamu walioanza kutoa huduma ya kupandikiza uloto Hospitali ya Benjamin Mkapa licha ya kupata mafunzo ya ndani ya nchi, pia imeongezewa ujuzi kupitia shirika lisilo la kiserikali la Help3 la nchini Italia ambako walisafiri kwenda kujifunza wenzao wanavyofanya.



MHESHIMIWA Waziri Mkuu Kassim Majaliwa akimsikiliza mtoto wodini baada ya kupandikizwa uloto.

"Pia tumefanya mafunzo kwa njia ya simu (teleconference) timu tuliyoshiriki ni madaktari wawili, wataalamu wa maabara wawili, wauguzi wanne, mtalaamu mmoja wa mionzi (radiologist) na mwingine ni mhandisi wa biomedical. Mafunzo ya kuanzisha hii huduma yalipamba moto wakati ambao ugonjwa wa Uviko-19 ulikuwa umeshika kasi duniani," alisema.

Dkt Stella aliweka wazi walipomaliza mafunzo na kukamilishwa maandalizi mengine muhimu, walianza kuwapandikiza uloto watoto watatu kwa kushirikiana na wataalamu hao wa kutoka nje ya nchi, lakini kuanzia mgonjwa wa nne hadi kufikia wa nane, alifanya yeye (Stella) kwa kushirikiana na Dkt Shakilu Jumanne.

Alisema anaamini kwao ni mafanikio makubwa sana kwa kuweza kufanya upandikizaji bila kuongozwa na wataalamu wa kigeni ambao wamekuwa wakija nchini na kuondoka kwa lengo la kuendeleza ushirikiano katika matibabu hayo.

"Tuko tayari kutoa huduma kwa Watanzania na raia wa kigeni kwa sababu tayari tumeshapokea maombi mengi sana ya kuhitaji huduma hizi kutoka nchi za Kenya, Uganda, Zambia, Zimbabwe," alisema.

Alisema pia kuna taasisi za afya kutoka nchi jirani ambazo zimefika Hospitali ya Benjamin Mkapa kuuliza utaratibu wa kuwatibu raia wa nchi hizo, jambo ambalo wanaona mwaka huu huenda wakapandikiza uloto hadi anga ya kimataifa.

**RASILIMALI WATU**

Alisema kwa kuwa malengo yao ni kuongeza wodi, wanatamani kwenda na viwango cha kimataifa kwa mgonjwa mmoja kuhudumiwa na muuguzi mmoja, tofauti na sasa nesi mmoja anahudumia mgonjwa mmoja na nusu au wawili jambo ambalo haliko sawa kitaalamu.

"Tukipata nafasi ya kuongeza wodi tutarajia kuwa na watumishi wengine, manesi, madaktari, wafamasia na wataalamu wa maabara. Pia tunatarajia kuwaendeleza wahudumu walio tayari kufanya kazi katika kitengo cha kupandikiza uloto."

Alisema kiu yao kuwa na madaktari bingwa wanne au watano badala ya wawili waliopo hivi sasa.

Hospitali ya Benjamin Mkapa ilizinduliwa rasmi Oktoba 13, mwaka 2015, ambapo kuanzishwa kwake imekuwa ni mkombozi kwa taifa dhidi ya magonjwa ya kuambukiza ambayo husababisha vifo vingi.



MHESHIMIWA Waziri Mkuu Kassim Majaliwa na Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu wakisikiliza maelezo kutoka kwa Dk. Stella Malangahe kuhusu kutibu uloto.

# HOSPITALI YA BENJAMIN MKAPA Inavyotekeleza Ilani kwa kishindo




Hospitali ya Benjamin Mkapa.

**>>Ni** kutokana na kufunga mtambo wa matibabu ya kibingwa na bobezi ya moyo ambao umeokoa maisha ya maelfu ya wagonjwa

**>>Daktari** Bingwa Kelvin Masava asema fedha alizowekeza Rais Samia zimewezesha Watanzania zaidi ya 1,400, raia wa kigeni kutibiwa

**>>Aeleza** mtambo huo wa kisasa umeokoa fedha nyingi za serikali kutokana na wagonjwa wengi kutibiwa nchini badala nje ya nchi

**Na FRED MAJALIWA**

HOSPITALI ya Benjamin Mkapa (BMH) ni miongoni mwa hospitali zenye hadhi ya juu inayotekeleza Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) kwa kishindo nchini.

Hospitali hiyo imekuwa ikifanya vema katika utoaji wa huduma za matibabu ya kibingwa na bobezi kwa magonjwa yasiyoambukiza mfano; moyo, figo, ini, nyonga na magoti, ubongo na mishipa ya fahamu. Pia, inachunguza na kutibu magonjwa mengine ikiwemo malaria, kifua, homa na mengineyo.

Dhahiri kufanikiwa katika utoaji huduma za matibabu ya kibingwa na bobezi kumeifanya Hospitali ya Benjamin Mkapa iliyoko mkoani Dodoma, kugeuka kimbilio la Watanzania na raia wa kigeni.

BMH ambayo 'ilizaliwa' rasmi Oktoba 13, mwaka 2015 ni hospitali yenye majukumu ya kuhudumia wagonjwa katika mikoa ya Kanda ya Kati na mikoa ya jirani nchini lakini kadiri miaka inavyosonga mbele, wagonjwa wa ndani na kutoka pembe ya Afrika kwa ujumla, wamekuwa wakifurika hospitalini hapo kufuata matibabu ya kibingwa.

Matibabu ya kibingwa na bobezi ya moyo, eneo mojawapo ambalo hospitali hiyo imepata mafanikio makubwa kwa uchunguzi na matibabu ya ugonjwa huo.

Kwa mujibu wa Daktari Bingwa Kelvin Masava ambaye ni Kaimu Mkuu wa Idara ya Moyo (Cardiology Department) katika Hospitali ya Benjamin Mkapa, uwekezaji mkubwa uliofanywa na serikali kwa kununua mtambo wa kisasa uitwao Catheterization Laboratory, umewasaidia kutoa huduma za kisasa na uhakika kwa wagonjwa.

"Mtambo huu (CathLab) umewezesha maelfu ya wagonjwa kupimwa na kutibiwa kibingwa na ubingwa bobezi kwa magonjwa yote yanayohusiana na moyo na mishipa ya damu," alisema Dkt Masava.

Mbali na mtambo huo ulionunuliwa kutoka nje ya nchi mwaka 2019, bingwa huyo wa magonjwa ya moyo alisema idara yao pia imekuwa ikitoa kliniki ya huduma za kichunguzi, matibabu kwa wagonjwa wa kila siku kupitia kliniki zao, vipimo vya kawaida na udaktari bingwa na bobezi.

Kwa mujibu wa Dkt Masava, majukumu yao mengine ni kufanya vipimo vya kawaida (non-invasive), kupima umeme wa moyo, ultra sound maalumu ya moyo, shinikizo la damu kwa kufunga kifaa kwa mgonjwa saa 24 kwa lengo la kupata uhakika wa presha za mtu.

"Vile vile tunafanya Stress ECG kupima umeme wa moyo kwa mgonjwa kutakiwa kukimbia katika mashine kama zinazotumika katika mazoezi ya 'gym'," alitaja majukumu hayo.

Alisema kutokana na Hospitali ya Benjamin Mkapa kuwa na hadhi ya kanda, ndiyo maana ilipatiwa mtambo wa Catheterization ambao kimsingi ni X-Ray inayofanya kazi kwa kutoa mionzi na kupata picha ya video papo hapo.

Daktari huyo alifafanua video hiyo huwezesha timu ya madaktari kuchunguza magonjwa ya moyo na kutoa matibabu yake kwa njia ya matundu madogo.

"Tunamshukuru Mungu serikali yetu ya awamu ya sita inayoongozwa na Mheshimiwa Rais Dk. Samia Suluhu Hassan kutuletea huu mtambo," alisema.

Alitaja faida nyingine za mtambo huo unawawezesha kubaini magonjwa ya mishipa ya damu inayolisha misuli ya moyo ambayo ikiziba ghafla inasababisha mshituko wa moyo na mtu kupoteza maisha.

"Au inaweza kutokea muda mrefu mtu anachoka haraka na hawezi kutembea hata kilometa sita hili ni tatizo kubwa sana kitaifa," alibainisha.



**Kaimu Mkuu wa Idara Moyo, Dk. Kelvin Masava.**

"Sasa mtambo huu ndiyo tunautumia kuchunguza na kugundua ni mshipa gani na kuweza kuuzibua na kuokoa maisha ya mgonjwa, tumefanikiwa kufanya hivyo kwa wagonjwa wengi kutokana na msaada wa kifaatiba hiki na vingine tunavyotumia," alisema.

Alieleza idara hiyo imeendelea kufanya hivyo kwa wagonjwa wa mshtuko wa moyo na ambao mshipa umeziba muda mrefu na kusababisha maumivu katika kifua au uchovu na kuwatibu kwa kutumia mtambo huo.

"Vile vile mtambo umetusaidia kugundua na kutibu magonjwa ya mtu mwenye tundu katika moyo, lakini kupitia mtambo huu tumegundua wagonjwa wengi, hasa watoto kwasababu huzaliwa na hayo matundu na hugundulika kwa dalili za moyo kushindwa kufanya kazi vizuri na ukuaji kutokuwa mzuri," alisema.



**Madaktari wa moyo wakifanya kipimo kwa kutumia mtambo wa CathLab.**



Wataalmu wa moyo wakimfanyia vipimo mgonjwa kupitia mtambo wa kisasa wa CathLab.

## SHILINGI BILIONI 5

**Ni thamani ya mtambo (Catheterization Machine) ulioko Hospitali ya Benjemin Mkapa (BMH). Aidha, mtambo huo wa kisasa kwa hospitali zote za serikali katika ukanda wa Afrika Mashariki unapatikana katika hospitali hiyo jijini Dodoma.**

# Watanzania 1,400 wanufaika kwa matibabu ya moyo BMH

Aliongeza: Kwa hiyo baada ya kufanya vipimo vya awali ECG na ECHO na kuona shida tunamleta mgonjwa katika mtambo huu kwa kufanya uchunguzi na kujiridhisha kisha tunamziba kwa vifaa tofauti. Tunafaidika na uwepo wa mtambo huu."

Alibainisha pia kuna aina ya tatu ya magonjwa ya mfumo wa umeme katika moyo ambao betri yake inashindwa kufanya kazi na misuli kushindwa kusisimua na kusababisha mtu kuanguka, hivyo kupitia mtambo wa CathLab wakigundua tatizo humsaidia kumweka betri katika kifua na nyaya zake.

"Ni hospitali mbili pekee za taifa zinazomilikiwa na serikali tulizobahatika kumiliki mtambo huu kwa Afrika Mashariki. Sehemu nyingine mtambo wanao, lakini unamilikiwa na hospitali ambazo siyo za serikali," alieleza.

Dkt Masava alimshukuru Rais Samia kwa kuendelea kuunga mkono na kusaidia huduma za afya, hasa katika matibabu ya magonjwa ya moyo.

**TAKWIMU WALIOTIBIWA**

Kwa mujibu wa Dkt Masava, kuanzia mwaka 2019 huduma ya mtambo huo ilianza, jumla ya wagonjwa 21 wamefaidika kwa kuwekewa betri (pacemaker) katika moyo katika miaka mitano ya utoaji huduma.

Kwa upande wa matundu katika moyo waliozibwa ni 22 ambao wengi wao ni watoto waliozaliwa na matundu katika moyo na waliofaidika kwa asilimia kubwa ni wagonjwa wa mishipa ya damu inayolisha misuli ya moyo ambao ni 1,400, lakini waliofaidika kwa uchunguzi na kuzibuliwa jumla yao ni 250.

Alisema hadi mwaka huu wageni waliofaidika na huduma za BMH ni wanne waliotibiwa matibabu ya mishipa ya damu inayolisha misuli ya moyo ambao kati yao, watatu kutoka DRC na mmoja Burundi.

"Kutokana na mtambo kufanikisha matatibu haya, serikali imeokoa fedha nyingi kwani jibu la uhakika ninaloweza kukupa zaidi ya asilimia 97 ni wagonjwa wanaotumia huduma za bima ya afya," alieleza.

Akichambua gharama, bingwa huyo wa magonjwa ya moyo alisema mishipa ya damu inayolisha misuli ya moyo uchunguzi wake tu, siyo kuzibua, sh. milioni mbili na mgonjwa akikutwa ana shida na kuzibuliwa gharama yake ni sh. milioni 6.

"Kwa hiyo unaweza kuzidisha hao wagonjwa 1,400 mara sh. milioni mbili (sh. bilioni 2.8), na waliozibuliwa mara sh. milioni 6 (sh. bilioni 1.5) utaona serikali imeokoa gharama kiasi gani," alisema.

Alibainisha gharama hizo ambazo kwa sehemu kubwa serikali imezipunguza kwa kununua mtambo huo na vifaa vingine vya matibabu ya moyo, zinazidi endapo wagonjwa hao wangesafirishwa nje ya nchi kufuata matibabu ya kibingwa.

"Kuna gharama ya nauli ya usafiri wa ndege na mgonjwa analazimika kusindikizwa na mtu mmoja au wawili na huko (nje) kuna gharama za malazi," alisema.

**OMBI KWA SERIKALI**

Dkt Masava alisema licha ya kuishukuru serikali, ameiomba iendelee kuboresha matibabu ya moyo kwa kununua mtambo wa kuchunguza magonjwa ya mfumo wa umeme kwa kuwa teknolojia inakua.

"Wagonjwa wanaoongeza kwa hiyo malengo yetu ndani ya miaka mitatu hadi mitano tunazamia kuweka mtambo wa kuchunguza magonjwa ya mfumo wa umeme wa moyo. Ukiacha haya tuliyosema ya kuweka betri, kuna watu wanakuja na magonjwa ya mfumo wa umeme wa moyo, lakini mtambo wake unahitajika mahususi kwa mfumo wa umeme wa moyo tu," alieleza.

Alisema mtambo huo kazi yake kubwa ni kuchunguza maeneo yenye changamoto kama moyo unakimbia sana.

"Wenye mahitaji bado wengi kwa hiyo ikimpendeza Mheshimiwa Rais Samia atusaidie ikizingatiwa hapa (BMH) ni katikati ya nchi na ndiyo makao makuu ya serikali, kijiografia ni rahisi kwa Watanzania na wageni kutoka nje ya nchi kufika hapa."

**WAFANYAKAZI BMH**

Kwa mujibu wa Dkt Masava, Idara ya Moyo ina mabingwa bobezi wa moyo wanne, madaktari wawili wa kawaida na wenye shahada ya kwanza.

"Pia kuna wataalamu wanaosaidia kuendesha mtambo wa Catheterization walioajiriwa ni wawili na watatu wana ajira za mkataba," alisema.

**HUDUMA KWA MWEZI**

Kwa mwezi uchunguzi mishipa ya damu ya moyo kunakuwa na watu 30, lakini wanne hadi sita wanakutwa mishipa yao imeziba na wanazibua, asilimia 60 hukutwa na shida na wanaorudi ni asilimia 30, lakini wengine hali yao haiwi ya kuzibuliwa isipokuwa hupewa dawa na kurejea kawaida.

**UHITAJI WA RASILIMALI WATU**

Dkt Masava aliongeza idara hiyo bado ina uhitaji wa wataalamu saba wakiwemo madaktari bingwa bobezi wawili na madaktari bingwa watatu na madaktari wawili wa kawaida kutokana na idadi kubwa ya wagonjwa wanaojitokeza na uhitaji wa hospitali.

Aidha, idara hiyo huwa inafanya upasuaji moyo kwa kufungua kifua kuwekwa 'valve' ama mlango wa moyo, kupandikiza mishipa kwa kuvuna mshipa mguuni 'bypass'.



Dkt. Masava (aliyekaa) akiwa na baadhi ya wataalamu moyo Hospitalini hapo.



# Wananchi waipongeza serikali kupunguza vifo vya wajawazito na watoto wachanga nchini



Na REHEMA MAIGALA

MIAKA mitatu ya Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, imekuwa na mageuzi makubwa katika sekta ya afya ikiwemo urahisishaji wa utoaji huduma kwa kina mama wajawazito, ulipaji wa huduma kwa makundi maalumu ikiwemo watoto na wazee.

Katika kipindi cha miaka mitatu ya uongozi wa Rais Dk.Samia hakuna mtoto yeyote atakayekwenda Kituo cha Afya cha Serikali akashindwa kupewa chanjo, hivyo bado sera ya afya inaendelea kutumika vile inavyotakiwa.

Gazeti hili lilizungumza na baadhi ya wajawazito na wazazi wenye watoto walio chini ya miaka mitano ambao walisema katika kipindi cha miaka mitatu ya Rais Dk. Samia wamekuwa wakipata huduma bora na bila malipo.

Walisema huduma za afya zimebadilika kwa sababu wauguzi wanaowahudumia wamekuwa wakiwapa elimu nzuri jinsi ya kumlea mtoto na kumlea mtoto aliye tumboni.

Wakizungumzia huduma za kujifungulia wazazi, wananchi hao walisema zimekuwa bora kwa sababu mzazi akishajifungua hapewi ruhusa ya kuondoka hadi mganga mkuu ahakikishe afya ya mtoto na mama zinaendelea vizuri.

Pia walisema kuongezeka kwa vituo vya afya imesaidia kuondoa mlindukano wa wajawazito wengi katika vituo vya afya.

Angela Sebastiani ambaye ni mjamzito anayepata huduma zake katika Kituo cha Afya cha Mbweni , alisema Serikali imejitahidi kuongeza vituo vya afya ambavyo vinasaidia kuondoa changamoto za kukaa kwa muda mrefu kupata huduma hizo.

"Naweza kwenda klini nakaa dakika 45 tu, napata huduma ninayohitaji halafu naondoka nyumbani kwangu kuendelea na shughuli zangu za uzalishaji mali,"alisema Angela.

Angela alisema awali ilikuwa ukienda kliniki kupata huduma ni lazima utakaa kwa muda, mrefu kwa sababu vituo vya afya vilikuwa vichache.

"Tunapongeza viongozi wetu akiwemo Rais Samia ametujali wananchi wake kwa kujenga vituo vingi vya afya ,"alisema.

Naye, Oliva Kayenga alisema mwaka jana alijifungua mtoto wake wa kike kwa hali ya usalama kutokana na wauguzi kumpatia huduma nzuri.

Oliva alisema huduma zinazotolewa na wauguzi katika vituo vya afya zimekuwa nzuri kwa sababu hakuna wingi wa wagonjwa hi vyo wagonjwa waliokuwepo wanaweza kuwamudu .

"Kuna unyenyekevu mkubwa sana hivi sasa, wakati wa kujifungua muuguzi anakubembeleza hadi wakati mwingine unasahau maumivu unayoyapata wakati unajifungua,"alisema Oliva.

Alisema hata ukijifungua wauguzi wanakuwa na uangalizi mzuri kati ya mama na mtoto kwa kuhakikisha mtoto aliyezaliwa anapata chanjo zote za awali huku mama akipewa matibabu yote yanayohitajika baada ya kujifungua.

Sabina Mkongi ni mzazi aliyepata huduma za mama na mtoto katika hospitali ya Nguvu Kazi iliyopo Chanika Dar es Salaam,alisema huduma yao nzuri imetokana na maboresho yaliyofanywa ndani ya hospitali hiyo.

Alisema vifaa tiba ndani ya hospitali hiyo imeboreshwa na kusababisha huduma za afya ya mama na mtoto kuwa nzuri zaidi.

"Licha ya kuboresha huduma hiyo pia Serikali i mejitahidi kwa kiasi kikubwa kufanya ununuzi wa vifaa tiba ambavyo vingine husaidia kujua hali ya mtoto aliye tumboni.

Alisema vifaa hivyo vinamanufaa mengi kwa wahitaji na watoa huduma kwa upande wa watoa huduma imewasaidia kurahisisha shughuli zao za kazi .

Kwa upande wa Mwajuma Issa alisema uboreshwaji wa huduma za afya zimepunguza changamoto nyingi zillizokuwa zinakabili hospitali na zahanati.

Mwajuma alisema uwekaji wa kamera ndani ya baadhi ya zahanati na hospitali zimesaidia kupunguza vitendo vya rushwa vilivyokuwa vinaendelea.

"Hii Serikali ya Rais Dk. Samia imesaidia kwa kiasi kikubwa kuondoa changamoto zilizokuwa ni kikwazo kikubwa katika utoaji wa huduma za afya,"alisema Mwajuma.

Alisema uwekaji wa kamera umesaidia kuondoa rushwa katika vituo vya kutolea huduma ya afya na hata hospitali.

Pia, alisema kamera hizo zimekuwa chachu ya mafanikio ya watoa huduma ya afya kufanya kazi kwa bidii na bila kumnyanyapaa mgonjwa.

Alisema awali kuliwa na wizi wa watoto wachanga katika hospitali,zahanati na vituo vya afya lakini tangu Serikali iweke kamera wizi huo umepungua au kwisha kabisa.

"Tunaishukuru Serikali ya Rais Dk. Samia imefanya mambo mengi katika ubojreshaji wa afya ya mama na mtoto hivyo hata kuweka kamera ndani hospitali kumekuwa na faida kubwa sana" alisema

Aliongeza; "Kwa sababu awali kulilkuwa na wizi wa watoto wachanga, tangu kamera zimewekwa hakuna tena tabia hiyo na kila kitu kinakwenda sawa naipongeza sana Serikali hii kwa kufanya jitihada ya kuboresha mfumo mzima wa huduma ya afya,"

Katika hatua nyingine, Christina Abdala alisema huduma za afya zi nazo olewa katika vituo vya afya vimeboreshwa na kusababaisha mjamzito asiende hospitali binafsi kupata huduma hiyo.

"Nilijifungua mtoto wangu miezi mitatu iliyopita katika hospitali ya mnazi mmoja iliyopo Dar es Salaam,huduma nilizozipata zinafanana na hospitali binafsi kwa sababu hivi sasa wauguzi wanawajali wagonjwa na kutoa huduma zilizo bora,"alisema Christina.

Hivyo, alisema mfuko wa dunia umekuwa ukifadhili huduma za afya kwa kutoa fedha kwa lengo la kununulia vifaa vya teknolojia, kuwajengea uwezo watoa huduma za afya 'wakiwemo madaktari, wauguzi ,wakunga na wataalamu mbalimbali wanaotoa huduma kwa mama na mtoto.

# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

## HOSPITALI YA RUFAA MKOA WA MANYARA







Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan

## HOSPITALI YA RUFAA MKOA WA MANYARA YAJIVUANIA MAFANIKIO LUKUKI MIAKA MITATU YA RAIS DKT SAMIA






Mganga Mfawidhi Hospitali ya Rufaa Mkoa wa Manyara Dk. Katherine Magali

MAFANIKIO

# Hospitali ya Rufaa Mkoa wa Manyara yajivuania mafanikio lukuki Miaka mitatu ya Rais Dkt. Samia S. Hassan

>>Dkt. Magali ameainisha namna walivyokamilisha ujenzi wa majengo na ununuzi wa vifaa tiba

>>Waeleza walivyoboresha utoaji wa huduma kwa wananchi




### HISTORIA

Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Manyara ipo katika makao makuu ya Mkoa wa Manyara mji wa Babati kando ya barabara kuu ya kueleke Singida kutokea makutano ya barabara ya Arusha na Dodoma. Mnamo mwaka 2006, Sekretarieti ya Mkoa ilipendekeza kwa serikali kujenga Hospitali ya Mkoa yenye uwezo wa vitanda 350 ambavyo vitatoa huduma za afya kwa ujumla na maalum. Baada ya maandalizi yote muhimu ikiwa ni pamoja na kupata ardhi mita za mraba 67,334 na upatikanaji wa fedha za ujenzi, mnamo mwaka 2009 ujenzi halisi wa Hospitali ulianza na iliamuliwa kuwa wa awamu. Serikali ilikubali kutoa jumla ya Tshs. Bilioni 16.5 kwa ajili ya ujenzi pamoja na ununuzi wa vifaa vya matibabu. Awamu ya kwanza ilihusisha ujenzi wa wodi ya mama na mtoto ambayo imekamilika kiujumla pamoja na sehemu ya vifaa.

Vile vile, sehemu ya maabara ilikamilishwa katika awamu hii kwa kutumia Mfuko wa Abbot. Kwenye awamu ya pili, ujenzi wa nyumba ya kufulia, ujenzi wa incinerator, tanki la maji la chini ya ardhi, nyumba ya walinzi pamoja na uzio wa ukuta vilikamilishwa na kuanza kutumika. Hospitali ilianza rasmi kutoa huduma za Afya mnamo mwezi Aprili 2013 kwa utoaji wa huduma za wagonjwa wa nje, kliniki maalumu za meno na macho, maabara, radiolojia, duka la dawa pamoja na afya ya uzazi na mtoto.

Mnamo Mei 2014, Hospitali ilianza kutoa huduma za idara ya wagonjwa wa ndani na na Mei 2015 kutoa huduma za uzazi, kujifungua pamoja na upasuaji. Kufikia mwaka 2016 hadi 2018, Hospitali iliendelea kupanua huduma zake kama ifuatavyo; kufunga mifumo ya elektroniki (GoT-HMIS na CRDB) kwa usimamizi wa rasilimali, kusanidi miundombinu ya Hospitali (LAN) kuwezesha mawasiliano, utangulizi wa huduma maalum katika dawa za ndani, watoto, upasuaji, vizuizi na idara ya magonjwa ya akili, uanzishaji wa idara ya ufundi na Vifaa tiba pamoja na idara ya utengamao.

"Tumepata ongezeko la Daktari Bingwa wa mama na uzazi, ambapo awali tulikua na Daktari 1 na sasa ameongezeka 1 jumla wapo wawili, madaktari Bingwa wengine tulionao ni pamoja na Madaktari Bingwa wa Upasuaji wapo 2, madaktari Bingwa wa magonjwa ya Dharura 2 ambao wameongezeka kwa kipindi cha miaka mitatu ya Rais Dkt. Samia Saluhu Hassan"



Mganga mfawidhi Hospitali ya Rufaa Mkoa wa Manyara Dkt. Katherine T. Magali

### MAFANIKIO

Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Rufaa Mkoa wa Manyara Dkt. Katherine T. Magali ameeleza mafanikio yaliyopatika katika kipindi cha miaka mitatu ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan katika hospitali alisema, "tumepata mafanikio mengi ambayo tunajivunia ikiwemo majengo ya kisasa ya kutolea huduma za Afya, kama huduma ya Radiolojia, jengo hilo liligharimu kiasi cha shilingi mil 370, jengo la magonjwa ya dharura liligharimu mil 650 na jengo la wagonjwa mahututi (ICU liligharimu shilingi mil 560 ambapo kwa sasa jengo linalotimika ni Radiolojia na huduma zake zinaendelea".

Pia Dkt. Katherine T. Magali alisema walifanikiwa kupokea CT-Scan ambayo ina thamani ya shilingi Bil 1.8, na vifaa tiba vyenye thamani ya shilingi Bil 3.4.

"Kwa kipindi hiki cha miaka mitatu tumefanikiwa kufanya utanuzi wa baadhi ya huduma, wodi ya kulaza wagonjwa wa Bima, VIP na Private", aliongezea Dkt. Katherine.T.Magali

Alinukuliwa Dkt. Katherine T. Magali kuwa katika kipindi hiki wamefanikiwa kupata ongezeko kubwa la watumishi; kwa kipindi chote walikuwa na idadi ya watumishi 130-200 ila mpaka sasa wameongezewa na kufikia watumishi 278 ambao wanafanya kazi katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Manyara wa kada mbalimbali wakiwemo madaktari bingwa, wauguzi na wataalamu wengine.









MAFANIKIO

# MAFANIKIO YA MIAKA MITATU YA RAIS DK, SAMIA KATIKA SEKTA YA AFYA NCHINI,



**Mashine ya CT-Scan**

Alinukuliwa Dkt. Katherine T. Magali kuwa katika kipindi hiki wamefanikiwa kupata ongezeko kubwa la watumishi; kwa kipindi chote walikuwa na idadi ya watumishi 130-200 ila mpaka sasa wameongezewa na kufikia watumishi 278 ambao wanafanya kazi katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Manyara wa kada mbalimbali wakiwemo madaktari bingwa, wauguzi na wataalamu wengine. Tumepata ongezeko la Daktari Bingwa wa mama na uzazi, ambapo awali tulikua na Daktari 1 na sasa ameongezeka 1 jumla watakua wawili, madaktari Bingwa wengine tulionao ni pamoja na Madaktari Bingwa wa Upasuaji wapo 2, madaktari Bingwa wa magonjwa ya Dharura 2 ambao wameongezeka kwa kipindi cha miaka mitatu ya Rais Dkt. Samia Saluhu Hassan.

Aliongezea, upatikanaji wa dawa katika kipindi hiki cha miaka mitatu kumekuwa na mabadiliko mengi ambayo yamepelekea uwepo wa upatikanaji wa dawa mpaka kufikia asilimia 95-98. Alifafanua, kuna njia mbalimbali ambazo zipo za upatikanaji wa dawa ikihusisha uwepo wa duka maalumu kwa wateja wa bima, duka la wagonjwa wa malipo ya papo kwa papo na duka la dawa linalojitegemea lenyewe.

Alieleza kwamba kila robo mwaka, hospitali inawezeshwa kutoa huduma za kibingwa kwa kuzunguka katika wilaya zilizopo mkoa wa Manyara sambamba na kuwaalika madaktari bingwa kwa fani ambazo hazipo ndani ya hospitali ili wateja wao waweze kupata huduma hapo.

**Upatikanaji wa dawa katika kipindi hiki cha miaka mitatu kumekuwa na mabadiliko mengi ambayo yamepelekea uwepo wa upatikanaji wa dawa mpaka kufikia asilimia 95-98. Alifafanua, kuna njia mbalimbali ambazo zipo za upatikanaji wa dawa ikihusisha uwepo wa duka maalumu kwa wateja wa bima, duka la wagonjwa wa malipo ya pesa taslimu na duka la dawa linalojitegemea lenyewe.**

Katika kipindi hiki cha miaka mitatu, idadi ya watumishi imeongezeka hadi kufikia 278, watumishi wamefanikiwa kupata stahiki zao ikiwemo kupandishwa madaraja na kubadilishwa kada.

Hadi sasa jumla ya watumishi 70 wameweza kubadilishwa kada na wengine kupandishwa vyeo pia ufadhili wa masomo kwa watoa huduma za Afya ikiwemo madaktari bingwa na wataalamu wengine.

Hospitali imefanikiwa kusogeza huduma za Kibingwa kwa wananchi ikihusisha ufanyikaji wa kambi za kibingwa hospitalini pamoja na kliniki mkoba zinazofanyikakatika kila robo ya mwaka.





**Vifaa tiba vilivyopo katika chumba cha wagonjwa wa dharura**

# MAFANIKIO



Mitungi ya kuzalisha gesi.

# MAFANIKIO YA MIAKA MITATU YA RAIS DKT. SAMIA KATIKA SEKTA YA AFYA NCHINI

## MIKAKATI

Dkt. Katherine T. Magali alisema, mikakati ya kuendelea kufanya vizuri zaidi kwa kipindi hiki cha miaka mitatu ya Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan baada ya kupata mtaji yaani kwa kupata majengo, watumishi, vifaa Tiba kama hospitali wamejipanga kuendelea kukusanya fedha ambazo zitawasaidia kuendeleza kuongeza vifaa tiba kwa ajili ya kuendelea kuboresha huduma, kuendelea kuwajengea uwezo watumishi kwa kuwapeleka wengine masomoni.

"Ukiacha masomo ya muda mrefu, baadhi watumishi tunawapeleka mafunzo ya muda mfupi kwa ajili ya kupata ujuzi mbalimbali na hapa hapa Hospitali pia tunatoa mafunzo kwa watumishi juu ya utoaji wa huduma bora na mafunzo ya hivi vifaa tiba tulivyonavyo ili waweza kuvitumia vyema maana unaweza ukawa na vifaa tiba lakini usiweze kuvitumia" alisisitiza Dkt. Katherine T. Magali

## MIPANGO YA BAADAE

Kwa maelezo ya Dkt. Katherine T. Magali, wanampango wa kumalizia majengo ambayo yapo na hayajakamilika vizuri kwa kupitia mapato ya ndani ili waendelee kuboresha huduma lakini pia wanampango wa kufanya ukarabati wa majengo ya zamani ambayo wamejipanga kuendelea kuyaboresha kupitia fedha ambazo wanazipata. "

Tuna jengo la kuhifadhia maiti, Jengo la Udobi, jengo la mama na mtoto pamoja na maabara haya yote tunaendelea kuyaboresha" alisema Dkt. Katherine T. Magali. Aidha wanampango wa kuongeza huduma mpya kama vile kusafisha figo (Dialysis) ambayo itaanza mwaka ujao wa fedha 2024/25, huduma ya "Fast Track" na kuanzisha sehemu za kutengeneza maji ya drip ambazo wananchi wa mkoa wa Manyara na maeneo jirani watafanikiwa kupata huduma hizo kwa ukaribu zaidi pamoja na kuhakikisha upatikanaji wa dawa kwa wakati.

**Ukiacha masomo ya muda mrefu lakini baadhi watumishi tunawapeleka mafunzo ya muda mfupi kwa ajili ya kupata ujuzi mbalimbali na hapa hapa Hospitali pia tunatoa mafunzo kwa watumishi juu ya utoaji wa huduma bora na mafunzo ya hivi vifaa tiba tulivyonavyo ili waweza kuvitumia vyema maana unaweza ukawa na vifaa tiba lakini usiweze kuvitumia**

## MIRADI

Akifafanua zaidi miradi inayoendelea kwa kipindi hiki cha miaka mitatu ya Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, wamepatiwa majengo lakini kuna baadhi hayajamaliziwa ikiwa jengo la magonjwa ya dharura ambalo bado halijamalizika lakini kama Hospitali wamejipanga kumalizia kwa kipindi hiki cha mwaka wa fedha , Hospitali itatumia fedha za ndani pamoja na kumalizia miundombinu ya umeme na hewa tiba.

## SHUKRANI

Tunamshukuru Mh. Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kutoa fedha za kuwezesha ujenzi, maboresho ya huduma ambazo zinaendelea kwa kuwaletea wataalamu wa fani mbalimbali, vifaa tiba ambavyo vimeendelea kuimarisha huduma kuwa bora sana ukilinganisha na hapo awali.

Pia alishukuru kwa ujenzi endelevu utasaidia sehemu za huduma ambazo zilikuwa na msongamano kuweza zitapunguza msongamano maeneo hayo na kuwezesha huduma kwa wakati.

## WITO

Aidha Dkt. Katherine T. Magali ametoa wito kwa jamii kuendelea kuiamini Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Manyara na kujivunia uwepo wa Hospitali hiyo kwa kuwa wamejipanga kutoa huduma bora kabisa pamoja na za kibingwa katika ngazi zote za utoaji huduma.

Ata hivyo, alisisitiza kwa jamii kuweza kujitokeza kwa ajili ya kuangali afya mara kwa mara ili kujilinda na magonjwa ya aina mbalimbali pamoja na kupata ushauri wa kitaalamu kwenye maswala yote ya afya kutoka na uwepo wa vifaa tiba vya kisasa, vipimo vya kimaabara na dawa na wataalam kwenye fani mbalimbali mpaka bobezi.



Jengo la idara ya Radiolojia






Wahandisi wa Vifaa Tiba wakijaza gesi kwenye mitungi



Mhandisi wa Vifaa Tiba Salaira Nyangoi akijaza gesi kwenye mitungi








HOSPITALI YA RUFAA MKOA WA SINGIDA
HR MS
Huduma Bora
Ni Kipaumbele Chetu



RAIS Dk. Samia Suluhu Hassan.



KAIMU Mganga Mfawidhi Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Singida Dk. David J. Mwasota.



WAZIRI wa Afya, Ummy Mwalimu

# Mafanikio ya miaka mitatu ya Rais Dk. Samia katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Singida

**HOSPITALI YA RUFAA YA MKOA SINGIDA**
**Anuani ya Posta: Box. 104 Singida**
**Simu: 026 2502397**
**Barua Pepe: barua@singidarrh.go.tz**

MIAKA MITATU YA RAIS DK. SAMIA NA UBORESHAJI SEKTA YA AFYA NCHINI

# Mafanikio ya miaka mitatu ya Rais Dk. Samia katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Singida

**Na MWANDISHI WETU**

UTOAJI huduma katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Singida, umeendelea kuwa bora kutokana na serikali chini ya Rais Dk. Samia Suluhu Hassan kufanya uwezeshaji ambao unaongeza kasi ya mabadiliko kwa kiasi kikubwa.

Kwa mujibu wa Kaimu Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Singida, David Mwasota, katika kipindi cha miaka mitatu ya Rais Dk. Samia kumekuwa na mafanikio makubwa katika sekta ya afya kwa ujumla ikiwemo hospitali hiyo.

Alisema ujenzi wa nyumba ya mtumishi ambayo imekamilika, ujenzi wa kituo cha huduma jumuishi (one stop centre) kwa manusura wa ukatili wa unyanyasaji wa kijinsia ambao umekamilika pia.

Alisema ununuzi wa magari matatu kwa ajili ya usimamizi shirikishi, pamoja na shughui za uendeshaji wa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Singida.

Alisema mafanikio yaliyopatikana kwa kipindi cha miaka mitatu ya Rais Dk. Samia yamegawanyika katika maeneo manne.

Alisema eneo la kwanza ni miundombinu, dawa vifaa tiba na mashine za uchunguzi, rasilimali watu na eneo la rasilimali fedha.

Anasema akianzia katika miundombinu katika kipindi cha miaka mitatu ya Rais Dk. Samia, wanashukuru kupatiwa miradi ya kuboresha miundombinu ya ujenzi ambayo imefanyika hadi sasa.

"Cha kwanza ni ujenzi wa miradi ya majengo ya dharula na wagonjwa mahututi (EMD na ICU), ambapo serikali ilitoa fedha kiasi cha sh. bili 1.426 kwa ajili ya ujenzi wa majengo hayo," alisema.

Alisema wanamshukuru Rais Dk. Samia ambapo hadi hivi sasa majengo hayo kwa upande wa EMD imefikia ujenzi wa asilimia 90 wakati ICU likifikia asilimilia 86 kukamilika.

"Tunamshukuru Rais Dk. Samia kwani ujenzi wa jengo la dharura lenye thamani ya sh. 766,017,863.52 ambalo limefikia asilimia 90, wakati ujenzi wa jengo la wagonjwa mahututi lenye thamani ya sh. 660,236,211.34 limefikia asilimia 86 kukamilika," alisema Kaimu Mganga Mfawidhi Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Singida, Mwasota.

Alisisitiza kwamba pia ujenzi wa jengo kubwa la ghorofa tatu lenye thamani ya sh. bilioni 19,525,525,130.57 litakalokuwa linatoa huduma mbalimbali, ambapo sakafu ya chini (Ground Floor) imefikia asilimia 78 na sakafu ya juu imefikia asilima 36.

## UNUNUZI WA VIFAA

Kaimu Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Singida, Mwasota alisema ununuzi wa vifaa maalum vya kuhudumia wagonjwa mahututi na mashine mbalimbali za kisasa kama vile CT-Scan, Digital X-Ray na Fluoroscope Mashine

Alisema pia ujenzi wa jengo la kusubiria wateja ambalo limefikia asilimia 70 na ujenzi wa eneo la kuegeshea magari ambao umefika asilimia 95.

## KUTOA MSAMAHA KWA WAGONJWA

Alisisitiza kwamba wametoa msamaha kwa huduma yenye thamani zaidi ya sh. bilioni 1.2 kwa wajawazito, watoto wenye umri chini ya miaka mitano na wazee wasiojiweza.



**"Tunamshukuru Rais Dk. Samia kwani ujenzi wa jengo la dharura lenye thamani ya sh. 766,017,863.52 ambalo limefikia asilimia 90, wakati ujenzi wa jengo la wagonjwa mahututi lenye thamani ya sh. 660,236,211.34 limefikia asilimia 86 kukamilika,"**

**alisema Kaimu Mganga Mfawidhi Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Singida, Mwasota.**



"Tumetoa msamaha wa huduma zenye thamani ya pesa za Tanzania zaidi ya sh. bilioni 1.2 kwa wajawazito, watoto chini ya umri wa miaka mitano, wazee na wasiojiweza.

"Serikali imetusaidia kusomesha madaktari bingwa wanne na mabingwa bobezi wawili na hivyo kuongeza madaktari bingwa kufikia 14," alisema.

Alisema mikakati yao ni kuendelea kufanya vizuri katika kipindi hiki cha Rais Dk. Samia kama ifuatavyo:-

*Kuyatunza vizuri majengo ambayo yamekamilika Pamoja na mashine zilizopo.

*Kuzifanyia 'service' kwa wakati mashine na magari yote yaliyopo.

*Kuwahudumia wananchi kwa wakati na kwa kuzingatia kanuni za huduma bora kwa mteja.

Alisema pia wamejipanga kuendelea kusimamia miradi iliyotekelezwa na inayoendelea kutekelezwa katika kuwahudumia wananchi kwa kufanya mambo yafuatayo:-

*Miradi iliyotekelezwa tumejipanga kuhakikisha miradi hiyo inatunzwa vizuri na inatoa huduma zilizokusudiwa.

*Miradi inayoendelea kutekelezwa tumejipanga kuhakisha miradi hiyo inakamilika kwa wakati.

Aliongeza wanatoa shukrani kwa Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Rais Dk. Samia katika kuendelea kuboresha sekta ya Afya nchini.

"Tunaishukuru sana Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Rais Dk. Samia kwa kuiboresha sana sekta ya afya, tunachomuahidi Mhe Rais Dk. Samia ni kuhakikisha tunafanya kazi kwa bidii na uadilifu wa hali ya juu pamoja na kuhakikisha tunawahudumia wananchi kwa wakati.

"Wito wetu kwa jamii tunayoihudumia tunawaomba wananchi wenye matatizo mbalimbali ya kiafya wafike Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Singida kwani huduma zetu zinatolewa kwa ubora wa hali ya juu sana, tuna maabara inayozingatia viwango vya kimataifa, tuna dawa za kutosha, tuna mashine ya CT-SCAN, Digital X-Ray, Fluoroscope Mashine, pia tuna madaktari bingwa 13 na daktari bingwa mbobezi mmoja.

## HUDUMA ZINAZOTOLEWA KATIKA HOSPITALI YA RUFAA YA MKOA WA SINGIDA

Hospitali ya Rufaa ya Mkoa Singida tunatoa huduma za upasuaji wa aina mbili ambazo





MIAKA MITATU YA RAIS DK. SAMIA NA UBORESHAJI SEKTA YA AFYA NCHINI



UJENZI wa jengo la wagonjwa mahututi.

# Mafanikio ya miaka mitatu ya Rais Dk. Samia katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Singida

ni upasuaji wa jumla na matatizo ya mkojo na upasuaji wa mifupa.

Ili mgonjwa apate huduma atatakiwa kuhudhuria kliniki ya huduma husika kwa ratiba ya kliniki husika kama ratiba inavyoonekana hapa chini isipokua kwa wagonjwa wa dharura tu.

Dharura za upasuaji hufanyika pale zinapojitokeza na hapa shughuli zingine huwa zinasitishwa kwa muda kupisha dharula husika.

**RATIBA YA HUDUMA ZA UPASUAJI WA JUMLA NA MATATIZO YA MKOJO**

| | | |
|---|---|---|
| JUMATATU | KLINIKI MAALUM | MZUNGUKO WA KAWAIDA (SERVICE WARD ROUND) |
| JUMANNE | UPASUJI WA KUPANGWA (ELECTIVE OPERATION) | MZUNGUKO WA KAWAIDA (SERVICE WARD ROUND) |
| JUMATANO | MZUNGUKO MKUU (MAJOR WARD ROUND | |
| ALHAMISI | KLINIKI MAALUM | MZUNGUKO WA KAWAIDA (SERVICE WARD ROUND) |
| IJUMAA | UPASUAJI WA KUPANGWA (ELECTIVE OPERATION) | MZUNGUKO WA KAWAIDA (SERVICE WARD ROUND) |

Ili mgonjwa apate huduma atatakiwa kuhudhuria kliniki ya huduma husika kwa ratiba ya kliniki husika kama ratiba inavyoonekana hapa chini isipokua kwa wagonjwa wa dharura tu.



UJENZI wa kituo cha huduma jumuishi (one stop centre).

**RATIBA YA HUDUMA ZA UPASUAJI WA MIFUPA**

| | | |
|---|---|---|
| JUMATATU | MZUNGUKO WA KAWAIDA (SERVICE WARD ROUND) | |
| JUMANNE | KLINIKI MAALUM | MZUNGUKO WA KAWAIDA (SERVICE WARD ROUND) |
| JUMATANO | MZUNGUKO MKUU (MAJOR WARD ROUND) | MZUNGUKO WA KAWAIDA (SERVICE WARD ROUND) |
| ALHAMISI | UPASUAJI WA KUPANGWA (ELECTIVE OPERATION) | MZUNGUKO WA KAWAIDA (SERVICE WARD ROUND) |
| IJUMAA | KLINIKI MAALUM | MZUNGUKO WA KAWAIDA (SERVICE WARD ROUND) |

**MAGONJWA YA NDANI**

Huduma hii huwahusisha wagonjwa wanaosumbuliwa na magonjwa ya ndani.

Wagonjwa hawa huwa wanaonwa kupitia kliniki husika kwa matibabu, pia huduma ya kulazwa kwa wagonjwa hawa inapatikani kupitia wodi zetu ambazo zimegawanyika katika makundi matatu:

1.Wodi ya wanaume (Wodi namba 7)
2.Wodi ya wanawake (wodi namba 10)
3.Grade A

**RATIBA YA MZUNGUKO WA WODI (WARD ROUND)**

| SIKU | HUDUMA |
|---|---|
| JUMATATU | MZUNGUKO MKUU |
| JUMANNE | MZUNGUKO WA KAWAIDA |
| JUMATANO | MZUNGUKO WA KAWAIDA |
| ALHAMISI | MZUNGUKO MKUU |
| IJUMAA | MZUNGUKO WA KAWAIDA |

Wagonjwa wanapopata nafuu huruhusiwa na kupewa tarehe maalumu za kuhudhuria kliniki ya kila siku za Jumatano.

Aidha huwa tunafanya huduma za kliniki kwa magonjwa mbali mbali kwa ratiba kama inavyoonekana hapa chini.

**RATIBA YA KLINIKI**

| SIKU | HUDUMA |
|---|---|
| JUMATATU | KLINIKI YA KISUKARI KWA WATU WAZIMA |
| JUMANNE | KLINIKI YA KISUKARI KWA WATOTO |
| JUMATANO | KLINIKI YA MAGONJWA YOTE YA NDANI |
| ALHAMISI | KLINIKI YA KISUKARI KWA WATU WAZIMA |

**MUHIMU**

Kliniki ya magojwa ya akili hufanyiki kila siku ya wiki.

Baadhi ya mgonjwa yanayotibiwa na idara ya magonjwa ya ndani ni shinikizo la damu, kifafa, pumu, seli mundu, magonjwa ya moyo na kadhalika.

**MAABARA**

Tuna maabara kubwa na ya kisasa ambayo inauwezo mkubwa wa kufanya vipimo mbalimbali kwani ni ya kisasa na inayoendana na kasi ya teknolojia.

Aidha tuna watumishi wenye uwezo mkubwa na wazoefu sana katika huduma hizi za maabara.

MIAKA MITATU YA RAIS DK. SAMIA NA UBORESHAJI SEKTA YA AFYA NCHINI

# Mafanikio ya miaka mitatu ya Rais Dk. Samia katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Singida

Majibu yote yanayotolewa na maabara yetu ni yakuaminika na tunaamini kuwa sampuli yeyote itakayopimwa katika maabara yetu itatoa majibu sawa na maabara zingine popote pale duniani yenye viwango bora vinavyokubalika kimataifa.

Hivyo tunakukaribisha/ tunawakaribisha kwa huduma bora kabisa za maabara.

**HUDUMA YA MIONZI NA PICHA**

Huduma hii inahusisha vipimo vya X Ray na Ultrasound.

Hospitali yetu ina mashine za kisasa kabisa kwa ajili ya vipimo hivyo tukiwa na wataalamu wazoefu kwa huduma, vipimo hivyo akiwemo daktari wa mionzi.

**HUDUMA YA TIBA YA VIUNGO (PHYSIOTHERAPY)**

Huduma hii inatolewa katika idara ya tiba ya tiba ya viungo ya Hospitali yetu ya Rufaa ya Mkoa wa Singida.

Ifuatayo ni orodha ya matibabu yanayofanyika katika idara hii;

*Mazoezi tiba kwa waliopooza.

*Mazoezi tiba kwa watoto waliochelewa ukuaji.

*Tiba ya maumivu ya pingili za mgongo.

*Tiba ya maumivu ya viungo.

*Tiba ya mguu kifundo (clubfoot) kwa watoto.

**MAGONJWA YA WANAWAKE NA AFYA YA UZAZI, MAMA NA MTOTO**

Akina mama wanapata huduma za uzazi pamoja na matibabu ya magonjwa ya wanawake.

Aidha tunafurahi kusema kuwa huduma tunazotoa kwa akinamama na wanawake kwa ujumla ni huduma za kibingwa kwani Hospitali ya Rufaa ya Mkoa tumebahatika kuwa na Daktari Bingwa.

**KLINIKI YA DAKTARI BINGWA WA UPASUAJI WA JUMLA NA MATATIZO YA MKOJO**

Ili mgonjwa apate huduma atatakiwa kuhudhuria kliniki ya huduma husika kwa ratiba ya kliniki husika kama ratiba ianvyoonesha isipokua kwa wagonjwa wa dharura tu.

Dharura za upasuaji hufanyika pale zinapojitokeza na hapa shughuli zingine huwa zinasitishwa kwa muda kupisha upasuaji husika.

**KLINIKI YA DAKTARI BINGWA WA UPASUAJI WA MIFUPA**

Kliniki ya Daktari Bingwa wa Upasuaji wa Mifupa hufanyika siku za Jumanne na Ijumaa kama inavyoonekana katika ratiba.



JENGO la Hospitali linalotoa huduma kwa sasa.

**HISTORIA**

**Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Singida ilijengwa mwaka 1954 kwenye eneo la hekta 1.5 ikitumika kama Hospitali ya Wilaya. Ilipandishwa daraja na kuwa Hospitali ya Mkoa mwaka 1963 wakati huo ikihudumia kiasi cha wakazi 336,204.**



UJENZI wa nyumba ya Mtumishi ambayo imekamilika.

Kliniki hii huendeshwa na Daktari Bingwa wa Mifupa. Kliniki hii ni moja ya kliniki za kibingwa tulizonazo katika hospitali yetu.

**KLINIKI ZINAZOFANYIKA IDARA YA WAGONJWA WA NJE**

Hii inahusisha kliniki za aina mbili;

*Kliniki maalumu za magonjwa ya ngozi, magonjwa ya sukari, magonjwa ya akili na magonjwa ya ndani.

*Kliniki za magonjwa mchanganyiko (ya kawaida)

**KLINIKI ZA TIBA USINGIZINI NA GANZI (ANAESTHESIA CLINIC)**

Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Singida tunaendesha kliniki za tiba usingizini na ganzi kwa siku zote za Juma.

Kliniki hii inaendeshwa na Daktari Bingwa wa Tiba Usingizini na Ganzi (Anaesthesiologist).

Tunaona wagonjwa wote wanaopangiwa kufanyiwa upasuaji.

**KLINIKI YA DAKTARI BINGWA WA WATOTO (PEDIATRICIAN CLINIC)**

Kliniki Ya Daktari Bingwa wa Watoto hufanyika siku za Jumanne na Ijumaa kama inavyoonekana katika ratiba.

Kliniki hii huendeshwa na Daktari Bingwa wa Watoto.

Kliniki hii ni moja ya kliniki za kibingwa tulizonazo katika hospitali yetu. karibu tukuhudumie.

**KLINIKI YA DAKTARI BINGWA WA MASIKIO PUA NA KOO (ENT)**

Watoto pamoja na watu wazima wenye matatizo ya masikio, pua na koo mfano. nyama za pua, masikio kuwasha kupita kiasi, tezi kuvimba kooni nakadhalika, wanapata huduma bora za kibingwa kutoka kwa Daktari Bingwa wetu.

**KLINIKI YA DAKTARI BINGWA WA MAGONJWA YA NDANI**

Kliniki hii ni kwa wagonjwa wote wanaosumbuliwa na magonjwa ya ndani Kwa mfano magonjwa ya figo, magonjwa ya moyo, magonjwa ya uvimbe, magonjwa ya ini nakadhalika. Tunawakaribisha wateja wote wanaosumbuliwa na magonjwa haya kuweza kufika na kupata huduma bora za kibingwa.

**KLINIKI YA DAKTARI BINGWA KINYWA NA MENO**

Kliniki hii ni kwa wateja wanaosumbuliwa na matatizo ya kinywa mfano madonda mdomoni, matatizo ya meno kwa ujumla, tunawakaribisha kupata huduma bora ya kinywa.

**KLINIK YA MAGONJWA YA MACHO**

Kliniki hii ni kwa wateja wanaosumbuliwa na matatizo ya macho mfano matatizo ya kutokuona karibu/mbali, matatizo ya macho kuwasha/kuwa mekundu/kuuma na huduma nyingine zinazohusiana na macho kwa ujumla, tunawakaribisha kwa huduma bora ya macho.

**HISTORIA YA HOSPITALI YA RUFAA YA MKOA WA SINGIDA**

Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Singida ilijengwa mwaka 1954 kwenye eneo la hekta 1.5 ikitumika kama Hospitali ya Wilaya. Ilipandishwa daraja na kuwa Hospitali ya Mkoa mwaka 1963 wakati huo ikihudumia kiasi cha wakazi 336,204.

Hivi sasa idadi ya wakazi imeongezeka na inakadiriwa kuwa 2,008,058, ongezeko hilo ni zaidi ya asilimia 462.

Kutokana na ongezeko hilo, Hospitali inahudumia wagonjwa kati ya 200 hadi 300 kwa siku.

Aidha, ina jumla ya vitanda 139 na inalaza wagonjwa wapatao 60 mpaka 100 kwa siku na kuna jumla ya wodi 13.

Mahitaji ya huduma bora yanaongezeka, wagonjwa wanaongezeka, magonjwa pia yameongezeka, uhitaji wa mafunzo kwa wafanyakazi wa Hospitali wakiwemo madaktari, wauguzi na wanafunzi kutoka vyuo vikuu mbalimbali hapa nchini pia umeongezeka.

Aidha, hayo yakijumuishwa na ongezeko la maradhi na ajali za barabarani vilisababisha kuzaliwa kwa wazo la kujenga Hospitali itakayoweza kukabiliana na changamoto hizo.





JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA AFYA
HOSPITALI YA RUFAA MKOA WA

# TABORA

## MIAKA MITATU YA RAIS DK. SAMIA NA UBORESHAJI SEKTA YA AFYA NCHINI

# Hospitali Ya Rufaa Mkoa wa Tabora (KITETE) inavyochanja mbuga miaka mitatu ya Rais Dk. Samia Suluhu Hassan



RAIS Dk. Samia Suluhu Hassan.



MGANGA Mfawidhi wa Hospitali ya Rufaa ya Tabora, Mark Waziri.









Anuani ya Posta: Box 22, Tabora
Simu: +255737763298
Simu ya Mkononi: +255737763298
Barua Pepe: kitete@taborarrh.go.tz

MIAKA MITATU YA RAIS DK. SAMIA NA UBORESHAJI SEKTA YA AFYA NCHINI



CT Scan.

# Hospitali Ya Rufaa Mkoa wa Tabora (KITETE) inavyochanja mbuga miaka mitatu ya Rais Dk. Samia Suluhu Hassan

Na MWANDISHI WETU

SEKTA ya afya imezidi kuimarika katika kipindi cha uongozi wa Rais Dk. Samia Suluhu Hassan kutokana na serikali kutoa fedha nyingi kuhakikisha inafanyiwa maboresho mbalimbali.

Maboresho yaliyofanywa katika sekta ya afya katika miaka mitatu ya Rais Dk. Samia yameonyesha dhahiri nia ya Rais kutaka kuhakikisha sekta hiyo inakuwa bora na kutoa huduma zinazokwenda na wakati.

Kimsingi katika kipindi cha miaka mitatu Rais Dk. Samia ameigusa sekta hiyo kwa kiasi kikubwa na kufanya watanzania kutibiwa hapa nchini tofauti na awali, baadhi ya wagonjwa walilazimika kwenda nje ya nchi kupata matibabu.

Vilevile sekta ya afya imekuwa bora zaidi kwa kutoa huduma bora kwa wananchi nchi nzima ambapo wengine husafiri umbali mfupi kwenda kutibiwa.



MGANGA Mfawidhi wa Hospitali ya Rufaa ya Tabora, Mark Waziri.

Hayo yote ni baadhi ya mafanikio makubwa yaliyofanywa na serikali iliyopo madarakani chini ya Rais Dk. Samia na kuifanya sekta ya afya kuwa bora na yenye kuridhisha kwa kiasi kikubwa.

Katika kipindi cha miaka mitatu ya Rais Dk. Samia, Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Tabora inayojulikana kwa jina la Kitete ni moja ya hospitali ambazo zilipata fedha nyingi kuhakikisha zinaboresha miundombinu mbalimbali kuwa rafiki kwa wagonjwa.

**"Tunamshkuru kwani Hospitali yetu hivi sasa imekuwa na mabadiliko makubwa ikiwemo mwonekano na vifaa vya kisasa ambapo tunahudumia wagonjwa kutoka wilaya zote za Tabora na maeneo ya karibu,"**

**Mganga Mfawidhi, Waziri.**

Hiyo imesaidia kupanua wigo wa kutoa huduma zake katika wilaya zote za mkoa wa Tabora na maeneo ya jirani ambapo wagonjwa wanapata fursa ya kutibiwa bila wasiwasi wowote.

Kwa mujibu wa Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Rufaa ya Tabora, Mark Waziri, wamepata mafanikio makubwa katika kipindi cha miaka mitatu ya Rais Dk. Samia kutokana na kubadilisha miundombinu kuwa ya kisasa zaidi.

Alisema wanajivunia kuwa na uongozi uliopo madarakani hivi sasa ambapo kupitia Mradi wa Global Fund na IMF wamepata mafanikio makubwa katika kuboresha miundombinu mbalimbali.

"Tunajivunia kuongozwa na serikali ya Rais Dk. Samia ambapo katika kipindi cha miaka mitatu tulishapokea fedha na kuanza kufanya maboresho ya miundombinu mbalimbali.

"Tunamshukuru kwani Hospitali yetu hivi sasa imekuwa na mabadiliko makubwa ikiwemo mwonekano na vifaa vya kisasa ambapo tunahudumia wagonjwa kutoka wilaya zote za Tabora na maeneo ya karibu," alisema Mganga Mfawidhi, Waziri.

**MAFANIKIO WALIYOYAPATA KATIKA KIPINDI CHA MIAKA MITATU YA RAIS DK. SAMIA**

1.Kuanzishwa kwa Mradi wa Jengo linalotoa huduma za wagonjwa Mahututi (ICU).

2.Kuanzishwa kwa Mradi wa Jengo la huduma za CT - Scan Radiolojia na Mionzi.

3.Wamepokea mashine Mpya ya CT-Scan (1.8B).

4.Kuanzishwa kwa Mradi wa Jengo la Tiba Mtandao (Telemedicine).

5.Kuanzishwa kwa Mradi wa Jengo la Mama na Mtoto (martinet complex (6.4B).



KITANDA cha ICU.

MIAKA MITATU YA RAIS DK. SAMIA NA UBORESHAJI SEKTA YA AFYA NCHINI

# Hospitali Ya Rufaa Mkoa wa Tabora (KITETE) inavyochanja mbuga miaka mitatu ya Rais Dk. Samia Suluhu Hassan

6.Kuanzishwa kwa Mradi wa Gesi Tiba (800M).

7.Kujengewa nyumba ya Mtumishi (Staff House).

8.Kuanzishwa kwa Mradi wa Jengo la kutolea huduma za dharura (EMD)

9.Gari la kubebea wagonjwa (Advanced Ambulace)

"Tayari tumefanya maboresho mbalimbali kama nilivyoainisha hapo juu, haya ni mafanikio makubwa kwetu katika kipindi cha miaka mitatu ya Rais Dk. Samia.

"Tunaamini tutaendelea kupatiwa fedha na kuhakikisha tunaiboresha zaidi hospitali yetu na kuendelea kutoa huduma kwa kiwango cha juu," alisema.

**MCHANGO WA HOSPITALI YA RUFAA YA MKOA WA TABORA - KITETE KWA WANANCHI WA TABORA NA SEHEMU JIRANI**

Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Tabora, Waziri alisema hospitali hiyo imekuwa na mchango mkubwa kwa wananchi wa Tabora na maeneo jirani ambapo awali walikuwa wakipata shida ya kupata huduma mbalimbali.

"Tumekuwa na mchango mkubwa kwa wananchi wa Tabora na maeneo jirani ambapo awali walikuwa wakipata shida kupata huduma," alisema Mganga Mfawidhi, Waziri.

Alisema hospitali imekuwa ikileta kambi za kibingwa kila mwaka kutoka hospitali mbalimbali ili kusogeza huduma karibu na kuwasaidia wananchi wa Mkoa wa Tabora na maeneo ya jirani kupata huduma hizo kwa ukaribu zaidi tofauti na kuzifuata maeneo ya mbali kama vile Muhimbili, JKCI, Benjamini Mkapa na nyingine nyingi.

Alisisitiza kuwa wamekuwa wakitoa huduma za kibingwa ambazo awali hazikuwepo ikiwemo upasuaji mkubwa, huduma za mama na mtoto, huduma za magonjwa ya ndani na huduma za dharura.

Alisema pia wamekuwa wakitoa huduma za CT – Scan Radiolojia na Huduma za Tiba Mtandao.

"Tumefanikiwa kuanza kutoa huduma mbalimbali ambazo hapo awali hazikuwepo zikiwemo upasuaji mkubwa, huduma za mama na mtoto, huduma za magonjwa ya ndani na huduma za dharura haya yote ni mafanikio tuliyoyapata kipindi cha miaka mitatu ya Rais Dk. Samia," alisema.

**MIKAKATI ILIYOPO**

Mganga Mfawidhi, Waziri alisema wamejipanga kuhakikisha wanaweka mikakati mbalimbali ikiwemo kuendelea kufanya vizuri na kutoa huduma bora zaidi kipindi chote cha uongozi wa Rais Dk. Samia.

Alisema kuwa wamefanikiwa kupeleka watumishi watatu kwenda kusomea fani za kibingwa.

Alisisitiza pia wataendelea kuwahimiza madaktari na kuwawezesha kwenda kusomea huduma za kibingwa ambazo hazitolewi kwa sasa.

Alisema wataendelea kuleta kambi za kibingwa ili kusogeza huduma karibu kwa wananchi wa Mkoa wa Tabora na maeneo ya jirani.

Mganga Mfawidhi, Waziri alisema wataendelea kulinda na kuzitumia vizuri rasilimali zilizopo na kuzifanyia marekebisho na uboreshaji kwa wakati stahiki.

**"Tumekuwa na mchango mkubwa kwa wananchi wa Tabora na maeneo jirani ambapo awali walikuwa wakipata shida kupata huduma," alisema Mganga Mfawidhi, Waziri.**



JENGO Jipya La ICU



JENGO Kwajili ya Wagonjwa wa Dharura (EMD).



OFISI ya CT-Scan.

MIAKA MITATU YA RAIS DK. SAMIA NA UBORESHAJI SEKTA YA AFYA NCHINI



VIFAA vya Gesi Tiba.

# Hospitali Ya Rufaa Mkoa wa Tabora (KITETE) inavyochanja mbuga miaka mitatu ya Rais Dk. Samia Suluhu Hassan

Pia wataendelea kutoa huduma bora kwa jamii kwa kufata muongozo wa STK.

**KUENDELEZA NA KUSIMAMIA MIRADI ILIYOTEKELEZWA NA INAYOENDELEA KUTEKELEZWA KATIKA KUHUDUMIA WANANCHI**

Alisema wataendeleza na kusimamia miradi iliyotekelezwa na inayoendelea kutekelezwa katika kuhakikisha wanatoa huduma bora kwa wananchi.

Alisema wataendelea kuboresha mapokezi mazuri kwa mteja (good customer care) na kufata mwongozo wa STK.

Alisisitiza kuwa wataendeleza na kuboresha upatikanaji wa vifaa tiba na dawa.

Alieleza wataendelea kutoa elimu kwa watumishi (job training) ili kuendelea kuboresha huduma kwa jamii.

Pia wataendelea kutoa huduma za mkoba kwa jamii, alisema Mganga Mfawidhi, Waziri.

**AINA YA WAGONJWA WANAOPOKEA KATIKA HOSPITALI YA RUFAA YA MKOA WA TABORA-KITETE**

1. Wagonjwa wanaolipia papo kwa papo
2. Wagonjwa wa BIMA ikiwemo NHIF
3. Wagonjwa wa makundi maalumu wanatibiwa kwa msamaha.


VIFAA vya mazoezi.

**HUDUMA ZINAZOTOLEWA NA HOSPITALI YA RUFAA YA MKOA TABORA-KITETE**

1.Huduma za Kibingwa.
•Upasuaji.
•Magonjwa ya ndani.
•Magonjwa ya Watoto.
•Magonjwa ya wanawake.
•Magonjwa ya dharura
2.Huduma za Macho.
3.Huduma za Uchunguzi.
•Maabara.
•Radiolojia na mionzi.
4.Huduma ya Afya ya akili.
5.Huduma za ustawi wa Jamii.

**IDADI YA WAGONJWA**

Hospitali inapokea wagonjwa 150-250 kwa siku.

Ina wodi 13 za kulaza wagonjwa na vitanda vipo 270.

**NENO LAO KWA SERIKALI YA AWAMU YA SITA ILIYOPO CHINI YA RAIS DK. SAMIA**

Alisema Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Tabora inatoa shukrani za dhati kwa Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Rais Dk. Samia katika kuendeleza, kuimarisha na kuboresha sekta ya afya nchini kwa ujumla na hasa Mkoa wa Tabora.

Alisema uwekezaji mkubwa umefanyika wa miundombinu, rasilimali watu na rasilimali pesa katika kuhakikisha wananchi wa mkoa wa Tabora na viunga vya jirani wanapata huduma bora za afya kwa wakati na huduma zinakuwa endelevu.

"Tunamshukuru Rais Dk. Samia kutokana na kuimarisha, kuendeleza na kuboresha sekta ya afya nchini hasa katika hospitali yetu, uwekezaji mkubwa umefanyika na tutahakikisha tunaendelea kutoa huduma bora kwa kila mwananchi," alisema Mganga Mfawidhi, Waziri.

**Tutaendelea kuboresha mapokezi mazuri kwa mteja (good customer care) na kufata mwongozo wa STK, kuendeleza na kuboresha upatikanaji wa vifaa tiba na dawa, kuendelea kutoa elimu kwa watumishi (job training) ili kuendelea kuboresha huduma kwa jamii na huduma za mkoba kwa jamii,"**

**alisema Mganga Mfawidhi, Wazir.**

**WITO KWA JAMII WANAYOIHUDUMIA**

Alisema Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Tabora inatoa wito kwa jamii wanayoihudumia kwa kutoa huduma bora na kujali afya kwa kuwapa kipaumbele kutokana na kaulimbiu ya Hospitali inavyosema kuwa ***AFYA YAKO KIPAUMBELE CHETU.***

**HISTORIA**

Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Tabora ijulikanayo kwa jina la Hospitali ya Kitete ilijengwa mwaka 1906 ikiwa ni kambi ya kuhudumia majeruhi wakivita enzi za utawala wa ukoloni wa Wajerumani.

Kambi hii ilikuwa inapokea majeruhi wa vita wakati ule na baadae ikabadilishwa kuwa hospitali ya jeshi.

Kadiri muda ulivyozidi kwenda, Mji wa Tabora uliendelea kukua na hospitali ya jeshi ikawa hospitali ya wananchi kwani ilionekana kuhudumia wananchi wengi zaidi kuliko wanajeshi.

Baada ya Uhuru, hospitali hii ilifanywa kuwa hospitali ya mkoa na ikaongezewa baadhi ya majengo ya utawala na wodi chache.

Tangu wakati huo hospitali hii imekuwa ikifanyiwa ukarabati kulingana na mahitaji.

Hospitali inahudumia Halmashauri nane (8) ambazo ni Manispaa ya Tabora, Uyui, Urambo, Kaliua, Sikonge, Igunga, Nzega na Nzega Mji.

Pia hospitali inahudumia wilaya za mikoa ya jirani kama vile Wilaya ya Uvinza iliyoko Mkoa wa Kigoma.

Kwa mujibu wa sensa iliyofanyika kwa mwaka 2022 idadi ya wakazi wa Mkoa wa Tabora ni 3,391,679.

Hospitali ina jumla ya watumishi 314 (45.5 %) wa kada mbalimbali kati ya watumishi 690 wanaohitajika kuwepo kwa kima cha juu, hivyo kuna upungufu mkubwa wa watumishi 376 (54.5%).

Jumla ya watumishi 26 wapo masomoni wakisomea fani mbalimbali zikiwemo udaktari bingwa, famasia, uuguzi na kada nyingine.


JENGO linaloendelea kujengwa la mama na mtoto.




## Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Tanga yajivunia Mafanikio na Mambo Mengi Mazuri yaliyofanyika ndani ya Miaka Mitatu ya Uongozi wa Rais Dkt Samia Suluhu Hassan.

# Kitengo cha CT SCAN

Katika kitengo cha Huduma ya Uchunguzi kwa kutumia (Mionzi) CT-Scan Serikiali imefanya uwekezaji mkubwa wa maboresho katika eneo hilo kwa kujengo jengo na ununuzi wa mashine za CT-Scan

Ambapo uwekezaji huo uliofanywa na Serikali umesaidia kwa kiasi kikubwa kuwaondolea wananchi adha kubwa waliokuwa wakikutana nayo kulazimika kusafiri nje ya mkoa kwa ajili ya kwenda kupata huduma hiyo.
Mafanikio uwepo wa huduma hiyo ilivyoanza mwezi February mwaka 2023 na mpaka sasa wamekwisha kutoa huduma kwa wagonjwa 900 ambao wangeweza kupewa rufaa kwenye hospitali mbalimbali za nje ya Tanga na hivyo uwepo wake umesaidia kupunguza gharama kwa wateja na usumbufu kwao.



Mashine ya CT SCAN.

Tunaishukuru Serikali kwa hili kwani wagonjwa hao wangelezimika kupatiwa rufaa kwenda nje ya mkoa wa Tanga kupata huduma hizo hivyo tunapenda kuishukuru Serikali kwa uwekezaji huo ambao umesaidia kuondoa kero kwa wananchi wa mkoa wa Tanga

# Kitengo cha Watoto Njiti (NIKU)

Watoto njiti ni watoto waliozaliwa kabla ya wakati wao ambapo kwa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Tanga napo kuna kitengo ambacho kinawahudumia watoto hao maarufu kama Nicu ambapo wakina mama ambao wanajifungua watoto hao hulazimikaa kukaa kwa muda Fulani kwa ajili ya uaangalizi maalumu kabla ya kuruhusiwa kwendaa nyumbani.

Watoto hao ni wale wanaozaaliwa kabla ya miezi 9  ambao wenye uzito mdogo ambao huhitaji huduma za uangalizi maalumu ikiwemo matibabu na lishe mpaka watakapotimiza umri wa mwaka mmoja.

Katika eneo hilo changamoto ni upungufu wa vifaa tiba ulikinganisha na idadi watoto wanaozaliwa kwenye Hospitali hiyo na sababu ya vifo vinavyowakabili watoto njiti  ni kushindwa kupumua mashine ambvagto inaawasaidia watoto hapo ,watoto hao wanakjuwa na kwenye wopdi yaa watoto



Watoto njiti wakiwa kwenye kifaa malum kwajili ya kupata joto (warmer)



Badhi ya vifaa vya kuhifadhia watoto njiti (Incubetor)

# Intensive Care Unit (ICU)

Katika kipindi cha miaka mitatu tu Huduma za ICU zimeendelea kuboreshwa kwa kuongezwa vifa vya kisasa pamoja na ukarabati mkubwa wa majengo ya kutolea huduma, hii imefanya kuwepo kwa mazingira rafiki kwa wateja na watoa huduma,

Mafanikio makubwa kaika hili ni kuokoa maisha ya watanzania wengi zaidi ya hapo awali. hakika kipindi cha miaka mitatu ya Rais Dkt Samia Suluhu Hasan kimekuwa kipindi cha mafanikio makubwa kwa sekta ya Afya katika mkoa wa tanga.



Vijaa vya kisas vya kutolea huduma




Mazingigra ya usafi ICU



Mtoa huduma wa ICU akiendelea na kazi



# Nyumba ya mtumishi

Hospitali imefanikiwa kupata nyumba ya mtumishi ikiwa imejengwa jirani na Hospitali, Mradi huu ni moja ya miradi iliyofakiwa kukamilika katika kipindi cha miaka mitatu ya Uongozi ya Rais Samia suluhu Hasan.

# Mradi ya Ujenzi wa Kituo cha damu salama

Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Tanga imeweza Kuanzisha Ujenzi mpya wa kituo cha damu salama. zifuatazo ni picha zikionesha ujenzi ukiwa katika hatua za awali.

Ukamilikaji wa Mradi hu ni moja ya sababu za zitakazo pelekea kuimarika zaidi kwa sekta ya Afya katika mkoa wa Tanga na Wilaya zake.



Hatua za Ujenzi wa Kituo cha damu salama



# Kituo cha uzalizashaji wa Hewa ya Oxygen
# **Oxygen Plant**

Katika kipindi hiki cha miaka mitatu ya Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan,Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Tanga imefanikiwa kuboresha Mitambo ya kuzalisha Hewa tiba ya Oksijeni ambapo tayari mitambo hiyo Imeanza kutumika kwa lengo la kuwasaidia wagonjwa wenye uhitaji kwa wakati huo wakiwemo Wagonjwa mahututi na waliopata ajali ambao wanahitaji kupumua kwa usaidizi basi mitambo hiyo imekuwa chachu ya kuwanusuru wahitaji hao na kupunguza idadi ya vifo vinavyotokana na changamoto ya upumuaji kwa wagonjwa pindi wakiwa katika Hospitali yetu.

# Medical Assisted Treatment (MAT)

Kitengo cha Huduma za Methadone katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Tanga-Bombo (MAT) kilianzishwa mwaka 2019 ambapo huduma hizo zimekuwa zikiwasaidia waraibu wa dawa za kulevya kupunguza matumizi na hatimaye kuweza kurudi kwenye hali yake ya kawaida.

Kwa mujibu wa wataalamu wa kituo hicho walioanza kupata huduma hizo wapatao 1336 tokea kuanzisha kwa Kituo hicho na wanaendelea kukua kila siku ambapo uwekezaji huo ulianza mwaka 2019 na umekuwa msaada mkubwa kwa waraibu wa dawa za kulevy



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA AFYA
HOSPITALI YA RUFAA MKOA WA

# SHINYANGA

SHINYANGA REGIONAL REFERRAL HOSPITAL








RAIS Dk. Samia Suluhu Hassan.

# MIAKA MITATU YA RAIS DK. SAMIA NA UBORESHAJI SEKTA YA AFYA NCHINI



MGANGA Mfawidhi wa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa Shinyanga (SRRH), Luzila John.

## HOSPITALI YA RUFAA MKOA WA SHINYANGA YAJIVUNIA MAFANIKIO TELE MIAKA MITATU YA MHE. DK. SAMIA

IKIWA ni miaka mitatu imetimia tangu aingie madarakani Machi 19, 2021, Rais wa jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan amekuwa chachu ya mafanikio makubwa ya uboreshaji wa huduma mbalimbali, hususani katika sekta ya afya.

Anuani ya Posta: Box17, Shinyanga / Simu: +255756568291
Simu ya Mkononi: 0756568291/ Barua Pepe: nshinyangarrh@afya.go.tz

MIAKA MITATU YA RAIS DK. SAMIA NA UBORESHAJI SEKTA YA AFYA NCHINI

# Hospitali ya Rufaa mkoa wa Shinyanga yajivunia mafanikio tele miaka mitatu ya Mhe. Dk. Samia



**MGANGA Mfawidhi wa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa Shinyanga (SRRH), Luzila John.**



**CHUMBA cha kuwezesha huduma ya CT-SCAN (CT-SCAN Control Panel) Hospitali ya Rufaa ya Mkoa Shinyanga.**

IKIWA ni miaka mitatu imetimia tangu aingie madarakani Machi 19, 2021, Rais wa jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan amekuwa chachu ya mafanikio makubwa ya uboreshaji wa huduma mbalimbali, hususani katika sekta ya afya.

Uwepo wa Dkt. Samia madarakani katika kipindi cha miaka mitatu umesaidia upatikanaji wa dawa za kutosha pamoja na ununuzi wa vifaa tiba ambavyo awali havikuwepo katika baadhi ya Zahanati, Vituo vya Afya na Hospitali za Rufaa za Mkoa hapa nchini.

Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa Shinyanga (SRRH), Luzila John, alieleza moja ya matokeo chanya makubwa ni kupunguza rufaa za wananchi mkoani Shinyanga na maeneo jirani kwenda kupata huduma katika Hospitali ya Rufaa Kanda Bugando.

Dkt. Luzila alibainisha miaka mitatu ya Dkt. Samia kwa sasa imesaidia wananchi katika mkoa wa Shinyanga wamekuwa wakipata huduma hizo katika Hospitali yao ya Mkoa, Hospitali ambayo imepunguza usumbufu pia gharama za wananchi kwenda Bugando kupatiwa huduma.

**SHUKRANI KWA DKT. SAMIA**

Shukrani za dhati na za kipekee zilitolewa Dkt. Luzila kwa Dkt. Samia kwa mchango wake mkubwa katika kuboresha huduma kwenye sekta ya afya, hususani katika Hospitali ua Rufaa ya Mkoa Shinyanga.

"Tunaishukuru serikali ya awamu ya sita chini ya Dkt. Samia kwa kuboresha huduma katika Hospitali yetu ambayo inahudumia jumla ya Halmashauri sita (6) zenye jumla ya Vijiji 513, ikiwemo ujenzi wa miundombinu na upatikanaji wa dawa na vifaa tiba", alisema.

> **"Tunaishukuru serikali ya awamu ya sita chini ya Dkt. Samia kwa kuboresha huduma katika Hospitali yetu ambayo inahudumia jumla ya Halmashauri sita (6) zenye jumla ya Vijiji 513, ikiwemo ujenzi wa miundombinu na upatikanaji wa dawa na vifaa tiba",**
>
> Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa Shinyanga (SRRH), Luzila John

**(MAFANIKIO) KUKAMILISHA UJENZI WA MIUNDOMBINU**

Alisema chini ya uwatawala wa Rais. Dkt. Samia, Hospitali hiyo ambayo ni mpya ilifanikisha kukamilisha ujenzi wa miundombinu ya majengo kwa awamu ya kwanza ikiwemo Jengo la Wagonjwa Mahututi (ICU) na Wahonjwa wa Nje (OPD).

**KUANZA KWA HUDUMA YA CT-SCAN**

Aidha, Hospitali imefanikiwa kuanza kutoa huduma ya CT-SCAN iliyogharimu sh. bilioni 1,810,000,000 ambayo haikuwepo hapo mwanzo, na ikisaidia kupunguza usumbufu wa wagonjwa kwenda Bugando, Mwanza, kwa ajili ya kupatiwa huduma hiyo.

Dkt. Luzila alisema huduma hiyo imesaidia kupata wateja kutoka mikoa jirani ikiwemo Simiyu, Geita, Tabora na hata Singida ambao wamekuwa wakisafiri kuja Shinyanga kutokana na ubora wa huduma zinazotolewa.

**HUDUMA YA X-RAY**

Hospitali imeboresha huduma zake katika uwatala wa Dkt. Samia kwa kufanikiwa kununua mashine ya kisasa ya X-RAY kwa sh. milioni 228,548,000 kupitia fedha za UVIKO-19.

**ULTRA SOUND MACHINE**

Dkt. Luzila alisema Hospitali hiyo imefanikiwa kununua



**UZALISHAJI wa hewa ya Oksijeni (Oxygen Plant) katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa Shinyanga.**



**MASHINE ya CT-SCAN katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa Shinyanga.**

## MIAKA MITATU YA RAIS DK. SAMIA NA UBORESHAJI SEKTA YA AFYA NCHINI



# Hospitali ya Rufaa mkoa wa Shinyanga yajivunia mafanikio tele miaka mitatu ya Mhe. Dk. Samia

Portable Ultra-Sound Mashine ya kisasa kwa gharama ya sh. milioni 71,540,000.

**UZALISHAJI WA TIBA HEWA (OXYGEN PLANT)**

Alibainisha kuwa, huduma za uzalishaji wa Tiba Hewa (Oxygen Plant) hospitalini kwa ajili ya wagonjwa ulifanikiwa kuanza katika utawala wa awamu ya sita, uzalishaji ambao umesaidia kuhifadhi na kupunguza gharama za ziada, kwenda Mwanza na Tabora kwa ajili ya kufanya manunuzi.

**KUANZISHA HUDUMA YA TIBA MTANDAO (TELEMEDICINE)**

Dkt. Luzila alisema huduma ya Telemedicine katika Hospitali hiyo imefanikiwa kuanzishwa. Huduma hiyo imesaidia kupunguza gharama za fedha kwa mgonjwa kusafiri kutoka Hospitali A kwenda B kwenda kupata huduma, kutokana na teknolojia yake inayoruhusu kutoa huduma kwa wagonjwa kwa njia ya mtandao bila kusafiri umbali mrefu.

**UJENZI WA MAJENGO**

Halikadhalika alieleza, Hospitali imefanikisha kupata majengo matatu muhimu (yote yanatumika) kwa fedha za UVIKO-19, ambayo ni Jengo la Wagonjwa Mahututi (ICU) kwa sh. milioni 560, Jengo la Magonjwa ya Dharura (EMD) sh. milioni 650, na Jengo la Mionzi (Radiolojia) milioni 329, Jengo la Magonjwa ya Mlipuko (Isolation), bilioni 2 zilizowezeshwa na Global Fund pamoja nyumba ya Mganga Mfawidhi iliyowezeshwa na fedha za UVIKO-19, iliyogharimu milioni 90.

**MIKAKATI WALIYOJIWEKEA**

Katika kuhakikisha Hospitali inastawisha maendeleo yenye afya chanya kwa wananchi wa mkoa wa Shinyanga na maeneo jirani, Dkt. Luzila alibainisha Hospitali itendelea kutoa huduma bora za kibingwa na kibingwa bobezi ili kukidhi matakwa yao, pamoja na kupunguza wananchi kusafiri maeneo ya mbali.

**Tunatoa shukrani za dhati kwa Rais. Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuimarisha upatikanaji wa huduma bora za afya katika mkoa wa Shinyanga, pia kwa kututengea pesa zitakazosaidia kukamilisha utoaji wa huduma katika hospitali kama vile Jengo la Mama na Mtoto, Maabara, Mochwari na Famasi ambapo serikali imeshatutengea kiasi cha zaidi ya bilioni 10 kwa ajili ya ujenzi huo katika mwaka wa fedha wa 2023/2024"**



Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa Shinyanga (SRRH), Luzila John

Aidha, alisisitiza kuendelea kuboresha huduma nzuri katika Kitengo cha Mrejesho (Huduma kwa Mteja) ili kuwafanya wananchi wanaofika hospitalini kufarijika na kutokata tamaa ya kurejea tena mara baada ya kupatiwa huduma.

Vilevile alisema wataendelea kuimarisha huduma ya upatikani wa dawa zote na kwa wakati pia vifaa tiba kuboresha huduma nyingine kwa maslahi mapana ya kuokoa maisha ya wagonjwa.

Aliongeza jitihada za kusimamia ipasavyo miradi yote ya ujenzi kwa muda na ubora stahiki itazingatiwa ipasavyo.

Dkt. Luzila alieleza pia kuendelea kusimamia miiko na maadili ya kazi yanayohusu utumishi wa umma ili kuimarisha nidhamu na uwajibikaji mahala pa kazi.

**NENO KWA SERIKALI**

Kutokana na jitihada ambazo serikali ya awamu ya sita inayoongozwa na Dkt. Samia, Dkt. Luzila alitoa shukrani zake kwa serikali.

"Tunatoa shukrani za dhati kwa Rais. Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuimarisha upatikanaji wa huduma bora za afya katika mkoa wa Shinyanga, pia kwa kututengea pesa zitakazosaidia kukamilisha utoaji wa huduma katika hospitali kama vile Jengo la Mama na Mtoto, Maabara, Mochwari na Famasi ambapo serikali imeshatutengea kiasi cha zaidi ya bilioni 10 kwa ajili ya ujenzi huo katika mwaka wa fedha wa 2023/2024", alisema.

**WITO**

Dkt. Luzila alitoa wito kwa jamii kwenda hospitalini hapo kwa ajili ya kupata huduma za kiafya kutokana na kuimarishwa zaidi tofauti na zamani, hususani uchunguzi wa magonjwa yasiyo ya kuambukiza, lakini vilevile alisema wanaendelea kutoa elimu kila siku kuhusiana na masuala ya afya, akiwataka wananchi wajitokeze kwa wingi sababu huduma inapatikana wakati wote.

**HISTORIA**

Hospitali ya Rufaa ya Mkoa Shinyanga (SRRH) ni zao la iliyokuwa Hospitali ya Wilaya ya Shinyanga ambayo ilianzishwa kwa ajili ya kutoa huduma katika wilaya ya Shinyanga miaka ya mwanzo ya uhuru na ilipopewa hadhi ya mkoa, hospitali hiyo ikawa Hospitali ya Mkoa.

Kadiri miaka inavyokwenda hospitali imekua siyo tu kwa ukubwa na aina ya huduma zinazotolewa, lakini pia kwa muundo na wataalamu wa afya. Ndiyo hospitali kubwa zaidi inayomilikiwa na serikali katika eneo hilo.

Ujenzi wa Hospitali mpya kwa lengo la kukidhi hadhi ya Rufaa ya Mkoa, ulianza mwaka 2014 na kukamilika rasmi 2022, mwaka ambao huduma zilianza kutolewa kwa awamu ya kwanza, kisha Julai 2023, Hospitali ilianza kutoa huduma zote katika majengo yake mapya.

Hospitali imejengwa Mwawaza, umbali wa kilomita 5.6 kutoka Shinyanga mjini.

**KLINIKI ZA KIBINGWA ZINAZOTOLEWA NA HOSPITALI HIYO**

Kliniki ya Magonjwa ya Wanawake na Upasuaji
Kliniki ya Magonjwa ya Moyo
Kliniki ya Magonjwa ya Wajawazito
Kliniki ya Magonjwa yasiyoambukizwa
Kliniki ya Watoto





CHUMBA cha watoto wachanga (NICU) Hospitali ya Rufaa ya Mkoa Shinyanga.

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA AFYA

# Hospitali ya Taifa Kibong'oto yazidi kupaa kimataifa



Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu.



Mkurugenzi wa Hospitali Maalum ya Taifa ya Magonjwa Ambukizi Kibong'oto, Dkt. Leonard Subi



Rais Mhe. Dkt Samia Suluhu Hassan

NA WILLIUM PAUL, KILIMANJARO

SEKTA ya Afya ni miongoni mwa sekta mtambuka nchini ambayo ni nguzo muhimu katika Taifa lolote Duniani hasa katika nchi zinazokuwa kiuchumi.

Hayati Rais wa kwanza wa Tanzania, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere alishawahi kusema maadui watatu wa nchi hii ni Ujinga, Maradhi na Umaskini.

Katika kupigana na adui maradhi, Serikali ya awamu ya sita inayoongozwa na Rais Dkt. Samia Suluhu Hasani imeonyesha kwa dhati kuendeleza mapambano hayo kwa kujenga vituo mbalimbali vya Afya, Zahanati, Hospitali za Wilaya katika Mamlaka za Serikali za Mitaa nchini sambamba na kuvipatia vifaa tib ana wataalam ili kupambana na maradhi.

Mbali na hiyo imeendelea kuboresha Hospitali za Mikoa, Hospitali za Kanda, Hospitali Maalum ngazi ya Taifa na Hospitali ya Taifa ya Muhimbili kwa ununuzi wa vifaa tiba vya kisasa, Ujenzi wa miundombinu ikiwemo majengo mapya na ya kisasa pamoja na kuhakikisha upatikanaji wa Dawa na vifaa tiba kwa wananchi kwa kiwango kikubwa.

Kwa sasa tujikite katika Hospitali Maalum ya Taifa ya Magonjwa ya Ambukizi ya Kibong'oto iliyopo wilayani Siha mkoani Kilimanjaro ambayo imepokea mabilioni ya fedha kwa ajili ya ujenzi wa miradi mikubwa nay a kimkakati ikiwemo Ujenzi wa Maabara ya Afya ya Jamii ya kisasa yenye hadhi ya kimataifa ya usalama wa kibailojia Daraja la tatu.

Kwa mujibu wa Mkurugenzi wa Hospitali Maalum ya Taifa ya Magonjwa ambukizi ya Kibong'oto, Dkt. Leonard Subi amesema kuwa hospitali hiyo imenufaika na fedha nyingi za miradi mbalimbali na utoaji wa huduma za kijamii na wasimamia ipasavyo miradi hiyo kwa manufaa ya taifa kazi zinafanyika kwa kwa kasi kubwa na viwango vinavyokubalika.

Dkt Subi amesema, hospitali hiyo ambayo ni kongwe ina miaka 98 toka kuanzishwa kwake, imejikita katika utoaji wa huduma za kibingwa na ubingwa bobezi katika kinga na udhibiti wa magonjwa ambukizi yanayosababishwa na virusi, bakteria, fangasi pamoja na protozoa.

Aidha, Dkt. Subi anasema kuwa, hospitali hiyo ina maono yake ya kuwa kituo bora cha kimataifa katika kukinga na kudhibiti magonjwa ya kuambukiza ambapo Hospitali inatumia hutumia mbinu kuu tatu katika kutimiza maono hayo, ambazo ni kutoa huduma bora za matibabu na kinga dhidi ya magonjwa ya kuambukiza, kufanya tafiti za kisayansi,mafunzo na ushauri dhidi ya magonjwa ya kuambukiza pamoja na kutoa huduma za afya za kijamii ikiwemo Maabara ya Afya ya Jamii ya Usalama wa Kibailojia Daraja la tatu, ufuatiliaji wa vimelea vya magonjwa na magonjwa nchini elimu na uchunguzi wa magonjwa katika jamii ikiwemo utayari katika kukabiliana na milipuko ya magonjwa.

Moja ya mafanikio makubwa ambayo hospitali hiyo imeweza kuyapata ni ujenzi wa maabara bora ya afya ya jamii ngazi ya kimataifa ya usalama wa kibailojia daraja la tatu ambayo ilifunguliwa rasmi Julai 16 mwaka 2022 na Mhe. Dkt Philip Isdor Mpango Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Dkt Subi amesema kuwa, maabara hiyo ambayo imegharimu fedha za kitanzania Bilioni 22.5 ni maabara ya kisasa ambayo ina malengo makuu ya kuongeza nguvu katika ufuatiliaji wa vimelea vya magonjwa mbalimbali, uchunguzi wa sampuli za magonjwa, utafiti wa kisayansi, mafunzo na uhifadhi wa sampuli za vimelea (Benki ya Sampuli).

"Hii ni maabara kubwa na ya kisasa iliyojengwa na Serikali ilianza mwaka 2016 na Serikali awamu ya sita chini ya Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan imetoa fedha na imekamilika na kuanza kutoa huduma ambapo ujenzi wa jengo na ununuzi wa baadhi ya vifaa na mitambo uligharimu Bilioni 12.5 na vifaa vya kisasa vya maabara, samani na vifaa vya TEHAMA unagharimu Bilioni 10 ili kuimarisha udhibiti wa magonjwa.



Maabara ya Afya ya Jamii ya Usalama wa Kibailojia Daraja la tatu ngazi ya Kimataifa iliyojengwa katika Hospitali ya Kibong'oto na kugharimu Shs Bilioni 22.5 ikiwa ni ujenzi na vifaa

MIAKA MITATU YA RAIS DK. SAMIA NA UBORESHAJI SEKTA YA AFYA NCHINI

# Hospitali ya Taifa Kibong'oto yazidi kupaa kimataifa

Mkurugenzi huyo anasema kuwa, mpaka sasa baadhi ya vifaa walivyoagiza vimeshafika na kufungwa katika maabara hiyo huku vingine vilivyosalia vikitarajiwa kufika ifikapo Juni mwaka huu.

Anasema kuwa, maabara hiyo itawezesha ufuatiliaji wa magonjwa ili kujua mwenendo wake, lakini kujua mwenendo wa vimelea vinavyosababisha magonjwa ikiwemo usugu wa vimelea hivyo kwenye dawa na jinsi vinavyojibadilisha ili kuweza kukabiliana na hali na kuweza kumwambukiza binadamu.

Anadai kuwa, maabara hiyo ambayo imejengwa na Serikali inauwezo ya kuhifadhi vimelea vya magonjwa ikiwemo virusi na bakteria kwa zaidi ya miaka 50 ambao watakuwa wakivitumia katika utafiti ambapo malengo makubwa ya maabara hiyo ni ni udhibiti wa magonjwa na hatimaye kuwezesha kutengeneza Dawa na chanjo za kudhibiti magonjwa , pamoja na kutengeneza vitendanishi vya kupimia magonjwa hayo.

"Tunajitofautishaje na maabara nyingine sisi tunabobea zaidi katika uchunguzi wa magonjwa wa hali ya juu ikiwemo kutumia njia za kimolekyuli katika uchunguzi wa melea ambapo tunapasua Bakteria na Virusi na kutoa vina saba ambapo tunazalisha kopi nyingi kwa kutumia mashine ya PCR na kuzisoma na baadaye kutafsiri nini kifanyike katika kudhibiti magonjwa haya ya kuambukiza".

Mkurugenzi huyo anadai kuwa, uwekezaji wa maabara hiyo ni mafanikio makubwa ya Rais Samia Suluhu Hassan kwani maabara ya hadhi hiyo hapa nchi zipo mbili moja ikiwa ni Kibong'oto na nyingine ni maabara ya Taifa

Anaidai kuwa tangu awali huduma za maabara katika hospitali hiyo zimekuwa zikitolewa ambapo vipimo 28 vilipata ithibati ya kimataifa mwaka 2022 yaani vinatambulika ubora wake katika ngazi ya kimataifa ambapo wameweza kutunukiwa cheti maalum na taasisi inayochunguza umahiri na ubora wa viwango vya kimataifa katika uchunguzi wa magonjwa mbalimbali ya binadamu (SADCAS).

Anasema kuwa,kupitia maabara hiyo wamekuwa wakitumia njia za kimolekiuli na kuweza kupunguza muda wa kugundua usugu wa dawa wa vimelea vya kifua kikuu na kutoa majibu ndani ya masaa 24 ukilinganisha na wiki 10 ya vipimo vingine.

"Hospitali yetu imeendelea katika kudhibiti ugonjwa wa kifua kikuu na mapambano dhidi ya ugonjwa huu ambapo tumechangia kwa kiasi kikubwa katika mabadiliko ya sera za matibabu katika shirika la afya Duniani na za Wizara yetu ya Afya kwani tumekuwa tukishiriki katika utafiti za kisayanzi" anasema Dkt. Subi.

Na kuongeza moja ya mafanikio katika ushiriki kwenye tafiti hizo "tumeweza kupunguza muda wa matibabu ya mgonjwa wa kifua kikuu sugu kutoka miaka miwili hadi miezi tisa na sasa tunaenda kwenye kupunguza kufikia miezi sita kama shirika la afya duniani lilivojikita".

Mkurugenzi huyo anasema kuwa, kwa hospitali hiyo hutoa huduma bora za matibabu kwa wagonjwa wa kifua kikuu ikiwemo lishe bora bure kwa wagonjwamwa kifua kikuu sugu na uponaji wao ni wa hali ya juu kwani hupona kwa zaidi ya asilimia 75 na wanaendelea na maisha yao. Dkt Subi amesema Serikali imekuwa pia ikiwapatia wagonjwa wa kifua kikuu sugu wanaoendelea na matibabu kiasi cha Tzs 100,000 kila mwezi ili kumudu gharama za usafiri wanapoenda kupata tib ana dawa na kuwasaidia lishe wakati wa matibabu. Hii ni Serkali inayojali wananchi wake hususani wanyonge na wahitaji alisema Dkt Subi kwani Hospitali hiyo mwaka jana imetumia zaidi ya shilingi Mil 400 kwa ajili ya nauli na lishe kwa wagonjwa wa kifua kikuu sugu .



Kokoto ambazo zitatumika kwa ajili ya ukarabati na ujenzi wa jengo la kisasa la Utawala hospitali ya Kibong'oto (Gorofa mbili)

**MRADI WA UJENZI WA JENGO LA UCHUNGUZI WA MAGONJWA KWA NJIA YA MIONZI NA MAWIMBI SAUTI.**

Katika kuhakikisha wananchi wanapata huduma bora na za kisasa katika hospitali hiyo ya Taifa ya magonjwa ya kuambukiza ya Kibong'oto serikali ya awamu ya sita imeamua kutoa fedha Bilioni 8.1 ambapo kiasi cha Billion 3.1 ni ujenzi wa jengo na Bil 5 ni ununuzi wa vifaa tiba na tayari Serikali imeshanunua mashine ya CT scan ambayo itasimikwa mwishoni mwa mwezi April mwaka huu 2024.

Mkurugenzi wa hospitali hiyo, anadai kuwa, awali ujenzi wa jengo hilo ulianza kwa kutumia mapato ya ndani kwani tangu mwaka 2021/22 wameimarisha ukusanyaji wa mapato kutoka vyanzo mbalimbali kutoka Mil 400 hadi kufikia Bil 1.3 mwaka 2023/24. Baada ya sisi kujiongeza Serikali ya awamu ya sita chini ya Samia imetenga shilingi Bil 3 na tayari imeshaleta fedha Bilioni 1.8 awamu ya kwanza kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wake na tunatarajia kukamilika ifikapo Juni mwaka huu 2024 hivyo wananchi watarajie kupata huduma bora za uchunguzi wa magonjwa na kuwapunguzia adhan a gharama zingine walizokuwa wanapata kwa kupeleka wagonjwa nje ya nchi na kwenye hospitali zilizo mbali.

"Vifaa tutakavyofunga katika jengo hili ni CT-Scan ambayo Serikali ya awamu ya sita imeshainunua hivyo inasubiria jengo kukamilika ifungwe, mashine ya MRI inayokadiriwa kuwa na thamani ya Bilioni 2.5 , ununuzi wa kipimo cha mamoghraphy cha uchunguzi wa saratani ya matiti na uchunguzi kwa njia ya "fluoroscopy" pamoja na huduma za tiba ya masafa za kiradilojia (Teleradiology).huu ni uwekezaji mkubwa wa Serikali ya awamu ya sita" anasema "big up" kwa Mhe.Dkt Samia Rais wetu na Serikali anayoiongoza.



Mchoro wa jengo la Utawala katika Hospitali Maalum ya Taifa ya Magonjwa Ambukizi Kibong'oto litakavyokuwa pindi ujenzi utakapokamilika



Jengo la kisasa la uchunguzi kwa njia ya mionzi pamoja na mawimbi sauti linalojengwa katika hospital ya Kibong'oto ambalo linagharimu Bilioni 8.1 (Ujenzi Bilioni 3.1 vifaa bilioni 5)

# Hospitali ya Taifa Kibong'oto yazidi kupaa kimataifa

**UJENZI WA MTAMBO WA KUZALISHA HEWA TIBA OKSIJENI.**

Mkurugenzi huyo anabainisha kuwa, kwa sasa Hospitali ya Kibong'oto ina mpango wa kujenga na kusimika mtambo wa kuzalisha hewa tiba ya Oksijeni unakadiriwa kugharimu zaid ya kiasi cha shilingi Bil 1.2 ambapo kipindi cha ugonjwa wa COVID 19, nchi iliingia katika wakati mgumu wa upungufu wa hewa tiba ya oksijeni kutokana mahitaji kuwa makubwa kuliko kawaida.

Ujenzi wa mtambo huo utakapokamilika utaisaidia Serikali na Hospitali yetu ya Kibong'oto kuokoa zaidi ya Milioni 500 ambazo zimekuwa zikitumika kwa ajili ya kununua Oksijeni kila mwaka, pia kutasaidia upatikanaji wa Oksijeni na kuhudumia hospitali nyingine za karibu zenye uhitaji kwa gharama nafuu.

Serikali ya awamu ya sita chini ya Mhe. Dkt Samia iliandika andiko la mpango mkubwa ambapo kama nchi ilipata mkopo Trilioni 1.3 ambazo zimewezesha kuboresha hospitali za mikoa yote nchini kuzifungia mashine za CT-Scan, huku hospitali za kanda zikifungiwa mashine za MRI, Ununuzi wa Magari ya kubebea wagonjwa, Ujenzi wa majengo ya dharura na wagonjwa mahututi na ununuzi wa vifaa nchini ambayo yalikuwa hayapo Hivi sasa Hospitali zote za wilaya nchini zimefungiwa mashine za X-RAY za kidigitali na pia kwenye baadhi ya vituo vya afya ikiwemo ununuzi wa mashine za Utrasound alisema Dkt Subi kwani yeye pia alishiriki katika uandishi wa andiko hilo kwa ridhaa ya Mhe. Dkt Samia ambapo haya ni mapinduzi makubwa kwa sekta ya afya nchini na barani afrika kwa muda mfupi alishika madaraka kama Rais wa nchi.

**UJENZI WA CHUMBA CHA WAGONJWA MAHUTUTI (ICU) LENYE THAMANI YA BILIONI 1.2.**

Katika kuhakikisha kuwa huduma zinazotolewa katika hospitali hiyo zinakidhi hadhi ya kimataifa Serikali ya awamu ya sita imefanikiwa kujenga jengo la kisasa la Wagonjwa mahututi lenye uwezo wa kuwahudumia wagonjwa 20 kwa pamoja ambapo thamani yake ni Bilioni 1.2.

Mkurugenzi huyo anasema kuwa, thamani ya ujenzi ni milioni 526, huku thamani ya ununuzi wa vifaa ikiwa ni zaidi ya milioni 727, pamoja na mafunzo ni milioni 28, ambapo jengo hilo ni la kisasa ambapo wameliwekea mfumo maalum wa kupitishia hewa tiba ya Oksijeni hivo hawatoingiza mitungi ya gesi katika jengo hilo mara watakapokamilisha ujenzi wa kinu cha kuzalisha hewa tiba ya oksjien hivi karibuni kwani mtambo wa kuzalisha hewa tiba ya oksijeni umeshanunuliwa tayari.

"Mgonjwa atakayekuwa anahitaji Oksijeni atakuwa anaipokea ukutani kupitia paipu maalum zilizowekwa pia jengo hili limefungwa vifaa vya kisasa vya ufuatiliaji wa maendeleo ya mgonjwa akiwa mahututi itasoma moyo wake unaendaje na kiwango chake cha oksijeni mwilini kikoje na presha na joto lake likoje".

Anaendelea kubainisha kuwa, vifaa hivo vya kisasa vitasidia katika kuokoa maisha ya wagonjwa ambapo inawezekana wangepoteza uhai kwa kutopata huduma stahiki za matibabu

Anasema kuwa, Hospitali hiyo ya Kibong'oto haijawahi kuwa na majengo hayo matatu tangu ianzishwe miaka 98 iliyopita yaani kuwa na maabara ya kisasa, jengo la uchunguzi wa mionzi la kisasa na jengo la wagonjwa mahututi la kisasa hivyo ni ukombozi mkubwa kwa Tanzania.



Mkurugenzi Dkt. Leonard Subi akionyesha moja ya vyumba ambacho kitafungwa mashine maalum ya MRI



Jengo la wagonjwa mahututi (ICU) lililojengwa katika hospitali ya Kibong'oto lenye gharama ya Bilioni 1.2 linauwezo wa kuchukua wagonjwa 20 kwa pamoja

**UANDAAJI WA MPANGO WA MATUMIZI YA ARDHI EKA 95.5 (MASTER PLAN)**

Mkurugenzi huyo anabainisha kuwa, Hospitali ya Taifa ya Kibong'oto imeandaa Master plan na mpango wa matumizi bora ya ardhi ambapo wanalo eneo la hekari 95.5 ambalo limeshapimwa na hati miliki wanayo ambapo wameweza kuzikamilisha hati hizo ndani ya kipindi cha awamu ya sita na matarajia ni kuitekeleza ndani ya kipindi cha miaka10 ijayo.

Anasema kuwa, katika mpango huo wa matumizi bora ya ardhi wanatarajia kuwa pia kujenga Jengo la utafiti na mafunzo ambapo litakuwa jengo la gorofa sita au zaidi, ambalo litatumika kutoa mafunzo kwa Watanzania hususani wanaotoka Mikoa yote nchini kwa kuwajengea uwezo wa namna ya kudhibiti magonjwa ambukizi, Ujenzi wa Nyumba za Watumishi, Hosteli, Uwanja wa Michezo, "Shopping Mall", Kituo kidogo cha polisi n.k ili kurahisha upatikanaji wa huduma n.k .



Ukarabati na upanuzi wa njia maalum za kupitia wagonjwa na watu wengine katika hospitali ya Kibong'oto

**HUDUMA ZA MKOBA ZA UCHUNGUZI WA MAGONJWA**

Mkurugenzi huyo anasema kuwa, kwa sasa Kibong'oto inalo gari maalum la kuhudumia wagonjwa ambalo lina mfumo wa X-RAY na mashine ya kisasa ya uchunguzi wa vimelea vya kifua kikuu kwa njia ya vina saba(Gene Expert) ambalo lilinunuliwa ndani ya Serikali.

Anasema kuwa, wamekuwa wakitumia gari hilo kuwafikia wananchi mbalimbali wakiwemo wachimbaji wa Madini pamoja na kuzifikia jamii za wachimbaji madini kwani zimekuwa zikiathirika sana na ugonjwa wa kifua kikuu na athari za uchimbaji wa madini unaotokana na vumbi.

Mkurugenzi huyo anasema kuwa, Hospitali ya Kibong'oto imekuwa ikishiriki katika tafiti za kimataifa ambapo hivi sasa wanaongoza kwenye utafiti wa kufupisha tiba ya kifua kikuu cha kawaida katika nchi sita za Afrika kutoka miezi sita kwa mgonjwa kifua kikuu cha kawaida kwenda miezi minne.

Anasema kuwa, kupitia mapato ya ndani wameendelea kuwajengea uwezo watumishi wake ambapo kwa tayari wamesomesha watumishi saba katika ngazi za Uzamivu (Phd) ambapo watatu walishahitimu na Wengine wako kwenye hatua mbalimbali kuhitimu ili kuhakikisha huduma inayotolewa inakuwa bora nay a kisayansi. Aidha pia Serikali imepeleka watumishi wengine wengi toka Hospitali mbalimbali Tanzania na Kibong'oto ikiwemo ambapo wanasoma ngazi ya uzamili (Masters) kupitia fedha za Dkt Samia ndani na nje ya nchi.

Aidha Mkurugenzi anasema katika kipindi cha miaka mitatu ya Mh.Rais Samia jumla ya watu 57 wameweza kuajiriwa ambao ni ,madaktari 11,manesi 19,Biomedical2,Labtechnician 6 na wengine 15.

Anaendelea kusema kuwa, kwa sasa wanatumia gharama za Serikali kuwafuata wagonjwa katika mikoa mbalimbali ya Tanzania bara na visiwani na kuwalipia gharama za vipimo wanapokuwa wanapata matibabu ya ugonjwa wa kifua kikuu na wale wanaobainika kuwa na ugonjwa wa kifua kikuu sugu na kushindikana kupata tiba huko walipo wamekuwa wakisafirishwa kwa gharama za serikali mpaka hospitali ya Kibong'oto na kupatiwa huduma za matibabu na chakula bure.Hii ndiyo Serikali inayojali wananchi wake amesema Dkt Subi

Aidha Mkurugenzi huyo anasema kuwa, kwa sasa wameanzaUkarabati na ujenzi wa ghorofa mbili wa jengo la utawala ambapo wanatarajia kugharimu kiasi cha shilingi Bil 2.4

Anasema kuwa, Serikali ya awamu ya sita imeamua kusogeza huduma za kibingwa na uchunguzi wa magonjwa karibu na wananchi na hili limeonekana kwa vitendo.




Gari maalum la kisasa la kuhudumia wagonjwa wa Kifua kikuu ambalo ndani linamfumo wa X-ray na mashine ya kisasa ya uchunguzi wa vimelea vya Kifua kikuu.

# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

## HOSPITALI YA RUFAA YA KANDA

# CHATO



Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan

# HOSPITALI YA RUFAA YA KANDA CHATO



Mkurugenzi mtendaji wa hospitali ya Rufaa ya Kanda Chato, Dk.Brian Mawalla









# HOSPITALI YA RUFAA YA KANDA CHATO YAJIVUNIA MAFANIKO LUKUKI MIAKA MITATU YA RAIS MHE. DKT. SAMIA SULUHU



**Mkurugenzi mtendaji wa hospitali ya Rufaa ya Kanda Chato, Dk.Brian Mawalla**

**Na MWANDISHI WETU,** *Chato.*

HOSPITALI ya Rufaa ya Kanda Chato (CZRH), iliyopo mkoani Geita, ilianza utoaji huduma za afya tangu Julai 30, mwaka 2021, ikiwa na uwezo wa kufanya vipimo kumi na tatu vya maabara, kipimo cha X-Ray pamoja na Ultra- Sound tu.

Hali hiyo ilipelekea wananchi kupewa rufani kwenda kufuata vipimo mbali na mkoa wa Geita, na wakati mwingine walikuwa wanalazimika kwenda mbali na kanda hiyo, ili kupata vipimo ambavyo havikuwa vikipatikana, jambo ambalo lilionekana kuwa na usumbufu kwa wagonjwa na hata kuwaongezea gharama wananchi kusafiri umbali mrefu.

UHURU ya Kijani ililifanya mahojiano na Mkurugenzi mtendaji wa hospitali ya Rufaa ya Kanda Chato, Dk.Brian Mawalla, kuhusu miaka mitatu ya Rais Dk.Samia Suluhu Hassan, madarakani na uboreshaji wa sekta ya afya nchini.

"Hadi kufikia sasa kwa juhudi za serikali ya awamu ya sita inayoongozwa na Rais Dk.Samia, hospitali ya Rufaa ya Kanda Chato inao uwezo wa kufanya vipimo vya MRI, CT Scan, ECHO (kipimo cha utendaji wa moyo), ECG (kipimo cha umeme wa moyo), pamoja na vipimo zaidi ya 120 katika maabara yetu hali ambayo imepelekea huduma kuimarika lakini pia kupunguza gharama kwa wananchi kwenda kupata matibabu mbali na maeneo ya kanda ya ziwa na hata nje ya nchi" alisema.

Dk.Mawalla aliongeza mafanikio hayo ni sehemu ahadi zilitolewa na Rais Dk.Samia ambaye akiwa katika ziara yake ya kikazi mkoani Geita, alifika katika hospitali hiyo na kukagua miradi ya maendeleo pamoja na utoaji huduma ndani ya hospitali hiyo.

Kwa mujibu wa Mkurugenzi mtendaji huyo, Rais Dk.Samia aliahidi kuendelea kuijenga hospitali ya Rufaa ya Kanda Chato, kama ilivyolengwa kujengwa na mtangulizi wake, Rais wa awamu ya Tano, Hayati Dk.John Pombe Magufuli, na sasa wananchi wa mkoa wa Geita na kanda ya Ziwa kwa jumla, wananufaika na ahadi hiyo kwa kupata vipimo vyote ndani ya mkoa huo.

**JUHUDI**

**Hadi kufikia sasa kwa juhudi za serikali ya awamu ya sita inayoongozwa na Rais Dk.Samia, hospitali ya Rufaa ya Kanda Chato inao uwezo wa kufanya vipimo vya MRI, CT Scan, ECHO (kipimo cha utendaji wa moyo), ECG (kipimo cha umeme wa moyo)**

### AJIRA ZA WATUMISHI WA KUDUMU.

Dk.Mawalla alisema katika kipindi cha utawala wa Rais Dk.Samia, ,hospitali imepata watumishi 248 wote wakiwa ni waajiriwa wa kudumu, ukilinganisha na hapo mwanzo ambapo hospitali ilianza kutoa huduma ikiwa na watumishi 128.

Aliongeza kwa idadi hiyo ya watumishi, ilikuwa inawawia vigumu katika kuwahudumia wagonjwa, na watumishi wengine walilazimika kuingia usiku na mchana, ili kuhakikisha wanatoa huduma za afya na kuokoa maisha ya wananchi.

"Hii ni faraja kwa hospitali na hata wananchi wanaopata huduma katika hospitali hii, ikidhihirisha kwamba serikali ya awamu ya sita inayoongozwa na Rais Dk.Samia, bado inaendelea kutekeleza ahadi yake ya kuhakikisha hospitali inajengwa kama ilivyokusudiwa, lakini pia huduma zilizokusudiwa kutolewa zinaimarika kwa kuleta wataalamu husika ambao wanatoa huduma ili kuokoa maisha ya wananchi wa Kanda ya Ziwa" alisema.

Mkurugenzi mtendaji wa hospitali ya Rufaa ya Kanda Chato, alisema vile vile wameanzisha huduma za matibabu ya moyo katika kanda ya Ziwa, ICU, EMD, kuchuja na kusafisha damu (Dialysis).

Kwamba serikali ya awamu ya sita, kupitia Wizara ya Afya, imesaidia kukamilika kwa jengo la wagonjwa mahututi (ICU), jengo la wagonjwa wa dharula na kuyawekea vifaa na vifaa tiba, ambavyo vinaendelea kuokoa maisha ya wananchi wanaofika katika hospitali ya Rufaa ya Kanda Chato.

Dk.Mawalla alisema



**Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dk. Samia Suluhu Hassani akipata maelezo kutoka kwa Mkurugenzi mtenda hospitali ya Rufaa kanda ya Chato Dkt. Brian C Mawalla,wakati alipotembelea Hospitali Hiyo.**



**Mashine ya MRI**



**Wataalamu wa afya wakifanya vipimo kutoka kwa mgonjwa.**



**Mashine ya CT Scan**

# HOSPITALI YA RUFAA YA KANDA CHATO YAJIVUNIA MAFANIKO LUKUKI MIAKA MITATU YA RAIS MHE. DKT. SAMIA SULUHU





Waziri wa Afya Mhe. Ummy Mwalimu akikagua vifaa tiba katika Hospitalini hapo.

hayo ni mapinduzi makubwa, yanayofanywa na serikali katika sekta ya afya kwani hapo mwanzo wagonjwa wa dharula na mahututi, walilazimika kupewa rufani kwenda mbali kufuata huduma sehemu ambayo wanaweza kuhudumiwa haraka.

Yote hiyo ilikuwa ni kwa kwa ajili ya kuokoa maisha ya wananchi, hali iliyopelekea wakati mwingine kuwapoteza baadhi ya wagonjwa (kufariki), lakini hadi sasa ujenzi wa majengo ya (EMD), (ICU) na Radiolojia, yamekamilika kwa asilimia mia moja yakiwa na vifaa vya kisasa kuweza kutoa huduma hizi.

### HUDUMA ZA KIBINGWA ZA MATIBABU YA MAGONJWA YA MOYO.

Dk.Mawalla alibainisha kuwa kabla ya uanzishwaji wa kitengo cha uchunguzi, na matibabu ya magonjwa ya moyo katika hospitali ya Rufaa ya Kanda Chato, wananchi wa mikoa ya Geita, Kagera, Mwanza, Kigoma na nchi za jirani, walilazimika kutibiwa katika taasisi ya moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI), iliyopo jijini Dar es Salaam.

"Hii ilikuwa changamoto hasa kwa wananchi wenye kipato cha chini, ambao wanahitaji matibabu ya magonjwa ya moyo, lakini gharama za usafiri pamoja na malazi kuwa juu,wananchi wengi walipoteza maisha" alisema Dk.Mawalla.

Aliongeza kwa kuliona hilo, serikali ya Rais Dk.Samia, kupitia Waziri wa Afy, Ummy Mwalimu, aliiagiza taasisi ya moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI), kuhakikisha inaisimamia hospitali ya Rufaa ya Kanda Chato, kutoa huduma za kibingwa na bingwa bobezi za magonjwa ya moyo kwa wananchi wa Kanda ya Ziwa hadi hapo hospitali hiyo itakapoweza kujitegemea.

Hiyo ni pamoja na Hospitali ya Rufaa ya Kanda Chato(CZRH), kuwa na jengo maalumu la uchunguzi pamoja na upasuaji kwa wagonjwa, wanaohitaji huduma za matibabu ya magonjwa ya moyo, ndani ya Hospitali ya Rufaa ya Kanda Chato (CZRH).

Kupitia agizo hilo, CZRH ilianza utoaji huduma za uchunguzi na matibabu ya magonjwa ya moyo mwaka 2023, huduma hiyo ikisimamiwa na Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI).

"Hadi sasa CZRH imeweza kutoa huduma kwa wagonjwa zaidi ya 1,000, na wengine wakiendelea kupata uangalizi wa karibu pamoja na kuhudhuria kliniki, iliyoanzishwa ndani ya hospitali ikiwapunguzia gharama za kusafiri kwenda taasisi ya moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI)" alisema Dk.Mawalla.

Dk.Mawala alisema wanatarajia ndani ya miaka mitatu ijayo, hospitali ya Rufaa ya Kanda Chato itakuwa tayari ikijitegemea, katika utoaji wa huduma za kibingwa na bingwa bobezi za uchunguzi na matibabu ya magonjwa ya moyo, kwa wananchi wa mikoa ya kanda ya Ziwa, lakini pia ikitoa huduma za kuchuja na kusafisha damu kwa wagonjwa wa Figo.

### SHUKRANI

**Tunaishukuru serikali ya Rais Dk.Samia, kwa kutenga fedha za maendeleo kwa ajili ya ujenzi ambao kukamilika kwa majengo haya, kunaenda kupunguza msongamano wa wagonjwa pamoja na kuimarisha utoaji huduma za kibingwa na bobezi ndani ya kanda ya Ziwa**

### MAGARI YA KUBEBEA WAGONJWA.

Alisema serikali chini ya Rais Dk.Samia, imeendelea kuboresha sekta ya afya, ambapo hospitali ya Rufaa ya Kanda Chato ni moja ya hospitali iliyopata gari moja (1), la kubebea wagonjwa pamoja na gari moja (1) la kutumia katika shughuli za kiutawala.

Gari ya kubebea wagonjwa linaenda kutatua changamoto ambazo kama hospitali imekutana nazo kutokana na ukosefu wa magari ya kubebea wagonjwa hapo awali. Ilichukua zaidi ya masaa mawili kutafuta gari kwa ajili ya rufaa za wagonjwa jambo ambalo lilikuwa usumbufu hasa kwa wananchi.

Dk.Mawalla alisema hadi sasa katika kipindi cha miaka mitatu ya Rais Dk.Samia, inaendelea kutekeleza miradi mbalimbali ndani ya hospitali ya Rufaa ya kanda Chato, ambayo hadi sasa ipo katika hatua za mwisho.

Kwa mujibu wa Mkurugenzi mtendaji wa CZRH,hadi kukamilika kwa miradi hiyo, hospitali hiyo itakuwa na uwezo wa kuwahudumia wananchi kuanzia 800 hadi 1,200 kwa siku, jambo ambalo litakuwa ni mafanikio makubwa.

Aliitaja miradi inayoendelea kutekelezwa hadi sasa kuwa ni ujenzi wa jengo la wodi ya kulaza wagonjwa ambao umefikia asilimia 82, na baada ya kukamilika kwa jengo hilo hospitali itaweza kulaza wagonjwa 201 kwa mara moja.

"Pia ujenzi wa uzio wa hospitali hadi sasa umefikia asilimia 75, ujenzi wa jengo la kuhifadhi maiti (Mortuary), jengo la kutakasa vifaa na vifaa tiba (CSSD), jengo la kufulia (Laundry),ujenzi wa jengo na usimikaji wa mitambo ya hewa tiba (Medical Oxygen Plant), ambalo lipo hatua za mwisho kukamilika" alisema Dk.Mawalla.

### MIPANGO MKAKATI YA TAASISI YA BAADAE

Alisema CZRH inaendelea kujipanga, kuhakikisha inakuwa kinara katika kutoa huduma za matibabu ya kibingwa na bingwa bobezi, katika kanda ya Ziwa na Nchi jirani kwa upande wa magonjwa ya moyo na upasuaji kwa njia ya matundu madogo (Endoscopic surgery)

Kuendelea na mchakato wa kupata ithibati (Accreditation) ya kitaifa na kimataifa katika utoaji huduma za afya

### NENO KWA SERIKALI YA AWAMU YA SITA CHINI YA RAIS DK.SAMIA.

Dk.Mawalla alisema CZRH inaendelea kukua, na kujipambanua katika utoaji wa huduma za afya kwa wananchi wa kanda ya Ziwa na kuwa maendeleo hayo ni pamoja na juhudi zinazofanywa na serikali katika kuhakikisha vifaa vinavyoletwa ni vya kisasa kuweza kuwahudumia wananchi huku gharama za matibabu zikipungua ukilinganisha na hapo mwanzo.

"Tunaishukuru serikali ya Rais Dk.Samia, kwa kutenga fedha za maendeleo kwa ajili ya ujenzi ambao kukamilika kwa majengo haya, kunaenda kupunguza msongamano wa wagonjwa pamoja na kuimarisha utoaji huduma za kibingwa na bobezi ndani ya kanda ya Ziwa" alisema Dk.Mawalla.





Mtaalamu akifanya vipimo

NHIF NDANI YA MIAKA 3 YA SERIKALI YA AWAMU YA SITA

# Sheria ya Bima ya Afya kwa wote yapita

**>>NDOTO** ya Matibabu Bora kwa kila Mwananchi Kutimia
**>>NHIF** Yafungua zaidi Milango Kuwafikia Wananchi
**>>YAIMARISHA** Mifumo Utambuzi Wanachama

NA MWANDISHI WETU

NI miaka mitatu chini ya uongozi wa Serikali ya Awamu ya Sita ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inayoongozwa na Mhe. Samia Suluhu Hassan ambaye alishika nafasi hiyo Machi 18, 2021. Katika kipindi hiki, mageuzi makubwa yamefanyika katika nyanja mbalimbali na yameleta mafanikio makubwa katika utaoji wa huduma kwa jamii ikiwezo ya kiuchumi, kijamii na kisiasa.

Kwa upande wa Sekta ya Afya hususan suala la Bima ya Afya, Rais aliweka kipaumbele kikubwa katika kuhakikisha wananchi wanapata huduma za matibabu kupitia vituo vya kutolea huduma ambavyo vimeboreshwa miundombinu yake lakini pia upatikanaji wa huduma za dawa, vifaa tiba na vitendanishi.

Pamoja na maboresho hayo makubwa kwenye sekta ya afya katika uongozi wake, Mhe. Rais pia amekuwa mhamasishaji mkubwa wa wananchi kujiunga na Bima ya Afya kupitia Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya ili waweze kupata huduma kwa utaratibu rahisi na kuondokana na changamoto ya kukosa huduma kutokana na kikwazo cha fedha.

Kwa dhamira hiyo ya Kiongozi Mkuu wa nchi, Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Novemba 1, 2023 lilipitisha kwa kishindo Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote ambayo utekelezaji wake utakwenda kutimiza ndoto ya upatikanaji wa huduma bora za matibabu kwa wananchi bila kikwazo cha fedha.

Ndani ya miaka hiyo mitatu ya Mhe. Rais Samia, Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya, umetekeleza mambo mbalimbali ambayo yamekuwa na mafanikio makubwa katika kuwapatia wananchi huduma za matibabu. Mafanikio hayo ni pamoja na:-

**KUPITISHWA KWA SHERIA WA BIMA YA AFYA KWA WOTE**

Ukiwa mdau muhumu katika Muswada wa Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote, Mfuko umeshiriki kikamilifu katika maandalizi ya muswada huo ambao Sheria yake imepitishwa kwa ajili ya kuanza utekelezaji mara Serikali itakapokamilisha maandalizi muhimu na kutangaza kwa umma. Muswada huo utawezesha kundi kubwa la wananchi kuwa na uhakika wa kupata huduma za matibabu bila kikwazo cha fedha kuimarisha uboreshaji wa huduma katika vituo vya kutolea huduma za afya vya Umma na binafsi ikiwa ni pamoja na kuimarisha zaidi upatikanaji wa dawa, vitendanishi na vifaa tiba.

Sheria hii inatambua na kuwezesha kupatikana kwa huduma za bima ya afya kwa makundi yote ikiwemo Watumishi wa Umma na wa sekta binafsi, waliojiajiri wenyewe katika sekta isiyo rasmi na wananchi wasio na uwezo. Aidha, wakati sheria hiyo imebainisha watumishi wa umma kusajiliwa na skimu ya umma, imetoa uhuru kwa watumishi wa sekta binafsi na wananchi wengine kuchagua skimu ya kujiunga kati ya umma na za binafsi.

Kwa upande wa wananchi wasio na uwezo ambao ni jumla ya wananchi milioni 15, Serikali inaanzisha mfuko rasmi kwa ajili ya kuwahudumia hivyo hakuna



*Dk. Samia Suluhu Hassan*
*Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania*

mwananchi ambaye atakuwa nje ya mfumo wa bima ya afya.

**UNGEZEKO LA WANUFAIKA WA NHIF**

Kila Mtanzania sasa amewekewa utaratibu wa kujiunga na kunufaika na huduma za NHIF ili kuhakikisha anapata huduma za matibabu bila kikwazo cha fedha. Idadi ya wanachama wanufaika iliongezeka kutoka 691,774 mwaka 2001/2002 wakati Mfuko unaanza hadi kufikia wanufaika 4,987,292 mwezi Disemba 2023 sawa na asilimia 8.3 ya Watanzania wote. Katika kipindi cha Julai, 2021 hadi Septemba 2023 ambacho ni kipindi cha ndani ya miaka mitatu ya Serikali ya Awamu ya Sita, Mfuko umefanikiwa kuwa na ongezeko wanufaika wapya 583,711.

**KUONGEZA WIGO WA VITUO VYA HUDUMA**

Mfuko umeendelea kuongeza wigo wa vituo vya huduma kwa wanachama wake. Jumla ya vituo 498 vimesajiliwa ndani ya miaka mitatu ya uongozi wa Mhe. Rais Samia ambapo mpaka sasa wanachama wanahudumiwa katika jumla ya vituo 9,467 vilivyopo Tanzania Bara na Zanziba. Kati ya vituo hivyo, asilimia 72 ni vituo vinavyomilikiwa na Serikali, asilimia 19 vinamilikiwa na watu binafsi na asilimia 9 ni vituo vinavyomilikiwa na Madhehebu ya Dini.

**URAHISISHAJI WA HUDUMA KUPITIA MIFUMO YA TEHAMA**

Matumizi ya TEHAMA ndani ya NHIF yameendelea kuimarishwa ambapo ndani ya miaka mitatu ya Mhe. Rais, Mfuko umefanikiwa kuimarisha mifumo ya uwasilishaji na uchakataji wa madai kwa watoa huduma za matibabu wanaohudumia wananchama wa NHIF (Claim Management Information System), mfumo wa usajili wa wanachama na uwasilishaji wa michango (Advanced Membership Management Information System), mfumo wa usajili wa vituo vya kutolea huduma, mfumo wa usimamizi wa masijala (Document Management System – e office), mfumo wa usimamizi wa rasilimali za Mfuko (Enterprises Resource Management System). Aidha, mfumo wa uwasilishwaji wa madai ya watoa huduma kwa njia ya mtandao mara baada ya mwanachama kupata huduma (Online claim submission na online e-claim) umeimarisha huduma na kupunguza gharama za uendeshaji kwa pande zote.

Katika jitihada za kuwafikia wananchi wengi zaidi na kurahisisha huduma za usajili wa wanachama, Mfuko umeendelea kuimarisha utaratibu rahisi wa kidigitali ambao unamwezesha mwanachi kujisajili au kuhuisha uanachama wake kwa kutumia simu ya mkononi hivyo kutokuwa na ulazima wa kufika kwenye ofisi za Mfuko.

Mfuko umefanikiwa kuanza matumizi wa mfumo wa utambuzi wa wanachama kwa njia ya kibiolojia (Biometric Identification System) za vidole na sura kabla ya kupata huduma katika vituo vya matibabu. Hadi kufikia Desemba 2023, vituo takriban 434 vinatumia mfumo huu kutambua wanachama kabla ya kupata huduma. Aidha kwa sasa Wanafunzi wa vyuo vikuu wanapata huduma kupitia namba zao za NIDA hivyo kutolazimika kuwa na kitambulisho cha matibabu cha NHIF.

**KUSOGEZA HUDUMA ZA MFUKO KARIBU NA WANANCHI**

Katika jitihada za kuhakikisha unarahisisha upatikanaji wa huduma zake kwa wananchi wengi zaidi hasa tunapoelekea kwenye utekelezaji wa Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote, Mfuko umeweka mkakati wa kufungua ofisi zake karibu zaidi na maeneo ya watu kwa kuanza na maeneo yenye watu wengi. Kwa kipindi cha miaka hii mitatu Mfuko umefungua ofisi mpya katika maeneo ya Kigamboni, Gongolamboto na Mbezi Magufuli Stand ambazo zimefanya idadi ya ofisi katika Jiji la Dar es Salaam kuwa tano.

**KUSIMAMIA UHAI NA UENDELEVU WA MFUKO**

Mfuko umeendelea kulinda uhai wa Mfuko kwa kuweka mifumo imara ili kuongeza ufanisi katika utendaji lakini pia kuimarisha mbinu za kuthibiti na kupambana na vitendo vya udanganyifu. Mfuko umeendelea kufanya uchunguzi wa kina kwa watoa huduma, waajiri, wanachama na watumishi wa Mfuko ili kubaini wanaojihusisha na vitendo vya udanganyifu.

Katika kipindi hiki cha miaka mitatu, Mfuko umefanikiwa kufanya jumla ya chunguzi 276 ambazo zimefanikisha kuokoa jumla ya Shilingi Bilioni 25.93 kutoka kwa waliobainika kufanya udanganyifu.

Aidha Mfuko umechukua hatua mbalimbali kwa wanaobainika kufanya udanganyifu kwa Mfuko zikiwemo za kusitisha mikataba na Vituo 42 vya matibabu, kusitisha mikataba na waajiri watano (5), Kuwafikisha wanataaluma 150 katika Mabaraza yao kwa hatua zaidi, kusitisha matumizi ya kadi 389 za wanachama, kuchukua hatua za kisheria kwa wanachama 61 na kuwafikisha wanachama 118 na vituo 29 kwenye Taasisi ya Kupambana na Kuzuia Rushwa.

**ELIMU KWA UMMA**

Katika kipindi cha miaka mitatu, Mfuko umeendelea kufikisha elimu kwa wadau wake kwa kutumia mbinu mbalimbali ikiwemo ya mikutano na wadau wake ambao ni pamoja na wanachama, watoa huduma, waajiri, vyama vya wafanyakazi, waandishi wa habari, Waheshimiwa Wabunge na viongozi wa madhehebu ya dini.

Njia zingine ni pamoja na kushiriki katika vipindi mbalimbali vya runinga na radio, kuandaa na kurusha vipindi vya elimu na uhamasishaji kupitia mitandao ya kijamii, radio za kijamii, vyombo vya habari vya kitaifa na kimataifa. Aidha Mfuko umerahisisha upatikanaji wa taarifa na kutatua changamoto za wanachama wake kupitia Kituo chake cha Huduma kwa Wateja ambacho hufanya kazi saa 24 siku zote za wiki.

Katika kipindi hiki cha miaka mitatu, Mfuko pia umefanikiwa kushiriki Maonesho ya Kitaifa ikiwemo Sabasaba, Nane Nane, Wiki ya Vijana na mengine lakini pia Maonesho ya kimkoa kwa lengo la kuwafikia wananchi katika maeneo yao na kuwapa elimu ya bima ya afya na faida za kujiunga. Mafanikio makubwa yaliyopatikana ni kuongezeka kwa ari ya wananchi ya kujiunga na kutumia bima ya afya katika kupata huduma za matibabu.

**UWEZESHAJI WA VITUO VYA MATIBABU KUBORESHA HUDUMA**

Mfuko katika kipindi cha miaka mitatu ya Serikali ya Awamu ya Sita, umeendelea kuunga mkono juhudi za Serikali za uboreshaji wa huduma za matibabu kupitia mpango wake wa Mikopo ya Vifaa Tiba na Ukarabati wa Majengo. Kupitia mpango huo, jumla ya Shilingi Bilioni 13.6 zimetumika kuwezesha uboreshaji wa vituo 93 vya kutolea huduma na maboresho hayo husaidia vituo husika kuongeza mapato kutokana na upatikanaji wa huduma.

Akizungumzia mafanikio haya kwa ujumla wake, Mkurugenzi Mkuu wa NHIF, Bw. Bernard Konga amepongeza juhudi za Serikali ya Awamu ya Sita chini ya uongozi wa Mhe. Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuimarisha sekta ya afya nchini na azma yake ya kuhakikisha kila Mtanzania anakuwa na bima ya afya ili kuwa na uhakika wa kupata huduma za matibabu bila kikwazo chochote.

"Mfuko umejipanga kuhakikisha makundi yote ya wananchi yanakuwa na utaratibu rahisi wa kujiunga hasa kupitia mifumo ya TEHAMA na kunufaika na bima ya afya katika kutekeleza azma ya Serikali ya bima ya afya kwa wote na Ilani ya Chama cha Mapinduzi. Nitumie fursa hii kuwahimiza wananchi wajiunge na NHIF ambayo ina wigo mpana wa huduma lakini pia wigo mpana wa vituo vya kupata huduma kwa uhakika wa matibabu" amesema Bw. Konga.




*MKURUGENZI Mkuu wa NHIF Bernard Konga*



*WAZIRI wa Afya Mhe. Ummy Mwalimu akimwangalia mtoto wodini.*

# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
## WIZARA YA AFYA
## HOSPITALI YA RUFAA MKOA WA
# GEITA






RAIS Dkt. Samia Suluhu Hassan.



WAZIRI wa Afya Ummy Mwalimu



Dkt. John Jingu Katibu Mkuu

# Hospitali ya Rufaa Mkoa wa Geita yajivunia utoaji wa huduma bora za Afya, Miaka mitatu ya Rais Mhe. Dkt. Samia

Anuani ya Posta: S.L.P 40 - Geita
Simu: +255 759 695 972
Simu ya Mkononi: +255 765 155 269
Barua Pepe: hospital@geitarrh.go.tz

MIAKA MITATU YA RAIS DK. SAMIA NA UBORESHAJI SEKTA YA AFYA NCHINI

# Hospitali ya Rufaa Mkoa wa Geita yajivunia utoaji wa huduma bora za Afya, Miaka mitatu ya Rais Mhe. Dkt. Samia

MACHI 19, 2024 Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan anatimiza miaka 3 katika uongozi wake. Katika kipindi cha miaka mitatu ya utawala wake tumeshuhudia mabadiliko chanya kwa ustawi wa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Geita (Geita RRH) na sekta ya afya. Tumeshuhudia mapinduzi makubwa katika utoaji na upatikanaji wa huduma za afya.

Kupitia Serikali ya awamu ya sita, Mhe. Rais Dkt. Samia amefanya maboresho makubwa na ya kipekee katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Geita ambayo ilipanda hadhi na kuwa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa mwaka 2016. Kwa sasa hospitali hii inakadiriwa kuhudumia wananchi takribani milioni tatu katika Mkoa wa Geita, na kuifanya hospitali hii kutegemewa na wananchi wa Mkoa wa Geita katika utoaji wa huduma za Afya hususani za kibingwa.

Kutokana na uhitaji mkubwa wa upatikanaji wa huduma za afya na huduma za kibingwa, Serikali ya awamu ya sita inayoongozwa na Mhe. Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan imefanya uwekezaji na kuboresha utoaji huduma katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Geita kwa kufanya yafuatayo;

**Ajira mpya za watumishi wa Afya:**

Katika Uongozi wa Mhe. Rais Dkt.Samia, Hospitali ya Mkoa wa Geita (GRRH) ni moja ya hospitali zilizofanikiwa kupata watumishi wa afya zaidi ya 90 ambalo ni sawa na ongezeko la asilimia 30. Ongezeko hili la watumishi limeondoa uhaba wa watumishi hasa katika utoaji wa huduma ukilinganisha na hapo mwanzo. Katika kipindi hiki Hospitali imefanikiwa kupata madaktari bingwa, madaktari wa kawaida, wauguzi, na wahandisi wa vifaatiba.

Wataalamu hawa wamesaidia kuimarisha utoaji wa huduma bora na matibabu katika hospitali na kuongeza uwezo wa utoaji wa huduma za kibingwa za afya ambazo hazikuwepo hapo awali; na sasa imekuwa ni tegemeo kwa wananchi katika huduma za kibingwa.

Katika kipindi hiki cha miaka mitatu serikali ya awamu ya sita imeweza kuongeza huduma za kibingwa kutoka aina moja hadi aina saba. Huduma hizi za kibingwa zifuatazo zinapatikana Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Geita; magonjwa ya Akina mama na Uzazi, magonjwa ya Watoto, magonjwa ya Ndani, Upasuaji, Mifupa, Radiolojia, na Pua, Koo na Masikio. Pamoja na kuajiri watumishi, serikali ya Mh. Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan imekuwa ikisomesha madaktari na wataalamu wengine. Mpaka sasa madaktari 10 wako masomoni wakisomea udaktari bingwa katika fani mbalimbali. Madaktari hawa watasaidia kuboresha huduma za kibingwa na kuhakikisha kuwa wananchi wa Mkoa wa Geita wanapata huduma za kibingwa karibu na maeneo yao.



RAIS Dkt. Samia Suluhu Hassan.

**Ujenzi wa majengo haya umefanyika sambamba na upatikanaji wa vifaa vya kisasa ili kuhudumia wagonjwa wa dharura na wagonjwa mahututi. Uwekezaji huu katika eneo la wagonjwa wa dharura na wagonjwa mahututi wa takribani shilingi bilioni 4 unasaidia utoaji huduma bora za kisasa kwa wagonjwa wote wa dharura na wagonjwa mahututi katika Hospitali.**

**Uanzishwaji wa miradi na uboreshaji wa Miundombinu ya Afya:**

Nia ya dhati ya Mh. Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan ni kuboresha miundombinu ya afya hasa katika kuanzisha miradi muhimu ya ujenzi wa majengo ya kutolea huduma.

Katika kipindi hiki serikali ya Mh. Dkt. Samia imejenga majengo ya wagonjwa wa dharura (EMD) na wagonjwa mahututi (ICU). Hapo awali majengo haya hayakuwepo.

Ujenzi wa majengo haya umefanyika sambamba na upatikanaji wa vifaa vya kisasa ili kuhudumia wagonjwa wa dharura na wagonjwa mahututi. Uwekezaji huu katika eneo la wagonjwa wa dharura na wagonjwa mahututi wa takribani shilingi bilioni 4 unasaidia utoaji huduma bora za kisasa kwa wagonjwa wote wa dharura na wagonjwa mahututi katika Hospitali.

Mpaka sasa zaidi wagonjwa 3,000 wamehudumiwa kama wagonjwa wa dharura na wagonjwa mahututi.

Katika eneo la huduma za mama na mtoto serikali ya awamu ya sita ilianza ujenzi la jengo la ghorofa mbili la mama na mtoto, mradi unaotegemewa kugharimu shilingi bilioni kumi na tatu (13). Ujenzi wa mradi huu umefikia asilimia 50, ambapo ukikamilika unatarajia kuwa na vitanda 160 na utasaidia juhudi za Serikali katika kupunguza vifo vya mama wajawazito na watoto wachanga. Hii inaakisi dhamira ya dhati ya Mh. Rais katika eneo la afya ya uzazi.



MGANGA Mfawidhi - Dkt. Mfaume Salum Kibwana.

**WAGONJWA 3,000**

Wamehudumiwa kama wagonjwa wa dharura na wagonjwa mahututi.

**Upatikajiwa Vifaa Tiba vya Kisasa:**

Sambamba na uwekezaji na upatikanaji wa Vifaa katika majengo wagonjwa wa dharura na mahututi Mhe. Dkt. Rais Samia Suluhu Hassan kupitia Wizara ya Afya, amefanikisha ununuzi na usimikaji wa mashineza kisasa za mionzi ili kusaidia huduma za uchunguzi wa magonjwa mbalimbali; mashine hizi yaani mashine ya CT-scan na mashine ya digital X-ray zilisimikwa katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa iliyopo eneo la Magogo.

Uwepo wa mashine ya CT–scan umesaidia hospitali kuhudumia wagonjwa zaidi ya mia tatu hamsini (350). Hapo awali wananchi walilazimika kusafiri kupata kipimo hiki cha CT-scan nje ya Mkoa wa Geita, jambo ambalo lilikuwa ni usumbufu kwa wananchi hasa wa kipato cha chini.

Pia ilikuwa ni mzigo kwa Hospitali kusafirisha wagonjwa kwenda Hospitali ya Kanda kwa ajili ya kipimo hiki. Hii inathibitisha dhamira ya Mhe. Rais Dkt. Samia kuhakikisha wananchi wanapata huduma za



JENGO la mbele la hospital (jengo la wagonjwa wa nje OPD).

MIAKA MITATU YA RAIS DK. SAMIA NA UBORESHAJI SEKTA YA AFYA NCHINI

# Hospitali ya Rufaa Mkoa wa Geita yajivunia utoaji wa huduma bora za Afya, Miaka mitatu ya Rais Mhe. Dkt. Samia



MASHINE ya kisasa ya maabara kwa ajili ya vipimo mbali mbali vya damu (chemistry and hormonal tests).

kibingwa za uchunguzi katika maeneo yao na kuwapunguzia adha na usumbufu wa kusafiri umbali mrefu kufuata huduma hizi za kibingwa za uchunguzi.

Katika kuhakikisha kuwa huduma za kibingwa na ubingwa bobezi zinapatikana kwa wagonjwa wetu, Hospitali imefunga huduma ya tibamtandao (telemedicine) ambapo Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Geita inaweza kuwasiliana moja kwa moja na Hospitali za Kanda au Taifa namna bora ya mgonjwa anayehitaji huduma hizi ili kuhakikisha huduma inatolewa bila mgonjwa kusafiri umbali mrefu.

Katika kipindi cha miaka mitatu ya Mh. Rais Dkt. Samia Hospitali imewezeshwa ujenzi wa mtambo wa kutengeneza hewatiba (Medical Oxygen Plant) ambao umesaidia upatikanaji wa hewatiba muda wote kwa wagonjwa wenye changamoto za upumuaji na wagonjwa na wagonjwa wanaofanyia upasuaji.

Mtambo huu umesaidia pia kusambaza hewatiba kwenye vituo vya kutolea huduma za Afya ngazi ya Msingi vilivyopo Mkoa wa Geita.

Mhe. Rais Dkt. Samia ametoa gari moja kwa hospitali ili kurahisisha shughuli za usimamizi shirikishi na kuhakikisha huduma za afya zinaimarika ndani ya hospitali. Pia hospitali inatarajia kupata gari jipya la kubebea wagonjwa (ambulance) mwaka huu 2024.

## MIPANGO MKAKATI YA HOSPITALI KATIKA USIMAMIZI WA MIRADI NA VIFAA

Katika kuunga juhudi za Serikali ya awamu ya sita inayoongozwa na Mhe. Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, uongozi wa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Geita unaendelea kuandaa mipango ya kuhakikisha upatikanaji wa huduma nyingi za ubingwa na ubingwa bobezi.



JENGO la mama na mtoto ujenzi wake unaendelea.

Mipango ya Hospitali kwa sasa ni kuanza kutoa baadhi ya huduma za ubingwa bobezi kama huduma za kusafisha damu (haemo dialysis), upasuaji na urekebishaji wa maumbile (plastic and reconstructive surgery) na uchunguzi njia ya koo na chakula (endoscopy). Uongozi wa Hospitali unaendelea kuhakikisha Hospitali inatoa huduma bora kwa wananchi wa Mkoa wa Geita ambapo wananchi wote wa Mkoa wa Geita wanahudumiwa bila ubaguzi wa kijinsia au kiuchumi na kuhakikisha makundi maalum katika jamii yanapewa kipaumbele.

**Mhe. Rais Dkt. Samia ametoa gari moja kwa hospitali ili kurahisisha shughuli za usimamizi shirikishi na kuhakikisha huduma za afya zinaimarika ndani ya hospitali. Pia hospitali inatarajia kupata gari jipya la kubebea wagonjwa (ambulance) mwaka huu 2024.**

## SHUKRANI

Uongozi wa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Geita unatoa shukrani za dhati kwa Wizara ya Afya inayoongozwa na Waziri wa Afya Mh. Ummy Mwalimu katika kuhakikisha sekta ya Afya inafanya vizuri ambapo Wizara imekuwa ikiandaa sera na mipango mbalimbali ya sekta ya Afya na kuhakikisha Hospitali inakuwa na miundombinu, vifaa tiba, dawa na vitendanishi pamoja na watumishi ili iweze kutoa huduma bora kwa Watanzania. Pia tunashukuru kwa Serikali ya Mkoa wa Geita na Mh. Mkuu wa Mkoa Ndugu Martin Shigella kwa usimamizi thabiti wa miradi hii ambayo ni utekelezaji wa ilani ya Chama cha Mapinduzi hasa katika sekta ya Afya.

Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Geita inatoa pongezi kwa Mh. Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kutimiza miaka mitatu ya uongozi wake na inashukuru sana juhudi zake binafsi katika kuboresha huduma za Afya nchini Tanzania.

## WITO WETU KWA SERIKALI YA AWAMU YA SITA.

Kutokana na uwekezaji mkubwa ambao Serikali inaendelea kutekeleza hasa katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Geita, ni matumaini yetu miradi inayoendelea ya ujenzi itakamilika kwa wakati ili kusaidia kuongeza ubora wa huduma na kuhakikisha upatikanaji wa huduma za kibingwa katika Mkoa wa Geita.



MTAMBO wa kutengeneza hewa tiba (medical oxygen plant).



KATIBU wa CCM Mkoa Bi. Alexandrina Katabi akiuliza swali juu ya uelewa wa kipimo na mashine ya CT Scan.

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
Wizara ya Afya
**Hospitali ya Rufaa ya Mkoa Mwananyamala**
(MRRH)

# Hospitali ya Mwananyamala inavyochanja mbuga miaka mitatu ya Rais Samia Suluhu

Na ABDUL DUNIA

HOSPITALI ya Mwananyamala ni moja ya hospitali tatu za Rufaa za Mkoa wa Dar es Salaam.

Hospitali hiyo iliyopo Mwananyamala, ndiyo hospitali kubwa zaidi na ya rufaa kwa upande wa manispaa ya Kinondoni na Ubungo.

Jitihada za Rais Dk. Samia Suluhu Hassan katika kuboresha sekta ya afya nchini, zimechangia kwa kiasi kikubwa hospitali hiyo kutoa huduma bora zaidi kwa wananchi wa manispaa hizo mbili.

Kwa mujibu wa Sensa ya watu na makazi ya mwaka 2022, Manispaa ya Kinondoni na Ubungo kwa pamoja, zinakadiriwa kuwa na wakazi milioni 2.2, hivyo basi Hospitali ya Rufaa ya Mkoa ya Mwananyamala inajukumu la kuwahudumia wananchi hao.

Pamoja na idadi kubwa ya watu katika manispaa hizo, lakini Dk. Zavery Benela ambaye ni Mganga Mfawidhi Hospitali ya Rufaa ya Mkoa ya Mwananyamala, alisema hospitali hiyo hivi sasa ina uwezo mkubwa wa kuwahudumia wananchi hao kutokana na maboresho yaliyofanywa katika kipindi cha miaka mitatu ya Rais Dk. Samia.

Dk. Benela alisema mwaka 2022, hospitali ilipokea sh. bilioni 3.3 za mradi wa UVIKO ambazo ziliwafanya kuongeza majengo na vifaa tiba kwaajili ya kuboresha huduma kuwa za kisasa zaidi.

"Mwaka 2022 tulipata fedha za UVIKO ambazo zilituwezesha kufanya ujenzi wa majengo matatu.

Jengo la wagonjwa wa dharura, wagonjwa mahututi na uangalizi maalumu (ICU) hayo hayakuwepo kabisa, lakini pia tulipata nafasi ya kukarabati na kuongeza upande wa vipimo na kununua mashine ya X-RAY mpya baada ya ukarabati wa jengo," alisema.

Dk. Benela anaeleza pia walifanya ukarabati wakaongeza huduma mpya ya kuchuja damu (dialysis) na kufanikiwa kuanza kutoa huduma mbalimbali ambazo awali zilikuwa zinapatikana Hospitali ya Taifa ya Muhimbili (MNH).

## UWEZO WA HUDUMA NA VIFAA TIBA

Anaeleza kuwa, Hospitali hiyo inajitosheleza katika utoaji huduma



MGANGA Mfawidhi Hospitali ya Rufaa ya Mkoa ya Mwananyamala, Dk. Zavery Benela.

kwa wananchi wake hasa upande wa dharura pamoja na madaktari bingwa ambapo hadi sasa hospitali hiyo ina madaktari bingwa 22.

"Hospitali ya Rufaa ya Mkoa ya Mwanyamala inahudumia manispaa mbili, Kinondoni ambapo ipo pamoja na Ubungo.

"Tunatoa huduma za kibingwa, tuna madaktari bingwa 22, katika zile idara zote za msingi ambazo ni idara ya wanawake, watoto, upasuaji, magonjwa ya ndani, lakini tunao pia madaktari bingwa upande wa meno, masikio, pua na koo pamoja na daktari bingwa wa ngozi," alisema Dk. Benela.

Dk. Benela alisema eneo muhimu zaidi kwao ni katika idara ya vipimo ambapo huko pia wana madaktari bingwa maeneo mbalimbali ikiwemo wawili waliopo katika upande wa kipimo cha Radiolojia.

"Sehemu ya umuhimu sana kwetu ni sehemu ya vipimo, upande wa radiolojia pia tuna madaktari bingwa wawili, kwa huduma za kibingwa hospitali ina madaktari wa kutosha," alisema.

## MAFUNZO KWA WATUMISHI

Aliongeza kuwa, mradi wa UVIKO ulisaidia watumishi wa hospitali hiyo kupata mafunzo, kwani walikwenda Muhimbili kupewa ujuzi kwa muda wa wiki tatu kuweza kutumia hivyo vifaa.

"Tunajivunia miradi mikubwa minne, Jengo la Emergency, ICU, Uchunguzi na jengo la kuchuja damu. Hayo ni makubwa. Lakini pia tulifanya ukarabati tukaanzisha jengo la upasuaji wa mifupa. Jumla ya fedha tulizopokea za UVIKO ni Sh. Bilioni 3.3," aliongeza.

Dk. Benela amemshukuru Rais Dk. Samia kwa kuendelea kuboresha sekta hiyo kuhakikisha kila mwananchi anapata huduma bora.

"Tunamshukuru sana Rais kwa sekta nzima ya afya na hospitali ya Mwananyamala, tunawashukuru sana viongozi wetu wa wizara kwa utendaji bora. Rais ameshafanya kazi yake, katupa fedha, katujengea miundombinu na ametupa watumishi, kilichobaki sasa ni sisi kuhakikisha tunasimamia wananchi wanapata huduma bora," alisema.

## RAIS SAMIA ALIVYOBORESHA HUDUMA

DK. Benela alisema Rais Dk. Samia amefanya uwekezaji mkubwa katika hospitali za rufaa za mikoa hatua inayochochea upatikanaji bora wa huduma za afya kwa wananchi.

"Hatua kubwa ambayo Rais ameifanya katika uwekezaji katika hospitali za mikoa ni jambo kubwa.

Awali, huduma kubwa lazima ilikua watu waende Muhimbili, lakini huduma nyingi zilizokua zinapatikana Muhimbili hivi sasa zinapatikana huku," alisema.

Pia aliongeza kuwa: "Tumekua na ongezeko kubwa la wateja, zamani tulikua tunalaza wagonjwa wastani 180 kwa siku, lakini sasa ni 240. Hii inatokana na kuongezeka kwa huduma,".

## ILIVYOJIPANGA KUSIMAMIA MIRADI

Dk. Benela alisema hospitali hiyo imejipanga kutoa huduma bora na ufanisi wa hali ya juu kwa wananchi.

"Tumejipanga kuhakikisha zile huduma zilizopangwa kutolewa zinatolewa kwa ufanisi mkubwa, pia tumepewa kazi ya kusimamia vituo vya chini, kila robo ya mwaka tumekuwa tukitembelea vituo hivyo kuhakikisha tunatoa ujuzi ili kuimarisha huduma," alisema.

## WITO

Mganga huyo mfawidhi alitoa wito kwa wakazi wa manispaa hizo kuiamini hospitali hiyo pamoja na watendaji wake katika utoaji wa huduma bora.

"Jamii ituamini, tumejipanga kuwahudumia, zile huduma nyingi walizokuwa wanapata hospitali binafsi sasa zinapatikana Mwananyamala,".




JENGO la huduma ya dharura.



MWONEKANO wa hospitali ya Mwananyamala.



JENGO Jipya la ICU lililokamilika na kuanza kutumika hivi karibuni.



CT Scan.



MASHINE ya kisasa ya X-Ray (Digital X-Ray).



WODI ya kuchuja damu.



MAGARI ya kubeba wagonjwa.

# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
## HOSPITALI YA RUFAA MKOA WA
# SIMIYU



Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. Samia Suluhu Hassan

## HOSPITALI YA RUFAA YA SIMIYU ILIVYOTUMIA SH. MIL. 943,698,955.89 KUNUNUA VIFAA TIBA









Mganga Mfawidhi Dk. Athanas Ngambakubi

MIAKA MITATU YA RAIS DK. SAMIA NA UBORESHAJI SEKTA YA AFYA NCHINI

# Hospitali ya Rufaa ya Simiyu ilivyotumia sh. mil. 943,698,955.89 kununua vifaa tiba



Mganga Mfawidhi Dk. Athanas Ngambakubi

**Na MWANDISHI WETU**

TANGU aingie madarakani Machi 19, 2021, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. Samia Suluhu Hassan amekuwa akijipambanua kama kiongozi anayeoongoza kwa kutumia mbinu ambazo zinalenga katika kuliunganisha Taifa la Tanzania katika nyanja zote ikiwemo sekta ya afya.

Katika kipindi cha miaka mitatu ya uongozi wa Rais Dk. Samia, huduma za afya katika hospitali mbalimbali nchini zimeboresha kwa kiasi kikubwa ikiwemo kununua vifaa tiba.

Vifaa hivyo kwa kiasi kikubwa vimerahisha upatikanaji wa huduma kwa wagonjwa ambapo awali walilazimika kuzifuata mbali zaidi.

Kwa mujibu wa Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Simiyu, Dk. Athanas Ngambakubi, maboresho ya hospitali hiyo yamechangiwa kwa kiasi kikubwa na serikali iliyopo madarakani chini ya Rais Dk. Samia.

### MAFANIKIO WANAYOJIVUNIA

Alisema wanamshukuru Rais Dk. Samia kwa kutoa fedha kwa ajili ya kununua dawa, vitendanishi na vifaa tiba kwa ajili ya Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Simiyu.

"Tunamshukuru Mhe. Rais Dk. Samia Suluhu Hassan kwa kutoa fedha kwa ajili ya kununua dawa, vitendanishi na vifaa Tiba kwa ajili ya hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Simiyu," alisema.

### UNUNUZI WA VIFAA TIBA

Alisema kuwa, jumla ya sh. milioni 943,698,955.89 zimetumika kununua dawa na vifaa tiba kwa mwaka wa fedha 2022/23 pamoja na mashine ya CT-SCAN na X-RAY.

### MAJENGO MAPYA

Aidha Dk. Ngambakubi alisema chini ya uongozi wa Mhe. Rais Dk. Samia, wamefanikiwa kupata majengo manne mapya ambapo hospitali ilipokea kiasi cha sh. 7,439,492,583.00 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya ujenzi wa jengo la mama na mtoto, jengo la utakasishaji vifaa, jengo la ufuaji na jengo la kuhifadhia maiti kwa vipindi tofauti kwa mchanganuo ufuatao:-

| Na | JINA LA MRADI | FEDHA ZILIZOPOKELEWA | CHANZO CHA FEDHA | MAONI |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Jengo la Huduma ya mama na mtoto | 6,760,689,988 | Global Fund na Serikali Kuu | Jengo limeanza kutumika |
| 2 | Jengo la Ufuaji | 233,749,665 | Benki ya Dunia | Jengo limeanza kutumika |
| 3 | Jengo la Utakasishaji Vifaa | 231,915,430 | Benki ya Dunia | Jengo limeanza kutumika |
| 4 | Jengo la Kuhifadhia Maiti | 213,137,500 | Benki ya Dunia | Jengo limeanza kutumika |



**"Tunamshukuru Mhe. Rais Dk. Samia Suluhu Hassan kwa kutoa fedha kwa ajili ya kununua dawa, vitendanishi na vifaa Tiba kwa ajili ya hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Simiyu.**

Mganga Mfawidhi Dk. Athanas Ngambakubi

### MIKAKATI WALIYOJIWEKEA

Dk. Ngambakubi alisisitiza mikakati yao waliyojiwekea kama watoa huduma kuhakikisha wanaendelea kutoa huduma bora na zenye staha kwa wananchi.

Alisema pia kuongeza wigo wa kutoa matibabu ya kibingwa na kibingwa bobezi kwa jamii.

Aliongeza jingine ni kuongeza upatikanaji wa dawa, vifaa tiba na vitendanishi kwa wakati na kwa ubora unaotakiwa.

"Mikakati yetu kama watoa huduma ni kuendelea kutoa huduma bora na zenye staha kwa wananchi pamoja na kuongeza wigo wa kutoa matibabu ya kibingwa na kibingwa bobezi kwa jamii.

"Kuongeza upatikanaji wa dawa, vifaa tiba na vitendanishi kwa wakati na kwa ubora unaotakiwa," alisema Dk. Ngambakubi.

### NENO KWA SERIKALI

Aliongeza kipekee anapenda kutoa shukrani za dhati kwa Mhe. Rais Dk. Samia kwa kuendelea kuwapatia fedha za kuanza ujenzi wa jengo jipya ya kulaza wagonjwa kwa mwaka wa fedha 2024/2025 kiasi cha sh. 2,000,000,000, katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Simiyu na wanamtakia kila la kheri katika majukumu yake.

"Kipekee tunatoa shukrani zetu za dhati kwa Mhe. Rais Dk. Samia kwa kuendelea kutupatia fedha za kuanza ujenzi wa jengo jipya ya kulaza wagonjwa kwa mwaka wa fedha 2024/2025 kiasi cha Tsh 2,000,000,000, katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Simiyu na tunamtakia kila la kheri katika majukumu yake," alisema Dk. Ngambakubi.



HOSPITALI YA RUFAA YA MKOA WA SIMIYU





### WITO KWA JAMII

DK. Ngambakubi alisema, wito wao kwa jamii wanayoihudumia ni kuiasa kwenda kupata matibabu katika vituo vya kutolea huduma za afya pale wanapoona dalili za kuumwa, kwani hospitali hivi sasa ina vifaa vya kisasa vya kuwawezesha kufanya uchunguzi wa kina pamoja na madaktari bingwa kwa ajili ya kuweza kutoa huduma stahiki kwa jamii

MIAKA MITATU YA RAIS DK. SAMIA NA UBORESHAJI SEKTA YA AFYA NCHINI

# Hospitali ya Rufaa ya Simiyu ilivyotumia sh. mil. 943,698,955.89 kununua vifaa tiba





inayowazunguka.

"Wito wetu kwa jamii tunayoihudumia ni kuihasa kwenda kupata matibabu kwatika vituo vya kutolea huduma za afya pale wanapoona dalili za kuumwa kwani hospitali hivi sasa ina vifaa vya kisasa vya kuweza kufanya uchunguzi wa kina pamoja na madaktari bingwa kwa ajili ya kuweza kutoa huduma stahiki kwa jamii inayotuzunguka," alisema Dk. Ngambakubi.

**HUDUMA ZINAZOTOLEWA**
**UPASUAJI**

Ni idara muhimu ya hospitali ambapo operesheni kubwa za upasuaji hufanywa.

Inapokea wateja wake kutoka kwa idara zote ikiwa ni pamoja na upasuaji mkuu, meno, ukoolojia, daktari wa watoto na wakati mwingine moja kwa moja kutoka eneo la ajali.

Jukumu kubwa la idara ni kutoa huduma zenye ufanisi na ubora wa hali ya juu pamoja na huduma maalum za upimaji kwa wagonjwa.

**WAGONJWA WA NJE**

Huduma zinazotolewa hapa zinajumuisha ushauri wa jumla, elimu ya afya, ushauri nasaha, kliniki za afya mbalimbali, uchunguzi wa kimatibabu, chanjo (chanjo homa ya ini, kichaa cha mbwa & pepopunda), huduma za utambuzi kwa ushirikiano na idara zingine.

**MAABARA**
***PARASITOLOJIA**

Sehemu hii inawajibika kwa utambuzi wa viumbe vingi vya vimelea katika mkojo, choo na damu kwa utambuzi wa malaria, mbinu zote za haraka na za kawaida hutumiwa.

**HEMATOLOJIA**

Sehemu ya Hematolojia inawajibika kwa kuainisha sampuli za wagonjwa wanaotakiwa na waganga kama picha kamili ya damu (FBP) kwa wagonjwa ili kujua sababu ya ugonjwa, kiwango cha chembechembe za damu, upimaji wa maambukizi ya virusi vya ukimwi, homa ya ini na kaswende.

Sehemu hii ndiyo inayowajibika kwa kutoa damu salama kwa wagonjwa wote wanaohitaji damu ndani ya hospitali.

**DHARULA**
**Idara ya Magonjwa ya Dharura (EMD)**

Ni idara inayopokea rufaa na kesi zote za dharura katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa Wa Simiyu.

Idara ya Magonjwa ya Dharura (EMD), inatoa huduma kwa wagonjwa walio na mashaka ya kuhatarisha maisha.

Malengo ya idara hii ni kuhakikisha wagonjwa wenye mashaka ya kuhatarisha maisha wanahudumiwa na kufanyiwa ufuatiliaji wa karibu kabla ya kuhamishiwa katika wodi za wagonjwa wa ndani kulingana na hali zao.

**KAZI ZA MSINGI ZA IDARA**
**Sehemu ya Triage**

Kupokea rufaa na kesi zote za dharura, kukusanya takwimu na tathimini ya upesi kwa hali ya mgonjwa ili kuipa kipaumbele na kuanzisha matibabu yanayostahili.

Kuwahamishia wagonjwa eneo linalofaa la EMD na matibabu kwa wagonjwa ambao hawahitaji huduma ya dharura, wanapelekwa idara ya magonjwa ya nje.

**USHAURI NA ENEO LA MATIBABU**

Kutibu wagonjwa kwa vipaumbele kulingana na hali zao pamoja na ufuatiliaji wa afya zao ndani ya masaa manne wagonjwa watapata ushauri wa daktari, huduma za kiuguzi kulingana na kipaumbele, wagonjwa wanalazwa wodini au kuruhusiwa kulingana na hali zao.

**FAMASI**

Sehemu ya dawa inawajibika kwa kuhakikisha upatikanaji wa dawa kwa wakati wote, dawa zenye ubora unaokubalika, usalama na ufanisi kwa jamii, pia hutoa habari ya dawa juu ya matumizi sahihi ya dawa, athari mbaya pamoja na huduma za kinga.

**HUDUMA ZA MIONZI**

Idara inajitahidi kuhakikisha kuwa vyombo vyote vya radiolojia vinapatikana na uchunguzi wa mionzi unafanywa kama inavyotakiwa na waganga.

Kawaida haitoi huduma ya muda mrefu au mwendelezo lakini magonjwa mbalimbali hutambuliwa na huduma sahihi hutolewa kulingana na utambuzi wa magonjwa ya papo hapo na magonjwa sugu.

Mashine zinazopatikana ni pamoja na; ultrasound inayoweza kuhamishika (Portable), mashine ya X-Ray ya kidijitali na mashine nzito ya ultrasound (heavy duty).

**HUDUMA YA MAMA NA MTOTO**

Jengo la huduma ya mama na mtoto limeshakamilika na lilianza kutoa huduma tangu Februari 5, mwaka huu.

Jengo hilo la ghorofa mbili ujenzi wake ulianza Oktoba mwaka 2019, hadi sasa limekamilika kwa asilimia 95.

Limejengwa kwa gharama ya kiasi cha sh. 6,760,689,988 na lina uwezo wa kuchukua vitanda 140 na litahudumia wamama 100 na watoto watakaolazwa 40.

**HISTORIA YA HOSPITALI**

Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Simiyu, ilizinduliwa rasmi na Hayati Rais Dk. John Magufuli mnamo Septemba 08, 2018.

Hospitali hii inamilikiwa na Wizara ya Afya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto.

Iko eneo la Nyaumata, Halmashauri Ya Mji wa Bariadi mkoani Simiyu.

Hospitali hii inahudumia na kupokea rufaa kutoka wilaya tano katika Mkoa wa Simiyu na kuhudumia idadi ya watu zaidi ya milioni 1.8 katika mkoa.

Wagonjwa wanaletwa kutoka ngazi ya chini ambayo ni pamoja na hospitali za wilaya na vituo vya karibu vya afya.

**JENGO LA MAMA NA MTOTO**

**Limejengwa kwa gharama ya kiasi cha sh. 6,760,689,988 na lina uwezo wa kuchukua vitanda 140 na litahudumia wamama 100 na watoto watakaolazwa 40.**







Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
Wizara ya Afya
**Hospitali ya Rufaa ya Mkoa Sekou-Toure**
(Mwanza)

# Mafanikio ya Hospitali ya Rufaa ya Mkoa Sekou Toure katika miaka mitatu ya Rais Dk. Samia



**Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Rufaa ya Sekou Toure, Dk. Bahati Msaki.**



**Jengo la huduma ya Afya ya Mama na Mtoto.**

**Na MWANDISHI WETU**

HOSPITALI ya Rufaa ya Sekou Toure mkoani Mwanza ni moja ya hospitali zinazotoa huduma nzuri kwa wakazi wa mkoa huo na maeneo jirani.

Hospitali hiyo imekuwa ikitoa huduma bora na kukidhi mahitaji ya wagonjwa wa Wilaya zote za Mkoa wa Mwanza baada ya kufanyiwa maboresho mbalimbali katika kipindi cha miaka mitatu ya Rais Dk. Samia Suluhu Hassan tangu aingie madarakani.

Kwa mujibu wa Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Rufaa ya Sekou Toure, Dk. Bahati Msaki, hospitali hiyo inatoa huduma mbalimbali za afya za kibingwa katika sekta tofauti.

"Tumekuwa tukitoa huduma mbalimbali zikiwemo za kibingwa na kukidhi mahitaji ya wagonjwa wa wilaya zote za Mwanza na maeneo ya jirani," alisema Dk Bahati.

**HOSPITALI INATOA UDUMA ZA AFYA ZA KIBINGWA KATIKA FANI ZIFUATAZO;**

*Uzazi na kizazi
*Watoto
*Upasuaji
*Magonjwa ya ndani
*Pua, Masikio na koo
*Mionzi

**HOSPITALI INATOA HUDUMA ZA UBINGWA BOBEZI KATIKA FANI ZA;**

*Magonjwa ya mfumo wa chakula
*Kusafisha damu
*Upasuaji wa watoto wenye migongo wazi na vichwa vikubwa.

Mganga Mfawidhi Dk. Bahati alisema kuwa, katika eneo la bidhaa eneo la bidhaa za afya (Dawa, vifaa tiba na reagent) hospitali inajitosheleza kwa asilimia 95.

**MIRADI ILIYOKAMILIKA**

Dk. Bahati alisisitiza, hospitali imekamilisha mradi mkubwa wa jengo la mama na mtoto, ambalo lina ghorofa tano na jengo lina uwezo wa kubeba vitanda 261.

Alisema kwa kiasi kikubwa jengo hilo limeboresha huduma ya mama na mtoto katika hospitali ya Sekou Toure.

Dk. Bahati alisema huduma katika jengo hilo zilianza kutolewa mwezi Juni 2022, ambapo hadi kufikia Desemba, 2023 wakinamama 16,851 walikuwa wamejifungua katika jengo hilo.

Aliongeza kuwa, kati ya hao waliojifungua kwa njia ya kawaida ni 14,120 na 3,331 wamejifungua kwa njia ya upasuaji.

Dk. Bahati alisema katika kipindi cha miaka mitatu cha uongozi wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dk. Samia, sekta ya afya imekuwa na mafanikio makubwa hasa katika maboresho ya miundombinu ikiwemo usimikaji wa vifaa tiba muhimu kama vile CT Scan na mashine mbili za X-ray.

**Dk. Bahati alisema katika kipindi cha miaka mitatu cha uongozi wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dk. Samia, sekta ya afya imekuwa na mafanikio makubwa hasa katika maboresho ya miundombinu ikiwemo usimikaji wa vifaa tiba muhimu kama vile CT Scan na mashine mbili za X-ray.**



**Mashine ya Endoscopy inatumika Kwa kuchunguza Magonjwa ya mfumo wa Chakula.**

Alisema vifaa hivyo vinasaidia kuboresha huduma za uchunguzi kwa wagonjwa kwani kabla ya usimikaji wa vifaa hivyo, wagonjwa walikuwa wanapewa Rufaa kwenda kufanya vipimo katika hospitali ya Kanda ya Bugando, jambo ambalo lilikuwa linachelewesha huduma kwa wagonjwa.

**USIMAMIZI WA MIRADI**

Alisema menejimenti ya hospitali imejipanga vizuri katika kuendelea kusimamia miradi iliyopangwa kutekelezwa na ambayo imeshatekelezwa kwa kuwa na mpango kazi maalumu wa matengenezo kinga ( Plan Preventive Maintanance) ya vifaa vilivyosimikwa ikiwa ni pamoja na mitambo na majengo ili yaendelee kuwa na ubora kwa muda mrefu

**SHUKRANI KWA RAIS DK. SAMIA**

Alisema wanatoa shukrani za pekee kwa Serikali ya Awamu ya



**Sehemu ya usindikaji wa gasi panaitwa Oxygen Plant.**

MIAKA MITATU YA RAIS DK. SAMIA NA UBORESHAJI SEKTA YA AFYA NCHINI

# Mafanikio ya Hospitali ya Rufaa ya Mkoa Sekou Toure katika miaka mitatu ya Rais Dk. Samia



CT Scan



X-Ray machine

**"Tunatoa shukrani za pekee kwa Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Rais wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kutoa fedha kwa ajili ya miradi ya ujenzi ikiwemo jengo hili la Mama na Mtoto ambalo limeanza kutumika na kuboresha huduma kwa Wananchi wa mkoa wa Mwanza," alisema Dk. Bahati.**

Sita inayoongozwa na Rais Dk. Samia kwa kuendelea kutoa fedha kwa ajili ya miradi ya ujenzi ikiwemo jengo hilo la Mama na Mtoto ambalo limeanza kutumika na kuboresha huduma kwa wananchi wa Mkoa wa Mwanza.

Vilevile kuidhinishwa na kutoa fedha ya uanzishwaji wa ujenzi wa jengo jipya la dharura, ajali na wagonjwa mahututi (EMD & ICU), ununuzi wa madawa, vifaa tiba na kuendelea kuajiri watumishi wa kada za Afya katika hospitali ya Rufaa ya Mkoa Sekou Toure.

"Tunatoa shukrani za pekee kwa Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Rais wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kutoa fedha kwa ajili ya miradi ya ujenzi ikiwemo jengo hili la Mama na Mtoto ambalo limeanza kutumika na kuboresha huduma kwa Wananchi wa mkoa wa Mwanza," alisema Dk. Bahati.

**HUDUMA ZINAZOTOLEWA**

Huduma ya mama na mtoto:

*Elimu ya afya kwa Mama na Mtoto.

*Chanjo za watoto na wakina mama.

*Huduma ya uzazi wa mpango.

*Upimaji wa saratani ya shingo ya kizazi.

**MENO**

Kitengo kinatoa huduma za:-

*Kung'oa meno.

*Kuziba, kutibu jino bila kung'oa.

*Kusafisha meno.

*Kufunga taya na wire (baada ya ajali).

*Elimu ya afya ya kinywa na meno.

*Upasuaji mdogo wa uvimbe.

*Upasuaji wa jipu.

*Mionzi.

*Kuweka jino bandia, kuvua na kuweka mara moja.

*Kuweka meno bandia kinywa chote.

*Kurekebisha meno yaliyoota vibaya.

**KITENGO CHA HUDUMA YA MACHO**

*Matibabu ya magonjwa ya macho.

*Upasuaji wa macho.

*Utambuzi na tiba za macho.

*Elimu ya afya.

**KITENGO CHA TIBA NA MATUNZO YA UKIMWI**

*Nasihi kabla na baada ya upimaji

Elimu ya afya juu ya VVU, uzazi wa mpango, saratani ya shingo ya kizazi na Kifua kikuu.

*Uanzishwaji wa dawa na unywaji wa dawa.

*Utambuzi na tiba ya magonjwa nyemelezi.

**KITENGO CHA MAZOEZI YA VIUNGO**

*Kutoa elimu ya afya kwa wagonjwa na watumishi.

Kutoa matibabu kwa:-

*Watoto wenye mtindio wa ubongo.

*Watoto wenye mguu kifundo.

*Wagonjwa wenye kiharusi.

*Wagonjwa wenye maumivu ya mgongo.

*Wagonjwa wenye maumivu ya viungo (joint).

*Wagonjwa/watoto waliopata ajali wakati wa kuzaliwa.

*Wagonjwa waliongua na moto.

*Wagonjwa waliopata ajali na kuumia kichwa.

*Wagonjwa waliopata ajali na kuvunjika uti wa mgongo.

*Wagonjwa waliopooza kutokana na sababu mbali mbali.

*Kutoa huduma kwa wagonjwa wenye ulemavu wa kudumu.

*Kutoa huduma kwa wagonjwa wenye mvujiko na mtenguko.

*Kutoa huduma kwa wagonjwa wanaotarajia kufanyiwa upasuaji na baada ya upasuaji.

*Kutengeneza vifaa saidizi kwa wagonjwa.

**FAMASI**

*Utunzaji na utoaji wa vifaatiba vya hospitali.

Utoaji wa dawa kwa wagonjwa wa nje na ndani katika vitengo vifuatavyo:-

*Bima ya Afya.

*Wagonjwa wa Ukimwi.

*Wagonjwa wa madawa ya kulevya.

*Wagonjwa wenye kifua kikuu na ukimwi.

**MATIBABU YA KIFUA KIKUU NA UKOMA NA UFUATILIAJI**

*Vipimo vya makohozi, x-ray, upimaji wa VVU.

*Kutoa huduma/rufaa kwa wagonjwa wenye kifua kikuu sugu.

*Elimu ya afya ya kifua kikuu na ukoma na VVU.

*Ushauri nasaha

*Kuwapa rufaa wagonjwa wenye dalili zinazofanana na kifua kikuu kwa wale ambao walishaugua kifua kikuu.

**HISTORIA**

Hospitali ya Sekou toure ni hospitali ya Mkoa wa Mwanza ambayo iko chini ya uangalizi wa Bodi ya Hospitali pamoja na Kamati ya Uendeshaji wa Hospitali ya Mkoa (RHMT).

Hospitali iko katika Wilaya ya Nyamagana, katika Jiji la Mwanza, ilianzishwa mwaka 1964 ikiwa kama kitengo cha wagonjwa wa nje.

Sekou Toure ni miongoni mwa hospitali zilizopandishwa hadhi Novemba, 2010 kama Hospitali ya Rufaa ya Mkoa.

Hospitali ina idara 13 na vitengo 5, vitanda 400 na jumla ya watumishi 468 wa kada/sifa tofauti.



Oxygen Plant



Mashine ya kusafisha Damu (Dialysis)





CT Scan.


WODI ya dharura.


WODI ya VIP.

# Miaka Mitatu ya Rais Samia,Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Iringa yapokea bilioni 4.4

**Na ESTA MALIBICHE,**Iringa

HOSPITALI ya Rufaa ya Mkoa wa Iringa ni miongoni mwa Hospitali 28 za Rufaa za mikoa Nchini Tanzania, ambayo inatoa huduma ya matibabu kwa wananchi wa mkoa wa Iringa na mikoa ya jirani.

Uwepo wa hospitali hii katika mkoa wa Iringa umesaidia sana kusogeza huduma karibu na wananchi jambo ambalo wakazi wake wanajivunia hasa katika matibabu ya huduma za kibingwa na upasuaji.

Hivi sasa hospitali ina wafanyakazi 400 katika fani mbalimbali na kwamba kati ya hao 12 ni madaktari bingwa, wafamasia, wateknolojia dawa, wateknolojia maabara, wauguzi na wasaidizi wa afya.

Mganga Mfawidhi hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Iringa Dkt. Alfred Mwakalebela amelielezea gazeti hili la Uhuru ya Kijani kuwa kazi kubwa iliyopo hivi sasa ni kuhakikisha hospitali hiyo inaendelea kutoa huduma bora kwa wananchi ili kuendana na adhma ya Serikali ya awamu ya sita chini ya uongozi wake Rais Dk. Samia Suluhu Hassan ya kuboresha huduma za afya nchini .

**MAFANIKIO**

Akizungumzia mafanikio waliyoyapata katika kipindi cha miaka mitatu ya uongozi wake Dk. Samia toka alipopokea kijiti kwa aliyekuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania hayati Dk.John Pombe Magufuli Machi 19/2021 anasema, yapo mafanikio mengi ambayo hospitali hiyo inajivunia ikiwa nipamoja na kutoa huduma za kibingwa ikiwemo huduma ya upasuaji wa kawaida, huduma ya magonjwa ya ndani, huduma ya magonjwa ya uzazi,huduma ya watoto,huduma ya mionzi, huduma ya idara ya magonjwa ya dharura.

Anaendelea kuzitaja huduma nyingine za kibingwa zinazopatikana katika Hospitali hiyo kuwa ni pamoja na huduma ya koo, pua na masikio.

Anasema"tuliona shida kubwa sana kuagiza kwa mwezi Daktari Bingwa wa magonjwa ya pua,koo na masikio kutoka Dodoma huku gharama ikiwa kubwa,tukachukua jukumu la kwenda kumsomesha wenyewe kupitia fedha zetu za ndani, tayari ameshamaliza na anaendelea na majukumu yake;

Pia tunajivunia kuweza kuwasomesha katika vyuo mbalimbali hapa nchini na nje ya nchi madaktari bingwa wawili wa Usingizi, madaktari bingwa watatu wa magonjwa ya ndani, madaktari bingwa wa magonjwa ya mifupa na figo, ambao wakishamaliza tunaamini Hospitali yetu itaendelea kutoa huduma za kibobezi katika vitengo vyote.

Anaeleza kuwa hapo awali walikuwa wanakabiliwa na changamoto ya ukosefu wa daktari bingwa wa mifupa na figo, lakini kwa jitihada za serikali ya awamu ya sita ilitenga fedha kwa ajili ya kumsomesha daktari mmoja ambae baada ya mika mitatu ijayo akihitimu mafunzo yake wananchi wataweza kupata matibabu kwa urahisi.

**VIFAA TIBA**

Anaelezea kuwa katika kipindi cha miaka mitatu ya uongozi wake Rais Dk,Samia Suluhu Hassan kumekuwa na ongezeko la vifaa tiba na dawa hali iliyochangia kwa kiasi kikubwa wananchi kupata huduma kwa urahisi.

"Katika kipindi cha miaka mitatu ya Rais Dk,Samia tumeongeza na kuboresha huduma ambazo hapo awali zilikuwa hazipatikani hapa kwetu hali iliyowalazimu wagonjwa kwenda kutibiwa katika mkoa wa Dodoma na Mbeya;

Tumeongeza vifaa tiba kama mashine za usingizi wakati wa upasuaji ambazo zimenunuliwa 5 kwa fedha zetu za ndani shilingi Milioni 300 .

Upatikanaji wa mashine hizo umepelekea swala la upasuaji kuwa la uhakika ambapo Mgonjwa anafanyiwa upasuaji na anatoka salama salimini.

**VIFAA VYA UGUNDUZI**

Anasema kwa upande wa vifaa vya ugunduzi wa magonjwa tumeletewa Digital X-Ray mbili, pia tumeletewa kifaa kikubwa ambacho ni mashine ya CTs Scan ambayo imekuwa ni msaada mkubwa kwa wananchi ambao wanapata majeraha na kuvunjika.

"Serikali kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo imeweza kujenga jengo la dharura (Emergence Department) [kwa shilingi milioni 600 pamoja na vifaa vyake,tumenunua vifaa vya ugunduzi wa magonjwa Digital X-ray mbili za kisasa ambazo zimerahisisha utendaji kazi kwa madaktari.

Pia tunajivunia miaka mitatu ya Rais Dk. Samia kwa kupata kifaa kikubwa ambacho ni mashine ya CT- Scan, ambayo imesaidia kutoa huduma bora za vipimo.

Pia imewapunguzia gharama kubwa wagonjwa kwenda kutibiwa katika Hospitali ya Taifa Muhimbili .

**MAJENGO**

Anaeleza kuwa,kwa upande wa majengo tumejenga 6 ambayo ni jengo la maabala ya viungo bandia na kuweka vifaa vyake, jengo la kuchuja damu (Dialysis) na vifaa vyake ambalo kuna vitanda 16, jengo la benki ya damu salama,ambalo limesaidia kupunguza vifo vya mama na mtoto vilivyokuwa vinatokea hapo awali kutokanana kukosa damu salama.

Pia Tumepata wadi maalum VIP ambayo ni wodi ya kisasa ambayo ina vigezo vya kulaza viongozi wakuu wanchi na wananchi wengi, jengo la ICU nzuri ambalo lina vitanda 20 pamoja na vifaa vya kisasa, jengo la tiba mtandao ambalo linavifaa ambavyo unaweza kuwasiliana na madaktari kutoka ndani ya nchi na nje ya Nchi, ambao madaktari wengine wanaweza kumuona mgonjwa wako kupitia mtandao na wakakusaidia ama kupata ufumbuzi wa ugonjwa unaomsumbua.


Mganga Mfawidhi wa hospitali ya mkoa wa Iringa Dr. Alfred Mwakalebela.

**MAFANIKIO SEKTA YA AFYA**

Tanzania imepiga hatua kubwa kwenye sekta ya Afya kutokana kusogeza huduma bora na za kibingwa kwa wananchi, ambapo hivi sasa huduma za kibingwa zote zinapatikana hapa nchini, hatua hiyo imepunguza gharama kubwa na usumbufu kwa wananchi waliokuwa wanaenda kutibiwa nje ya nchi.

Anaeleza kuwa hivi sasa hospitali zote zina kitengo cha tiba utalii ambacho kimechangia kwa kiasi kikubwa watu kuja Tanzania kuona tunaendesha vipi huduma zetu kwenye hospitali zetu hapa Nchini na wengine wanakuja kutibiwa. Haya yote ni mafanikio makubwa sana ambayo tumeyapata ndani ya miaka mitatu ya Rais Samia Suluhu Hassan.


WODI ya VIP.




JENGO la wodi ya dharura.

**MATARAJIO**

Mbali na hilo, Dkt. Mwakalebela anasema katika kipindi hiki cha serikali ya awamu ya sita wameweka mkakati wa kuhakikksha wanaongeza vifaa mbalimbali kwa kutumia mapato ya ndani ili kukidhi hitaji la wananchi.

Anaeleza kuwa kwa kuwa Serikali imetoa vifaa tiba na dawa ,kazi yetu iliyobaki ni kutoa huduma bora kwa wananchi ili kuendana na kasi ya Rais Dk. Samia Suluhu Hassan. Ninapenda kuwaabia wananchi wa mkoa wa Iringa kwamba,huduma zote muhimu zinapatikana katika hospitali yao ya mkoa wa Iringa,ninawaomba watumie waje kupata huduma za matibabu.

Tunaishukuru Sana serikali ya awamu ya sita chini ya uongozi wake Rais Dk,Samia Suluhu Hassan kwa kutenga fedha kiasi cha Bilioni 4.4 kwa ajili ya kutekeleza miradi,vifaa tiba na dawa katika Hospitali ya Rufaa ya mkoa wa Iringa katika kipindi chake cha miaka mitatu ya uongozi wake.

# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZNIA
## TAASISI YA SARATANI OCEAN ROAD

ORCI OCEAN ROAD CANCER INSTITUTE

# MAFANIKIO YA TAASISI YA SARATANI OCEAN ROAD MIAKA MITATU YA SERIKALI YA RAIS MHE. DKT. SAMIA SULUHU



**Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. Samia Suluhu Hassan**



**Dkt. Mark Mseti (aliyevaa suti nyeusi),ambae ni mkurugenzi wa huduma za Tiba katika Taasisi ya saratani Ocean road,akimpatia maelezo mbalimbali waziri wa Afya alipotembelea taasisi hiyo**



**Mashine ya CYCLOTRON**



**Mkurugenzi mtendaji wa Taasisi ya Saratani Ocean Road Dk. Julius Mwaiselage**





JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZNIA
TAASISI YA SARATANI OCEAN ROAD

ORCI OCEAN ROAD CANCER INSTITUTE

# Mafanikio ya Taasisi ya Saratani Ocean Road miaka mitatu ya Serikali ya Rais Mhe. Dkt. Samia Suluhu



Mkurugenzi mtendaji wa Taasisi ya Saratani Ocean Road Dk. Julius Mwaiselage

**Na SUPERIUS ERNEST**

SERIKALI ya Rais Dk. Samia Hassan Suluhu imepata mafanikio makubwa katika miaka mitatu ya utendaji wake, hususan katika sekta ya afya kwa kuimarisha huduma za saratani nchini ikiwemo Taasisi ya Saratani Ocean Road (ORCI).

ORCI ilianzishwa kwa Sheria Na 3 (Cap 86) ya mwaka 1996 ya Bunge la Tanzania na kuendelea kutoa huduma mbalimbali za uchunguzi na matibabu ya saratani.

Mkurugenzi Mtendaji wa Dk. Julius Mwaiselage, alitaja huduma zinazotolewa hospitalini hapo ni za kibingwa za kinga ya saratani, kliniki za wagonjwa wa nje, uchunguzi wa radiolojia na nyuklia na uchuguzi wa maabara.

Alitaja huduma zingine kuwa ni tiba za kemia na mionzi, tiba shufaa, kulaza wagonjwa, mafunzo ya shahada ya kwanza, uzamili na utafiti.

Mkurugenzi Mwaiselage alisema Taasisi hiyo imeanza kutoa huduma za kibingwa bobezi za tiba ya saratani ya IMRT na hivi karibuni huduma za PET/CT zitaanza kutolewa.

Alisema kwa mujibu wa sera ya afya inaeleza kuwa, tiba ya saratani itatolewa bila malipo kwa wale wasio na uwezo, hivyo serikali imechukua jukumu la kugharamia matibabu ya wagonjwa wa saratani.

"Serikali ya awamu ya sita inagharamia huduma za matibabu ya saratani nchini kwa wananchi wasio na uwezo kwa msamaha, kwa wananchi wenye uwezo au bima za afya, huweza kugharamia sehemu ya gharama za tiba kwa kulipa au kutumia bima zao,"alisema Dk. Mwaiselage.

**Utekelezaji wa Majukumu ya Taasisi**

Alieleza kuwa, katika kipindi hiki, kumekuwepo na ongezeko la wagonjwa wa saratani wanaofika ORCI kupata huduma za kibingwa na ubingwa bobezi wa uchunguzi na tiba.

Alisema ongezeko la wagonjwa limetokana na mwamko wa jamii kuhusu vyanzo na athari za saratani kwa jamii na uchumi kwa ujumla, kuimarika kwa mawasiliano na huduma ya uchunguzi wa awali wa saratani, kuongezeka kwa vituo vya kutolea huduma za saratani nchini kote hasa mikoani na wilayani.

**Huduma za Mkoba**

Dk. Mwaiselage alisema katika kipindi cha Rais Dk. Samia, uchunguzi wa saratani umeendelea kufanyika kupitia huduma za Mkoba na katika Taasisi.

Alisema uchunguzi huo ulifanyika Mikoa 19 ambayo ni Dar es Salaam, Geita, Lindi, Ruvuma, Dodoma, Iringa, Manyara, Njombe, Arusha, Rukwa, Katavi, Pemba, Mwanza, Singida, Kagera, Morogoro, Tanga, Unguja na Dodoma.

"Kwa kipindi hicho, jumla ya wateja 38,770, walifanyiwa uchunguzi wa saratani ya matiti, saratani ya mlango wa kizazi, ngozi, utumbo mpana, huku wanawake 1,891, walionekana kuwa na dalili za awali za saratani na wanawake 865 waligundulika kuwa na saratani,"alisema.

Aidha, alisema katika kipindi hicho, wanaume 13,991, walifanyiwa uchunguzi wa saratani ya tezi dume, ambapo wanaume 993 sawa na asilimia 7.0 waligundulika na dalili za kuvimba tezi dume na 48 tu ndio waligundulika na saratani ya tezi dume.

Alitaja saratani 10 zinazoongoza ni ya mlango ya kizazi asilimia 25.3, matiti asilimia10, njia ya chakula kooni asilimia 6.5, utumbo mpana asilimia 5.8, tezi dume asilimia 9, saratani ya kichwa na shingo asilimia 9, Kaposi sarcoma asilimia 6, Thyroid asilimia 2, Lymphoma asilimia 1 na Damu asilimia 1.

Idadi ya Wagonjwa wa Nje (OPD) Waliohudumiwa

Dk. Mwaiselage alisema katika kipindi cha miaka 3 cha awamu ya sita, Taasisi ilihudumia jumla ya wagonjwa wa saratani wa nje (OPD) 169,939, ikiwa ni asilimia 98 ya lengo la miaka mitatu.

**Idadi ya Wagonjwa wa Ndani (IPD).**

Alisema Taasisi inauwezo wa kulaza wagonjwa 272, vikiwemo vitanda vya kulaza wagonjwa wa kawaida wa binafsi (VIP) na wa uangalizi maalum (ICU), huku katika kipindi cha miaka 3 cha awamu ya sita, Taasisi ililaziza jumla ya wagonjwa wa saratani 12,802 wodini (IPD), ikiwa ni asilimia 92 ya lengo kwani huduma za ICU zimeanza kipindi cha serikali ya awamu ya sita hazikuwepo hapo awali.

**Huduma za Uchunguzi wa Radilojia**

Mkurugenzi Mwaiselage alisema katika kipindi cha miaka mitatu cha awamu ya sita, taasisi hiyo iliendelea kuimarisha huduma za kibingwa za uchunguzi wa radilojia kwa vipimo vya Digital X-ray, Ultrasound, CT scan, na MRI.

" Jumla ya vipimo 84,415 vya radiolojia vilitolewa sawa na asilimia 112 ya lengo, vipimo hivyo vikihusisha 35,940 vya X-ray, 36,699 vya ultrasound, 9,181 vya CT Scan,1,236 vya mammograph na 1,359 vya MRI,"alisema.

Alisema katika kipindi hiki, huduma za MRI na Digital X-ray zilianzishwa na hazikuwepo awali.

Vilevile, alisema Taasisi imeanzisha huduma za ubingwa bobezi za Interventional radiolojia, ambapo wagonjwa wa saratani hupatiwa matibabu ikiwemo ya figo, mishipa ya damu, ini, kongosho, nyongo, utumbo, na mapafu.

**Huduma za Uchunguzi wa Maabara**

Dk. Mwaiselage alisema katika kipindi cha miaka mitatu ya Rais Dk. Samia huduma za maabara zimezidi kuimarika, huku vipimo vya histopathology, cytology, Immunoassay (tumor markers), haematology, clinical chemistry, immunology, parasitology, na blood transfusion vinafanyika.



Mashine ya CYCLOTRON

Alieleza kuwa, katika Taasisi hiyo ilitoa, jumla ya vipimo 198,734 vya maabara ikiwa ni asilimia 96 ya lengo huku vipimo mahsusi vya saratani vya vinafanyika na husaidia kutoa tiba mahsusi na ya kibingwa kwa wagonjwa wa saratani.

Katika kipindi cha Serikali ya Awamu ya sita ya Rais Dk. Samia, maabara ya taasisi hiyo ilifanyiwa tathmini ya ithibati ya Kimataifa na kupewa ithibati katika vipimo vya aina tano kutoka Shirika la Viwango la Ukaguzi la Kimataifa (SADCAS).

**Kuongezeka kwa bajeti ya dawa za Saratani**

Alisema katika miaka ya nyuma, kero kubwa na malalamiko kutoka kwa wagonjwa ilikua na ukosefu wa dawa za tiba kemia za wagonjwa wa saratani, lakini katika miaka ya Rais Dk. Samia, serikali imeweza kuongeza bajeti ya dawa za saratani kufikia sh. bilioni 10 kila mwaka kutoka sh. bilioni sita ya awali.

Dk. Mwaiselage alisema wameimarisha upatikanaji wa dawa za saratani katika Taasisi kutoka asilimia 97 mwaka 2020/21 hadi wastani wa upatikanaji wa dawa asilimia 100 mwaka 2022/23.

Alieleza kuwa, bei za dawa kwa wagonjwa wa saratani zipo nchini kwa asilimia 30, kulinganisha na maduka mengine ya binafsi, hivyo ni nafuu zaidi.

**Huduma za Tiba ya Nyuklia**

Mkurugenzi huyo alisema taasisi hiyo iliendelea kutoa huduma za uchunguzi wa mifupa, figo, ubongo na tezi kwa mashine za nyuklia kuona ugonjwa wa saratani kupitia mashine ya Gamma Camera na tiba ya dawa nyuklia.

Alisema katika kipindi cha miaka mitatu ya Rais Dk. Samia, jumla ya wagonjwa 3,924 walipatiwa huduma za kliniki sawa na asilimia 98 ya lengo.

**Kuanza Utoaji wa Uchunguzi na Tiba ya Saratani kwa Kutumia PET/CT**

Mkurugenzi huyo, alisema huduma za tiba ya nyuklia zilikuwa zinatolewa kwa kutumia mashine za gamma camera, lakini serikali ya awamu ya sita imeboresha huduma ya uchunguzi na tiba ya nyuklia kupitia utekelezaji wa mradi wa PET/CT scan ambao umekamilika.

Alisema mradi huu unahusisha ujenzi wa jengo (maalum la kusimika mashine, maabara za kuchanganyia dawa za nyuklia na vyumba vya huduma, ununuzi na usimikaji wa mashine ya cyclotron na ununuzi na usimikaji wa mashine ya PET/CT scan.

Mkurugenzi huyo alisema gharama za mradi huu ni sh. bilioni 18.2, huku akiishukuru serikali ya Rais Dk. Samia kwa kugharamia utekelezaji wa mradi huu, ambapo kwa sasa ujenzi umefikia asilimia 99 na mabapo mashine za PET/CT na Cyclotron zimesimikwa.

Alieleza kuwa, mradi huo unafanyiwa majaribio ambapo unatarajiwa kuanza Mwaka huu kwani kwa sasa, Taasisi imepata vibali mbalimbali kuanza utoaji wa huduma.

**Manufaa ya Mradi**

Alisema kuwa, mradi huu utakuwa na manufaa kwa Taifa katika utoaji wa huduma za uchunguzi na tiba kwa wagonjwa wa saratani, utaboresha huduma za saratani nchini ziwe katika kiwango cha kimataifa hasa katika uchunguzi, kwani mashine hiyo ndiyo ya kisasa kabisa katika uchunguzi wa saratani duniani kote.

"Utasaidia katika kupunguza rufaa za nje na hivyo kuokoa fedha ambazo serikali hugharamia wagonjwa nje ya nchi hasa India, utachangia utekelezaji wa sera ya serikali ya ujenzi wa viwanda, utaongeza mapato ya Taasisi, mionzi-dawa itauzwa kwa hospitali zingine nchini na nchi jirani ambazo zitafunga mashine za PET/CT scan,"alisema.

"Uuzaji wa mionzi-dawa, utaongeza mapato kwa Taasisi kuvutia wagonjwa kutoka nchi jirani ikiwemo Uganda, Kenya, Malawi, Msumbiji, DRC, Burundi, Zambia, Rwanda, Comoro, Sudan ya Kusini na Somalia na hivyo kutekeleza kwa vitendo adhima ya serikali ya kuimarisha medical tourism,"alisema.

Alisema katika kipindi cha miaka mitatu cha awamu ya sita, taasisi hiyo ilitoa tiba kemia kwa jumla ya wagonjwa 39,474 na katika mizunguko 68,571 ya tiba kemia, huku Taasisi inatoa huduma ya tiba kemia kwa kutumia vifaa vya kisasa vya infusion pumps ambapo dawa huingia katika mwili wa mgonjwa kwa utaratibu maalum.



Dkt. Mark Mseti (aliyevaa suti nyeusi),ambae ni mkurugenzi wa huduma za Tiba katika Taasisi ya saratani Ocean road,akimpatia maelezo mbalimbali waziri wa Afya alipotembelea taasisi hiyo

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZNIA
TAASISI YA SARATANI OCEAN ROAD

ORCI OCEAN ROAD CANCER INSTITUTE



Mtaalamu wa Radiolojia Dkt. Latipha Rajabu kutoka Taasisi ya Saratani Ocean Road akimpunguza Nyongo mgonjwa bila ya kufanya upasuaji ili kurahisisha matibabu mengine ya Saratani.

# Mafanikio ya Taasisi ya Saratani Ocean Road miaka mitatu ya Serikali ya Rais Mhe. Dkt. Samia Suluhu

Alisema dawa za saratani za aina zote zinapatikana ikiwemo za kemia na vichocheo katika kipindi cha serikali ya awamu ya sita, ambapo dawa za tiba maalumu za saratani za immunotherapy zilianzishwa kufanya maboresho yaliyofanyika ya tiba.

**Huduma za Tiba Mionzi**

Kuhusu tiba mionzi, Mkurugenzi alisema taasisi ilitoa tiba mionzi kwa kutumia mashine nne za mionzi ya nje (2 za Cobalt-60 na 2 za LINACs) na mashine mbili za mionzi ya ndani (brachytherapy).

Alisema jumla ya tiba 671,943 kwa wagonjwa zilitolewa, hii ni sawa na asilimia 95 ya lengo, ikiwa ni muda wa kusubiri tiba mionzi kwa wagonjwa wa saratani imefikia ndani ya wiki mbili ikilinganishwa na wiki sita ya miaka iliyopita.

**Kuanza kutoa Huduma za Ubingwa Bobezi za Tiba mionzi kwa IMRT**

Katika kuimarisha huduma za tiba mionzi bobezi kwa wagonjwa wa saratani nchini, Mkurugenzi Mwaiselage alisema, Taasisi imeanzisha huduma za tiba mionzi bobezi za Intensity Modulated RadioTherapy (IMRT).

Alisema tangu mwaka 2018, wakati mashine za mionzi ziliposimikwa na kuanza kutoka tiba ya kibingwa ya 3D Convectional Radiotherapy (3D CRT), wagonjwa wengi wametibiwa kwa ufanisi mkubwa na kuongezeka kwa wagonjwa kutoka nje ya nchi ambapo wagonjwa kutoka nje ya nchi wanaofika katika taasisi hiyo imeendelea kuongezeka kila mwaka.



Chumba cha wagonjwa mahututi

Alisema hii ni kutokana na kuimarishwa kwa huduma za uchunguzi na tiba na hivyo kutekeleza kwa vitendo maono ya Rais Dk. Samia kuhusu utalii wa tiba.

Alieleza kuwa katika kipindi cha miaka mitatu ya Rais Dk. Samia, wagonjwa 1,241 kutoka nje ya nchi walipatiwa huduma za uchunguzi na tiba ya saratani. Wagonjwa hao walitoka nchi za Malawi, Marekani, Brazili, Burundi, Comoro, Cuba, Ujerumani, Indonesia, Urusi, Senegal, Uswisi, Uturuki, Yemeni, Zambia, Uturuki, Norway, Mozambique, Kenya, Congo DRC, na Zimbabwe

Pia, alisema tayari wameingia makubaliano na serikali za nchi za Malawi na Zambia kuleta wagonjwa wao wa uchunguzi na tiba ya saratani ya makubaliano yataongeza wagonjwa zaidi na hivyo kutoka nchi hizo.

**Huduma Mpya Zilizoznzishwa**

Alisema katika kuanza kutoa huduma ya uchunguzi za MRI, baada ya mashine kununuliwa kupitia fedha za mkopo nafuu kutoka IMF, huduma za kibingwa za uchunguzi za MRI zimeanza kunufaisha wananchi kwa gharama nafuu ambapo takribani wagonjwa 200 kila mwezi hufanyiwa uchunguzi.

Alieleza kuwa, serikali ya Rais Dk. Samia, imewawezesha kuanza utoaji wa huduma kwa wagonjwa wanaohitaji uangalizi wa karibu (Intensive Care Unit) yaani ICU na kwa sasa wagonjwa wanaohitaji huduma ya ICU hupatiwa huku wap wana uwezo wa kulaza wagonjwa 24 kwa wakati.

Alisema katika kipindi cha miaka mitatu ya Rais Dk. Samia, imeweza kutoa kiasi cha fedha jumla ya sh. bilioni 31.269 kugharamia utekelezaji wa miradi mbalimbali ikiwemo mradi wa PET/CT, ukarabati wa majengo na ununuzi wa vifaa vya ICU, ununuzi wa mashine za MRI, CT Scan na digital x-ray, ujenzi wa jengo la onkolojia, ununuzi wa mashine ya CT Scan.

Dk. Mwaiselage alisema wanaishukuru serikali kwa uwekezaji mkubwa ambao umeimarisha huduma za uchunguzi na tiba kwa magonjwa ya saratani nchini na uwekezaji huo wa tiba ya saratani umepunguza rufaa ya wagonjwa nje ya nchi na kuvutia wagonjwa wengi kutoka nje ya nchi.

**Fedha ambazo Serikali Imeokoa**

Mkurugenzi Mwaiselage alisema kwa uboreshaji mkubwa wa miundombinu uliofanywa na serikali eneo la matibabu na uchunguzi wa kibingwa na ubingwa bobezi, rufaa za matibabu nje ya nchi zimepungua, ambapo kipindi cha miaka mitatu ya awamu ya sita wagonjwa 41, walipatiwa rufaa nje ya nchi, ukilinganisha na wagonjwa 164 waliopatiwa rufaa nje ya nchi mwaka 2015/16 kwa uchunguzi na tiba.

Alisema sh. bilioni 12, zitaeendelea kuokolewa kila mwaka kwa matibabu ya kibingwa yanayotolewa nchini badala kupeleka wagonjwa nje ya nchi.

**Idadi ya Misamaha kwa Wagonjwa Iliyotolewa**

Alisema wametekeleza maelekezo ya serikali ya wagonjwa kuchangia huduma kulingana na uwezo, ambapo wanachangia huduma bila malipo za OPD, IPD, maabara, radiolojia, tiba mionzi na tiba kemia, hivyo kwa wale wagonjwa wasiokuwa na uwezo wa kuchangia na taasisi hutoa misamaha.

"Katika kipindi cha miaka mitatu ya awamu ya sita Taasisi ilitoa misamaha kwa wagonjwa 42,952 yenye thamani ya sh. bilioni 102.98,"alisema

**Utekelezaji wa Bajeti ya Mwaka 2023/24**

Mkurugenzi Dk. Mwaiselage alisema katika mwaka wa 2023/24, Taasisi iliidhinishiwa jumla ya sh. 38,801,092,603 ambapo, kati ya fedha hizo, sh. 17,142,793,996 kwa ajili ya matumizi mengineyo, sh. 8,908,298,607 ni ya mishahara na sh. 7,750,000,000 ya miradi ya maendeleo na sh. 6,000,000,000 ya dawa na vitendanishi.

Aidha, mwaka 2023/24, ORCI itaendelea kuimarisha huduma za kibingwa na ubingwa bobezi katika uchunguzi na tiba kwa magonjwa ya saratani nchini.

**Alisema miradi ya maendeleo kwa Mwaka 2023/24**

Ujenzi wa Kituo cha Saratani Mbeya, taasisi itaanza utekelezaji wa jengo la kisasa lenye huduma za famasia, wodi za tiba kemia, wodi za binafsi, maabara na mradi wa ujenzi wa jengo la famasi na tiba kemia ambalo vyumba vya upasuaji.



Mashine ya MRI

"Kukamilika kwa mradi huu kutaongeza huduma za upasuaji kwa magonjwa wa saratani, ambapo kwa sasa, tumeanza matayarisho ya utekelezaji wa mradi huu muhimu ambao utaweza kuhudumia wagonjwa kutoka wananchi wa mikoa 11 na nchi jirani zipatazo 6,"alisema.

Alitaja mikoa hiyo ni Mbeya, Iringa, Songwe, Njombe, Songea, Lindi, Mtwara, Kigoma, Tabora, Rukwa na Katavi huku nchi jirani za Malawi, Zambia, DRC, Msumbiji, Angola na Zimbabwe zitaweza kupatiwa huduma za kibingwa za uchunguzi na tiba ya saratani na utekelezaji wa kazi ulianza kwa kutangaza zabuni ya kumpata mkandarasi mshauri ambaye tayari amepatikana na amekamilisha michoro.

Alisema kwa sasa taratibu zinaendelea za kumpata mkandarasi wa ujenzi na mwishoni ya mwezi Februari 2024 zabuni itatangazwa ambapo mradi huu utagharamiwa na serikali ya awamu ya sita chini ya Rais Dk. Samia.

**Ujenzi wa Jengo la Onkolojia Ocean Road**

Alieleza kuwa katika kipindi hiki, Taasisi hiyo imetangaza kwa mara ya pili katika NeST, kumpata mkandarasi wa kutekeleza ujenzi wa jengo la onkolojia kwani mradi wa huo unahusisha ujenzi wa jengo, ambalo litakuwa na kliniki ya kibingwa, wodi za wagonjwa binafsi, wodi za tiba kemia, maabara na duka la dawa la jamii ambapo kwa sasa tathmini ya zabuni inafanyika kwa wazabuni waliowasilisha maombi, huku taasisi imetenga sh. bilioni 2.5 kutoka kwenye mapato ya ndani kwa mradi huu.

**Ununuzi wa Mashine ya CT Scan**

Alifafanua kuwa, Taasisi imenunua mashine mpya ya CT Scan yenye 128 slices na kupanga matibabu ya mionzi ambapo usimikaji unaendelea, ambapo jumla ya sh. bilioni 1.8 zimetolewa na serikali ya Rais Dk. Samia kununua mashine mpya na ya kisasa ya CT scan.

Mkurugenzi Dk. Mwaiselage, alimshukuru Rais Dk. Samia kwa kusaidia kuimarisha huduma za saratani, huku akiwataka Watanzania kuwa na desturi ya kufanya uchunguzi wa afya angalau mara moja kila mwaka kupunguza vifo vya mapema na kuimarisha uchumi wao, familia na Taifa kwa ujumla.



Mashine ya CT SCAN

AMANA HOSPITAL

## HOSPITALI YA RUFAA YA MKOA - AMANA

## TOLEO MAALUMU LA MIAKA MITATU YA UONGOZI WA

# RAIS DKT. SAMIA SULUHU HASSAN KATIKA SEKTA YA AFYA

Afya bora ni muhimu katika maisha ya mwanadamu yoyote, kila Mwanadam anahitaji kuwa na Afya bora ili aweze kumudu shughuli na majukumu yake ya kila siku. Kwa kuzingatia hilo serikali ya awamu ya sita ya Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan. imezipa kipaumbele kwa kuboresha huduma zinazotolewa kwa wananchi kuanzia ngazi ya jamii kwakutoa mafunzo wahudumu wa afya ngazi ya jamii. , serikali imefanikisha hilo kwa kupeleka wataalamu wa Afya wenye ujuzi katika Zahanati zote nchini, vituo vya Afya, hospitali za Wilaya, hospitali za rufaa, hospitali za kanda, hospitali maalumu, na hospitali ya Taifa.



**Dkt Bryceson Kiwelu**
Mganga mfawidhi Hospitali ya Rufaa ya Mkoa Amana.

Miongoni mwa hospitali za rufaa zilizoboreshwa na serikali ya awamu ya sita ni Hospitali ya Rufaa ya Mkoa – Amana.

Hospitali ya Amana ni kati ya hospitali 28 za rufaa nchini, iliyoanzishwa mwaka 1954 kama zahanati na kupandishwa kuwa kituo cha Afya mwaka 1982. Mwaka 1999 hospitali ya Amana iliboreshwa na kuwa hospitali ya wilaya ya Ilala chini ya TAMISEMI, ilipofika mwaka 2018 ilipandishwa kuwa hospitali ya rufaa na kuwa chini ya wizara ya Afya.

Hospitali ya Amana inahudumia wagonjwa 13,000 hadi 16,000 kwa mwezi hii ni kutokana na kuwa hospitali ipo katikati ya jiji ambapo kuna mkusanyiko wa watu kutoka sehemu mbalimbali na vituo vya usafirishaji ikiwemo vya mabasi, treni, uwanja wa ndege pamoja na bandari zinazo pokea wageni kutoka ndani na nje ya nchi.

Serikali ya awamu ya sita ya Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kupitia Wizara ya Afya inayosimamiwa na Waziri wa Afya Mhe. Ummy Mwalimu imefanikisha maboresho katika hospitali ya Rufaa ya Mkoa - Amana , imeboresha miundombinu na manunuzi ya vifaa tiba vya kisasa ili kuimarisha utoaji wa huduma bora. Maboresho yaliyofanyika ni pamoja na;







Lango kuu la kuingilia pamoja na mapokezi katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa – Amana.

Huduma za radiolojia ikiwemo ujenzi wa jengo la X – ray, ununuzi wa mashine za kisasa za huduma ya X – ray , mashine ya CT Scan. Maboresho haya yamesaidia kupunguza utoaji wa rufaa za wagonjwa wanaohitaji huduma za tiba mionzi kwenda Hospitali ya taifa Muhimbili.

Safari ya mafanikio katika kuboresha huduma za vipimo vya maabara imefanywa ununuzi wa mashine zenye teknolojia za kisasa katika maabara ambazo zilifanikisha maabara ya hospitali ya Rufaa ya mkoa Amana kupatiwa cheti cha ITHIBAT.

Hospitali hii ilipata nafasi na uwezo wa kutoa na kupima



Mashine ya kisasa kwaajili ya vipimo vya CT scan katika hospitali ya Amana.



Maabara yenye mashine na vifaa vya kutosha vyenye teknolojia ya kisasa

# TOLEO MAALUMU LA MIAKA MITATU YA UONGOZI WA RAIS DKT. SAMIA SULUHU HASSAN KATIKA SEKTA YA AFYA


Wodi ya wagonjwa wanaohitaji uangalizi maalumu (ICU)

virusi vya Uviko – 19 ikiwa ni moja ya kambi zilizochaguliwa kuwahudumia wagonjwa hao wa Uviko – 19.

Kupitia maboresho ya Serikali ya awamu ya sita, hospitali imafanikiwa kupata karakana ya kutengenezea miwani kwa watu wenye uoni hafifu, pamoja na mashine za kisasa za kutengeneza meno bandia.

Kitengo cha huduma za wagonjwa wanaohitaji msaada na uangalizi maalumu (ICU) kimeboreshwa kwa kununua mashine za kisasa na zenye ubora, pia uwepo wataalamu wenye ujuzi wa kutoa huduma kwa ukaribu.

Huduma ya usafishaji damu kwa wagonjwa wenye matatizo ya figo.Kwakupitia wiara ya Afya serikaliiilianzisha huduma ya usafishaji figo kwa kununua mashine za kisasa,uwepo wa wataalamu wabobezi wenye mafunzo ya kitaalamu ya kutumia mashine za kisasa za matibabu ya figo(dylisis).

Kwa jitihada za uongozi wa Dkt. Samia hospitali imefanikiwa kupata mashine za uzalishaji wa Gesi ya Oxygen kwaajili ya kusaidia wagonjwa wenye shida ya upumuaji, gasi hii inasaidia katika Hospitali ya Amana na hospitali za jirani.

Maboresho ya miundombinu ni moja kati ya mafanikio muhimu katika hospitali ya Rufaa ya Mkoa – Amana, ambapo majengo ya zamani yameboreshwa na kuwa katika muonekano wa kisasa ikiwemo jengo la Huduma za Dharura (emergency) lenye vifaa na mashine za kisasa pamoja na wataalamu walioboboea katika kutoa huduma za dharura.

Jengo jipya la Ofisi za Utawala, Jengo la upasuaji, jengo la utakasaji wa vifaa vya kutolea huduma. Pamoja na hayo pia kuna maboresho ya jengo la kutolea huduma za wagonjwa binafsi (Private).

Matumizi ya mfumo wa tehama katika utoaji wa huduma umesaidia upatikanaji wa haraka wa huduma za Afya kwa wagonjwa, hii imesaidia kufuatilia hatua za matibabu ya mgonjwa kutoka sehemu moja kwenda sehemu nyingine.

Katika uongozi wa awamu ya sita umesaidia uboreshaji wa mfuko wa bima za afya kwa kuwapa watumishi wanaohusika na bima mafunzo pamoja na ushirikiano na mifuko mingine ya bima ambazo hazikupatikana hapo awali ikiwemo.

Uboreshaji wa huduma saidizi za Afya umefanyika kwa kutoa mafunzo mara kwa mara ili kuboresha huduma za Afya .

Upatikanaji wa huduma ya kusafirisha wagonjwa wa haraka kwa kutumia magari maalumu ya wagonjwa (Ambulance) pamoja na uwepo wa magari ya uendeshaji wa shughuli za kiutawala.

Serikali ya Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan iliona sababu ya kuweka kitengo cha habari na Uhusiano ambacho ndio daraja kati ya hospitali, serikali na wananchi kupitia taarifa na urejeshwaji wa maoni kwa taasisi kutoka kwa wananchi. Kupitia kitengo hiki, Pamoja na mafanikio mengine Amana Hospitali iliibua huduma ya mama aliyejitolea kulea kwakukumbatia watoto wenye uzito pungufu (njiti) na Rais aliliona hili akatoa mkono wa pongezi kwa mama huyo Mariamu Mwakabungu.

Serikali ya Rais Samia imefadhili watumishi kupata mafunzo katika ngazi mbalimbali ikiwa pamoja na ngazi za kibingwa na uzamili ili kuongeza ujuzi utakao saidia utoaji wa huduma bora za Afya nchini.

Maboresho haya yaliyofanyika katika sekta ya Afya yamerahisisha utoaji wa huduma bora za Afya katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa - Amana.


Jengo la huduma za usafishaji figo katika hospitali ya Rufaa ya Mkoa - Amana

"AFYA YAKO NI AMANA YAKO"




Muonekano wa jingo la huduma za Dharura( Emegency) katika hospitali ya Amana.




Jengo la kutolea huduma za Binafsi (Private Service)


Magari mawili mapya kutoka serikali ya awamu ya sita moja la kubebea wagonjwa na la pili la kuendesha shughuli za kiutawala katika hospitali ya Amana.

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA AFYA
HOSPITALI YA RUFAA YA MKOA WA NJOMBE

# Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Njombe yajivunia huduma bora kwa miaka mitatu ya Rais Dk. Samia



Na ELIZABETH JOHN

HOSPITALI ya Rufaa ya Mkoa wa Njombe ni moja ya hospitali zinazojivunia miaka mitatu ya Rais Samia Suluhu Hassan, kuwa madarakani.

Wiki hii kuelekea kilele cha maadhimisho ya miaka mitatu ya Rais Dk. Samia madarakani tangu alipoanza majukumu hayo makubwa akipokea kijiti cha aliyekuwa Rais Hayati Dk. John Magufuli.

Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Rufaa Mkoa wa Njombe, Dk. Gilbert Kwesi, alisema yapo mafaniko mengi ambayo wanajivunia katika uongozi wa Rais Dk. Samia.

"Tunajivunia kukamilishwa kwa ujenzi wa jengo la huduma za afya ya mama na mtoto jengo lenye uwezo wa kulaza wagonjwa 152, lina sehemu ya kujifungulia yenye uwezo wa kuhudumia wajawazito 12 kwa wakati mmoja.

"Jengo hilo lina vyumba vya upasuaji viwili, sehemu ya kuhudumia watoto wachanga wenye mahitaji maalum na kliniki kwa wajawazito na akina mama waliotoka kujifungua," alisema.

Alisema pia walikamilisha ujenzi wa jengo la magonjwa ya ndani na Upasuaji ambapo walitumia zaidi ya sh. bilioni 3.3 katika kukamilisha ujenzi wa Jengo hilo.

Dk. Kwesi alisema katika kipindi hicho waliweza kununua mashine za kisasa kwa ajili ya vipimo na uchunguzi ikiwemo Digital x-rays machine na CT Scan.

"Ujenzi wa Jengo la CT Scan ambalo ndilo linalotumika kuhifadhia mashine hiyo, tulinunua mashine za kisasa katika jengo la huduma za dharura na wagonjwa mahututi.

Alisema wameweza kukamilisha jengo la huduma za dharura na wagonjwa mahututi yaani (EMD&ICU), pia wamepokea watumishi 101 wa ajira mpya.

"Kuna fedha za miradi ya Uviko-19 ambapo sh. bilioni 3.8 zilipokelewa katika mwaka wa fedha 2021/2022 ambazo zilielekezwa katika ujenzi wa Jengo la Radiolojia.



Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Rufaa Mkoa wa Njombe, Dk. Gilbert Kwesi.

"Kuna fedha za miradi ya Maendeleo ambazo zilitumika kujenga majengo mapya na kukamilisha yale ambayo yalikuwa tayari utekelezaji wake umeanza tangu serikali ya awamu ya tano, mwaka wa fedha 2021/2022 Hospitali ilipokea Tsh. 2,974,085,285.00, mwaka wa fedha 2022/2023 hospitali ilipata tena fedha kiasi cha Tsh. 698,228,402.57 kwaajili ya miradi ya maendeleo.

Alisema fedha hizo zilitumika katika kukamilisha ujenzi wa majengo ya kituo cha damu salama Mkoa wa Njombe, ujenzi wa jengo la kuhifadhia maiti, jengo la kufulia nguo, jengo la kuchomea taka na ukamilishaji wa majengo ya huduma za mama na mtoto, jengo la huduma za magonjwa ya ndani, pamoja na jengo la huduma za dharura na wagonjwa mahututi.

**JINSI WALIVYOJIPANGA KUSIMAMIA MIRADI**

Alisema uwepo wa usimamizi mzuri wa miradi kupitia kamati ya ujenzi, Kamati ya fedha na kamati ya manunuzi ili kuhakikisha fedha zinazotolewa kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa miundombinu inafanya kazi, sawa na ilivyokusudiwa kutumika.

"Kuwepo na usimamizi na utunzaji wa vifaatiba, mashine na majengo ni kati ya vitu ambavyo tunavizingatia ili kuhakikisha tunaenda sambamba na kasi ya Serikali ya Awamu ya sita katika utoaji huduma zilizo bora, nafuu na zenye kukidhi haja ya watanzania.

"Kudhibiti na kusimamia utoaji huduma bora na zenye viwango vinavyoendana na hadhi ya Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Njombe, uwepo wa vifaa vya kisasa, mashine na majengo bora, ni sababu tosha zinazotupa msukumo wa kuendelea kusimamia ubora wa huduma ili yale yote ambayo serikali inatamani watanzania wafaidike nayo kupitia sekta hii waweze kuyapata kwa kiwango stahiki," alisema.

**NENO KWA SERIKALI**

"Kwanza tunamshukuru sana Rais Samia kwa kiasi kikubwa tumeshuhudia mapinduzi makubwa sana katika sekta hii muhimu kwa wananchi.

"Ni katika awamu hii tumeshuhudia ununuzi wa vifaatiba vya kisasa na mashine zenye uwezo mkubwa wa utambuzi wa magonjwa na hitilafu katika mwili wa binadamu," alisema daktari huyo.

Alisema wanaiomba serikali yetu iendelee kutoa fedha za uendeshaji wa Hospitali ikiwemo fedha za ruzuku (OC) ili kuongeza ufanisi katika utoaji huduma na kupunguza uwezekano wa kuingia katika madeni.

Dk. Kwesi aliomba serikali iendelee kutoa fedha za kuwasomesha wataalamu wanaojiendeleza katika taaluma zao, kwa kusimamia na kuwapatia ufadhili wa masomo ya nje na ndani ya nchi ili kuongeza wigo mpana wa utoaji wa huduma za kibingwa karibu na wananchi.






















Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan



MKURUGENZI MKUU WA MSD, MAVERE TUKAI

# MSD

## NA MAFANIKO LUKUKI MIAKA MITATU YA RAIS SAMIA









MIAKA MITATU YA RAIS DK. SAMIA NA UBORESHAJI YA SEKTA YA AFYA NCHINI

# MSD na mafaniko lukuki miaka mitatu ya Rais Samia

## >>Yajivunia kuwa na viwanda vya Gloves, Barakoa





Mkurugenzi Mkuu wa MSD, Mavere Tukai







Na MWANDISHI WETU

BOHARI ya Dawa (MSD) ni idara ya serikali iliyopo chini ya Wizara ya Afya ambayo ilianzishwa mwaka 1993 kwa Sheria ya Bohari ya Dawa, Sura ya 70 kama ilivyorekebishwa mwaka 2021.

MSD ina majukumu makuu manne ambayo ni Uzalishaji, Ununuzi, Uhifadhi na Usambazaji wa bidhaa za afya kwa ajili ya vituo vya kutolea huduma za afya vya umma zaidi ya 7,600 nchi nzima na baadhi vya binafsi vilivyoidhinishwa na Wizara ya Afya.

Katika kuadhimisha miaka mitatu ya Rais Samia Suluhu Hassan, yapo mambo mengi ya kujivunia ambayo Bohari ya Dawa (MSD) imeweza kufanikisha katika sekta ya afya, ambayo yamechangia kwa kiasi kikubwa kuboresha afya za wananchi chini ya uongozi wa serikali ya awamu ya sita.

Maboresho haya ya huduma za Bohari ya Dawa yamekuwa na matokeo chanya katika utoaji wa huduma za afya nchini, kuanzia ngazi ya msingi yaani zahanati, vituo vya afya, hospitali za wilaya, mikoa na kanda mpaka taifa.

Mafanikio ya Bohari ya Dawa MSD Miaka Mitatu ya Samia.

### UPATIKANAJI WA BIDHAA ZA AFYA NCHINI.

Kwamujibu wa Mkurugenzi Mkuu wa MSD Mavere Tukai, hali ya upatikanaji wa bidhaa za afya nchini imeendelea kuimarika siku hadi siku, hapo nyuma upatikanaji wa bidhaa za afya ulikuwa kwa kiwango cha kati, kwani mnamo Julai mwaka 2021 upatikanaji wa bidhaa za afya kwenye maghala ya Bohari ya Dawa ulikuwa ni asilimia 57 na ilivyofikia Desemba 2023 upatikanaji wa dawa ulipanda hadi kufikia asilimia 84.

Aidha, hali hii ilichangiwa na maboresho yanayoendelea Bohari ya Dawa na dhamira ya Serikali kuimarisha sekta ya afya ambapo kwa mwaka wa fedha 2022/23, Serikali ilitoa kiasi cha sh. bilioni 190.9 kati ya bajeti yake ya sh. bilioni 200 sawa na asilimia 95.5 kwa ajili ya ununuzi wa bidhaa za afya.

Mbali na hilo, Bohari ya Dawa pia imeingia mikataba ya muda mrefu na washitiri hatua ambayo imesaidia sana kuimarisha hali ya upatikanaji wa bidhaa za afya nchini. Aidha, MSD imeimarisha kitengo cha ufuatiliaji wa mikataba (Contract Compliance Management) ili kuhakikisha mikataba baina ya MSD na Washitiri inatekeleza kwa mujibu wa matakwa ya mkataba na sheria.

"Katika hatua nyingine serikali imekuwa ikihakikisha inaboreshaupatikanaji wa vifaa tiba ambavyo sasa hivi vimeweza kufika ngazi mbalimbali za utoaji huduma hivyo kupunguzia wananchi umbali mrefu wa kufuata huduma.

"Baadhi ya vifaa tiba ambavyo Serikali imesambaza vinahusika na uangalizi wa dharura na vifaa vinavyotumika katika uangalizi maalum, vikiwepo vifaa vya ICU sambamba na mitambo maalum inahitajika kama mitambo ya oksijeni," alisema Tukai.

Anasema ili kuhakikisha afya ya mama na mtoto inakuwa salama, serikali ilitoa kiasi cha shilingi bil. 105 kwa ajili ya ununuzi wa vifaa tiba kuwezesha uzazi pingamizi, huku fedha hizo zikitolewa kwa vituo 398 nchi nzima, ambapo hadi sasa bidhaa za afya zenye thamani ya shilingi bilioni 83.2 zimekwisha pelekwa katika vituo hivyo.

### UANZISHAJI WA VIWANDA VYA BIDHAA ZA AFYA

Katika Miaka mitatu ya Rais Samia Madarakani, kuna mambo mengi ya kujivunia kwa Bohari ya Dawa (MSD), kufuatia mageuzi mbalimbali yaliyofanyika katika sekta ya afya kwa lengo la kuboresha hali ya upatikanaji wa bidhaa za afya nchini, hususani uanzishwaji wa viwanda.

Tukai anasema moja ya maboresho hayo ni kuanza kwa uzalishaji wa bidhaa za afya, ikiwa ni jukumu geni lililoanza kutekelezwa mwaka 2021 baada ya sheria ya MSD kufanyiwa marekebisho bungeni.

Kutokana na mabadiliko hayo ya kisheria, serikali kupitia bohari ya dawa ikaamua kufanya jitihada ambapo moja ni ujenzi wa kiwanda cha kuzalisha bidhaa za mpira wa mikono (Gloves).

"Ujenzi huu ulikamilika na Januari mwaka huu 2024 na kiwanda hiki kimeanza kufanya uzalishaji, fedha zilizotumika ni za serikali na hii ni mara ya kwanza tunamiliki kiwanda kinachozalisha mipira hiyo," alisema.

Tukai anasema malengo ya kujenga kiwanda hicho ni kuiwezesha nchi kujikinga na magonjwa ya dharura pale yanapotokea ambapo walijifunza ilipotokea UVIKO 19 na kuleta taharuki duniani hivyo serikali iliamua kujiwekeza na kuhakikisha nchi inaweza kupambana na dharuara za aina hii

Tukai anasisitiza kuwa kiwanda hicho kina uwezo wa kuzalisha jozi elfu 10 za mipira ya mikono kwa saa, ambazo ni sawa na mipira ya mikono elfu 20 kwa saa na kupitia kiwanda hicho wataweza kutoa ajira zaidi ya 200 na tayari kiwanda hicho kimeanza kuzalisha na matarajio ni kuzalisha mipira ya mikono jozi milioni 86.4.

"Kupitia uzalishaji huo nchi itaweza kujitegemea kwa silimia 83.4 kwenye bidhaa hii hivyo kupunguza gharama za uagizaji wa bidhaa hii kutoka nje ya nchi na kuweza kuhifadhi fedha za kigeni ambazo bidhaa hizo zilikuwa na thamani ya zaidi ya sh. bilioni 20," alisema.

Katika hatua nyigine serikali kupitia MSD imeweza pia kujenga kiwanda kidogo cha bidhaa kinga cha barakoa ambapo kinazalisha barakoa za kawaida na barakoa maalumu.

Barakoa hizi zinatumika katika matumizi mbalimbali ya kujikinga na maambukizi au vihatarishi, pia zinatumiwa na watoa huduma katika vituo vya kutolea huduma za afya nchini, ambapo mpaka hii leo, kiwanda hiki kimezalisha barakoa zenye thamani ya sh. bilioni 4.

Tukai anasema katika kuhakikisha uzalishaji wa bidhaa za afya unakuwa wa uhakika, endelevu na shindani, MSD iliweza kuanzisha kampuni tanzu ambayo itatumika kusimamia uanzishaji na uzalishaji wa bidhaa za afya, lakini pia itakuwa na uwezo wa kuingia ubia na wawekezaji wengine.

"Kampuni hii itaweza kusimamia mradi wa mipira wa mikono uliopo mkoa wa Njombe, eneo la viwanda Zegereni lililopo mkoa wa Pwani, kiwanda cha barakoa kilichopo mkoa wa Dar es Salaam na uzalishaji wa pamba tiba eneo la Simiyu. Alisema Tukai.

Aidha, MSD kupitia balozi za Tanzania zilizopo Korea ya Kusini, China, Algeria, Urusi, na maeneo mengine duniani wamekuwa wakifanya kazi ya kutambua wazalishaji na wawekezaji kuhakikisha wananunua bidhaa za afya za uhakika na zenye ubora na kuwezesha bidhaa nyingine kuzalishwa nchini.

Katika hatua nyingine, Tukai anasema kupitia ushirikishwaji huu wa sekta binafsi wameweza kutangaza na kuwaalika wawekezaji wenye nia kuja kuwekeza katika viwanda vyetu vikuu kikiwemo kiwanda cha Pamba mkoani Simiyu.

Mkurugenzi huyo anasisitiza kwamba MSD wameonesha nia na uwekezaji unaendelea na wanahitaji ushirikiano kwenye uanzishaji na uendelezaji wa viwanda.

### UHIFADHI WA BIDHAA ZA AFYA.

Akieleza kuhusu uimarishwaji wa eneo la uhifadhi wa bidhaa za afya, ambalo ni miongoni mwa majukumu ya msingi ya Bohari ya Dawa, anasema serikali kupitia MSD imeweza kuanzisha






## MIAKA MITATU YA RAIS DK. SAMIA NA UBORESHAJI YA SEKTA YA AFYA NCHINI

# MSD na mafaniko lukuki miaka mitatu ya Rais samia

ujenzi wa maghala makubwa ya kisasa, na yenye kukidhi viwango vya kimataifa katika kanda zake za Mtwara na Dodoma.

Kuhusu Ghala kubwa linalojengwa Dodoma litakuwa na ukubwa wa sqm.7,200 na litatumika kama kitovu cha uhifadhi kwa kanda nyingine za karibu na kupunguza mrundikano wa bidhaa kwa ghala kubwa lililoko Dar es salaam. Sambamba na hilo ghala hili litaokoa muda wa usafirishaji, kwani kanda zetu zilizoko Kanda ya Ziwa, pamoja na nyanda za juu kusini hawatalazimika kusafiri mpaka Dar es salaam kufuata bidhaa bali zitapatikana hapa hapa Dodoma.

Kwa upande wa ghala la Mtwara litakuwa na ukubwa wa sqm. 4,800 na kusaidia upatikanaji wa bidhaa za afya kwa mikoa ya kusini, kwani hivi sasa ghala lililopo halikidhi mahitaji, lakini pia linahusisha gharama kubwa za uendeshaji kutokana na uwezo mdogo wa kuhifadhi bidhaa.

Juu ya hilo, anasisitiza kuwa ujenzi huo umefikia hatua nzuri na utakamilika katika mwaka ujao wa fedha 2024 na utagharimu kiasi cha shilingi. bilioni 39, huku fedha zote za ujenzi zikiwa zimetolewa na Serikali ya Rais Samia Suluhu Hassan.

Tukai anasema kuwa matarajio ya MSD ni kuongeza uwezo wa nchi kuhifadhi bidhaa za afya katika kipindi chote, ili kukidhi mahitaji ya ongezeko la watu na ongezeko la idadi ya vituo vya afya nchini, ikiwemo vilivyoongezwa hadhi na vingine kujengwa upya.

Aliongeza kuwa wanalenga kuimarisha uhifadhi wa bidhaa za afya kwa kujenga maghala mengine katika mikoa ya Mwanza, Iringa, Kilimajaro, Dar es salaam na Kagera.

**USHIRIKISHAJI WA SEKTA BINAFSI**

Katika kipindi hiki cha awamu ya sita, ili kuongeza tija na ushirikishwaji wa sekta binafsi katika eneo la uzalishaji, na kupunguza utegemezi wa bidhaa kutoka nje, serikali kupitia MSD iliona kuna haja ya kuitisha wazalishaji wa ndani ili washiriki kikamilifu katika uzalishaji wa bidhaa za afya nchini.

MSD imetengeneza mfumo wa baadhi za bidhaa kununuliwa kutoka kwa wazalishaji wa ndani ya nchi, na kwa hatua hiyo imeanza kuleta tija, kwani kwa mwaka wa fedha wa 2021/22 bidhaa za afya zenye thamani ya sh. bilioni 14.1 zilinunuliwa kutoka kwa wadhalishaji wa ndani.

Aidha, Mwaka wa 2022/23 kiasi hicho kiliongezeka na kufikia sh. bilioni 39.77. Hatua hii ya serikali kushirikisha wazalishaji wa ndani, inalenga kuhakikisha wanakuwa ni sehemu ya uzalishaji maalum, kuhakikisha tunapunguza utegemezi kutoka nje ya nchi.

Kwa upande mwingine, katika kipindi hiki cha Rais Samia mapato yanayotokana na kazi ya MSD yameongezeka maradufu, ambapo mwaka wa fedha 2020/21, MSD ilipata jumla ya sh. bilioni 230.5 huku kwa mwaka jana 2022/2023 mapato hayo yaliongezeka na kufikia sh. bilioni 379 ambalo ni ongezeko la asilimia 64%

"Mwaka huu wa fedha 2023/2024 tumejiwekea malengo ya kufikisha zaidi ya sh. bilioni 500, kwa sababu serikali ilitoa fedha katika vituo vya huduma za afya na kuweka fedha bohari ya dawa kwa ajili ya kuimarisha upatikanaji toshelevu wa bidhaa za afya nchini," alisema.












**MSD ILIVYOBORESHWA**

Tukai anasema kitu kingine kilichofanyika chini ya uongozi imara wa Rais Dk. Samia ni uteuzi wa bodi ya wadhamini na mabadiliko ya Menejimenti ili kuimarisha uongozi wa Taasisi. Katika mabadiliko hayo, Serikali ya Jamhuri wa Muungano wa Tanzania ilitoa kibali cha ajira ya nafasi nane (8) za uongozi, ambapo nafasi nne (4) kati ya nane (8) zilizotangazwa tayari zimejazwa na hatua za kujaza nafasi nne (4) zilizosalia zinaendelea.

, sambamba na kubadilisha watumishi na kupeleka watumishi wengi zaidi wanaokidhi mahitaji ya utendaji wa upatikanaji wa bidhaa za afya.

Aidha, kwa kipindi cha miaka mitatu kuanzia Machi 2021/24, Serikali imeajiri jumla ya watumishi mia mbili na ishirini na tisa (229) kwa upande wa bohari ya dawa kwa Kada mbalimbali ikiwemo Wafamasia, Wataalamu wa Ununuzi na Ugavi na Wahandisi wa Vifaa Tiba, Lengo likiwa ni kuiwezesha Bohari ya Dawa kutekeleza kwa ufanisi Majukumu ya Msingi yaani Kuzalisha, Kununua, Kutunza na Kusambaza dawa, vifaa tiba na vitendanishi vya maabara.

Maboresho hayo yamekwenda kuimarisha utendaji na kuhakikisha sheria, taratibu na kanuni zinazingatiwa. Aidha, maboresho haya yamekwenda sambamba na kuhakikisha kunakuwepo na mikataba ya muda mrefu ya ununuzi na kuimarisha mifumo ya tehema; haya ni sehemu ya mafanikio kwa kipindi chote cha Rais Samia.

Mbali na hayo, Mikakati iliyopo ni kuongeza uwezo wa kifedha wa Bohari ya Dawa, ambapo sasa tutahakikisha tunaendeleza viwanda vinavyotaka kuanzishwa vya kimkakati na kuvisimamia ili kuhakikisha vinafanya uzalishaji wenye tija," alisema.

Anasisitiza kuwa MSD inaendelea kushirikiana na Serikali na kutambua mabadiliko mbalimbali yanayofanywa ikiwemo ya bima ya afya kwa wote na kutambua nafasi yake kuhakikisha Watanzania wanapata huduma stahiki.

**SHUKRANI**

Tukai, anasema wanaishukuru serikali kwa kuiwezesha kufikia mafanikio hayo kutokana kuweka kipaumbele katika sekta ya afya.

"Serikali ya awamu ya sita imeweka kipaumbele katika sekta ya afya hasa utoaji wa fedha za ununuzi wa bidhaa za afya, tunaishukuru kwa kutuwezesha kupiga hatua hizi ambazo leo tumeweza kusema kwa uwazi.

"Tunaomba serikali iendelee kutuunga mkono na izidi kutuamini na kutuelewa kama inavyotuelewa ili kuweza kutekeleza ilani ya chama ambapo inatutaka tuhakikishe bidhaa za afya zinafika katika vituo vya kutolea huduma za afya, lakini pia inatuhitaji tuwe na hivyo viwanda," alisema.

Anasema wanaushukuru uongozi wa Wizara ya afya chini ya Mhe. Ummy Mwalimu kwa usimamizi thabiti wa majukumu ya bohari ya dawa, na kuahidi kuendelea kuboresha sekta hiyo kwa mujibu wa maelekezo ya serikali.

Tunaomba wananchi watambue MSD ni taasisi ya umma na huduma inazofanya zinazingatia misingi ya sheria, kanuni na taratibu kwa hiyo waamini kwamba majukumu ambayo MSD imepewa, yanafanywa na kuwataka wananchi wawe na imani kuwa MSD itahakikisha bidhaa za afya zinapatikana kwenye vituo vya umma vya kutolea huduma za afya.

"Yote yanayofanywa na MSD ni maelekezo ya serikali, na kama kuna changamoto yoyote, inayotokana na utendaji wa MSD, ningependa kuwafikia wananchi na kuwahakikishia kuwa huduma zinazotolewa na MSD kwaniaba ya serikali zitazidi kuimarika," alisema.

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

Wizara ya Afya

**Hospitali ya Rufaa ya Mkoa Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere - Mara**




# Hospitali ya Rufaa ya Mkoa ya Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere - Mara na ubora wa huduma miaka mitatu ya Rais Dk. Samia

**Na ELIZABETH JOHN**

HOSPITALI ya Rufaa ya Mkoa ya Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere, inajivunia mafanikio makubwa yanayoendelezwa chini ya uongozi wa Rais Dk. Samia suluhu Hassan.

Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa ya Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere, Dk. Osmundi Dyegura, alisema chini ya Wizara wanaendelea na ukamilishaji wa ujenzi wa ambapo hadi sasa sh. 15,495,850,136.85 zimetumika katika ujenzi.

Alisema serikali ya awamu ya sita imeendelea na utekelezaji wa mradi wa sekta ya afya kwa fedha za mkopo wa masharti nafuu kutoka shirika la fedha Duniani (IMF) kwa ajili ya ununuzi wa vifaa tiba.

"Kwa upande wa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa ya Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere Serikali ilitenga kiasi cha sh. 4,190,444,000 kwa ajili ya ununuzi wa vifaa tiba mbalimbali kama vile CT Scan, digital x-ray mashine na vingine.

Alisema serikali ya awamu ya sita imeendelea kutenga fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo ikiwemo ukamilishaji wa ujenzi wa Hospitali ya Kumbukumbu ya



MGANGA Mfawidhi wa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa ya Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere, Dk. Osmundi Dyegura.

Mwalimu Nyerere.

Alisema pia serikali imeajiri watumishi mbalimbali wa kada za afya kutoa huduma bora kwa wanachi , halikadhalika serikali inafadhili masomo kwa watumishi mbalimbali walioko masomoni katika fani mbalimbali za kibingwa.

> **Kwa upande wa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa ya Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere Serikali ilitenga kiasi cha sh. 4,190,444,000 kwa ajili ya ununuzi wa vifaa tiba mbalimbali kama vile CT Scan, digital x-ray mashine na vingine.**
>
> **Dk. Osmundi Dyegura.**

**HUDUMA ZA KIBINGWA**

Dk. Dyegura alisema hospitali inatoa huduma za kibingwa kama vile, magonjwa ya ndani, upasuaji, magonjwa ya akina mama na uzazi, mifupa na magonjwa ya watoto.

Alisema hospitali hiyo imejipanga kupanua wigo wa huduma za kibingwa kwa kusomesha madaktari bingwa katika fani za magonjwa ya dharura, sikio, pua na koo, mifupa, magonjwa ya ndani, macho, magonjwa ya kina mama na uzazi, magonjwa ya watoto pamoja na watoa dawa za usingizi.

"Hali ya upatikanaji wa dawa na vifaa tiba ni ya kuridhisha, katika Hospitali, serikali imejitahidi kuongeza vifaa tiba vya kibingwa kama vile mashine ya CT Scan, mashine za uchujaji wa damu na vingine," alisema.

**ILIVYOJIPANGA KUSIMAMIA**

Dk. Dyegura alisema uongozi wa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa ya Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere umejipanga kikamilifu katika kuitunza na kuendeleza miundombinu ya miradi iliyotekelezwa na serikali ili iweze kutoa huduma bora na endelevu ambazo ni nafuu na zinazofikika kwa wananchi wa Mkoa wa Mara na maeneo ya jirani kwa kutumia rasilimali zilizopo.

Alisisitiza kuwa hospitali imejipanga kuongeza idadi ya huduma za kibingwa pamoja na kuimarisha tiba utalii ili kuwavutia wateja wengi zaidi.

**SHUKRANI KWA RAIS DK. SAMIA**

Daktari huyo aliishukuru serikali ya awamu ya sita inayoongozwa na Rais Dk. Samia kwa jitihada zake za kuboresha sekta ya afya kwa kuhakikisha uwepo wa miundombinu thabiti ya kutolea huduma kama vile majengo ya kisasa, vifaa tiba, watumishi na vitendea kazi muhimu katika utoaji wa huduma za afya nchini.

"Tunajivunia uongozi huu, tumepiga hatua kwa asilimia kubwa kwa sasa hivi sekta afya ni moja ya sekta zilizoendelea tunajivunia hilo," alisema.

**WITO KWA JAMII**

Dk. Dyegura alisema hospitali ya Rufaa ya Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere ingependa kutoa wito kwa jamii ya Mkoa wa Mara na maeneo jirani kutumia huduma za afya zilizobora zinazotolewa hospitalini hapo.

"Huduma zetu ni bora, kwa kushirikiana na serikali yetu tunaendelea kuboresha huduma hizi," alisema Mganga huyo.



CT - Scan



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA AFYA
HOSPITALI YA RUFAA MKOA WA

# SONGEA



RAIS Dk. Samia Suluhu Hassan.






MGANGA Mfawidhi wa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa Songea Dk. Magafu Majura.



WAZIRI wa Afya, Ummy Mwalimu.

# HOSPITALI YA RUFAA ILIVYOMALIZA ADHA YA WAGONJWA KWENDA MUHIMBILI

Ruvuma
Anuani ya Posta: P.O.BOX 5, Songea
Simu: +255 025 2602048
Simu ya Mkononi: +255 737 683544
Barua Pepe: songearrh@afya.go.tz

MIAKA MITATU YA RAIS SAMIA




PICHANI ni jengo la kutolea huduma za dharura (EMD) katika hospitali ya Rufaa ya Mkoa Songea ambalo serikali kupitia Wizara ya Afya ilitoa zaidi ya shilingi milioni 630 kutekeleza mradi huo uliokamilika kwa asilimia 100 na jengo limeanza kutumika tangu Oktoba 2022.

# Hospitali ya rufaa ilivyomaliza adha ya wagonjwa kwenda Muhimbili

SERIKALI ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Rais Dkt.Samia Suluhu Hassan kupitia Wizara ya Afya imetenga zaidi ya shilingi bilioni 6.57 kutekeleza mradi wa hospitali ya Rufaa ya Mkoa Songea.

Fedha hizo ni kwa ajili ya ujenzi wa majengo mapya,ukarabati wa vyumba vya kutolea huduma za afya na ununuzi wa vifaa tiba vya kisasa kwa ajili ya kutolea huduma bora za afya kwa wananchi wa Mkoa wa Ruvuma.

Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa, Songea Dk. Magafu Majura anasema katika mwaka wa fedha 2023/2024 Wizara ya Afya imetenga kiasi cha shilingi bilioni moja kwa ajili ya ukamilishaji wa ujenzi wa jengo wagonjwa wa nje (OPD).

Akizungumzia utekelezaji wa mradi hiyo, Mganga Mfawidhi wa Hospitali Dr. Magafu Majura anayataja majengo yaliyokamilika kwa asilimia 100 kuwa ni ujenzi wa nyumba ya daktari,ujenzi wa jengo la radiolojia kwa ajili ya CT Scan,Digital X Ray na ukarabati wa wodi ya wagonjwa wanaohitaji uangalizi wa karibu (ICU).

Dr.Majura anayataja majengo mengine ambayo yamekamilika kwa asilimia 100 kuwa ni ukarabati wa chumba cha tiba masafa (Telemedidicine), ununuzi wa vifaa kwa ajili ya majengo ya wagonjwa mahututi (ICU), jengo la dharura (EMD), maabara na radiolojia.

> ***"Kutokana na ufinyu wa eneo la hospitali ya Rufaa ya Mkoa Songea, Mkoa uliona umuhimu wa kuwa eneo jipya lenye ukubwa wa hekari 270 katika Kata ya Mwengemshindo Manispaa ya Songea,ambako kumeanzisha ujenzi wa hospitali mpya ya Rufaa ya Mkoa wa Ruvuma"***
>
> **MGANGA MFAWIDHI WA HOSPITALI YA RUFAA YA MKOA, SONGEA DK. MAGAFU MAJURA**



MGANGA Mfawidhi wa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa Songea Dk. Magafu Majura.

"Kutokana na ufinyu wa eneo la hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Songea, Mkoa uliona umuhimu wa kuwa na eneo jipya lenye ukubwa wa hekari 270 katika Kata ya Mwengemshindo Manispaa ya Songea,ambako kumeanzisha ujenzi wa hospitali mpya ya Rufaa ya Mkoa wa Ruvuma",anasema Dr.Majura.

Analitaja jengo muhimu ambalo wameanza nalo ni la wagonjwa wa nje (OPD) ambapo anasema mradi wa jengo hilo unagharimu zaidi ya shilingi bilioni 3.8 ambapo hadi sasa jengo limefikia asilimia 71.

Akizungumzia jengo la radiolojia,Mganga Mfawidhi anasema katika jengo hilo ndani yake kuna mashine mbili za CT Scan na Digital Xray ambazo zinafanya kazi na kwamba vifaa hivyo vina thamani ya zaidi ya shilingi bilioni mbili.

Anasema huduma za CT Scan zilianza kutolewa Machi 2023 hali ambayo imepunguza adha kwa wananchi wa Mkoa wa Ruvuma na mikoa jirani ambao awali walikuwa wanapata huduma hiyo katika hospitali ya Kanda ya Mbeya na hospitali ya Taifa Muhimbili.

Pia Dr. Majura ametoa wito kwa wananchi wa mkoa wa Ruvuma waendelee kuiamini hospitali ya rufaa kwani inatoa huduma nzuri ambapo mpaka sasa inamadaktari bingwa nane ambao wapo kwenye idara za kimkakati.

"Hizi idara nane zinazo madaktari bingwa japo mmoja mmoja lakini wanatoa huduma za kibingwa ikiwemo madaktari bingwa wa maogonjwa ya upasuaji, akina mama na uzazi, magonjwa ya ndani, magonjwa ya dharura, magonjwa ya macho, mionzi na radiolojia kwa ajili ya CT Scan, idara ya watoto pua, masikio na koo" amesema Dr. Majura.

Hata hivyo Mganga Mfawidhi wa Hospitali Dr. Magafu Majura ameishukuru serikali inayoongozwa na Rais samia Suluhu Hassan kwa kuzidi kuendelea kuiboresha hospitali hiyo katika kipindi cha miaka mitatu ya utawala wake madarakani kwa kujali afya za wananchi wake, akiwa na Imani kuwa wakiwa na afya njema wataweza jiletea maendeleo binafsi ambayo yateleta chachu ya maendeleo kwa taifa kwa ujumla.

Mkoa wa Ruvuma una vituo 419 vinavyotoa huduma za afya,kati ya vituo hivyo hospitali zipo 17,vituo vya afya 50 na zahanati 352.

MIAKA MITATU YA RAIS SAMIA

# Makamu wa Rais azindua jengo la mionzi hospitali ya Rufaa Ruvuma




**MAKAMU wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe, Dkt. Philip Mpango akikata utepe kuashiria uzinduzi wa jengo la mionzi la hospitali ya Rufaa ya mkoa wa Ruvuma tarehe 22 julai 2023 alipofanya ziara mkoani Ruvuma.**

MAKAMU wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Philip Mpango azindua Jengo la Mionzi la Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Ruvuma iliyopo katika Kijiji cha Mwengemshindo Manispaa ya Songea.

Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Philip Mpango amesema serikali itaendelea kuboresha maslahi ya wahudumu wa afya kwa kuhakikisha inaboresha Maisha yao na vitendea kazi

Makamu wa Rais amesema hayo tarehe 22 Julai 2023 wakati akizindua Jengo la Mionzi la Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Ruvuma akiwa katika siku ya tatu ya ziara yake ya kikazi mkoani Ruvuma. Ametoa wito kwa watoa huduma za afya kutunza vifaa tiba ikiwemo kuweka utaratibu mzuri wa matengenezo ili viweze kutoa huduma kwa wananchi wakati wote.

Makamu wa Rais amesema ni dhamira ya Serikali inayoongozwa na Rais Samia Suluhu Hassan kuhakikisha inasogeza huduma bora za afya karibu na wananchi ikiwemo kupeleka vifaa tiba vya kisasa katika hospitali za mikoa ili kuwapunguzia gharama wananchi kufuata huduma hiyo maeneo ya mbali.

Aidha Makamu wa Rais amesema Serikali inathamini mchango wa watoa huduma za afya kwa kuwa wanamchango mkubwa katika kuwahudumia wananchi na kuokoa Maisha yao. Amewasihi wahudumu wa afya kuendelea kuwahudumia wananchi kwa upendo mkubwa.

**BILIONI 7 KUWEKEZWA SEKTA YA AFYA MKOA WA RUVUMA**

Serikali ya Awamu ya 6 inayoongozwa na Rais, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan imetoa bilioni 7 kwa lengo la kuboresha utoaji huduma ya Afya kwa wananchi katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Ruvuma

Akizungumza mbele ya wataalamu kutoka Hospitali ya kanda ya Mbeya Mganga Mfawidhi Hospitali ya Rufaa ya Mkoa Songea. Dr, Magafu Majura amesema Hospitali imepokea Shilingi bilioni 7 kukamilisha mipango mikakati ya utoaji huduma kwa wananchi.

> ***"Hii itatusaidia kwa wagongwa watakao hitaji kutibiwa katika Hospitali zetu za kanda na taifa kuweza kuanza kupata matibabu wakiwa bado wapo hapa kwa maana ya kuwasiliama kupitia tiba mtandao na madaktari wabobezi waliopo katika Hospitali zetu kubwa na kutupa majibu"***
>
> **AMESEMA DR. MAJURA**

Dr. Majura amesema fedha hizo zimeelekezwa katika kujenga jengo la wagonjwa wa nje, jengo la huduma ya mionzi pamoja na nyumba moja ya mtumishi pia na ukarabati wa jengo la wagonjwa wenye uangalizi maalumu na jengo la dawa

Mbali na ujenzi na ukarabati huo ameeleza kuwa Serikali imeamua kuboresha utoaji huduma kwa wananchi kwani imenunua vifaa tiba kimoja wapo ni Mashine ya uchunguzi ya CT-Scan ambayo itahudumia na kutoa matibabu kwa haraka na itasaidia kuondoa msongamano wa wagonjwa.

"Hii itatusaidia kwa wagonjwa watakao hitaji kutibiwa katika Hospitali zetu za kanda na taifa kuweza kuanza kupata matibabu wakiwa bado wapo hapa kwa maana ya kuwasiliana kupitia tiba mtandao na madaktari wabobezi waliopo katika Hospitali zetu kubwa na kutupa majibu" Amesema Dr. Majura.

Kwa upande wake Mkuu wa Idara ya magonjwa ya dharura na ajali Dr. Edson Francis ameeleza hali ilivyo sasa baada ya kukamilika kwa jengo hilo la wagonjwa wa dharura ambapo limesaidia kuhudumia wagonjwa wengi kwa haraka na kupata matibabu kwa muda mfupi.

Hata hivyo Serikali imeboresha upatikanaji huduma mbalimbali katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa Songea kwa kununua mashine ya uchunguzi ya CT-Scan kwa mara ya kwanza ambayo itasaidia wananchi wa Mkoa wa Ruvuma kutosafiri umbali mrefu kwenda Mbeya, Dodoma na Dar es salaam kwaajili ya vipimo.



**MRADI wa Ujenzi wa hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Ruvuma inayojengwa Kata ya Mwengemshindo Manispaa ya Songea,hadi sasa serikali imetoa shilingi bilioni tatu kutekeleza mradi huo.**

MIAKA MITATU YA RAIS SAMIA

# Serikali yakabidhi vifaa tiba mtandao hospitali ya Rufaa Ruvuma



SERIKALI kupitia Wizara ya Afya imekabidhi vifaa vya tiba mtandao katika hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Ruvuma hali ambayo itawawezesha wananchi kupata huduma bobezi za kibingwa ndani ya Mkoa.

Akizungumza mara baada ya kukabidhi vifaa hivyo katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Ruvuma, mwakilishi wa Wizara ya Afya ambaye pia ni Mratibu wa Tiba Mtandao, Dr. Ligile Vumilia amesema huduma hiyo ni muhimu hasa kwa wananchi wanaoishi pembezoni mwa Mkoa wa Ruvuma.

Amesema wananchi wote ambao watakuwa wanahitaji huduma za afya za kibingwa na bobezi sasa watazipata katika hospitali ya Rufaa ya Ruvuma badala ya kusafiri umbali mrefu ambapo serikali imeichagua hospitali hiyo kuwa ni miongoni mwa hospitali tano za mwanzo kabisa nchini kupatiwa huduma hiyo.

Dr.Vumilia amesema kuletwa kwa vifaa hivyo katika hospitali ya Rufaa Mkoa wa Ruvuma ni kutekeleza maagizo ya Waziri Mkuu Kassim Majaliwa alipofanya uzinduzi wa X-Ray katika hospitali ya Mkoa wa Ruvuma mwaka 2019,aliagiza kuanzisha huduma ya tiba mtandao katika hospitali hiyo.

Amesema Mfuko wa Mawasiliano kwa wote umetoa shilingi bilioni moja kwa ajili ya kununua vifaa tiba mtandao kwa ajili ya hospitali tano nchini na kwamba vifaa vya tiba mtandao vinapelekwa katika hospitali hizo na vitaunganishwa kwajili ya kuanza kazi ya kutoa huduma za kibingwa kwa wagonjwa.

Hata hivyo amesema Taasisi ya Teknolojia nchini inatarajia kufunga vifaa vya tiba mtandao baada ya makabidhiano hayo ambapo katika hospitali ya Rufaa ya Ruvuma chumba maalum kimeshaandaliwa kwa ajili ya kufungwa vifaa hivyo.

Kwa mujibu wa Mratibu huyo,huduma hiyo inatarajiwa kutolewa katika hospitali za Rufaa 21 nchini na kwamba huduma ya tiba mtandao katika hospitali hizo itaunganishwa na hospitali za Kanda za Bugando Mwanza,Kanda ya Benjamin Mkapa Dodoma na Kanda ya Mbeya.

"Tutakuwa na hospitali nne za kitaifa ambazo zitakuwa na huduma bobezi za kibingwa ambazo ni Hospitali ya Taifa Muhimbili, Hospitali ya Mifupa na Mishipa ya Fahamu (MOI), Hospitali ya Saratani ya Ocean Road na Taasisi ya Jakaya Kikwete ambayo ni maalum kwa magonjwa ya moyo", alisisitiza Dr.Vumilia.

Amesema huduma ya tiba mtandao katika hospitali ya Rufaa ya Ruvuma itamwezesha mgonjwa yeyote kupata huduma bobezi za kibingwa bila kusafiri umbali mrefu kama hospitali ya Taifa ya Muhimbili.

Kwa upande wake Mganga Mkuu wa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Ruvuma Dr.Magafu Majura amemshukuru Rais Samia Suluhu Hassan kwa msaada wa vifaa vya tiba mtandao ambao utawawezesha wananchi kufanyiwa vipimo mkoani Ruvuma na vipimo hivyo kutumwa kwa njia ya mtandao hivyo mgonjwa kufahamu ugonjwa wake akiwa Ruvuma hivyo kupunguza gharama za usafiri na malazi kwa mgonjwa.

"Kwa kutumia vifaa vya tiba mtandao tutakuwa sawa na waliopo Dar es salaam,wananchi wa Mkoa wa Ruvuma na nchi jirani za Msumbiji na Malawi sasa watapata huduma za kibingwa wakiwa Songea",alisisitiza Dr.Majura.

Naye Afisa Mawasiliano wa Wizara ya Afya Catherine Sungura amesema serikali pia imetoa shilingi milioni 630 kwa ajili ya ujenzi wa jengo la wagonjwa wa dharura katika hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Ruvuma na kwamba katika nchi nzima serikali inajenga majengo ya wagonjwa wa dharura katika hospitali nane za rufaa.

Sungura amesema pia serikali imetoa shilingi milioni 150 kwa ajili ya ukarabati wa jengo la wagonjwa mahututi (ICU) katika hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Ruvuma ambapo miradi yote hiyo imetekelezwa kwa asilimia 100.

***"Tutakuwa na hospitali nne za kitaifa ambazo zitakuwa na huduma bobezi za kibingwa ambazo ni Hospitali ya Taifa Muhimbili, Hospitali ya Mifupa na Mishipa ya Fahamu (MOI), Hospitali ya Saratani ya Ocean Road na Taasisi ya Jakaya Kikwete ambayo ni maalum kwa magonjwa ya moyo"***

**MRATIBU WA TIBA MTANDAO,DR. LIGILE VUMILIA**



CT-Scan.



**PICHANI ni vitanda vya kisasa kwenye jengo la wagonjwa mahututi katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Songea ambapo serikali imenunua vitanda nane kwa ajili ya kuboresha upatikanaji wa matibabu kwa wangonjwa wenye uangalizi maalumu.**

## MIAKA MITATU YA RAIS DK. SAMIA NA UBORESHAJI WA SEKTA YA AFYA NCHINI

### JAMHURI YA MUUUGANO WA TANZANIA
### WIZARA YA AFYA
# HOPITALI YA RUFAA YA MKOA WA TEMEKE








## MAFANIKIO MIAKA MITATU YA RAIS SAMIA

**>>SERIKALI ya Awamu ya sita imefanya jitihada kubwa katika kuboresha huduma za Afya. Alisema katika kipindi cha miaka mitatu ya Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, kupitia Wizara ya Afya, Hospitali ya Rufaa ya Mkoa ya Temeke imewezeshwa ...**

## MIKAKATI YA KUENDELEA KUFANYA VIZURI

**>>HOSPITALI imejipanga kuandaa na kutekeleza mipango yenye lengo la kutatua changamoto za afya kwa wanachi wa Temeke na maeneo ya jirani. "Uongozi wa hospitali umeanza kuandaa michoro yenye mpangilio mpya...**

## MWAKA 2010

**Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa Temeke, Dk. Joseph Kimaro, alisema mwaka 2010 hospitali ya Temeke ilipandishwa hadhi kuwa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa...**



**DK.** Joseph Kimaro, Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa Temeke,





MIAKA MITATU YA RAIS DK. SAMIA NA UBORESHAJI WA SEKTA YA AFYA NCHINI

# Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Temeke inavyojivunia miaka mitatu ya Rais Samia




MANDHARI YA NJE ENEO LA HOSPITALI YA TEMEKE

Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa Temeke, Dk. Joseph Kimaro, alisema mwaka 2010 hospitali ya Temeke ilipandishwa hadhi kuwa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa na mwaka 2018 hospitali hiyo ilihamishwa kutoka mamlaka ya Serikali za Mitaa (TAMISEMI) kwenda Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto.

"Hospitali hii inahudumia wastani wa wagonjwa wa nje 1800 hadi 2000 kwa siku na wagonjwa wa ndani 250 hadi 300 kwa siku na inajumla ya vitanda 289.

"Hospitali inahudumia wakazi wa Temeke wapatao 1,346,674 (NBS, 2022) na pia wakazi wengine wanaotoka katika wilaya za Kinondoni, Ilala, Kigamboni, Kisarawe, Mkuranga na Rufiji.

**Na ELIZABETH JOHN**

HOSPITALI ya Temeke ni moja ya hospitali ya Rufaa ya Mkoa ya Temeke iliyopo barabara ya Temeke, Kata ya Tandika wilaya ya Temeke katika Mkoa wa Dar es salaam.

Hospitali hiyo ilianzishwa mwaka 1972 ikiwa kama Zahanati ambapo mwaka 1980 ilipandishwa hadhi kuwa kituo cha afya na miaka mitano baadae ikapanda hadhi kuwa Hospitali ya Wilaya ya Temeke.

Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa Temeke, Dk. Joseph Kimaro, alisema mwaka 2010 hospitali ya Temeke ilipandishwa hadhi kuwa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa na mwaka 2018 hospitali hiyo ilihamishwa kutoka mamlaka ya Serikali za Mitaa (TAMISEMI) kwenda Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto.

"Hospitali hii inahudumia wastani wa wagonjwa wa nje 1800 hadi 2000 kwa siku na wagonjwa wa ndani 250 hadi 300 kwa siku na inajumla ya vitanda 289.

"Hospitali inahudumia wakazi wa Temeke wapatao 1,346,674 (NBS, 2022) na pia wakazi wengine wanaotoka katika wilaya za Kinondoni, Ilala, Kigamboni, Kisarawe, Mkuranga na Rufiji.



WATENDA KAZI WA HOSPITALI YA TEMEKE

### MALENGO YA HOSPITALI

Dk. Kimaro alisema Kuwa malengo ya hospitali hiyo ni kuwa kitovu cha utoaji wa huduma bora za afya kwa Watanzania wote kupitia watoa huduma wenye ujuzi na ari ya utoaji huduma bora za afya kwa kutumia rasilimali, vifaa na nyenzo za kisasa zilizopo kwa ufanisi na ufasaha.

"Tumepanga kuwa na huduma bora kwa jamii, kwa asilimia kubwa malengo yetu yamefikiwa na tunaendelea na uboreshaji huduma wa hali ya juu," alisema Dk. Kimaro.

### MAFANIKIO MIAKA MITATU YA RAIS SAMIA

Alisema serikali ya Awamu ya sita imefanya jitihada kubwa katika kuboresha huduma za Afya.

Alisema katika kipindi cha miaka mitatu ya Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, kupitia Wizara ya Afya, Hospitali ya Rufaa ya Mkoa ya Temeke imewezeshwa katika uboreshaji wa miundombinu ya kutolea huduma kupitia fedha za Uviko 19.

"Katika kipindi hicho, hospital iliweza kutekeleza miradi mbalimbali, pia ilipokea kiasi cha sh.4,651,779,049.00, kutokana na fedha hizo hospitali iliweza kunufaika kwa kupata miradi mbalimbali," alisema.

Alisisitiza kuwa, fedha hizo zilitumika katika kukarabati jengo la huduma za dharura (EMD) kwa gharama ya sh. 130,000,000.00 ambapo ukarabati huo umesaidia kuongeza uwezo wa hospital katika kutoa huduma za dharura.

Alisema tangu kuanza kufanya kazi kwa jengo hilo Oktoba, mwaka 2022 hadi Desemba mwaka jana, jumla ya wagonjwa 11,354 wamepatiwa matibabu kwa kupitia huduma za dharura.

"Pia tulikarabati jengo la wagonjwa mahututi (ICU) kwa gharama ya sh. 180, 000, 000. 00 ujenzi huo umekamilika na mafunzo kwa watoa huduma juu ya wagonjwamahututi ya mefanyika," alisema.

Alisema walijenga jengo la huduma za Radiolojia pamoja na kununua mashine za ugunduzi ikiwemo CT-Scan na Digital X-ray kwa gharama ya TZS.2,600,000,000.00.

"Kuanzia Mei mwaka jana hadi Desemba mwaka jana, jumla ya wateja 1454 walipata huduma za CT Scan na kupunguza rufaa, pia watumishi 15 walipata mafunzo mbalimbali kwa ufadhili wa fedha za Mradi wa IMF kwa mapambano dhidi ya Uviko-19," alisema.

Alisema vilevile jumla ya watumishi sita wakada waliajiriwa kwa njia ya mkataba wa miezi sita kwa kutumia fedha hizo.

MIAKA MITATU YA RAIS DK. SAMIA NA UBORESHAJI WA SEKTA YA AFYA NCHINI



# Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Temeke inavyojivunia miaka mitatu ya Rais Samia

**MIRADI ILIVYOTEKELEZWA**

Dk. Kimaro alisema kutokana na usimamizi mzuri wa mifumo ya ukusanyaji wa mapato ya ndani chini ya serikali ya awamu wa sita, kwa kipindi cha miaka mitatu hospitali imeweza kutekeleza miradi mbalimbali kwa lengo la kuboresha huduma.

"Ujenzi wa vyumba viwili vya upasuaji (Operating Theatre) kwa wagonjwa kuweza kupunguza msongamano katika jengo la upasuaji hasa kwa wagonjwa wa dharura na kuokoa maisha kwa haraka, ujenzi huo uligharimu kiasi cha sh. 98,000,000.00.

"Pia tumenunua wa Jenereta mpya ya KV 275, kwa ajili ya kuhakikisha kuwa kuna nishati mbadala wakati wote wa utoaji huduma kwa wagonjwa, manunuzi hayo yamegharimu kiasi cha sh. 178,457,652.00," alisema.

Daktari huyo alisema wamenunua mashine 10 za huduma za ushafishaji Damu (dialysis machine) kwa mapato ya ndani, ambapo zilitumika sh. 414,645,600.00.

Alisema kutokana na usimamizi mzuri wa taasisi za serikali na ushirikiano, Hospitali ya Temeke kwa kushirikiana na Mamlaka ya Bandari imeweza kukarabati jengo kwa ajili ya huduma za usafishaji damu ( Dialysis).

**Dk. Kimaro aliwataka wakazi wa Temeke na mikoa ya jirani kuendelea kuwaamini kwa huduma za afya wanazotoa na kusisitiza kuwa ni zenye ubora na uhakika. "Tunawasihi kuzingatia tabia zenye kuboresha afya zao ikiwemo kula mlo kamili, kunywa maji ya kutosha, kufanya mazoezi pamoja na kujiepusha na tabia zenye kuleta madhara kwa afya zao," alisema. Alimaliza kwa kuitaka jamii ianze kujiunga na bima ya afya ili waweze kupata huduma za afya bila msongo wa mawazo.**

Aliongeza kuwa wamejenga wodi ya wazazi waliojifungua kwa njia ya kawaida na kufanikiwa kupunguza msongamano katika wodi ya wazazi.

"Ujenzi wa wodi hiyo ni sh. 86,000,000.00, ujenzi huu umesaidia katika kuongeza namba ya wajawazito wanakuja kujifungua ambapo kuanzia Mei mwaka jana hadi Desemba mwaka jana, jumla ya Wajawazito 2,278 wamejifungua kwa njia ya kawaida.

Pia fedha hizo zilitumika katika uboreshaji wa huduma za chumba cha maiti kwa kununua jokofu moja kwa sh.32,276,652.82 lenye uwezo wa kuhifadhi miili sita na kufanya uwezo wa chumba kuwa ni miili 21.

**MIKAKATI YA KUENDELEA KUFANYA VIZURI**

Dk. Kimaro alisema hospitali imejipanga kuandaa na kutekeleza mipango yenye lengo la kutatua changamoto za afya kwa wanachi wa Temeke na maeneo ya jirani.

"Uongozi wa hospitali umeanza kuandaa michoro yenye mpangilio mpya wa majengo na huduma (Master Plan) kwa kushirikisha wataalamu wa majenzi kutoka Hospitali ya Mifupa Muhimbili (MOI).

"Mpangilio wa majengo hayo unalenga kuwa na majengo yaliyoinuka au ghorofa, huu ni muelekeo wa kuwa na taswira mpya yenye kuvutia ya hospital ya Rufaa ya Mkoa Temeke," alisema.

Daktari huyo alisema maboresho haya yatapelekea kupata nafasi kwa ajili ya kutoa huduma bora za tiba, ufundishaji na ufanyaji wa tafiti.

Alisema pia maboresho hayo yataongeza imani ya wananchi kwa hospitali na serikali kwa ujumla ambapo pia wataendelea kuelimisha watumishi katika eneo la utoaji wa huduma bora ili wananchi waweze kupenda huduma za matibabu katika kituo hicho.

Alisisitiza kuendelea kutoa huduma za mkoba za kibingwa kwa wananchi katika maeneo yao ya karibu ili waweze kunufaika na uwekezaji katika huduma za afya.

Alisema uongozi umejipanga kusimamia miradi yote ya kuboresha huduma za afya kwa uaminifu na kwa kuzingatia sheria, taratibu na kanuni zilizopo kuweza kupata matokeo chanya na kuleta manufaa kwa wananchi ambao ndiyo wahitaji wa huduma hizi.

**WITO KWA JAMII**

Dk. Kimaro aliwataka wakazi wa Temeke na mikoa ya jirani kuendelea kuwaamini kwa huduma za afya wanazotoa na kusisitiza kuwa ni zenye ubora na uhakika.

"Tunawasihi kuzingatia tabia zenye kuboresha afya zao ikiwemo kula mlo kamili, kunywa maji ya kutosha, kufanya mazoezi pamoja na kujiepusha na tabia zenye kuleta madhara kwa afya zao," alisema.

Alimaliza kwa kuitaka jamii ianze kujiunga na bima ya afya ili waweze kupata huduma za afya bila msongo wa mawazo.

**SHUKRANI**

Dk. Kimaro alisema kwa niaba ya Uongozi wa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa ya Temeke, anatoa pongezi na shukrani kwa Rais Dk. Samia Suluhu Hassani kwa jitihada zake za kuboresha huduma za afya hususani huduma za mama na mtoto.

Pia aliishukuru Wizara ya Afya chini ya uongozi wa Ummy Ally Mwalimu kwa usimamizi makini, sera na miongozo mbalimbali ya Wizara.

Alisema wanashukuru kwa maono na jitihada zilizopelekea kupata fedha za IMF zimesaidia kuboresha huduma za afya.



**MIAKA MITATU YA RAIS DK. SAMIA NA UBORESHAJI YA SEKTA YA AFYA NCHINI**

# SERIKALI INAVYOZIDI KUIPAISHA HOSPITALI YA RUFAA YA MKOA MAWENZI MKOANI KILIMANJARO.



Mganga Mfawidhi hospitali ya Rufaa ya mkoa Mawenzi Dk Edna-Joy Munisi

**Na WILLIUM PAUL,** *Kilimanjaro*

SERIKALI ya awamu ya sita chini ya Rais Dk. Samia Suluhu Hassan imeonyesha kwa dhati malengo yake ya kuboresha huduma za Afya pamoja na kusogeza karibu na wananchi.

Dhana hii imeonekana wazi kwa kipindi hiki cha miaka mitatu ambapo Hospitali mbalimbali zimepewa fedha nyingi kwa ajili ya kuboresha miundombinu yake na kununua vifaa tiba vya kisasa.

Jambo hili halikuiacha Hospitali ya Rufaa ya Mkoa Mawenzi mkoani Kilimanjaro iliyojengwa mwaka 1920 ambapo nayo imeweza kupatiwa zaidi ya Bilioni 10.780 kwa ajili ya miradi mbalimbali pamoja na kuboresha upatikana wa huduma bora.

Kwa mujibu wa Mganga Mfawidhi wa Hospitali hiyo, Dokta Edna-joy Munisi anasema kuwa Hospitali hiyo ni miongoni mwa Hospitali kongwe hapa nchini ambapo ilianza kujengwa kama zahanati ya kutibu Askari wa Kijerumani na baadaye kupandishwa hadhi kuwa kituo cha Afya mwaka 1922.

Dkt. Edna-joy anaendelea kudai kuwa, iliendelea kuwatibu viongozi wa kikoloni na baadhi ya Waafrika wachache waliokuwa wanawatumikia wakoloni na mnamo mwaka 1956 ilipandishwa daraja na kuwa Hospitali ya mkoa.

Anasema kuwa, kwa sasa hospitali hiyo ya Rufaa inatoa huduma mbalimbali ikiwemo matibabu kwa wagonjwa wa nje na ndani wa rufaa kutoka vituo vyote vya kutolea huduma za Afya ndani ya Mkoa.

Huduma nyingine ni matibabu kwa wagonjwa wasiokuwa wa rufaa, kutoa wataalam wa kusaidia katika halmashauri kupambana na magonjwa ya mlipuko pindi yanapojitokeza pamoja na huduma za Mkoba.

"Tumekuwa tukifanya uchunguzi wa magonjwa mbalimbali pamoja na kutoa huduma za maabara na vipimo mbalimbali kama huduma za CT-Scan, Ultrasound, X-ray pamoja na kutoa ushauri wa kitaalam" Anasema Mganga Mfawidhi huyo.

Na kuongeza "tunatoa huduma ya mazoezi ya viungo na tiba kwa vitendo kwa wagonjwa wenye matatizo ya viungo, huduma ya tiba shufaa, kufanya tafiti mbalimbali za kiafya katika hospitali kwa kushirikiana na taasisi mbalimbali".

Mtaalam huyo wa Afya anasema kuwa, katika kipindi cha miaka mitatu ya Rais Dokta Samia Suluhu Hassan hispitali hiyo imeweza kupata mafanikio makubwa ambayo ni uanzishwaji wa huduma za kibingwa kwa magonjwa ya dharura, upasuaji wa mifupa pamoja na huduma za kibingwa za Pua, Koo na masikio.

***Tumekuwa tukifanya uchunguzi wa magonjwa mbalimbali pamoja na kutoa huduma za maabara na vipimo mbalimbali kama huduma za CT-Scan, Ultrasound, X-ray pamoja na kutoa ushauri wa kitaalam***

Mafanikio mengine ambayo yamepatikana kipindi hiki cha serikali ya awamu ya sita ni uanzishwaji wa huduma mpya za vipimo vya kisasa vya CT-Scan, uanzishwaji wa huduma za wagonjwa mahututi (ICU, NICU), kupata vifaa tiba vipya kama mashine ya X-ray, ultrasound na mashine mpya za maabara.

Pia katika hospitali hiyo upatikanaji wa dawa na vifaa tiba na vitendanishi unapatikana kwa asilimia 95, uboreshwaji wa miundombinu ya majengo ambao ni ukarabati wa jengo la Wagonjwa mahututi, ujenzi wa jengo la Afya ya Mama na Mtoto, ujenzi wa nyumba ya mtumishi, ujenzi wa uzio na ukarabati wa veranda.



Wodi maalum kwa ajili ya watoto njiti katika hospitali ya Rufaa ya mkoa Mawenzi (NICU).



Mashine ya CT-Scan iliyosimikwa katika hospitali ya Rufaa ya Mkoa Mawenzi

**UJENZI WA JENGO LA AFYA YA MAMA NA MTOTO.**

Katika kuhakikisha kuwa wakinamama wajawazito wanajifungulia sehemu salama na rafiki kwa watoto wachanga Serikali iliamua kuja na mpango wa ujenzi wa jengo kubwa na la kisasa la Mama na Mtoto katika hospitali hiyo ambalo ni la gorofa.

Kwa mujibu wa Dkt. Edna-Joy Serikali ya awamu ya sita katika awamu ya nane ya ujenzi wa jengo hilo imeweza kutoa fedha Bilioni 5.999 kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa jengo hilo ambalo kwa sasa linatoa huduma katika ghorofa ya chini na ghorofa ya kwanza

Ujenzi wa jengo hili umekuwa mkombozi mkubwa kwa wananchi wa Mkoa wa Kilimanjaro pamoja na jirani kwani kupitia jengo hilo sasa hospitali hiyo inatoa huduma maalum ya watoto njiti ambapo hapo awali ilikuwa ikipatikana katika Hospitali ya kanda pekee.

Aidha kupitia jengo hilo, hospitali hiyo imeweza kufunga mashine ya CT-Scan ambapo huduma hiyo haikuwa kutolewa kwenye hospitali hiyo toka kuanzishwa kwake.

Anasema lengo la Serikali ni kuhakikisha kuwa huduma zote muhimu zinazohusiana na Afya zinapatikana karibu zaidi na wananchi wake haswa za kibingwa na bobezi.

MIAKA MITATU YA RAIS DK. SAMIA NA UBORESHAJI YA SEKTA YA AFYA NCHINI



Jengo la Afya ya mama na mtoto katika hospitali ya Rufaa ya Mkoa Mawenzi ambapo awamu ya nane ya ujenzi Serikali imetoa Bilioni 5.999 kuendelea na ujenzi

# SERIKALI INAVYOZIDI KUIPAISHA HOSPITALI YA RUFAA YA MKOA MAWENZI MKOANI KILIMANJARO.

**UKARABATI WA JENGO LA WAGONJWA MAHUTUTI (ICU)**

Tangu kuanzishwa kwa hospitali ya Mawenzi mwaka 1920 huduma ya ICU haikuwai kutolewa lakini Serikali ya awamu ya sita chini ya Rais Dokta Samia Suluhu Hassan imeweza kuandika historia.

Anabainisha kuwa, katika kuhakikisha huduma hiyo inatolewa hospitalini hapo Serikali ilitenga fedha Milioni 149 kwa ajili ya ukarabati wa jengo la ICU ambalo kwa sasa linatoa huduma huku likichukua wagonjwa 12 kwa pamoja.

Mganga Mfawidhi anaendelea kubainisha kuwa, katika kuhakikisha mazingira ya ufanyaji kazi yanaboreshwa kwa watumishi wake, Serikali imeweza kutoa fedha Milioni 136 kwa ajili ya ujenzi wa nyumba ya Mtumishi pamoja na ujenzi wa uzio.

**UJENZI WA JENGO LA WAGONJWA WA DHARURA.**

Dokta Edna-joy anabainisha kuwa, katika kipindi hiki cha miaka mitatu ya Serikali ya awamu ya sita hospitali ya Rufaa ya Mawenzi imeweza kupokea Milioni 776.4 kwa ajili ya ujenzi wa jengo la wagonjwa wa Dharura ambalo limeshaanza kutoa huduma.

Aidha hospitali hiyo imeweza kupokea Bilioni 3.574 kwa ajili ya ununuzi wa vifaa tiba mbalimbali.

Mganga Mfawidhi huyo anabainisha kuwa, mikakati waliyonayo ni kuhakikisha upatikanaji wa dawa, vifaa tiba na vitendanishi unazidi kukuwa, kutoa huduma bora na kwa wakati kwa wateja wote, kuimarisha na kuboresha ukusanyaji wa mapato kwa kuanzisha huduma mbalimbali katika hospitali, kuendelea kuwajengea uwezo na kutoa huduma za kibingwa hospitali za halmashauri na kuendelea kuimarisha na kuboresha miundombinu ya hospitali kwa kutumia vyanzo vya mapato ya ndani

Dkt. Edna-joy anasema kuwa, hospitali itahakikisha inasimamia miradi yote inayotekelezwa na hospitali kwa kufuata miongozo na taratibu na kuhakikisha miradi inakamilika kwa wakati kulingana na mpango kazi wa utekelezaji wa miradi hiyo na hatimaye kutoa huduma iliyokusudiwa kwa wananchi.




Jengo maalum la wagonjwa wa dharura katika hospitali ya Rufaa ya Mkoa Mawenzi lililogharimu Milioni 776.4 limeshaanza kutoa huduma.



Jengo maalum la wagonjwa mahututi (ICU) katika hospitali ya Rufaa ya Mkoa Mawenzi ambapo ukarabati wake umegharimu Milioni 149



Ukarabati wa Veranda za hospitali ya Rufaa ya Mkoa Mawenzi uliogharimu Milioni 37

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
Wizara ya Afya
**Hospitali ya Rufaa ya Mkoa Maweni**
(Kigoma Region)








# Hospitali ya Maweni, mkombozi kwa wananchi wa Mkoa Kigoma



**Na MWANDISHI MAALUMU**

JUHUDI mbalimbali zinazofanywa na Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, katika kuimarisha sekta ya afya nchini, zimewezesha kupata mafanikio makubwa ndani ya miaka mitatu.

Serikali imeendelea kuweka mazingira mazuri kwa wananchi wote, kuwa na uhakika wa kusogeza huduma za afya kwa kufanya uwekezaji mkubwa wa ujenzi wa miundombinu ya utoaji wa huduma za afya mijini na vijijini.

Katika kuthibitisha hilo, Serikali imeendelea kutoa kipaumbele kwa sekta ya afya ambapo mwaka 2021/2022 ilitenga shilingi trilioni 2.1, mwaka 2022/2023 shilingi trilioni 2.2 na mwaka 2023/24 imetenga shilingi trilioni 2.4.

Aidha, Wizara imeendelea kusimamia upatikanaji wa huduma za afya nchini, zinazotolewa kupitia vituo vya kutolea huduma vya Serikali, binafsi na mashirika ya dini lengo ni kuhakikisha wananchi wanakuwa na afya bora.

Kati ya Julai 2022 hadi Machi, 2023, vituo vya kutolea huduma za afya nchini viliongezeka kufikia 11,040 ikilinganishwa na vituo 8,549 vya mwaka 2021.

Hospitali zilikuwa 430, vituo vya afya 1,030, zahanati 7,458, kliniki 906 na maabara binafsi 1,216 huku Serikali ikiendelea kukamilisha ujenzi wa Hospitali za Rufaa za Mikoa katika mikoa ya Njombe, Songwe, Geita, Simiyu na Katavi.

Pia, Serikali imeimarisha miundombinu ya kutolea huduma za dharura nchini, kwa kujenga majengo ya huduma za dharura (EMD) 128 katika Hospitali ngazi ya Taifa, Maalumu, Kanda, Mkoa na kuziwekea vifaa na vifaatiba.

Kuimarika kwa huduma hizi kumewezesha hospitali kuokoa maisha ya wagonjwa, ambao wanauhitaji wa huduma hizo kwa asilimia 20 hadi 40. Uwekezaji huu katika miradi ya maendeleo umegharimu zaidi ya shilingi billioni 891.5.

Katika kipindi cha miaka mitatu, Serikali imekamilisha ujenzi wa hospitali tano za mikoa, imeboresha miundombinu ya kutolea huduma za afya katika Hospitali za Rufaa za Kanda, imeendelea na ujenzi wa hospitali za halmashauri 127 na kuanzisha huduma 13 za kibingwa bobezi.

Mkoa wa Kigoma ni miongoni mwa mikoa ambayo imepata mafanikio makubwa katika sekta ya afya, baada



ya Rais Dk. Samia kupeleka fedha nyingi za utekelezaji wa miradi.

Wananchi wa Kigoma hivi sasa wanajivunia huduma bora inayotolewa katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Kigoma, baada ya Serikali kufanya uwekezaji mkubwa.

katika awamu yake ya sita, Rais Dk. Samia, amefanikiwa kuboresha miundombinu ya kutolea huduma na vifaatiba katika Hospitali ya Mkoa Maweni, ili kuhakikisha wananchi wanapata huduma bora.

Rais Dk. Samia ametekeleza miradi mingi ya kujivunia katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Kigoma chini ya kaulimbiu yake ya "Kazi iendelee", kauli hii inathibitishwa na kuimarika kwa miundombinu ya hospitali kwa kasi kubwa.

Moja, Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Kigoma Maweni ilipatiwa fedha shilingi 1,933,404,356/= kwa ujenzi wa jengo la dharula na huduma mahututi kwa wagonjwa wanaohitaji uangalizi maalumu (Emergency and ICU).

Mradi huo umekamilika kwa asilimia 100 pamoja na vifaatiba vyake na tayari jengo hilo limeanza kutoa huduma kwa wagonjwa wa dharula na wagonjwa mahututi. Jengo hili lilizinduliwa na Rais Dk. Samia Oktoba 18, 2022 alipofanya ziara mkoani Kigoma.

Mbili, Katika kipindi cha awamu ya sita chini ya Rais Dk. Samia, hospitali imepokea fedha za ujenzi wa jengo la wagonjwa wa nje (OPD) na jengo la kuhifadhia maiti (MORTUARY).

Ujenzi wa majengo haya mawili umekamilika kwa asilimia 100 na tayari huduma zinatolewa katika majengo. Mradi huu umegharimu shilingi 3,000,000,000/=. Ujenzi huo kwa awamu ya kwanza umekamilik na hospitali inasubiri fedha za awamu ya pili ili kukamilisha ujenzi wa jengo la wagonjwa wa nje (OPD).

Tatu, Katika kipindi cha uongozi wa Rais Dk. Samia, hospitali imepokea fedha za ujenzi wa jengo la kituo cha Damu Salama, ujenzi wa jengo hili utasaidia kuimarisha upatikanaji wa damu salama kwa wagonjwa wa Mkoa wa Kigoma na mikoa jirani.

Jengo hili litagharimu shilingi 1,108,000,000/= hadi kukamilika kwake. Hadi sasa ujenzi umefikia asilimia 90 na jengo hilo linatarajia kuanza kazi hivi karibuni.

Nne, Rais Dk. Samia ameendelea kuimarisha huduma za afya kwa kutoa shilingi 151,000,000 za ununuzi wa mashine ya kisasa ya CT SCAN na ukarabati wa jengo la Radiolojia (mionzi). Pia Serikali imetoa shilingi 500,000,000/= kwa za ununuzi wa mashine ya kupima saratani ya matiti (Mamography), mradi huu umekamilika asilimia 100.

Huduma hizo zinatolewa katika Hospitali ya Mkoa wa Kigoma Maweni. Lengo la mradi huu ni kuwapunguzia adha wananchi wa ili waweze kuchunguzwa magonjwa katika mkoa wao, badala kufuata huduma Mwanza na Dar es Salaam.

Tano, Serikali imetoa shiling 1,000,000,000/= kwa ajili ya ujenzi wa jengo la utakatishaji vifaatiba na ufuaji (CSSD and LAUNDRY), Mradi huu unalenga kutakasisha vifaatiba vinavyotumika kutolea huduma kwa wagonjwa na kufua nguo za wagonjwa, mradi huu umekamilika asilimia 85.

Sita, Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Kigoma Maweni katika kipindi cha cha uongozi wa Rais Dk. Samia imepokea shilingi 40,955,375/= kukarabat chumba cha tiba mtandao (TELEMEDICINE).

Ujenzi huu umekamilika kwa asilimia 100 na mradi huu utawasaidia watoa huduma za afya wa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Kigoma, kuwasiliana na watoa huduma za afya walio katika hospitali za Kanda na Taifa ili kuhakikisha wagonjwa wanapata huduma stahiki.

Saba, Pia, Rais Dk. Samia ametoa fedha za ujenzi wa nyumba moja ya watumishi shilingi 90,000,000/= mradi huu umetekelezwa kwa asilimia 100, Serikali imejipanga kuimarisha mazingira wanayoishi watumimishi ili waendelee kutoa huduma bora kwa wananchi.

Nane, Idadi ya watumishi katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Kigoma, imeongezeka kutoka 218 mwaka 2020/2021 hadi kufikia 278 mwaka 2022.

Hatua hiyo imetokana baada ya kupokea watumishi 23 mwaka 2021 na watumishi 57 mwaka 2022. Mwaka 2022/2023 ongezeko la watumishi 55 na kufanya jumla ya watumishi kufikia 264, mwaka 2023/2024.

Watumishi 30 wameongezeka na kufanya jumla ya watumishi mpaka sasa kufikia 294. Ongezeko hili limepunguza upungufu wa watumishi na hivyo kuboresha utoaji wa huduma kwa wananchi wa Kigoma.

Tisa, Hospitali imejenga na kusimika mtambo wa kuzalisha hewa tiba ya oksjen (Oxygen plant), mradi huu umegharimu shilingi 623,369,462/= na umekamilika kwa asilimia 100 na huduma zimeanza kutolewa.

Mradi huu umekuwa msaada katika mkoa mzima wa Kigoma na mkoa jirani wa Katavi. Awali, hospitali ilikua inalazimika kufuata gesi ya Oksijen mkoani Mwanza kilometa zaidi ya 600.

Uboreshaji huu mkubwa umepunguza changamoto kwa wananchi wa Kigoma, ambapo awali huduma zilikuwa hazipatikani katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Kigoma sasa zinapatikana kutokana na juhudi za Serikali. Baadhi ya huduma hizo ni; huduma za kusafisha damu (Hemodialysis) mashine tisa zimesimikwa, huduma za kibingwa za magonjwa ya ndani, magonjwa ya mifupa, ICU na mengine mengi.

Pia, Serikali kupitia Wizara ya Afya, imehakikisha ongezeko la gari katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa Maweni, ambapo hospitali imepokea gari moja kwa shughuli za usimamizi shirikishi.

Vilevile, katika kipindi hiki malalamiko ya wananchi yamepungua katika Hospitali ya Mkoa wa Kigoma Maweni, kutokana na jinsi ambavyo huduma zimeimarika kuanzia miundombinu vifaatiba na upatikanaji wa dawa.

Idadi kubwa ya wananchi wanapofika katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Kigoma Maweni, wameendelea kusifu kuimarika huduma na kusifu jitihada za Rais Dk. Samia na Serikali yake ya Awamu ya Sita.

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA AFYA
HOSPITALI YA RUFAA YA MKOA,

# BUKOBA



RAIS Dk. Samia Suluhu Hassan.



Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa, Bukoba, Dkt. Museleta Nyakiroto.



# Rais Dk. Samia alivyoboresha Hospitali ya Rufaa ya Mkoa, Bukoba

Anuani ya Posta: Box 265, Kagera
Simu: +2552220351
Simu ya Mkononi:
Barua Pepe: bukobarrh@afya.go.tz

MIAKA MITATU YA RAIS DK. SAMIA NA UBORESHAJI SEKTA YA AFYA NCHINI

# Rais Dk. Samia alivyoboresha Hospitali ya Rufaa ya Mkoa, Bukoba

AFYA ni ile hali ya mtu kuwa vizuri ima kimwili, kiakili na hata kijamii, hii ina maana ya kwamba mtu huambiwa ni mwenye afya endapo mambo hayo matatu yakiwa yamekamilika hivyo kutokana na hayo Serikali ya awamu ya sita inayoongozwa na Rais Samia Suluhu Hassan kwa kipindi cha miaka mitatu tangu aingie madarakani imeboresha sekta ya Afya ili kuhakikisha wananchi wanapata huduma stahiki na bora zinazokidhi matakwa ya jamii hiyo.

Hospitali ya Rufaa ya mkoa, Bukoba, ilijengwa mwaka 1923 ikiwa kambi ya Wajerumani baada ya kukoma kuwa kambi ya jeshi la Wajerumani ilianza kutoa huduma mbalimbali za afya ambapo hatua kwa ilipandishwa hadhi na kuwa Zahanati, Kituo cha Afya na hatimaye kuwa hospitali kamili.

Kutokana na Tangazo la Serikali namba 828 katika gazeti la Serikali la Novemba 12 mwaka 2010 hospitali hiyo ilipandishwa hadhi na kuwa ya Rufaa ya mkoa Bukoba, ambapo inauwezo wa vitanda 340, hupokea wagonjwa wanaolazwa 20 hadi 25 na wa nje 200 hadi 250 kwa siku.

**HUDUMA ZA KIBINGWA ZINAZOTOLEWA NA HOPSITALI HIYO.**

Museleta Nyakiroto ni mganga mfawidhi wa hospitali ya Rufaa Mkoa, Bukoba anasema wanao wajibu wa kutoka huduma za kibingwa na zisizo za kibingwa kwa wakazi 2,989,299 wa Mkoa huo ambao wanaongezeka kwa 3.2% kila mwaka (sensa 2022) ambapo ina jumla ya Idara 11 na vitengo vitano.

Anazitaja idara zilizopo ni pamoja na Idara ya Magonjwa ya ndani, Idara ya Upasuaji, Idara ya Upasuaji maalum (Surgical Specialities), Idara ya magonjwa ya akina mama na Afya ya uzazi, Idara ya watoto, Idara ya Uuguzi, Idara ya Mionzi, Idara ya Pharmacy, Idara ya Maabara, Idara ya Mipango na Bajeti na Idara ya Utawala na Rasilimali Watu.

Aidha vitengo walivyonavyo ni pamoja na kitengo cha Uhakiki wa Ubora wa Huduma, Kitengo cha Habari, Mawasiliano na Tehama (ICT), Kitengo cha Uhasibu na Fedha, Ukaguzi wa Ndani pamoja na kitengo cha Manunuzi na Ugavi.

Anazitaja huduma za Kibingwa zinazotolewa katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Kagera kuwa ni tisa ambazo zinao madaktari Bingwa na Bingwa Bobezi 14 sawa na 58.3% ya mahitaji yote ambapo madaktari wa watoto ni wawili, uzazi na kizazi ni wawili,upasuaji wawili, Afya ya kinywa na meno kwa watoto mmoja,upasuaji mifupa wawili, magonjwa ya ndani mmoja, masikio, pua na koo mmoja na Afya ya macho wawili.

Anasema kwa kipindi cha miaka mitatu ya Serikali ya awamu ya sita zimeongezeka huduma za Kibingwa nne hospitalini hapo na madaktari wanane wanaosomea Udaktari Bingwa katika nyanja za Upasuaji mifupa ni watatu, Mfumo wa Mkojo mmoja, Magonjwa ya Ndani wawili, Watoto mmoja na Magonjwa ya Dharura mmoja.

Anataja changamoto iliyokuwa ikiwakabili siku za nyuma katika eneo hili hadi kufikia 2020/2021 huduma za Kibingwa za magonjwa ya ndani, huduma za Kibingwa za Mifupa, huduma za Kibingwa za Pua Sikio na Koo na Radiolojia hazikuwa na Madaktari Bingwa.

*Museleta Nyakiroto ni mganga mfawidhi wa hospitali ya Rufaa Mkoa, Bukoba anasema wanao wajibu wa kutoka huduma za kibingwa na zisizo za kibingwa kwa wakazi 2,989,299 wa Mkoa huo ambao wanaongezeka kwa 3.2% kila mwaka (sensa 2022) ambapo ina jumla ya Idara 11 na vitengo vitano.*



**Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa, Bukoba, Dkt. Museleta Nyakiroto.**

Uwepo wa daktari bingwa wa Pua, Sikio na koo imesaidia kupunguza rufaa na kuwapunguzia wananchi adha ya kufuata huduma katika Hospitali ya Kanda ya Bugando.

**HARI YA DAWA NA VIFAA TIBA**

Nyakiroto anasema hali ya upatikanaji wa dawa muhimu hospitalini hapo kwa sasa ni asilimia 95 – 98 tofauti na kipindi cha 2019/2020 ambayo ilikuwa sawa na asilimia 85 ya dawa zote zinazohitajika hivyo, hospitali inaendelea kusimamia upatikanaji wa mapato ya ndani kwa kuhakikisha asilimia 50+ ya mapato hayo inatengwa kwa ajili ya dawa na vifaa tiba na pia kuhakikisha kuwa duka la dawa linakuwa na dawa na vifaa tiba kwa wakati wote.

**MAMBO YA KUJIVUNIA YALIYOFANYIKA KIPINDI CHA MIAKA MITATU YA RAIS DK. SAMIA.**

Anasema kuwa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa imepokea kiasi cha shilingi bilioni 4,956,844,000.00 kutoka Serikali Kuu kwa ajili ya kutekeleza miradi mikubwa ifuatayo, kujengwa kwa jengo la dharura (EMD) lenye Thamani ya Tsh.650,000,000/= (Milioni Mia sita hamsini) na fedha kununua vifaa vyake kiasi cha Tsh.691,554,000,kujengwa kwa Jengo la wagonjwa mahututi lenye thamani ya Tsh.560,000,000 (Milioni Mia tano sitini) na fedha ya vifaa yenye thamani ya Tsh. 770, 000,000/= (Milioni mia saba sabini) ilitengwa.

Ujenzi mwingine ni wa nyumba ya Mtumishi ambayo iligharimu kiasi cha Tsh.90, 000,000 (Milioni tisini), Ununuzi wa vitanda vya kisasa vya wagonjwa, Makabati vyenye Thamani ya Tsh.31,800,000 (Milioni thelathini na moja na laki nane), Blood Gas Machine ambayo iligharimu kiasi cha Tsh.56, 000,000 (Milioni hamsini na sita),nunuzi wa CT-Scan na Ujenzi wa jengo lake ambayo yaligharimu kiasi cha Tsh. Bil 2,041,280,000 (Bilioni mbili, Milioni arobaini na moja laki mbili na themanini Elfu).

Vingine ni Mafunzo na Ajira Tsh mil. 40,970,000.00, Huduma ya Tiba Mtandao (Telemedicine) Tsh mil. 25,240,000.00, kuanzishwa kwa huduma za kusafisha damu (Dialysis) ambapo wagonjwa wapatao 11 wanahudumiwa ndani ya Hospitali, kabla ya kuanzishwa huduma hii wagonjwa wengi walikuwa wakitibiwa



Mashine ya kisasa ya CT-SCAN iliyopo katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa, Bukoba

MIAKA MITATU YA RAIS DK. SAMIA NA UBORESHAJI SEKTA YA AFYA NCHINI

# Rais Dk.Samia alivyoboresha Hospitali ya Rufaa ya Mkoa, Bukoba



Muonekano wa jengo jipya la Wagonjwa Mahututi (ICU) katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa, Bukoba.

hospitali ya Kanda ya Bugando.

Anasema walipatiwa gari moja na Serikali kwa ajili ya huduma za usimamizi shirikishi kwa ngazi ya vituo vilivyopo ndani ya Mkoa kwa ajili ya Kliniki tembezi za kibingwa,Kuongezeka kwa madaktari Bingwa wapatao wanane katika maeneo ya Kibingwa ya Mifupa wawili, Radilojia mmoja, Watoto mmoja, Upasuaji mmoja, magonjwa ya Uzazi na Kizazi mmoja, Magonjwa ya ndani na Masikio, Pua na Koo mmoja.

Anasema wameweza kufanya ukarabati wa majengo mbalimbali katika kipindi cha mwaka 2022/2023 hadi Februari 2023/2024 ikiwemo Wodi ya Upasuaji moja, Wodi ya magonjwa ya Ndani, wodi kwa ajili ya wagonjwa wa Bima (jumla ziko tatu), Wodi ya Private sita, Jengo la Dialysis, OPD ya zamani, kuweka pavement katika jengo la EMD na ICU ambapo kazi hizo zimefanyika kwa gharama jumla ya kiasi cha Tsh. 100, 645, 041.37.

Pia kwa kutumia fedha za mapato ya ndani tumeweza kununua gari kwa ajili ya uendeshaji wa Hospitali kiasi cha Tsh.168,000,000 (Milioni mia moja sitini na nane elfu).

### MAFANIKIO YA SEKTA YA AFYA KWA KIPINDI CHA MIAKA MITATU

Anasema ni kupungua kwa rufaa nyingi zilizokuwa zinaenda kwenye hospitali za ngazi za juu ikiwemo Hospitali ya Kanda Bugando jijini Mwanza, kuongezeka kwa huduma za kibingwa katika Hospitali Rufaa ya Mkoa Kagera kumesaidia Wananchi wengi wa mkoa huo kupata huduma bora za kibingwa na kusaidia kuwapunguzia gharama za kwenda kupata huduma za matibabu umbali mrefu.

Pia kuboresha muonekano mzuri wa mazingira ya Hospitali kutokana na kuwepo kwa majengo mapya, upatikanaji wa huduma ya Tiba Mtandao (Telemedicine) unaosaidia wataalamu wetu kuwasiliana na wataalamu wa hospital nyingine (hususani zile za rufaa Kanda na za kitaifa) kuhusu matibabu ya wagonjwa.

Anasema hii imepelekea wananchi wa Mkoa wa Kagera kuongeza imani kwa serikali.

Kulingana na huduma zinazotolewa ndani ya Hospitali, Kuongezeka kwa Mapato ya Hospitali kutoka fedha za papo kwa papo tulikuwa tunapata kati ya Tsh mil.50 hadi 60 na Bima kati Tsh mil.130 hadi 150 ya mwaka 2021 na sasa wa Bima madai ya Januari, 2024 ambayo tulipeleka tulidai Tsh Mil.330 na papo kwa papo tunaenda hadi mil.150 kwa mwezi kutokana na kuongezeka kwa wateja kupata huduma ndani ya Hospitali hiyo.

Anasema wagonjwa wale wanaokuja wameumia vichwa hawawapeleki tena Bugando na badala yake wanapigwa picha ya kuonyesha kama kuna tatizo la namna gani na kisha wanafanyiwa upasuaji hapa hapa wenyewe,kuongezeka kwa mtaalamu wa pua, sikio na koo inapunguza umbali huo na magonjwa ya ndani pia

### MKAKATI WA KUSIMAMIA MIRADI AMBAYO INAENDELEA KUTEKELEZWA KATIKA KUHUDUMIA WANANCHI

Anasema wanapanga kuwa na Mpango Mahususi kwa ajili kufanya Matengenezo Kinga, Kuendelea kutenga bajeti kila mwaka kwa ajili ya ukarabati, uendeshaji wa miundombinu na vifaa Tiba, Kuendelea kutoa elimu kwa watumishi na wateja kwa ujumla juu ya matumizi sahihi na utunzaji wa miundombinu na vifaa Tiba na kuwa na wataalamu kwa ajili ya kusimamia miundo mbinu (Waandisi – Ujenzi, Vifaa tiba).

***"Tunamshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan na serikali hii ya awamu ya sita anayoingoza kwa jitihada zake za kuboresha huduma za Afya ndani ya Mkoa, kwa kuendelea kutoa rasilimali fedha na watu katika kuhakikisha wananchi wa mkoa huu wanapata huduma stahiki na endelevu kwasababu Hospitali yetu ni kongwe kwa maana ya miundombinu na ina eneo finyu tunaomba kuboreshewa miundombinu kwa kujenga majengo ya ghorofa"amesema Nyakiroto.***

### NENO LA TAASISI KWA SERIKALI

"Tunamshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan na serikali hii ya awamu ya sita anayoingoza kwa jitihada zake za kuboresha huduma za Afya ndani ya Mkoa, kwa kuendelea kutoa rasilimali fedha na watu katika kuhakikisha wananchi wa mkoa huu wanapata huduma stahiki na endelevu kwasababu Hospitali yetu ni kongwe kwa maana ya miundombinu na ina eneo finyu tunaomba kuboreshewa miundombinu kwa kujenga majengo ya ghorofa"amesema Nyakiroto.

Anasema tayari wameishaandaa mpango mkakati wa ujenzi (Master plan) ya hospitali inayoweza kumudu majengo yote na hopsitali bado ikaendelea kufanya kazi hivyo, tunaomba Serikali iendelee kutuwezesha kwa kutupatia fedha ya kujenga majengo ya kwenda juu .

### WITO WETU KWA JAMII INAYOHUDUMIWA

Anaiomba jamii kuendelea kuwa na imani na Taasisi hiyo kwa huduma zinazotolewa, waendelee kutoa maoni, mapendekezo na ushauri juu ya huduma zinanzotolewa hospitalini hapo kupitia njia mbalimbali zilizowekwa na uongozi wa hospitali kama vile masanduku na madaftari ya maoni (yanapatikana kila sehemu ya kutolea huduma), kurasa za mitando ya kijamii, tovuti ya hospitali, simu za viongozi wa hospitali na kitengo cha Huduma kwa wateja au kufika moja kwa moja Ofisi za viongozi wa hospitali.

Nawasihi wananchi wapatapo changamoto za huduma zetu kuwasiliana na viongozi wa hospital ili wapate majibu sahihi kwasababu kwa sasa hospitali imeboreshwa, inao wataalam na huduma zinazotolewa ni za uhakika ambazo zinatakiwa kuthaminiwa na kuenziwa na wananchi wa mkoa huu, nawasihi jamii tuendelee kusaidiana pale wananchi wanapopata changamoto ya kiafya husani wanaopata ajali kufika kwenye vituo vya kutolea huduma kwa wakati.

"Msianzie kwingine ndipo mje hospitali kwani kufanya hivyo ni kuchelewa kupata huduma kwa wakati ndivyo hivyo wataalam wanavyokuwa na nafasi kubwa sana ya kumpatia tiba ambayo itasaidia apone mapema na kuzuia madhara mengine yanayoweza kutokea ambayo yanakwepeka kwasababu unaweza kuugua ukatibiwa kwa kuchelewa hivyo hutorudi kwenye hari yako ya kawaida ili usifike huko ni kuwahi kufika vituo vya kutolea huduma, lakini naomba niliweke sawa hili huko nyuma hatukuwa na dk.bingwa wa mifupa walikuwa wakifika hapa tunawapeleka Bugando"ameeleza Dkt. Nyakiroto

Anasema kutokana na usumbufu wa watu kwenda Bugando walikuwa wakiamua kwenda kwa waganga wa tiba asili hivyo kwasasa tunao wataalam tunafanya huduma zote za upasuaji wa mifupa ambao unatakiwa kufanyika kwa wagonjwa na kushauri wagonjwa nini kifanyike na kupokea ushauri huo kwasababu tunapata wagonjwa wengi wa mifupa na wanapoambiwa kufanya upasuaji wa kuondoa matatizo ya mifupa hawakubali.



Mashine Mpya na Saidizi za Upumuaji (Ventillator Mashine) zinazotumika katika chumba cha Wagonjwa Maututi.



Muonekano wa jengo la Wagonjwa wa Dharura (EMD) katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa, Bukoba.

MIAKA MITATU YA RAIS DK. SAMIA NA UBORESHAJI SEKTA YA AFYA NCHINI

# Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Katavi inavyojivunia miaka mitatu ya Rais Samia




**Na ELIZABETH JOHN**

HOSPITALI ya Rufaa ya Mkoa wa Katavi ni moja ya Hospitali za Rufaa za Mikoa nchini Tanzania zinazojivunia mafanikio mbali mbali kwa kipindi cha miaka mitatu ya Rais Dk. Samia Suluhu Hassani, tangu aingie madarakani Machi 19, 2021.

Hospitali hiyo ilianza kutoa huduma za rufaa katika majengo ya Hospitali ya Manispaa ya Mpanda mwaka 2018 na imekuwa ikitoa huduma za rufaa kwa Halmashauri tano za Mkoa wa Katavi pamoja na Mikoa ya Jirani.

Kwa mujibu wa Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Rufaa Mkoa wa Katavi, Dk. Serafini Patrice, hospitali hiyo ilianzishwa kutekeleza lengo la serikali la kusogeza huduma za Rufaa karibu na wananchi, hivyo kupunguza gharama na muda wa kufuata huduma hizo mbali.

Alisema Februali 15, mwaka jana huduma za hospitali za wagonjwa wa rufaa zilihamishiwa katika majengo mapya yaliyojengwa katika eneo la Rungwa, Manispaa ya Mpanda baada ya kukamilika kwa ujenzi wa jengo la Wing A.

"Shughuli za ujenzi wa Wing B na majengo mengine zitaendelea kutekelezwa baada ya Hospitali kupokea fedha zilizotengwa katika bajeti kwa mwaka wa fedha 2023/2024.

**MAFANIKIO YA HOSPITALI**

Dk. Patrice anasema katika kipindi cha miaka mitatu ya Rais Dk. Samia wamefanikiwa kukamilisha ujenzi wa majengo na miundo mbinu ya hospitali.

Alisema katika kipindi cha mwaka 2021 hadi mwaka huu, shughuli ya kukamilisha majengo ilitekezwa ambapo jengo la Wing A lilikamilika, ujenzi wa maabara, EMD, ICU,Nyumba ya Mtumishi, Ukarabati wa chumba cha tiba Mtandao, ujenzi wa chumba za kuzalishia gesi tiba, chumba cha kuhifadhia jenereta kwa ajili ya umeme wa dharura.

Mchanganuo wa gharama ni kama inavyoonekana katika jedwali lifuatalo:

**Jedwali 1: Utekelezaji wa Miradi ya ujenzi katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa Katavi**

| S/N | AINA YA JENGO/MAJENGO YANAYOJENGWA | GHARAMA ZA MRADI(Fedha iliyotolewa) | (%) HATUA ILIYOFIKIWA | KIASI CHA FEDHA KILICHOTUMIKA(TSHS) | KAZI ZINAZOENDELEA |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Ujenzi wa jengo la OPD, Uchunguzi na Afya ya uzazi – Miundombinu ya ICT, HVAC, Lift, na Hewa Tiba | 9,820,000,000 | 99 | 9,820,000,000 | Ujenzi wa Wing A na Mifumo mingine imekamilika na kuanza kutumika isipokuwa Ufungaji wa "Lift" ambao unaendelea na upo kwenye hatua za mwisho. Ujenzi wa Wing B unaendelea ambapo kwa sasa tunasubiria fedha Tshs.5,000,000,000.00 iliyotengwa katika bajeti ya 2023/2024kwa ajili ya kuendelea na ujenzi. |
| 2. | Nyumba ya Mtumishi | 90,000,000 | 100 | 90,000,000 | Ujenzi umekamilika na nyumba inatumika. |
| 3. | Ukarabati wa chumba cha tiba mtandao (Telemedicine) | 19,000,000 | 100 | 19,000,000 | Ukarabatiumekamilika na samani zimesimikwa bado tunasubiri server kwa ajili ya kuunganisha na kuanza kutumika. |
| 4. | Ujenzi wa jengo la huduma za CT-Scan | 2,180,000,000 | 100 | 2,180,000,000 | Mashine ya CT-Scan imeshasimikwa na huduama zinaendelea kutolea. |
| 5. | Ujenzi wa Jengo la Huduma za dharura (EMD) | 300,000,000.00 | | 300,000,000.00 | Ufungaji wa milango, kuingiza umeme, Kukamilisha vyoo, kuingiza maji pamoja na Mfumo wa TEHAMA. |
| 6. | Ujenzi wa Jengo la wagonjwa mahututi (ICU) | 560,000,000.00 | 99 | 560,000,000.00 | Ujenzi umekamilika isipokuwa ufungaji wa AC hata hivyo jengo limeanza kutumika. |
| 7 | Ujenzi wa Jengo la Maabara | 987,000,000.00 | 100 | 987,000,000.00 | Ujenzi umekamilika na maabara inatumika |
| 8 | Ujenzi wa Jengo la Dialysis | 196,920,363.72 | 0 | 0.00 | Mradi upo katika hatua za awali za ujenzi, na uandaaji wa BOQ na michoro |
| | **Jumla** | **14,152,920,363.72** | | **13,956,000,000** | |

MIAKA MITATU YA RAIS DK. SAMIA NA UBORESHAJI SEKTA YA AFYA NCHINI



# Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Katavi inavyojivunia miaka mitatu ya Rais Samia

**UPATIKANAJI WA BIDHAA ZA AFYA**

Dk. Patrice alisema hospitali ya Rufaa ya Mkoa Katavi imekuwa ikipokea bidhaa za afya ambazo zinanunuliwa kupitia ruzuku inayotolewa na Serikali Kuu, fedha za uchangiaji wa malipo kwa huduma na bima ya afya.

Alisema katika kipindi cha 2021-2024 kiasi cha sh. 4,987,529,330.14 kilitumika kwa ununuzi wa bidhaa za afya (dawa, vifaa tiba na vitendanishi).

Alisisitiza kuwa baadhi ya vifaa vimekuwa vikiletwa kama ruzuku kutoka Wizara ya Afya, hali ya upatikanaji wa bidhaa za afya sasa ni asilimia 95.6.

"Fedha za uchangiaji wa huduma za afya zimekuwa zikipokelewa kwa wakati hivyo kuweza kupata fedha kwa ajili ya ununuzi wa bidhaa za afya kulingana na mwongozo.

"Upatikanaji wa bidhaa za afya MSD umeongezeka kutoka asilimia 30 hadi kufikia asilimia 50," alisema Dk. Patrice.

Alisema hadi sasa hopitali hiyo ina mashine ya mionzi moja, Mashine ya Mionzi ya Ultra sound, Mashine ya CT Scan, Mashine tatu za uchunguzi wa huduma za afya ya kinywa na meno, Mashine ya dawa ya usingizi, Mtambo wa kuzalisha Hewa Tiba, Mashine za Maabara zote zinafanya kazi na Mashine sita za Dialysis ambazo bado hazijafungwa kwa kuanza kutumika.

**HUDUMA KWA WAGONJWA**

Dk. Patrice alisema hadi Januari mwaka huu, jumla ya wateja 36,044 (OPD-32,330 na IPD 3,714) walipatitwa huduma tangu kuanzishwa kwa huduma za Afya katika hospitali hiyo, hali inayoonyesha kwa kiwango kikubwa ya uhitaji wa huduma hii kwa wananchi wa Katavi na wale wa Mikoa ya jirani.

"Ni kiwango kikubwa cha idadi ya wateja waliopatiwa huduma, kutoka Katavi na Mikoa ya jirani, tunajivunia hilo na tunaendelea na kuboresha huduma zetu," alisema.

*Dk. Patrice alisema hospitali ya Rufaa ya Mkoa Katavi imekuwa ikipokea bidhaa za afya ambazo zinanunuliwa kupitia ruzuku inayotolewa na Serikali Kuu, fedha za uchangiaji wa malipo kwa huduma na bima ya afya.*



Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Rufaa Mkoa wa Katavi, Dk. Serafini Patrice,

Alisema hospitali hiyo ina jumla ya magari matano kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli mbali mbali za utawala, utoaji wa huduma za afya, usambazaji na usimamizishi shirikishi.

**UPUNGUFU WA WATUMISHI**

Dk Patrice alisema hospitali ya rufaa ya Mkoa ina jumla ya watumishi 320 sawa na asilimia 43.5 ya watumishi 734 wanaohitajika kulingana na ikama.

"Hivyo upungufu wa watumishi 414, katika kipindi cha 2021 hadi 2024 wameajiriwa watumishi wapya 125 wa kada mbali mbali," alisema.

Dk. Patrice alisema hospitali ya rufaa Katavi ina jumla ya vitanda 40 vya kulaza wagonjwa kati ya vitanda 170 Vinavyohitajika, hivyo bado wahaitaji vitanda vingine.

**IDARA ZILIZOPO**

Daktari huyo alisema hospitali ya Rufaa ya Mkoa imekuwa ikitekeleza majukumu yake kwa kupitia idara na vitengo mbalimbali kulingana na ujuzi wa wataalamu wa husika.

Alitaja baadhi ya idara na vitengo hivyo katika hospitali Teule ya Rufaa kuwa ni Idara ya Manunuzi, Idara ya ICT,

Idara ya Upasuaji, Idara ya Afya ya Mama na Uzazi, Idara ya Fedha, Idara ya Utawala, Kitengo cha Meno, Kitengo cha Macho na kitengo cha Maabara.

Vitengo vingine ni kitengo cha Mionzi, kitengo cha Famasi, kitengo cha Wagonjwa wa nje, kitengo cha Bima, kitengo cha Dharura, Kitengo cha USTAWI wa Jamii na Kitengo cha Watoto.

**MALENGO YA HOSPITALI.**

Dk. Patrice alisema katika utekelezaji wa shughuli zake Hospitali Teule ya Rufaa imejiwekea malengo ya kuboresha huduma za afya kwa kutoa huduma bora zaidi na za viwango kwa kuboresha huduma ya mteja (customer care) na ubora (QI) ikiwemo kuweka umuhimu wa mrejesho kwa wateja.

Alisema pia wanahakikisha upatikanaji wa dawa na vifaa tiba katika hospitali muda wote kukidhi mahitaji.

"Tunaboresha utoaji na upatikanaji wa huduma za afya ya mama na mtoto kupunguza vifo vya mama na watoto wachanga.

"Tunaboresha na kuongeza upatikanaji wa mapato kwa kudhibiti mianya ya upotevu wa mapato na kuimarisha mifumo ya ukusanyaji wa mapato," alisema.

Pia alisisitiza kuimarisha huduma za dharura na wagonjwa mahututi na kuboresha utoaji wa elimu kwa jamii katika magonjwa yasioambukiza na umuhimu wa mazoezi kwa afya.



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA AFYA
HOSPITALI YA RUFAA YA MKOA SUMBAWANGA

# Bilioni 2.5 zilivyo boresha huduma Hospitali ya Rufaa Mkoa Sumbawanga miaka mitatu ya Rais Mhe. Dkt. Samia



MGANGA Mfawidhi wa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa Sumbawanga, Dk. Ismail Macha.

**Na JANE MWAKYOMA,** Rukwa

Bilioni 2.5 zilivyosaidia kuleta mageuzi katika hospitali ya Rufaa ya mkoa sumbawanga.

Sekta ya Afya ni miongoni mwa sekta ambayo imeendelea kukua siku hadi siku nchini na kupunguza adha kwa wananchi kutembea umbali mrefu kufuata huduma za matibabu na kupunguza vifo vya mama na mtoto kutokana na miradi mingi ya Afya kujengwa karibu na wananchi.

Katika utekelezaji wa miradi ya Afya kwa miaka mitatu ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania DK Samia Suluhu Hassan yapo mengi aliyoyafanya kuhakikisha wananchi wanapata matibabu karibu na makazi yao ususani katika mkoa wa Rukwa ambao umehakiakisha vituo vya Afya,Zahanati na hospitali zinajengwa pamoja na ununuzi wa vifaatiba ili kuimarisha huduma za matibabu kwa wananchi na kupunguza umbali mrefu wa kufuata huduma hiyo.

Akizungumza ofisini kwake na gazeti hili Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa Sumbawanga Dk. Ismail Macha alisema katika kipindi cha miaka mitatu kuna mafanikio ambayo wameyapata kupitia serikali hii ya awamu ya sita ambapo miradi mingi ya Afya imetekelezwa na kuna miradi saba iliyotekelezwa katika hospitali ya Rufaa ya mkoa sumbawanga kwa kipindi cha miaka mitatu kupitia fedha za IMF.

Anasema kuna miradi ambayo ilijengwa na miradi mingine ilifanyika ukarabati pamoja na ununuzi wa vifaatiba ili kuhakikisha wananchi wanapata huduma bora na katika mazingira bora ikiwa mkoa wa Rukwa unawakazi wapatao 1,540,519 wanaume ni 743,119 na wanawake 797,400 katika sensa ya watu na makazi ya mwaka 2022, ambapo wasitani kwa siku inapokea wagonjwa wa nje ( OPD) 172 kwa siku na wanaolazwa(IPD) ni wagonjwa 69 kwa siku.

"Mimi binafsi ni kama miaka inaendana na miaka ya mama yetu Rais wetu DK Samia Suluhu Hassan, kipindi nilipofika Desemba mwaka 2021 nilikutana na miradi ya IMF ambayo ilikuwa inatekelezwa hapa ambayo ilikuwa ni miradi 7 na tayari imetekelezwa na ujenzi wake umekamilika kwa fedha za IMF" anaeleza

*"Mimi binafsi ni kama miaka inaendana na miaka ya mama yetu Rais wetu DK Samia Suluhu Hassan, kipindi nilipofika Desemba mwaka 2021 nilikutana na miradi ya IMF ambayo ilikuwa inatekelezwa hapa ambayo ilikuwa ni miradi 7 na tayari imetekelezwa na ujenzi wake umekamilika kwa fedha za IMF"*

**DK Ismail Macha**



Anataja miradi saba ulitotekelezwa kwa kipindi cha miaka mitatu ya serikali ya awamu ya sita mganga mfawidhi wa hospitali ya Rufaa ya mkoa sumbawanga DK Ismail Macha alisema kuna miradi ambayo ilijengwa na mingine ilifanyiwa ukarabati kutokana na hospitali hiyo kuwa kongwe sana na miundombinu ya majengo ilikuwa imechakaa.

"Serikali ya awamu ya sita imeleta fedha nyingi za miradi na Miradi iliyotekelezwa kwa kipindi cha miaka mitatu ya mama yetu Rais Dk Samia Suluhu Hassan ipo saba na tumekuwa tukijivunia kutekelezwa kwa miradi hii kwasababu ni miradi mikubwa imejengwa kwa gharama kubwa na pili hospitali yetu haikuwa na mashine kama CT- Scan, mtambo wa hewatiba vyote hivi tulikuwa tunategemea mbeya lakini leo hivi vitu tunavyo na vinafanya kazi ni mafanikio makubwa sana katika hospitali yetu hii, moja ya miradi iliyotekelezwa moja ni ukarabati wa jengo la wangonjwa mahututi (ICU) ambapo ujenzi huo uligharimu milioni 270,300,680, ujenzi wa jengo la CT-Scan na ununuzi wa mashine yenyewe uliogharimu bilioni 1,652,326,338.6, ukarabati mkubwa wa chumba cha Tibamtandao (Telemedicine) na ununuzi wa Samani na gharama ni milioni 62,942,000, ujenzi wa nyumba ya mtumishi ambayo kwa sasa inatumika na iligharimu shilingi milioni 90,000,000, ununuzi wa vifaatiba vingine zaidi vya ICU na EMD bilioni 1,461,554,000, ununuzi wa magari mawili mapya kwa ajili ya hospitali moja la kazi za utawala na ambulance ( advanced ambulance) gharama yake ni milioni 211,150,280, namba saba ni mradi mkubwa katika hospitali yetu hii ambao ni ununuzi wa mtambo wa kuzalishia hewatiba ( oxygen) uliogharimu milioni 333.3" anaeleza.

"Moja tulikuwa na chumba cha wagonjwa mahututi (ICU) ndogo ambayo ilikuwa na uwezo wa vitanda 5 na tungeweza kujenga ICU kubwa zaidi lakini tumejenga jengo la ICU lenye uwezo wa vitanda 13, kwanini hatukujenga kubwa zaidi.

Kwahiyo tukaenda kutoka vitanda 5 mpaka vitanda 13, lakini hata hivyo vitanda 5 vilikuwa havina mashine muhimu zinazo hitajika kwaajili ya kila kitanda zilikuwa mashine chache na wangonjwa walikuwa wanatumia kwa kupokezana lakini kwa sasahivi kila kitanda tulivyonavyo ICU kina mashine yake tofauti na ujenzi huu ulighalimu kiasi cha shilingi milioni 270.3, na ujenzi huu ulilenga kwanza kuipanua zaidi iwe kubwa kuliko awali lakini pili kuikarabati kwasababu hospitali hii ni ya zamani kidogo" anaeleza.

Aidha anasema awali hospitali hiyo haikuwa na mashine ya CT Scan, mtambo wa hewatiba ambapo huduma hizo zilikuwa zikifuatwa katika hospitali ya rufaa ya kanda mbeya hali iliyokuwa ikisababisha wangonjwa wengi kushindwa kumudu gaharama za matibabu pamoja na gharama za usafiri.

"Katika mradi huu kwanza tulikuwa tunafanya vitu viwili tulikuwa hatuna jengo, pili katika mkoa wetu tulikuwa hatuna kifaa hiki kabisa hii ni mashine ya kwanza kufika katika mkoa wetu,wangonjwa wote waliotakiwa kufanyiwa kipimo hiki cha CT Scan walitakiwa kwenda mbeya, kwasasa ipo hapa imenunuliwa na tayari inafanya kazi, kwenye mradi huu tumefanya vizuri kwanza tulijenga jengo lililogharimu shilingi milioni 205 na tukanunua mashine shilingi bilioni 1.4 ukichukua gharama ya jengo na gharama ya ununuzi wa mashine hiyo jumla inakuja shilingi bilioni 1.6" anaeleza.

"Mradi wa kuzalisha hewatiba (Oxygen) mradi huu umetubadilishia sana maisha kipindi cha nyuma kabla mtambo huu wa gesi haujaja kwenye hospitali yetu tulikuwa tunakwenda kuchukua,kujaza Dar es saalamu ambapo kuna umbali takribani zaidi ya km 1000,kuna gharama za gari na gharama za watu kwenda kupeleka na kuchukua mitungi ya hewatiba na siyo sisi peke yetu hata vituo vya afya vyote vilikuwa vinafanya hivyo lakini sasahivi tuna mtambo hapa hap hospitali unaendelea kufanya kazi na umetuondolea gharama kubwa sana ya kufuata huduma hiyo Dar es saalamu"anaeleza.

Aidha anasema katika utekelezaji wa miradi ya afya ambapo mwaka 2020 hospitali hiyo ilikuwa imejenga jengo la dharula lakini jengo hilo lilikuwa halina vifaa tiba lakini kwasasa jengo hilo limekamilika pamoja na vifaatiba vimenunuliwa na tayari jengo hilo linatumika.

Pia anasema wamefanikiwa kununua gari mbili moja ni ya



CT - Scan



MTAMBO wa kuzalisha hewatiba ( oxygen).

MIAKA MITATU YA RAIS DK. SAMIA NA UBORESHAJI SEKTA YA AFYA NCHINI

# Bilioni 2.5 zilivyo boresha huduma Hospitali ya Rufaa Mkoa Sumbawanga miaka mitatu ya Rais Mhe. Dkt. Samia



Wodi ya wangonjwa mahututi ( ICU).

utawala na ya pili ni gari ya wangonjwa ( ambulance) ambapo awali hospitali hiyo ilikuwa na gari moja tu ya wangonjwa ambapo ilikuwa inasababisha kutumia gari binafsi kufanya kazi za kiofisi.

"Tulikuwa na changamoto ya gari tayari tumenunua lakini hatujatatua kwa asilimia100 lakini tumepunguza kwasasahivi kwanza tulikuwa hatuna gari kwaajili ya usimamizi na utawala mara nyingi tulikuwa tunatumia magari binafsi kwenda Kufanya kazi za utawala kwahiyo tumepata gari 2 moja kwaajili ya shughuli za utawala na pili kwaajili ya wagonjwa ( ambulance) ninaposema ambulance ni pamoja na vifaa vyote vilivyomo ndani ambapo ukiwa unamsafirisha mgonjwa lazima huduma za matibabu ziendelee na sisi rufaa zetu tunapeleka Mbeya kama km 325,hapa tunaongelea advance ambulance kuna ambulance kama gari tu la kubeba wagonjwa lakini kuna advance ambulance kama chumba cha daktari chenye vifaa vyote, kwasasa tuna magari mawili ya wagonjwa ukiunganisha lile la zamani na hili mpya tuna ambulance mbili" anaeleza.

Anasema katika ujenzi mkubwa wa miundombinu katika hospitali pamoja na ukarabati mkubwa iliyofanyika na uboreshaji wa huduma na ununuzi wa vifaa tiba wameweza kupunguza vifo vya mama na mtoto ambapo mwaka 2021 vilitokea vifo 18, 2022 vifo 13 na mwaka 2023 vilitokea vifo 9 hii ni kutokana na jitihada za kuendelea kutoa huduma bora kwa akina mama wajawazito na watoto chini ya miaka 5 ili kuondoa kabisa vifo vya watoto wachanga na akina mama wakati wa kujifungua.

DK Ismail Macha anasema palipo na mafanikio hapakosi changamoto, kutokana na uboreshaji wa hospitali hiyo bado kuna changamoto kadhaa zinazosababisha upungufu wa wataalamu na madaktari bingwa ambapo asilimia kubwa madaktari bingwa wapo 7, waliopo wapo katika fani 5 na fani hizo zinatumiwa na madaktari bingwa wawili na fani nyingine zinatumiwa na daktari mmoja mmoja.

"Sisi kwasasahivi hatuna fani zote, tuna madaktari bingwa 7 lakini katika fani 5 kuna madaktari ambao wanakuwa wawili katika fani moja kuna fani mbili ambazo zina madaktari bingwa wa wili wa wili lakini fani nyingine zina daktari mmoja mmoja na kwa sasahivi tuna madaktari kadhaa ambao wako shuleni kwaajili ya kujifunza kuja kujaza nafasi nyingine za kibingwa kwa mfano tunahangaika sana na daktari bingwa wa mifupa hapa hospitalini kwetu hatuna" anaeleza.

"Ukarabati wa chumba cha Tibamtandao ( telemedicine) tunaweza kuwa tumeleta changamoto nyingine katika hospitali kwasababu huwezi kutafsiri picha hizo lakini tumekuwa tukituma picha za CT scane Mbeya kwa bahati mbaya hatuna mtaalamu wa kutafsiri hizo picha tunatuma Mbeya wanazitafsiri na hakuna haja ya mgonjwa kufuata huduma hizo" anaeleza.

DK Ismail anasema wanamikakati kadhaa ambapo kwanza wanajivunia kutokuwa na madeni kwa watumishi wao ambapo suala muhimu kwao ni pamoja na kuhakikisha sitahiki zote za wafanyakazi zinalipwa ili kuwapa morali ya kuendelea kufanya kazi.

"Tuna mikakati kadhaa kwanza wanasema kitu muhimu na cha kwanza ni rasilimali watu na sisi kitu cha kwanza tunajari stahiki za wafanya kazi kuhakikisha stahiki zinalipwa kulingana na miongozo,hapo nyuma tulikuwa na deni kubwa sana wakati mwingine inafanya morali ya kufanya kazi inapungua lakini kwa mwaka wa fedha Juni 2023 hatukuwa na deni lolote la mtumishi tulihakiakisha stahiki za watumishi zinalipwa na wakati mwingine zilipwe kwa wakati ili waendele kufanya kazi kwa ufanisi" anaeleza.

"Kuendeleza watumishi kitaaluma kwa kushirikiana na wizara ya afya ili kuongeza fani za kibingwa tulizonazo kwa sasa na kuongeza ubora wa huduma,kuendelea kuwashirikisha madaktari bingwa kutoka hospitali mbalimbali kutoa huduma mkoa wa Rukwa mathalani tumewahi kushirikiana na ocean Road cancer Institute na Mbeya Zonal Referral Hospital, kutengeneza mpango kabambe wa uendelezaji wa hospitali ( Master plan) na kubadilisha majengo mengi ya zamani yaliyopitwa na wakati kujenga majengo ya kisasa zaidi katika hospitali yetu tuna majengo machache sana ambayo yanakizi vigezo vya wizara kwahiyo inampango kabambe wa kubadilisha majengo ili kufikia viwango vya wizara mpango huo labda ndani ya miaka kumi ijayo tuendele kubadilisha majengo haya taratibu tukishirikiana na wizara ya fedha ili kuboresha huduma na mwisho tutaendelea kuongeza huduma ambazo hazipatikani Rukwa mfano kwa sasa tunashughulikia huduma ya kuchuja damu (Haemodialysis) uzuri uliopo tulisha nunua

**"Sisi kwasasahivi hatuna fani zote, tuna madaktari bingwa 7 lakini katika fani 5 kuna madaktari ambao wanakuwa wawili katika fani moja kuna fani mbili ambazo zina madaktari bingwa wa wili wa wili lakini fani nyingine zina daktari mmoja mmoja na kwa sasahivi tuna madaktari kadhaa ambao wako shuleni kwaajili ya kujifunza kuja kujaza nafasi nyingine za kibingwa kwa mfano tunahangaika sana na daktari bingwa wa mifupa hapa hospitalini kwetu hatuna" anaeleza.**

mashine zipo MSD tunaendelea kuzilipia na kitu cha kwanza ni ukarabati wa jengo kwaajili ya huduma hiyo"anaeleza.

Aidha anasema katika suala la madaktari bingwa kwa fani ambazo hospitali hiyo hakuna madaktari bingwa wataendelea kushirikiana na hospitali zingine ili kuhakikisha wagonjwa wanapata matibabu sahihi na ya uhakika.

"Tumekuwa tukishirikiana na madaktari bingwa kutoka hospitali zingine kwa mfano kama miezi saba ivi imepita walikuja madaktari bingwa hapa kutoka mbeya ambao tulishirikiana kutoa huduma za kibingwa kama dakitari wa mifupa ambapo hospitali yetu haina daktari wa mifupa pamoja na madaktari kutoka hospitali ya ocean Road tulikuwa nao hapa yote hii ni kuimarisha huduma za afya kwa wagonjwa" anasisitiza.

Dk Ismail Macha anasema kwasasa hakuna mradi mikubwa inayoendelea ila wapo tayari kusimamia miradi yoyote inayoanza wakati wowote ili kuendelea kuboresha huduma za matibabu kwa wananchi wa mkoa huo.

Anaishukuru serikali ya awamu ya sita inayoongizwa na Rais DK Samia Suluhu Hassan kwa kutoa fedha nyingi na uwekezaji mkubwa alioufanya katika sekta ya afya kuhakikisha huduma za afya zinawafikia wananchi katika maeneo yao na kuahidi kuchapa kazi bila kuchoka ili kuhakikisha wanafikia utekelezaji wa asilimia 100 wa ilani ya chama cha mapinduzi ( CCM) ya mwaka 2020.

" Kwaniaba ya bodi ya ushauri ya hospitali, kwaniaba ya menejimenti ya hospitali na wananchi wa mkoa wa Rukwa tunaomba tutoe shukrani za dhati sana kwa serikali ya awamu ya sita inayoongozwa na Rais DK Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kutoa fedha nyingi na kutekeleza miradi mingi katika sekta ya afya,hatuongelei hospitali yetu tu pekee yake lakini tukiangalia kwenye mkoa wetu kuna miradi mingi imetekelezwa lakini sisi tumekuwa sehemu ya mkoa kutekeleza miradi hiyo,miradi yote hii imegharimu fedha na siyo kidogo ni fedha nyingi na matokeo yake tunayaona sasahivi lakini vilevila tutoe ahadi yetu kuwa tutaendelea kuchapa kazi tunajua kuna ilani ya CCM ya mwaka 2020 kuna vitu lazima tuvitekeleze kabla ya mwaka 2025 tutachapa kazi bila kuchoka tuhakikishe kuwa tumetekeleza ilani ya CCM ya mwaka 2020 kwa100%," anaeleza.

Anawataka wanajamii wenye matatizo mbalimbali ya kiafya kuja hospitalini hapo kupata huduma za matibabu na kushirikiana katika utunzaji wa miundombinu ya hospitalini hapo ili iweze kudumu vizazi na vizazi.

" Wito wangu kwa jamii hizi fedha zote zilizotumika kujenga miradi yote hii itakuwa ni kazi bure kama jamii haitumii, kwahiyo nitumie frusa hii kuwakaribisha wanajamii na wananchi kwa ujumla wote wa mkoa huu na mikoa jirani hata na nchi jirani kuja kutumia huduma sisi tupo hapa kwaajili yao na hospitali ipo kwajili yao tunawakaribisha waje watumie huduma zetu,kitu cha pili kutunza miundombinu hii ili iendelee kuwa uendelevu naomba sana jamii inayotuzunguka pamoja na kuwa sisi wa hospitali ndiyo tunatakiwa tuwe wa kwanza kutunza miundombinu hii lakini na jamii itusaidie kutunza miundombinu hii" anaeleza.



Nyumba ya mtumishi.



Gari ya usimamizi na ya kubebea wagonjwa.

MIAKA MITATU YA RAIS DK. SAMIA NA UBORESHAJI WA SEKTA YA AFYA NCHINI

# HOSPITALI YA LIGULA INAVYOKATA MAWIMBI KWA UBORA WA HUDUMA





Rais Dk. Samia Suluhu Hassan

## MAFANIKIO MIAKA MITATU RAIS SAMIA MADARAKANI



MIAKA MITATU YA RAIS DK. SAMIA NA UBORESHAJI WA SEKTA YA AFYA NCHINI

# Hospitali ya Ligula inavyokata mawimbi kwa ubora wa huduma



JENGO la mama na Mtoto(vyumba 7 vya kujifungulia Kwa mara moja)

**Na ABDUL DUNIA**

HOSPITALI ya Rufaa ya Mkoa wa Mtwara (Ligula), ni miongoni mwa hospitali kubwa na kongwe katika mkoa huo uliopo kusini mwa Tanzania.

Hospitali hiyo iliyopo mtaa wa Chuno katika Halmashauri ya Manispaa ya Mtwara, ilifunguliwa Oktoba 14, 1964 na Rais wa kwanza, Hayati Mwalimu Julius Nyerere.

Pamoja na kuwa na miaka takriba 60 tangu kuanzishwa kwake, lakini hospitali hiyo imekuwa na historia nzuri na ya kuvutia.

Miongoni mwa historia ya kusisimua juu ya hospitali hiyo ni kutokana na baadhi ya majengo yake yalitokana na hospitali nyingine iliyokuwa ikiitwa FRELIMO (ikiwa na maana ya Chama cha siasa Msumbiji).

Hospitali ya FRELIMO iliyokuwa umbali wa mita 300 kutoka katika hospitali ya Ligula, ilikuwa ikitumika kuwahudumia wapiganaji na majeruhi wa vita ya Msumbiji.

Hata hivyo, mwaka 1976 majengo ya FRELIMO yalikabidhiwa kwa Hospitali ya Lugula na ndio ukawa mwanzo wa utanuzi wa eneo la hospitali hiyo kongwe na kubwa mkoani humo.

> “**HOSPITALI** ya Rufaa ya Mkoa wa Mtwara (Ligula) inaendelea kunufaika na miaka mitatu ya Rais Samia Suluhu Hassan kutokana na mpango wa kuendeleza wataalamu wa afya ambao serikali imeutekeleza kwa kishindo,” alisema.
> Alisema hospitali hiyo inajivunia kuwa na wataalamu wengi ambao wamekwenda kusomea udaktari bingwa....
>
> *Mganga Mfawidhi wa hospitali hiyo, Dk. Zawadi Bwanali*

Awali, Ligula ilikuwa miongoni mwa hospitali ambazo zilikua zikihudumu katika majengo chakavu na miundombinu finyu, huku ikiwa na waatalamu wachache ambao hawakuwa toshelezi katika utoaji wa huduma bora kwa wananchi wa mkoa humo na Kanda ya Kusini.

Jitihada za Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, katika kuboresha sekta ya afya nchini, zimechangia kwa kiasi kikubwa hospitali hiyo kutoa huduma bora zaidi na za kisasa kwa wananchi wa mkoa huo.

Mganga Mfawidhi wa hospitali hiyo, Dk. Zawadi Bwanali, amesema serikali ya awamu ya sita chini ya Dk. Samia imekuwa ikiendelea kufanya jitihada mbalimbali kuhakikisha hospitali hiyo inatoa huduma bora kwa wananchi.

Dk. Zawadi alisema katika kipindi cha miaka mitatu ya Rais Dk. Samia, kumekuwa na mabadiliko makubwa ya uboreshaji wa huduma za afya.

Mganga huyo mfawidhi



MUONEKANO wa Ndani jengo la mama na Mtoto

## MIAKA MITATU YA RAIS DK. SAMIA NA UBORESHAJI WA SEKTA YA AFYA NCHINI



JENGO la ICU limehudumia zaidi ya Wagonjwa 100 Zote ni Neema za mama Kwa kipindi Cha Miaka mitatu

# Hospitali ya Ligula inavyokata mawimbi kwa ubora wa huduma

alisema hospitali hiyo inamshukuru Rais Samia na serikali yake kwa kuweka jitihada za kila namna kuhakikisha huduma bora zaidi zinapatika katika hospitali hiyo.

Dk. Zawadi alisema katika mwaka wa fedha 2021/2022, serikali iliitengea hospitali hiyo kiasi cha sh. bilioni 5.4 kwa ajili ya ujenzi wa majengo mbalimbali.

Alisema majengo hayo ni kwa ajili ya kutolea huduma za dharura (Emergency Department), wagonjwa mahututi na uangalizi maalumu (ICU), wagonjwa wa nje (OPD) na tiba mtandao (Telemedicine).

Mengine ni ununuzi wa vifaa tiba na vifaa vya uchunguzi wa maabara, ujenzi wa jengo la upasuaji na ujenzi wa jengo la mama na mtoto.

Pia, Dk. Zawadi aliweka wazi kuwa, Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Mtwara (Ligula), imejipanga kuendeleza utoaji wa huduma bora kwa jamii.

Alisema miongoni mwa huduma walizojipanga kutoa kwa ubora ni zile za kibingwa na za mkoba katika maeneo mbalimbali yanayozunguka mkoa wa Mtwara.

"Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Mtwara (Ligula) inaendelea kunufaika na miaka mitatu ya Rais Samia Suluhu Hassan kutokana na mpango wa kuendeleza wataalamu wa afya ambao serikali imeutekeleza kwa kishindo," alisema.

**MWAKA 2021 / 2022**

**SERIKALI** iliitengea hospitali hiyo kiasi cha sh. bilioni 5.4 kwa ajili ya ujenzi wa majengo mbalimbali.



JENGO jipya la upasuaji(uwezo wa pasuaji 5 Kwa mara moja)

Alisema hospitali hiyo inajivunia kuwa na wataalamu wengi ambao wamekwenda kusomea udaktari bingwa na ubingwa bobezi, ambao alikiri ni kioo tegemezi kwa hospitali hiyo katika utoaji wa huduma bora.

"Uwezo wa vitanda ni zaidi ya 250 na watumishi wa taaluma za afya (zaidi ya) 270 wakiwemo madaktari bingwa wa fani za upasuaji na magonjwa ya kina mama, madaktari, wauguzi na wakunga waliosajiliwa, wafamasia, wateknolojia na watumishi wengineo," alisema.


Katika kuhakikisha jamii inanufaika zaidi ma miradi iliyotekelezwa na serikali ya awamu ya sita, Dk. Zawadi alisema hospitali inaendelea kuhakikisha utunzaji mzuri wa mazingira na miundombinu kupitia fedha za ndani na kufanya ukarabati wa baadhi ya majengo ambayo yataongeza nguvu ya uboreshaji wa huduma na kuondoa msongamano kwa wagonjwa.

"Hospitali inatoa shukrani za dhati kwa serikali ya awamu ya sita ya Dk. Samia kwa uboreshaji mkubwa wa huduma za afya katika kipindi cha miaka mitatu ya uongozi wake na kuomba kuendeleza maboresho hayo yazidi kuinufaisha jamii," alisema.

Pia, uongozi wa hospitali hiyo ulitoa rai kwa wananchi wa mkoa wa Mtwara na Kanda ya Kusini kufika katika hospitali hiyo kupata huduma bora na za kisasa.

"Uongozi unatoa rai kwa wananchi wa Mtwara na Kanda ya Kusini kwa ujumla kufika katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa-Ligula kwa ajili ya huduma mbalimbali za kibingwa ambazo zimetokana na uboreshaji mkubwa wa huduma za afya katika kipindi cha miaka mitatu ya Rais Samia Suluhu Hassan kwa lengo kuu la kuinufaisha jamii kwa ujumla," alisema.

# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
# WIZARA YA AFYA
# HOSPITALI YA RUFAA MKOA WA
# DODOMA






MGANGA Mfawidhi wa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa Dodoma Dkt. Ibenzi Ernest.





RAIS Dk. Samia Suluhu Hassan





# Rais Dk.Samia alivyoifanyia mageuzi Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Dodoma

**DODOMA REGIONAL HOSPITAL**
**Anuani ya Posta: P.O.BOX 904 DODOMA**
**Simu: 0262323045**
**Simu ya Mkononi: +255738100120**
**Barua Pepe: dodomarrh@afya.go.tz**

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA AFYA
HOSPITALI YA RUFAA YA MKOA WA DODOMA

# Rais Dk. Samia alivyochochea huduma za kibingwa Hospitali ya Rufaa Dodoma



MGANGA Mfawidhi wa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa Dodoma Dkt. Ibenzi Ernest.



**Na FRED ALFRED**

HOSPITALI ya Rufaa ya Mkoa wa Dodoma ni mojawapo ya hospitali 28 za rufaa za mikoa, lakini ni hospitali ambayo ni kubwa katika hospitali za rufaa za Mikoa.

Ni hospitali inayotoa huduma za kibingwa katika fani mbalimbali, mojawapo ni fani ya mifupa ambayo inasifika hadi katika ngazi za Kimataifa.

Akizungumza na gazeti hili ofisini kwake Mganga Mfawidhi wa Hospitali Dk. Ibenzi Ernest alisema wanafaya mambo makubwa na inashika hadi nafasi ya kwanza kidunia katika huduma za mifupa.

"Ni hospitali inayotoa huduma za kibingwa katika fani mbalimbali, mojawapo ni fani ya mifupa ambayo inasifika sana, mpaka kwenye ngazi za kimataifa, pia inashika nafasi ya kwanza kidunia katika huduma za mifupa.

Aliongeza: "Tunatoa huduma za kibingwa za upasuaji, magonjwa ya kina mama na watoto, magonjwa ya ndani kama vile kisukari na presha lakini pia huduma za masikio, pua, koo."alisema.

Alisema kwa sasa wananchi wana uhakika wa kupata huduma za kibingwa wakati wote.

Dk.Ibenzi alisema katika hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Dodoma madaktari bingwa wanapatikana muda wote wanapo hitajika.

"Hapa tunatoa huduma za kibingwa tu, kwahiyo mtu yeyote akifika katika hosptali yetu anauhakika wa kupata huduma za kibingwa, na bahati nzuri tunafanya kazi masaa 24 kwa kila kitengo na kubwa zaidi madaktari wanapatikana muda wote wanapohitajika,"alisema

**NI MAGEUZI YA KIHISTORIA**

Dk.Ibenzi alisema katika kipindi cha serikali ya Awamu ya Sita chini ya Uongozi wa Rais Dk.Samia Suluhu Hassan wamepata mafanikio makubwa sana ikiwemo kutoa fedha kwa ajili ya kuboresha miundombinu ya hosptali hiyo.

Alisema serikali ya Awamu ya Sita imetoa fedha kwa ajili ya kuboresha ujenzi wa jengo la ICU pamoja na ununuzi wa vifaa.

"Katika Hospitali yetu ni mojawapo ya hospitali ambazo zimefaidika sana katika kipindi hiki cha Rais Dk. Samia, miundombinu ya kutolea huduma imeimarika sana tofauti ilivyokuwa mwanzo,:"alisema

Aliongeza kuwa: "Tulikuwa hatuna jengo la ICU, mwanzo tulikuwa na jengo lenye vitanda vitatu, lakini kwasasa tunavyoongea tuna jengo lenye vitanda 38 vya kuhudumia wagonjwa mahututi.

Alifafanua kuwa kabla ya maboresho hayo hakukuwa na Jengo la huduma za dharura kama Emergency Department lakini kwasasa tuna jengo letu ambalo limesimama.

Dk Ibenzi alisema kabla ya kupatikana kwa fedha kwa ajili ya kuboresha miundombinu ya hospitali kulikuwa na changamoto kubwa ya madaktari bingwa ambapo vipimo kama CT Scan ilikuwa inawalazimu wananchi kuwapeleka wagonjwa katika hospitali nyingine kwa ajili ya kupata kipimo hicho.

"Sasa hivi tuna hicho kipimo ambapo wananchi hawana haja ya kwenda sehemu nyingine wakija hapa kwetu wanamaliza kila kitu na haya ni mambo makubwa ambayo yametekelezwa chini ya uongozi wa serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Rais Dk.Samia Suluhu Hassan,"alisema.

Aliongeza kuwa: "Haya ni maendeleo makubwa sana ambayo wengi wetu hatukutegemea lakini imewezekana katika kipindi hichi cha miaka mitatu ya Rais Samia, tunamshukuru sana kwa kazi kubwa ambayo ameifanya,".

***"Ni hospitali inayotoa huduma za kibingwa katika fani mbalimbali, mojawapo ni fani ya mifupa ambayo inasifika sana, mpaka kwenye level za kimataifa, ni hospitsli ambayo inafanya mambo makubwa, ni hospitali inayoshika mpaka nafasi ya kwanza kidunia katika huduma za mifupa.***

**UPATIKANAJI WA DAWA**

Akizungumza hali ya upatikanaji wa dawa katika hospitali hiyo katika kipindi cha miaka mitatu ya uongozi wa Rais Dk. Samia Dk. Ibenzi alisema hali ya upatikanaji wa dawa imeimarika hadi kufikia asilimia 98.

Alisema upatikanaji wa dawa katika hospitali hiyo umesaidia kuongeza idadi ya wananchi wanaoenda kutibiwa.

"Lakini sio hilo tu awali vitendeakazi vilikuwa changamoto lakini kwasasa vipimo vya maabara vinapatikana kwa asilimia 99 huku hali ya upatikanaji wa dawa ikiendelea kuimarika hadi kufikia asilimia 98.

Aliongeza kuwa:" Kwa sasa tuna uhakika kila tukimuandikia mgonjwa dawa anauhakika wa kuzipata hapa hapa, haya ni mafanikio makubwa tofauti na mwanzo hali ya upatikanaji dawa katika hospitali yetu ilikuwa ni kati ya asilimia 60 na 70 hivyo haya ni mageuzi makubwa sana ambayo kuna haja ya kuendelea kumshukuru Rais Dk.Samia kwa kazi nzuri anayoifanya katika sekta ya afya,".

Akizungumzia suala la watumishi Dk. Ibenzi alifafanua katika hospitali hiyo kuna watumishi wa kutosha wa kada mbalimbali.

**AMTAJA RAIS DK.SAMIA**

Dk. Ibenzi alisema kuendelea kuimarika kwa sekta ya afya nchini kuna haja ya kuendelea kumshukuru Rais Dk. Samia kwa kujipambanua kwake na kuendelea kutoa fedha nyingi kwa ajili ya kutekeleza miradi mbalimbali ya afya na kuisimamia ili kuhakikisha inakamilika kwa wakati na kuwahudumia wananchi.

Alisema hatua hiyo imesaidia kuongeza uhakika kwa wananchi kupata huduma za uhakika na kuwapunguzia mzigo wa gharama za matibabu ambazo wangezibeba kusafirisha wagonjwa wao kutibiwa katika



MIAKA MITATU YA RAIS DK. SAMIA NA UBORESHAJI SEKTA YA AFYA NCHINI

# Rais Dk. Samia alivyochochea huduma za kibingwa Hospitali ya Rufaa Dodoma



maeneo mbalimbali nchini.

"Mwanzo tulikuwa na changamoto ya huduma bora katika hospitali zetu lakini sasa hivi tunapoongea huduma zimeimarishwa sana, utendaji kazi wa watumishi ni mzuri na wananchi wanapata huduma za uhakika,"alisema.

Aliongeza kuwa: "Ni sekta ya afya ambayo ilikuwa imetetereka lakini kwasasa ni kimbilio. Najua watanzania wengi tulikuwa tunatabia ya kupenda sana kwenda kwenye hospitali binafsi lakini leo hii hospitali zetu za rufaa na za mikoa serikali imeimarisha sana huduma, kwani vitu vyote vilivyokuwa vinapatikana katika hospitali binafsi kwenye hospitali za serikali vinapatikana pia.

Katika hatua nyingine Dk. Ibenzi alisisitiza kuwa: "Tunapongeza mageuzi ni makubwa Rais Dk. Samia amefanya mengi, sisi kwetu ametupa deni na tutalilipa kwa kuwapa huduma bora wananchi waridhike, huduma zetu zitakuwa bora kulingana na kiwango cha uwekezaji uliuofanywa na serikali.

**MIKAKATI YA HOSPITALI**

Dk. Ibenzi alifafanua kuwa katika kuhakikisha wanaendelea kuunga mkono jitihada za Rais Dk. Samia wamejipanga kuyaendeleza na kuyatafsiri mageuzi yaliyo fanyika katika kipindi cha miaka mitatu kwa vitendo.

Alisema katika kipindi cha mwaka ujao wa fedha wanatarajia kujenga ghorofa kubwa sana kwaajili ya kutoa huduma kwa watoto wachanga.

Alisema huduma ya watoto wa changa imekuwa ni changamoto kubwa ambapo kuna wakati wagonjwa wanalala wawili katika kitanda kimoja.

"Kutokana na changamoto hiyo serikali ya awamu ya sita chini ya uongozi wa Rais Dk.Samia uliona hilo na kuwa mstari wa mbele kusimamia sekta ya afya, inatujengea Jengo hilo litakalokuwa na ghorofa tano ambazo zitajengwa katika hospitali yetu ya Rufaa ya Dodoma,"alisema

***"Tunashukuru upatikanaji wa huduma za afya umeimarika, yaani ukienda katika hospitali ya rufaa ya Dodoma unapata huduma zote za matibabu. Huu ni uwekezaji mkubwa na tunaendelea kumuombea mama eti Rais Dk. Samia ili aendelee kufanya kazi nzuri.***

Dk.Ibenzi alitaJa mkakati mwingine kuwa ni kuendelea kuimarisha utoaji wa huduma na kuweka mazingira chanya ya utendaji kazi kwa watumishi.

"Sisi kama watendaji ujumbe ambao ni mkubwa kabisa ni kwamba sisi kama watendaji tumepewa jukumu kubwa na tunaahidi kulitekeleza. Lakini tumwambie Rais Dk. Samia kuwa aendelee kuiamini sekta ya afya lakini pia hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Dodoma kwasababu huduma bora ndo kipaumbele chetu, na sisi ni ndugu namba moja wa wagonjwa,"alisema.

**WANANCHI WAELEZA**

Wakizungumza kwa nyakati tofauti wananchi wa Mkoa wa Dodoma wamempongeza Rais Dk.Samia kwa kuendelea kuiboresha sekta ya afya ili kuhakikisha wananchi wanapata huduma bora.

Mfanyabiashara wa Soko la majengo Asha Ramadhani amesema katika kipindi hiki cha serikali ya awamu ya sita hali ya upatikanaji wa huduma za afya imeimarika hasa katika vituo vya kutolea huduma hiyo katika ngazi zote.

Alisema kwa sasa ukienda hospitali unapata huduma zote za msingi ikiwemo na upatikanaji wa dawa za uhakika tofauti na kipindi cha nyuma ambapo dawa zilikuwa zinapatikana katika maduka binafsi.

"Tunashukuru upatikanaji wa huduma za afya zimeimarika, yaani ukienda katika hospitali ya Rufaa ya Dodoma unapata huduma zote za matibabu. Huu ni uwekezaji mkubwa na tunaendelea kumuombea mama etu Rais Dk. Samia ili aendelee kufanya kazi nzuri.

Aliongeza: "Kuimarika kwa huduma kumesaidia kupunguza vifo hasa vya mama na mtoto ambavyo vilikuwa vinatokea kwasababu ya kukosekana kwa huduma katika maeneo mbalimbali nchini,".

Kwa upande wake Mkazi wa Kata ya Kikuyu Hosea Chihanga aliupongeza uongozi wa hospitali ya Mkoa wa Dodoma kwa kuendelea kusimamia upatikanaji wa huduma bora na kuhakikisha watumishi wanatoa huduma zinazotakiwa kwa wananchi.

Alisema kwasasa hospitali ya mkoa wa Dodoma imekuwa ni kimbilio la wananchi wa Dodoma na mikoa ya karibu kwasababu utoaji wa huduma umeimarika sana ikiwemo upatikanaji wa wataalamu wa afya waliobobea.

"Mimi nina ushaidi ndugu yangu alipelekwa pale namna alipata huduma pasipo vikwazo na kwa wakati na sasa amepona na anaendelea na shughuli zake. Kiukweli tunaendelea kuishukuru serikali kwa kuona umuhimu wa kuwekeza katika sekta ya afya kwasababu mtu ni afya," alieleza.







JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
## TAASISI YA MOYO YA JAKAYA KIKWETE (JKCI)

# Mafanikio ya JKCI miaka mitatu ya Rais Dk. Samia Suluhu Hassan

>>Yamshukuru Rais Dkt. Samia kutoa fedha za mashine za kisasa na kuimarisha utalii tiba



**Wataalamu wa upasuaji wa moyo kwa watoto wa Taasisi ya Moyo Jakaya Kikwete (JKCI) na wenzao wa hospitali ya Taifa ya Moyo ya nchini Zambia wakimfanyia mtoto upasuaji wa kuziba tundu la moyo katika kambi maalumu ya upasuaji inayofanyika nchini Zambia mwezi wa kwanza mwaka huu. Watoto saba wenye matatizo ya moyo ya kuzaliwa nayo walifanyiwa upasuaji katika kambi hiyo ya siku tatu.**



**Wataalamu wa magonjwa ya moyo na mishipa ya damu wa Taasisi ya Moyo Jakaya Kikwete (JKCI) na wenzao wa Hospitali ya Starcare ya nchini India wakifanya upasuaji mdogo wa moyo wa kubadilisha valvu ya mshipa mkubwa wa damu (Aortic Valve) bila kufungua kifua (Transcatheter Aortic Valve Implantation procedure – TAVI) katika kambi maalumu ya siku mbili ya matibabu ya moyo inayofanyika JKCI. Upasuaji huo mdogo wa kubadilisha valvu ulifanyika kwa mara ya kwanza hapa nchini.**

**Na SUPERIUS ERNEST**

TAASISI ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI) kwa kipindi cha miaka mitatu ya uongozi wa Serikali ya awamu ya sita wa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan imepata mafanikio makubwa katika utoaji wa matibabu ya Moyo.

Akieleza mafanikio hayo Mkurugenzi Mtendaji wa JKCI, Dkt. Peter Kisenge alisema katika miaka mitatu ya Rais Dk.Samia, wameona jumla ya wagonjwa 361,894 ambapo watu wazima ni 331,557 na watoto 30,337 na wagonjwa waliolazwa walikuwa 13,325 watu wazima wakiwa 10,781 na watoto 2,544.

"Wagonjwa waliotibiwa kutoka nje ya nchi walikuwa 316, wakitoka mataifa ya Somalia, Malawi, Kenya, Rwanda, Visiwa vya Comoro, Msumbiji, Nigeria, Siera Leone, Zimbabwe, Zambia, Uganda, Congo, Ethiopia na Burundi.

" Sio hao tu bali kwa ubora wa huduma zetu, pia, tulipata wagonjwa wengine kutoka nje ya Afrika zikiwemo nchi za Armenia, China, Ujerumani, India, Norway, Ufaransa na Uingereza," alisema.

Alieleza kuwa, wagonjwa waliofanyiwa upasuaji mkubwa wa moyo wa kufungua kifua na kubadilishwa Valvu za moyo moja hadi tatu, upasuaji wa kupandikiza mishipa ya damu ya moyo (Coronary Artery Bypass Graft Surgery —CABG), upasuaji wa mishipa ya damu na mapafu walikuwa 2,161 kati ya hao watu wazima walikuwa 1,257 na watoto 904.

Mkurugenzi Mtendaji Kisenge, alisema upasuaji mpya wa moyo wa kufungua kifua uliofanyika ni wa kurekebisha mshipa mkubwa wa damu uliotanuka kifuani na tumboni, kurekebisha mshiba uliotanuka katika begani.



**Naibu Waziri wa Afya na Mbunge wa jimbo la Siha Mhe. Dkt. Godwin Mollel akizungumza na wananchi waliofika katika Hospitali ya Wilaya ya Siha Kwa ajili ya kupata huduma za upimaji na matibabu ya moyo zilizotolewa na wataalamu wa Taasisi ya Moyo Jakaya Kikwete (JKCI) kwa kushirikiana na wenzao wa Hospitali hiyo.**

Pia, kupandikiza mishipa ya damu wakati moyo unafanya kazi bila ya kuusimamisha moyo, kukarabati mlango wa moyo wa mshipa mkubwa wa damu iendayo kwenye mapafu kwa kutumia chumba cha moyo cha juu kulia, kutoa dawa ya kuzuia maumivu sehemu ya uti wa mgongo wakati wa upasuaji mkubwa wa moyo.



**Mkurugenzi Mtendaji - JKCI Dkt. Peter Kisenge**

Alisema kupitia mtambo wa Cathlab (Catheterization Laboratory) ambao ni maabara ya uchunguzi wa matatizo na tiba ya magonjwa ya moyo inayotumia mionzi maalum, wagonjwa 6,260 walipata huduma ya matibabu kati yao watu wazima 5,693 na watoto 567.

Dk.Kisenge alieleza kuwa wagonjwa hao walipata huduma za uchunguzi, matibabu ya mishipa ya damu ya moyo iliyokuwa imeziba na kuwekewa vifaa visaidizi vya moyo, Aidha, wagonjwa 401 walitibiwa tatizo la mfumo wa umeme wa moyo kwa kutumia mtambo wa kawaida na 81 walitibiwa kwa kutumia mtambo wa Carto 3.

Alisema matibabu mapya yaliyofanyika katika mtambo wa Cathlab ni na upasuaji mdogo wa moyo wa kubadilisha valvu ya mshipa mkubwa wa damu (Aortic Valve) bila kufungua kifua (Transcatheter Aortic Valve Implantation procedure — TAVI) kutanua valvu za moyo kwa muda.

"Pia, uchunguzi na kufanya upasuaji wa kuzibua mishipa ya damu ya miguu (Peripheral Interventions) ambayo haipitishi damu vizuri na kuzibua mishipa ya damu ya shingoni.

"Taasisi yetu imesaini mikataba ya miaka mitatu ya makubaliano na Hospitali za Taifa za nchini Rwanda na Zambia ya kutibu wagonjwa wa moyo na kuwajengea uwezo wataalamu wa afya wa hospitali hizo wa jinsi ya kuwatibu wagonjwa wa moyo," alisema.

Mkurugenzi Mtendaji Dk.Kisenge alisema wamesaini mikataba na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na Chuo cha Madaktari wa upasuaji Afrika Mashariki, Kati na Kusini mwa Afrika (COSECSA) katika kutoa mafunzo bobezi ya matibabu ya moyo kwa wataalamu wa afya.

Vilevile, wanashirikiana na Chuo Kikuu cha Jagiellonian cha nchini Poland na Chuo Kikuu cha New York kilichopo nchini Marekani kufanya utafiti, elimu na utoaji wa huduma kwa wagonjwa wa moyo na wamesaini mkataba na Taasisi ya Afya Ifakara (IHI) kufanya utafiti wa magonjwa ya moyo.

Alieleza kuwa, kupitia kozi ya miezi sita ya mafunzo ya kuwahudumia wagonjwa mahututi na wa dharura inayotolewa kwa wauguzi kati ya wanafunzi 63 waliomaliza wanafunzi sita walitoka katika Hospitali za King Faisal iliyopo nchini Rwanda na Hospitali ya Taifa ya Moyo ya nchini Zambia.

Alifafanua kuwa, wameendelea kutoa huduma za tiba mkoba zijulikanazo kwa jina la Dkt. Samia Suluhu Hassan Outreach Services zimetolewa katika mikoa 12 ambapo watu 10,807 walifanyiwa uchunguzi wa magonjwa ya moyo.

"Kati ya hao 4375 waliokutwa na matatizo mbalimbali ya moyo na kuanzishiwa matibabu. Wagonjwa 1323 walikutwa na matatizo yaliyohitaji matibabu ya kibingwa walipewa rufaa ya kuja JKCI Makao Makuu Muhimbili Upanga kufanyiwa uchunguzi na matibabu zaidi, " alisema.

Aliongeza kuwa, wataalamu wa JKCI walivuka mipaka ya nchi na kwenda kutoa huduma za matibabu ya moyo katika nchi za Zambia na Malawi kwa wagonjwa 731.

Mkurugenzi Mtendaji Dk.Kisenge alisema sh. bilioni 2.16 zilitolewa na serikali kufanya ukarabati wa vyumba vya watoto mahututi na chumba cha wagonjwa mahututi cha watu wazima, ukarabati na utanuzi wa ICU ya watoto ambayo hapo awali ilikuwa na vitanda nane na hivi sasa inavitanda 16 na ICU ya wakubwa ambayo imetanuliwa na kuwa na vitanda kumi kutoka nane ambapo shilingi 503,450,051 zilitumika katika ukarabati huo.

" Sh. 1,465,683,469 zilitumika kununua vifaa tiba, sh.170,000,000 zilitumika kutoa tiba mtandao (Telemedicine) na sh. 28,340,000 zilitumika kugharamia mafunzo ya wataalamu wa fani ya radiolojia na huduma za wagonjwa mahututi," alisema.

Alisema serikali kupitia sekretarieti ya ajira katika utumishi wa umma iliajiri wafanyakazi wapya 131 wa kada mbalimbali, wafanyakazi 208 walipandishwa vyeo katika madaraja mbalimbali.

Alisema ujenzi unaoendelea wa jengo la ghorofa nne la utawala na vipimo ambalo hadi kukamilika kwake litagharimu kiasi cha sh. bilioni 3.6.

Alisema serikali iliwapatia Hospitali ya Dar Group iliyopo wilayani Temeke jijini Dar es Salaam, kuwa sehemu ya JKCI kwa kuwapatia hospitali hiyo kutatua changamoto ya nafasi ambayo walikuwa wanakabiliana nayo kwa muda mrefu na kuwasaidia kuboresha huduma za matibabu tunazozitoa kwa wananchi.

Alisema wagonjwa waliotibiwa walikuwa 119,881 kati ya hao watu wazima 99,540 na watoto 20,341, wagonjwa waliolazwa walikuwa 8,950 watu wazima wakiwa 7,890 na watoto 1,060.

"Huduma zinazotolewa Hospitali ya JKCI Dar Group ni matibabu ya moyo, kinywa na meno, huduma za dharula, kliniki ya wanawake na wajawazito, kliniki ya watoto, macho, pua, masikio na koo, kliniki ya ngozi, vibofu vya mkojo, upasuaji mkubwa na mdogo, magonjwa ya tumbo na ini, figo na matibabu mengine ya magonjwa yanayoambukiza kama malaria," alisema.



**Watoa huduma kwa wagonjwa wa dharula na mahututi wa Taasisi ya Moyo Jakaya Kikwete (JKCI) Hospitali ya Dar Group iliyopo TAZARA wilayani Temeke wakimuhudumia mgonjwa.**

# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
## WIZARA YA AFYA
## HOSPITALI YA RUFAA YA
# MOUNT MERU



RAIS Dk. Samia Suluhu Hassan



MGANGA Mfawidhi Dkt. Alex Ernest.









# Hospitali ya Rufaa ya Mount Meru iliyopiga hatua utoaji wa huduma za afya

**Anuani ya Posta: Box 3092, Arusha**
**Simu: 250-335751-2**
**Simu ya Mkononi:**
**Barua Pepe: mt.merurrh@afya.go.tz**

MIAKA MITATU YA RAIS DK. SAMIA NA UBORESHAJI SEKTA YA AFYA NCHINI

# Hospitali ya Rufaa ya Mount Meru iliyopiga hatua utoaji wa huduma za afya



Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan.



Mganga Mfawidhi Dkt. Alex Ernest.

**Na MWANDISHI WETU**

UTOAJI huduma za afya nchini umeboreshwa zaidi na kuyafanya mazingira kuwa rafiki kwa wagonjwa mbalimbali katika kipindi cha miaka mitatu ya Rais Dk. Samia Suluhu Hassan.

Kwa kipindi cha miaka mitatu, Rais Dk. Samia amefanya mabadiliko makubwa katika sekta ya afya ikiwemo kutoa fedha zilizosaidia kutengeneza miundombinu bora.

Vilevile kuna baadhi ya wagonjwa walikuwa wakilazimika kusafiri umbali mrefu kwenda kufuata matibabu lakini hivi sasa hali imekuwa tofauti kwani huduma nyingi zinapatikana karibu.

Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Arusha Mount Meru, Dk. Alex Ernest alisema wamepiga hatua katika uboreshaji wa utoaji wa huduma za afya na hiyo imechangiwa na maendeleo yanayoletwa na Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Rais wa Jamhuri wa Muungano wa Tanzania Mhe. Dk. Samia Suluhu Hassan katika kuboresha miundombinu, ununuzi wa vifaa tiba na dawa ndani ya kipindi cha miaka mitatu tangu alipoingia madarakani.

"Tumepiga hatua katika uboreshaji wa utoaji wa huduma za afya na hii imechangiwa na maendeleo yanayoletwa na Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Rais Dk. Samia katika kuboresha miundombinu, ununuzi wa vifaa tiba na dawa ndani ya kipindi cha miaka mitatu tangu alipoingia madarakani," alisema Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Arusha Mount Meru, Dk. Ernest.

**FEDHA ILIYOPOKEA HOSPITALI YA RUFAA YA MOUNT MERU**

Alisema Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Arusha Mount Meru imepokea Jumla ya fedha kiasi cha sh. 4,761,586,686, kwa kipindi cha miaka mitatu ya awamu ya sita na fedha hizo zimetumika kutekeleza miradi mbalimbali ndani ya hospitali.

**MIRADI YA MAENDELEO**

Miradi ya maendeleo ilifanyika katika kipindi cha miaka mitatu ni pamoja na ujenzi wa jengo la wagonjwa wa dharura (EMD) iliotumia jumla ya kiasi cha sh. 400,000,000.

Ukarabati wa jengo la wagonjwa mahututi (ICU) ya watu wazima na watoto jumla ya kiasi cha sh. 130,000,000.

Ukarabati wa chumba cha huduma ya tiba mtandao (Telemedicine) jumla ya kiasi ya sh. milioni 120.

Ukarabati wa jengo la kliniki ya waraibu wa dawa za kulevya (Methadone) jumla ya kiasi cha sh. milioni 321.

***"Katika kipindi cha miaka mitatu tumefanya maboresho mbalimbali ikiwemo kununua mashine za kisasa kuhakikisha tunaendelea kutoa huduma zenye hadhi ya juu kwa jamii inayotuzunguka ikiwemo maeneo ya jirani," alisema Dk. Ernest.***

**UNUNUZI WA VIFAA TIBA**

Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Arusha Mount Meru, Dk. Ernest alisema vilevile wametumia jumla ya sh. milioni 768 kufanya ununuzi wa vifaa tiba, ikiwemo vifaa tiba vya wodi ya wagonjwa mahututi (ICU) vilivyotumia jumla ya kiasi cha sh. milioni 400 vikiwemo vitanda vinane vya kielektroniki.

Dk. Ernest alisema pia ununuzi wa mashine za Radiolojia ikiwemo mashine ya kisasa ya mionzi (Digital Xray) jumla ya sh. milioni 337,449,880.

Aliongeza kuwa ununuzi wa CT Scan jumla ya kiasi sh. 2,180,000,000, ununuzi wa mashine ya xray ya kinywa na meno CBCT jumla ya kiasi cha sh. 276,000,000 na ununuzi wa mashine za kisasa za maabara 10 zilizotumia jumla ya kiasi cha sh. 250,000,000.

"Katika kipindi cha miaka mitatu tumefanya maboresho mbalimbali ikiwemo kununua mashine za kisasa kuhakikisha tunaendelea kutoa huduma zenye hadhi ya juu kwa jamii inayotuzunguka ikiwemo maeneo ya jirani," alisema Dk. Ernest.

Alisisitiza kuwa upatikanaji wa kliniki tembezi ya kisasa yenye uwezo wa kutoa huduma za afya kwa wananchi mahali popote hasa sehemu zilizo mbali na huduma za afya, pia gari la kubebea wagonjwa lenye vifaa muhimu vya kuendelea kumuhudumia mgonjwa anapokuwa anasafirishwa.

**WATUMISHI KUJIENDELEZA**

Alisema jumla ya watumishi 29 wamefanikiwa kwenda kujiendeleza na masomo ambapo madaktari 13 wanasomea udaktari bingwa na mmoja anasomea udaktari bingwa bobezi huku 15 wakiwa ni watumishi wengine wa kada mbalimbali kwa ufadhili wa Mama Samia Scholarship kwa watumishi wa afya.

**MIKAKATI YAO**

Dk. Ernest alisema kwamba mikakati ya hospitali kuendelea kufanya vizuri kipindi hiki cha Serikali ya Awamu ya Sita ni kuendelea kupanua wigo wa utoaji huduma za afya ndani ya hospitali kwa kuongeza huduma kama vile;

I.Ufunguzi wa maabara za Pathiolojia ikiwa ya kwanza katika hospitali zote za Rufaa za Mikoa Nchini.

II.Ufunguzi wa huduma ya uchunguzi kwa njia mmeng'enyo wa chakula (Endoscopy).

III. pasuaji kwa njia ya



Mashine ya Endoscopy



Kliniki ya Methadone kwa waraibu wa dawa za kulevya.

MIAKA MITATU YA RAIS DK. SAMIA NA UBORESHAJI SEKTA YA AFYA NCHINI



Mashine ya mionzi ya kinywa na meno CBCT.



Vifaa tiba vya upasuaji

# Hospitali ya Rufaa ya Mount Meru iliyopiga hatua utoaji wa huduma za afya

matundu.

IV.Upandikizaji wa nyonga.

V.Upandikizaji wa viungo bandia.

VI.Huduma ya mionzi ya kinywa na meno kwa kutumia mashine ya kisasa ya CBCT, Mount Meru ikiwa hospitali ya kwanza ya Rufaa kuwa na huduma hiyo.

"Mikakati yetu tuliyojiwekea ni kuhakikisha tunaendelea kutoa huduma bora kwa jamii katika kipindi chote cha uongozi uliopo madarakani chini ya Rais Dk. Samia," alisema Dk. Ernest.

**KUAJIRI WATUMISHI WAPYA**

Alisema kuwa hospitali inaendelea kuajiri watumishi wa wapya wa mikataba maeneo yenye upungufu ili kuendeana na kasi ya utoaji huduma bora ndani ya hospitali vilevile inawaongezea mafunzo wataaluma wa afya waweze kupata ujuzi wa kutumia mashine za kisasa zinazoletwa na hospitali.

Alisema pia hospitali inaendelelea kununua vifaa tiba na kukarabati majengo yawe rafiki na huduma zinazoboreshwa ndani ya hospitali.

**SHUKRANI KWA RAIS DK. SAMIA**

Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Arusha Mount Meru inatoa shukrani kwa Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Rais Dk. Samia kwa kufanikisha maboresho katika sekta ya afya kupitia Wizara ya Afya chini ya Waziri mwenye dhamana, Ummy Mwalimu kwa kufanikisha fedha za miradi, vifaa tiba na dawa kufika kwa wakati, hali inayowezesha hospitali kuendelea kutoa huduma bora za afya kwa wananchi.

"Tunatoa shukrani zetu kwa Rais Dk. Samia kutokana na kufanikisha maboresho katika sekta ya afya kupitia Wizara ya Afya chini ya Waziri mwenye dhamana, Ummy Mwalimu kwa kufanikisha fedha za miradi, vifaa tiba na dawa kufika kwa wakati, hali inayowezesha hospitali kuendelea kutoa huduma bora za afya kwa wananchi," alisema.

**WITO**

Alisema wanatoa wito kwa wananchi wanaowahudumiwa na Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Arusha na kuwahakikisha vipimo vya maabara muhimu kwa asilimia 98.9 ambavyo vinamwezesha mwananchi kufanyiwa vipimo vyote muhimu bila yakupewa rufaa

Alisema pia kuna mashine muhimu za Radiolojia ambapo vipimo mbalimbali vinapatikana vikiwemo CT Scan, Digital Xray pamoja na CBCT kwa ajili ya uchunguzi wa kinywa na meno hali ambayo imeondoa rufaa ya vipimo hivyo kwenda katika hospitali za Kanda na Taifa

Alisema pia kuna upatikanaji wa madaktari bingwa wa fani mbalimbali unayorahisisha matibabu ya uhakika na haraka na uwepo wa kliniki za madaktari bingwa ndani ya hospitali kila siku katika magonjwa mbalimbali hali inayopelekea urahisi wa mwananchi kutibiwa ndani ya hospitali ya Rufaa ya Mkoa kwa ufanisi zaidi.

Alisisitiza wana wodi zenye vifaa tiba vya kisasa kuanzia wodi ya watu wazima na za watoto hali inayopelekea kupunguza vifo vya mama na mtoto kutoka vifo 102 mwaka wa fedha 2019/2020 hadi vifo chini ya 50 kwa mwaka wa fedha 2023/2024 hali inayopelekea kupungua kwa Rufaa kutoka wagonjwa wanane hadi 10 kwa siku kwa mwaka wa Fedha 2019/2020 hadi wagonjwa 0 hadi watatu kwa siku kwa mwaka wa fedha 2023/2024.



***"Mikakati yetu tuliyojiwekea ni kuhakikisha tunaendelea kutoa huduma bora kwa jamii katika kipindi chote cha uongozi uliopo madarakani chini ya Rais Dk. Samia,"***

***alisema Dk. Ernest.***



Mashine ya CT Scan

**HISTORIA**

Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Arusha ilianzishwa ikiwa kama kambi ya kutibu majeruhi katika Vita Kuu ya Kwanza ya Dunia mwaka 1915 na ilizinduliwa rasmi kama hospitali ya mkoa tarehe 26.11.1926.

Hatimaye ilipandishwa hadhi na kuwa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa mnamo tarehe 12.11.2010.

Hospitali ina Idara Kuu saba ambazo ni Idara ya Utawala, Dharura na ajali, Uzazi, Watoto, Upasuaji, Upasuaji (Mifupa) na Idara ya Tiba. Vilevile hospitali ina vitengo 16 ambavyo ni Famasi, Maabara, Mionzi, Meno, Macho, 'Anaesthesia' Masikio, Pua na Koo (ENT), Magonjwa ya njia ya mkojo, Afya ya Akili, Mazoezi ya Viungo, Uhasibu, Manunuzi, BIMA ya afya, kitengo cha ubora wa huduma (QI) na HDU na Kitengo cha Ustawi wa Jamii.

Hospitali ina uwezo kubeba vitanda 500 na inahudumia wagonjwa wa nje kati ya 1500 hadi 1800 kwa siku, wagonjwa wanaolazwa ni 250 hadi 300 kwa siku.

Hospitali ina Jumla ya watumishi 567 wakiwemo Madaktari bingwa 26, Madaktari 31, Wauguzi 274, Watumishi wa kada saidizi 91 na Watumishi 145 wa ajira za mkataba.



Chumba cha uangalizi maalumu (NICU) ya watoto wachanga.




Jengo jipya la Wagonjwa wa dharura.

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA AFYA
HOSPITALI YA RUFAA YA KANDA BUGANDO

# Miaka mitatu ya mafanikio makubwa Hospitali ya Rufaa ya Kanda Bugando



Mkurugenzi Mkuu wa Hospitali ya Rufaa ya Kanda ya Bugando Dkt Fabian A. Massaga



Rais Dk. Samia Suluhu Hassan amezindua mashine ya kupima magonjwa mbalimbali (MRI) katika Hospitali ya Rufaa ya Kanda ya Bugando (BMC).

**UTANGULIZI**

HOSPITALI ya Rufaa ya Kanda Bugando mkoani Mwanza, ilifunguliwa rasmi Novemba 3, 1971 na Rais wa Kwanza wa Tanzania, Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere.

Hospitali hiyo inahudumia mikoa minane ya Kanda ya Ziwa na Magharibi, inayokadiliwa kuwa na wakazi milioni 22 ikimilikiwa na Kanisa Katoliki na inaendeshwa kwa ubia na Serikali ya Jamhuri wa Muungano wa Tanzania.

Hospitali ya Rufaa ya Kanda Bugando, inashika nafasi ya pili kwa ukubwa nchini ikiwa na vitanda zaidi ya 1,000. Inahudumia wastani wa wagonjwa 1200-1400 kwa siku.

**HUDUMA ZITOLEWAZO**

Hospitali ya Rufaa ya kanda Bugando, imejikita katika utoaji wa huduma za kibingwa na kibingwa bobezi katika Nyanja za Tiba, upasuaji na huduma za afya Saidizi.

Kwa upande wa huduma za tiba, hospitali imeendelea kutoa huduma na kwa miaka mitatu Hospitali imehudumia jumla ya wagonjwa nje na ndani 654862. Katika huduma za Upasuaji Hospitali imeendelea kutoa huduma za Upasuaji na kwa kipindi cha miaka mitatu Hospitali imefanya jumla ya pasuaji 47,108 za wagonjwa. Upasuaji maalumu wa Watoto, zaidi ya wagonjwa 1493 wamefanyiwa upasuaji wa magonjwa mbalimbali.Katika huduma za vipimo hospitali imeendelea kutoa huduma ya vipimo vya mionzi na maabara kama ifuatavyo;-

Ultra sound
CT- SCAN
X-RAY
Mammography
Dental X-RAY
Intervational Radiology
Maabara ya uchunguzi wa vina saba
Maabara ya uchunguzi wa vivimbe



COBAS 6800

**UPATIKANAJI WA DAWA**

Hali ya upatikanaji wa dawa muhimu na maalumu katika hospitali umeendelea kuimarika na imefikia asilimia 96. Dawa hizo zinatoka MSD na zingine hununuliwa kwa mapato ya ndani kutoka kwa wazabuni mbalimbali.

Pia, hospitali ina kitengo cha uzalishaji wa maji tiba ambacho kina saidia kupunguza gharama za hospitali, katika kuagiza baadhi ya dawa ambazo ni ngumu kupatikana katika masoko, hususan hapa nchini.

**UBORESHAJI WA HUDUMA ZA DHARURA.**

Tunaishukuru Serikali ya Awamu ya Sita kuendelea kuboresha huduma za dharura katika Hospitali ya Bugando, kwa kununua gari la kisasa la wagonjwa lenye thamani ya shilingi milioni 163, gari hilo litasaidia kutatua changamoto kwa wagonjwa mbalimbali wa dharura na wakati wa majanga, kutokana na uwezo wake wa kutoa huduma zote za dharura hata ikiwa nje ya hospitali.

Aidha, kupitia fedha za Uviko-19 zilizotolewa na Serikali, hospitali imenunua vifaatiba katika idara ya dharura (EMD), ili kupunguza changamoto kwa wagonjwa wa dharura wanaoletwa kila siku katika hospitali kuokoa na kuboresha maishaya Watanzania wanaofika hospitalini hapa kupatiwa matibabu hususan katika idara ya dharura.






**UBORESHWAJI WA MIUNDOMBINU**

**(i) ICU**

Kutokana na idadi kubwa ya wagonjwa tunaowahudumia hospitali ilionekana kuwa na upungufu mkubwa wa vyumba vya wagonjwa mahututi, hasa kipindi cha majanga mbalimbali ya kidunia yanayohitaji huduma za uangalizi wa karibu kwa wagonjwa, kwa mfano tatizo kubwa la kidunia la Uviko-19.

Kwa kuliona hilo, Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, alitoa fedha kwa ajili ya ukarabati na upanuzi wa vyumba vya ICU shilingi milioni 500 ili kukidhi mahitaji ya wagonjwa ambao wamekua wakihangaika kutokana na upungufu huu.



ICU

**(ii) JENGO LA MACHO**

Hospitali imefanikiwa kujenga jengo la matibabu ya macho kwa kushirikiana na wadau mbalimbali. Hospitali imeanza kuhakikisha huduma ambazo zilikuwa zinatolewa nje ya nchi, sasa zinapatikana hapa nchini kwa kutumia wataalamu wetu.

Jambo hilo limekuwa faraja sana kwa wananchi ambao hawakuwa na uwezo wa kuwapeleka wagonjwa wao nje ya nchi, vilevile serikali imeweza kuokoa fedha nyingi kutokana na jengo hili la matibabu. Jumla ya bajeti ya ujenzi wa jengo la macho ni shilingi billioni 3.7, wafadhili wametoa shilingi bilioni 2.4, Hospitali ya Bugando shilingi bilioni 1.3.



JENGO LA MACHO

**(iii) WODI ZA SARATANI**

Hospitali ya Rufaa ya Kanda Bugando imefanikiwa kujenga jengo la matibabu ya saratani kwa kushirikiana na Serikali na wadau mbalimbali, ambapo jengo hili lina huduma zote za msingi kama vyumba vya madaktari (consultation rooms), maabara, chumba cha uchunguzi wa mionzi, chumba cha dawa (pharmacy), ultra sound, chumba cha kutunza kumbukumbu za mgonjwa na chumba cha wagonjwa maalum (VIP).

Hivyo huduma zote muhimu zitapatikana katika jengo hili hatua inayopunguza mizunguko kwa wagonjwa. Wodi ya saratani imesaidia kupunguza urasimu na adha kwa wagonjwa kusafiri kwenda Dar es Salaam (Ocean Road) na nchi za jirani kutafuta huduma na pia wagonjwa wanapata matibabu sahihi kwa wakati,

Kwa namna moja ama nyingine imepunguza vifo kwani wagonjwa wanahudumiwa kwa wakati.



WODI ZA SARATANI

**MTAMBO WA KUFUA OKSIJENI**

Mtambo huu una uwezo wa kuzalisha mitungi ya oksijeni 400 ambapo hospitali ina tumia mitungi takriban 100 kwa siku, hivyo hospitali zingine zitanufaika na mtambo huu. Ujenzi huu umegharimu shilingi Milioni272 kutoka katika mapato ya ndani ya hospitali. Gharama ya mashine kutoka kwenye pesa za Uviko-19 shilingi milioni 600.



**RASILIMALI WATU**

Hospitali ya Rufaa ya Kanda Bugando, ina jumla ya watumishi 2,068 ambapo wanaolipwa na serikali ni zaidi ya watumishi 1,200. Pia serikali imefadhili watumishi 27 kimasomo katika ngazi mbalimbali za kibingwa na kibingwa bobezi.

Hospitali inapenda kuishukuru Serikali ya Awamu ya Sita kupitia Wizara ya Afya, kwa ufadhili wa wataalamu katika kujiendeleza kimasomo ya ubingwa na ubingwa bobezi katika sekta ya afya.

**RASILIMALI FEDHA**

Serikali imeendelea kulipa mishahara kwa wafanyakazi wa taasisi ni shilingi 21,073,416,750, fedha za madawa kutoka MSD shilingi 734,838,491 na fedha za gharama za uendeshaji kutoka serikalini shilingi milioni 210,990,114.

**KUBORESHWA KWA MAHUSIANO KATI YA TAASISI ZA DINI NA SERIKALI**

Hospitali ya Rufaa ya Kanda ya Bugando inayomilikiwa na kanisa Katoliki Tanzania, imeendelea kuwa na ushirikiano na serikali kwa kiasi kikubwa na ushirikiano huu umezidi kuimarika siku hadi siku, mfano Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dk. Samia Suluhu Hassan alifanikiwa kuwa mgeni rasmi katika maadhimisho ya Jubilee ya Miaka 50 ya Bugando, na alizindua miradi mbalimbali ikiwemo mashine ya MRI.

Pia, Makamu wa Rais Mhe.Dk Philip Isdori Mpango alipokuja katika Hospitali ya Bugando kuzindua jengo la saratani, Waziri Mkuu wa Tanzania Kassim Majaliwa Kassim alipozindua jengo la macho. Vilevile serikali kupitia Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Mwanza imekua ikihamasisha na kutafuta wadau mbalimbali ili waweze kutoa msaada hasa katika ujenzi na maendeleo.

Pia kubadilishana ujuzi katika sekta ya afya, kama sehemu ya ushirikiano kati ya Serikali na taasisi za dini, wataalamu wetu wamekuwa wakibadilishana ujuzi na madaktari wengine kutoka hospitali za serikali ikiwemo Hospitali ya Taifa Muhimbili, Taasisi ya Mifupa – Muhimbili Orthopedic Institute (MOI), Hospitali ya Benjamin Mkapa na Hospitali ya Rufaa ya Kanda Mbeya na Hospitali nyingine. Vilevile Hospitali ya Bugando imeendelea kulea hospitali za mikoa, wilaya na vituo vya afya kupitia huduma za tiba mkoba.

**WITO KWA JAMII**

Tunaomba wananchi kubadili mitindo ya maisha na kuondoa kasumba iliyojengeka miongoni mwetu, kuwa hospitali ni kwa ajili ya wagonjwa tu, badala yake tutambue kuwa kila mmoja ni mgonjwa na tunahitaji uchunguzi mara kwa mara na kupata ushauri wa kitaalamu kwa ustawi wa afya zetu.

**NENO KWA SERIKALI YA AWAMU YA SITA**

Tunaishukuru, Serikali yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia Wizara ya Afya, kuendelea kuwajali wananchi kwa kuboresha huduma za afya katika vituo vya afya na hospitali za ngazi zote.

Pia, hospitali inapenda kuishukuru Serikali ya Awamu ya Sita kupitia Wizara ya Afya, kwa ufadhili wa wataalamu katika kujiendeleza kimasomo ya ubingwa na ubobezi katika sekta ya afya.

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA AFYA
HOSPITALI YA RUFAA MKOA WA

# SONGWE



RAIS Dk. Samia Suluhu Hassan



Mganga Mfawidhi Hospitali ya Rufaa ya Mkoa Songwe Dkt. Juma R. Juma



Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu.

# Fedha za Rais Samia zilivyoboresha huduma Hospitali ya Rufaa Songwe









**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA AFYA**
**HOSPITALI YA RUFAA YA MKOA WA SONGWE**




Jengo la wagonjwa wa nje hospitali ya rufaa ya mkoa wa songwe.

# Fedha za Rais Samia zilivyoboresha huduma Hospitali ya Rufaa Songwe



Mashine ya kisasa ya mionzi (X-RAY MACHINE).

RAIS Dk. Samia Suluhu Hassan, amepata mafanikio makubwa katika utekelezaji wa miradi ya kimkakati tangu alipoapishwa Machi 19, 2021.

Miongoni mwa sekta zinazofanya vyema ni afya, ambapo Rais Dk. Samia, ameendelea kutoa fedha nyingi kuboresha eneo hilo ili wananchi wawe na afya njema.

Serikali inaamini wananchi wake wakiwa na afya njema, watakuwa na uwezo mkubwa wa kufanya shughuli za uzalishaji mali ili kujenga uchumi imara.

Katika kipindi cha miaka mitatu ya uongozi wake, Rais Dk. Samia ametoa fedha kwa lengo la kuboresha Hospitali ya Rufaa Mkoa wa Songwe.

Miongoni mwa mafanikio iliyopata hospitali hiyo ni kuzindua jengo la wagonjwa wa nje (OPD), lililokamilika asilimia 99.9 likigharimu shilingi za kitanzania bilioni 5.2.

Hivi sasa jengo hilo linatoa huduma za matibabu ya kulaza wagonjwa, mafanikio ambayo ni makubwa tangu ilipoanza rasmi kutoa huduma za matibabu kwa wananchi wa Songwe na maeneo mengine.



Mganga Mfawidhi Hospitali ya Rufaa ya Mkoa Songwe Dkt. Juma R. Juma

***Pia, hospitali imekamilisha ujenzi wa jengo la mama na mtoto lenye ghorofa nne kwa asilimia 60 ya utekelezaji huku likitarajiwa kugharimu shilingi za kitanzania bilioni 9.7.***

MIAKA MITATU YA RAIS DK. SAMIA NA UBORESHAJI SEKTA YA AFYA NCHINI

# Fedha za Rais Samia zilivyoboresha huduma Hospitali ya Rufaa Songwe



Pia, hospitali imekamilisha ujenzi wa jengo la mama na mtoto lenye ghorofa nne kwa asilimia 60 ya utekelezaji huku likitarajiwa kugharimu shilingi za kitanzania bilioni 9.7.

Aidha, sakafu ya chini ya jengo imekamilika na kuanza kutumika rasmi kutolea huduma za mionzi CT SCAN na X-RAY ambapo mashine hizo zinafanya kazi asilimia 100.

Imeelezwa mashine hizo zimegharimu fedha za kitanzania shilingi bilioni 1.4 kukamilika na kuanza kutoa huduma kwa wananchi wa Songwe na mikoa jirani.

***Mafanikio hayo yametokana na juhudi za Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Rais Dk. Samia katika kuhakikisha anaboresha sekta ya afya nchini ambapo kwa kushirikiana na Wizara ya Afya, imezidi kusambaza vifaa tiba hususan katika hospitali za rufaa za mikoa.***



Mashine ya CT Scan

Usimikaji wa mashine za CT SCAN na X-RAY zimesaidia kupunguza adha ya wananchi kwenda mikoa jirani kupata huduma za matibabu.

Mafanikio hayo yametokana na juhudi za Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Rais Dk. Samia katika kuhakikisha anaboresha sekta ya afya nchini ambapo kwa kushirikiana na Wizara ya Afya, imezidi kusambaza vifaa tiba hususan katika hospitali za rufaa za mikoa.

Sekta ya Afya nchini imeboreshwa asilimia 98 na Hospitali ya Rufaa Mkoa wa Songwe ni miongoni mwa wanufaika wakubwa wa uboreshaji huo.

Vilevile, hospitali hiyo imeendelea kupokea vifaatiba mbalimbali kama mitungi ya gesi (OXYGEN GAS CYLINDER), inayosaidia wagonjwa katika upumuaji na vifaa vya jengo la dharura na wagonjwa mahututi (ICU).

Pia, hospitali hiyo inaipongeza Wizara ya Afya kutambua umuhimu wa madaktari bingwa huku Songwe ikiwa ni wanufaika wakubwa baada ya kupelekewa madaktari bingwa wa macho, magonjwa ya ndani, watoto, wanawake, uzazi na magonjwa ya akili.

Pia kwa upande wa dawa, hospitali hiyo ina dawa za kutosha na imepongeza juhudi za Serikali ya Awamu ya Sita kwa juhudi zake za kuhakikisha vifaatiba vinasambazwa kwa wingi.

Aidha, miradi iliyopo mbioni kukamilika ni (jengo la wagonjwa wa dharura na jengo la wagonjwa mahututi (ICU), taasisi itasimamia na kuhakikisha inakamilisha na kutunza vizuri ili kuendelea kuboresha utoaji wa huduma bora kwa wanachi.

Hospitali ya Rufaa Songwe inatoa huduma kwa wagonjwa wa nje na ndani ya mkoa na wamejiandaa kuwahudumia wananchi wote, ili wasipate changamoto ya kutembea umbali mrefu kupata matibabu.

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

# MAMLAKA YA MAABARA YA MKEMIA MKUU WA SERIKALI

GCLA ISO 9001:2015 Certified





# MAFANIKIO YA MAMLAKA YA MAABARA YA MKEMIA MKUU WA SERIKALI KWA KIPINDI CHA MIAKA MITATU YA RAIS DK. SAMIA SULUHU HASSAN



Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, akimsikiliza Mkemia Mkuu wa Serikali, Dkt. Fidelice Mafumiko, akielezea kazi za uchunguzi wa kimaabara zinazofanywa na Mamlaka ikiwemo uchunguzi wa kimaabara wa vielelezo mbalimbali vya dawa za kulevya zinazowasilishwa na Mamlaka za udhibiti na vyombo vya ulinzi na usalama na utoaji wa ushahidi mahakamani baada ya uchunguzi kukamilika wakati Mhe. Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kutembelea banda la Mamlaka kabla ya kufunga Maadhimisho ya Siku ya Kitaifa ya Kupiga Vita Dawa za Kulevya, yaliyofanyika katika uwanja wa Sheikh Amri Abeid, jijini Arusha, Juni 25, 2023. Katikati ni Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Kassim Majaliwa.

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
MAMLAKA YA MAABARA YA MKEMIA MKUU WA SERIKALI

GCLA ISO 9001:2015 Certified

# MAFANIKIO YA MAMLAKA YA MAABARA YA MKEMIA MKUU WA SERIKALI KWA KIPINDI CHA MIAKA MITATU YA RAIS DK. SAMIA SULUHU HASSAN



Mkemia Mkuu wa Serikali, Dk. Fidelice Mafumiko



Rais Mhe. Dkt Samia Suluhu Hassan

**Na MWANDISHI WETU**

HISTORIA ya Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali (Government Chemist Laboratory Authority-GCLA) ilianza tangu enzi za utawala wa ukoloni wa Mjerumani mwaka 1895.

Enzi hizo maabara ilikuwa na jukumu la kufanya utafiti wa magonjwa ya ukanda wa joto (Tropical Diseases) hususani malaria na kifua kikuu.

Baada ya Uhuru, Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali ilikuwa mojawapo ya Idara chini ya Wizara ya Afya hadi mwaka 1999 ilipopandishwa hadhi na kuwa Wakala chini ya Sheria ya Wakala za Serikali, Sheria Na. 30 ya mwaka 1997.

Aidha, Mwaka 2016, Wakala ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali ilipandishwa hadhi tenana kuwa Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali chini ya Sheria ya Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali, Sheria Na. 8 ya mwaka 2016.

**UWEKEZAJI KATIKA MIUNDOMBINU YA UCHUNGUZI WA KIMAABARA**

Kwa mujibu wa Mkemia Mkuu wa Serikali, Dk. Fidelice Mafumiko, alisema katika kipindi cha miaka mitatu ya Serikali ya Awamu ya Sita chini ya uongozi wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. Samia Suluhu Hassan, Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali imeweza kujenga jengo la Makao Makuu ya Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali, eneo la Medeli jijini Dodoma lenye Thamani ya sh. Bilioni 8.14.

Aidha, Mkemia Mkuu wa Serikali, Dk. Mafumiko alisema mamlaka ipo katika hatua za awali za ujenzi wa majengo ya Ofisi na Maabara katika Ofisi za Kanda ya Kusini iliyopo Mtwara, Kanda ya Ziwa jijini Mwanza na Kanda ya Mashariki jijini Dar es Salaam unaokadiriwa kugharimu kiasi cha jumla ya sh. Bilioni tano.

"Miradi hii ikikamilika itaboresha mazingira ya kufanyia kazi na utoaji huduma kwa wananchi wa mikoa ya Dar es Salaam na Pwani, mikoa ya Kanda ya Ziwa na mikoa ya Kanda ya Kusini.

> **Uwekezaji katika mitambo na vifaa vya kisasa vya uchunguzi wa kimabaara katika kipindi cha miaka mitatu ya Serikali ya Awamu ya Sita, Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali imeweza kununua mitambo na vifaa vya kisasa kwa ajili ya kuendelea kuboresha huduma za uchunguzi wa kisayansi wa kimaabara vyenye thamani ya sh. Bilioni 14.**

"Uwekezaji katika mitambo na vifaa vya kisasa vya uchunguzi wa kimabaara katika kipindi cha miaka mitatu ya Serikali ya Awamu ya Sita, Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali imeweza kununua mitambo na vifaa vya kisasa kwa ajili ya kuendelea kuboresha huduma za uchunguzi wa kisayansi wa kimaabara vyenye thamani ya sh. Bilioni 14.

"Mitambo na vifaa hivi ni pamoja na mitambo mikubwa 12 na midogo 205," alisema Mkemia Mkuu wa Serikali, Dk. Mafumiko.

Mkemia Mkuu wa Serikali, Dk. Mafumiko, alisema mitambo hii ni kwa ajili ya kuimarisha uchunguzi wa kimaabara na kuendelea kutoa huduma bora za uchunguzi wa kisayansi wa kimaabara kwa wananchi kwa haraka na kwa wakati.

Aliongeza, wekezaji0 katika mafunzo kwa wataalam katika kipindi cha miaka mitatu ya Serikali ya Awamu ya Sita chini ya uongozi wa Rais, Dk. Samia, Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali imewezesha watalaam 28 kuhudhuria mafunzo ya muda mrefu.

Aidha, alisema watumishi 147 walihudhuria mafunzo ya muda mfupi ndani na nje ya nchi.

"Watumishi 56 waliwezeshwa kuhudhuria mikutano ya kitaaluma (Professional Bodies), na watumishi 23 waliwezeshwa kupata mafunzo ya awali ya Utumishi wa Umma baada ya kuajiriwa.

"Mafunzo haya yameweza kuwajengea uwezo watumishi wa mamlaka katika kutekeleza majukumu yao kwa weledi na ufanisi mkubwa.

Alisema pia, mafunzo hayo yamewezesha mamlaka kuongeza ubora wa utoaji huduma kwa wananchi kwa ufanisi wa huduma za uchunguzi wa kimaabara.

**UCHUNGUZI WA KIMAABARA**

Mkemia Mkuu wa Serikali, Dk. Mafumiko alisisitiza uwekezaji wa miundombinu wezeshi ya uchunguzi wa maabara umeongeza ufanisi wa uchunguzi ambapo mwaka 2021 wastani wa sampuli/vielelezo 155,817, sawa na asilimia 139.94 ya lengo la wastani wa kuchunguza sampuli/vielelezo 111,349 ulifanyika.

Aidha, alisema katika mwaka 2022, sampuli 212,306 sawa na asilimia 133.9 ya lengo la kuchunguza sampuli 158,600 zilifanyiwa uchunguzi wa kimabaara.

Vilevile, katika kipindi cha Julai hadi Desemba 2023, sampuli 84,352 zilifanyiwa uchunguzi sawa na asilimia 87.45 ya lengo la kuchunguza sampuli 96,450.

"Matokeo ya uchunguzi huu yanasaidia mamlaka ombezi na vyombo vya maamuzi kisheria kufanya maamuzi stahiki na kwa wakati.

"Mchango wa utoaji wa matokeo ya uchunguzi wa sampuli kwa wakati

uchunguzi wa kisayansi wasampuli na utoajima tokeo kwa wakati unasadia kuleta haki, amani na utulivu wa nchi kwa kutoa ushahidi wa kitalaamu," alisema Mkemia Mkuu wa Serikali, Dk. Mafumiko.

Alisema, mahakamani kwenye yanayotokana na uchunguzi wa sampuli na



**Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, akimsikiliza Mkemia Mkuu wa Serikali, Dkt. Fidelice Mafumiko, akielezea kazi za uchunguzi wa kimaabara zinazofanywa na Mamlaka ikiwemo uchunguzi wa kimaabara wa vielelezo mbalimbali vya dawa za kulevya zinazowasilishwa na Mamlaka za udhibiti na vyombo vya ulinzi na usalama na utoaji wa ushahidi mahakamani baada ya uchunguzi kukamilika wakati Mhe. Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kutembelea banda la Mamlaka kabla ya kufunga Maadhimisho ya Siku ya Kitaifa ya Kupiga Vita Dawa za Kulevya, yaliyofanyika katika uwanja wa Sheikh Amri Abeid, jijini Arusha, Juni 25, 2023. Katikati ni Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Kassim Majaliwa.**

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

MAMLAKA YA MAABARA YA MKEMIA MKUU WA SERIKALI

ISO 9001:2015 Certified

# MAFANIKIO YA MAMLAKA YA MAABARA YA MKEMIA MKUU WA SERIKALI KWA KIPINDI CHA MIAKA MITATU YA RAIS DK. SAMIA SULUHU HASSAN

vielelezo mbalimbali vya masuala ya jinai.

Mkemia Mkuu wa Serikali, Dk. Mafumiko alisisitiza, vile vile uchunguzi huo huwezesha kuzi kwa miili ya wahanga wa majanga mbalimbali kwa kuzingatia dini, mila na desturi za wahusika.

Alisema pamoja na kutatua migogoro katika jamii (uhalali wa wazazi kwa mtoto, mirathi).

Dk. Mafumiko alisisitiza uchunguzi wa kisayansi wa kimaabara una mchango pia kwa wagonjwa wanaotakiwa kupandikizwa figo na utambuzi wa jinsi tawala kwa ushirikiano na Madaktari Bingwa.

"Mchango mwingine wa uchunguzi wa kimaabara ni pamoja na kutambua aina ya sumu kwa wagonjwa wanaodhaniwa kuvuta, kula au kunywa chakula chenye sumpuli kupata tiba sahihi na kwa wakati na kuokoa maisha.

"Uchunguzi wa kimaabara unasaidia pia kuhakiki ubora na usalama wa bidhaa za viwandani na kilimo kwa ajili ya kulinda afya ya jamii na mazingira.

"Usimamizi wa kemikali ili kulinda afya ya binadamu na mazingira, mamlaka inatekeleza jukumu la usimamizi na udhibiti wa kemikali kupitia utekelezaji wa Sheria ya Usimamizi na Udhibiti wa Kemikali za Viwandani na Majumbani, Sheria Na. 3. ya mwaka 2003," alisema.

Aidha, alisema utekelezaji wa sheria hiyo unafanyika kupitia usajili wa wadau, ukaguzi wa maghala na maeneo ambapo kemikali zinatumika na utoaji vibali vya kuingiza au kusafirisha kemikali.

**a)USAJILIWAWADAU**

Alisema mamlaka imeendelea kufanya maboresho ya kuharakisha mchakato wa usajili wa kampuni zinazojihusisha na biashara ya kemikali.

"Katika kipindi cha miaka mitatu ya Serikali ya Awamu ya Sita kumekuwa na ukuaji wa biashara kwa wadau wanaojihusisha na biashara ya kemikali, ambapo wadau wameongezeka kutoka wadau 2,125 mwaka 2021 hadi wadau 4,181 kufikia Desemba, 2023 sawa na ongezeko la asilimia 97 la wadau waliosajiliwa," alisema Mkemia Mkuu wa Serikali, Dk. Mafumiko.

**b) UKAGUZI WA MAGHALA**

Dk. Mafumiko alisema katika kuhakikisha kuwa kemikali zinatumika kwa usalamana kwa kufuata taratibu zote zinazohitajika ili kulinda afya za binadamu na mazingira pia kuhakikisha kuwa kemikali zinazoingizwa nchini ni zile ambazo zinaruhusiwa kuingia, mamlaka hufanya ukaguzi wa mara kwa mara katika maghala yanayohifadhi kemikali na maeneo ya mipaka, katika kipindi cha miaka mitatu

Dk. Mafumiko alisema, mamlaka imefanya ukaguzi wa maghala 5,335 ya kuhifadhia kemikali sawa na asilimia118.6 ya lengo la kukagua maghala 4,500.

**c)UTOAJI WA VIBALI VYAKUINGIZA AU KUSAFIRISHA KEMIKALI**

Dk. Mafumiko alisema, mamlaka imeweza kudhibiti uingizaji na usafirishaji wa kemikali hatari shina zile zinazodhibitiwa chini ya mikataba ya kimataifa, kulinda afya ya binadamu na mazingira kwa kutoa vibali vya kuingiza na kusafirisha kemikali hizo.

Alisema katika kipindi cha miaka mitatu, kumeku wa na ongezeko la vibali vya uingizaji wa kemikali kutoka 40,270 kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 hadi 101,057 kufikia Desemba, 2023 sawa na ongezeko la asilimia 151 ya vibali vilivyotolewa.

"Sababu ambayo imepelekea kuongezeka kwa vibali ni kuwepo kwa mazingira mazuri ya biashara na uwekezaji yaliyowekwa na Serikali ya Awamu ya Sita," alisema Dk. Mafumiko.

**d) KUBORESHA MAZINGIRA YA BIASHARA NA KUKUA KWA BIASHARA YA KEMIKALI**

Katika kipindi cha miaka mitatu cha uongozi wa Serikali ya Awamu ya Sita, mamlaka imendelea kuboresha mazingira ya biashara ya kemikali nchini hasa zile za kimkakati zinazotumika katika uchimbaji na uchenjuaji wa madini hapa nchini na nchi za Zambia na Congo.

i.Kemikali ya Ammonium Nitrate ambayo hutumika hasa katika ulipuaji wa miamba wakati wauchimbaji madini nchini na nchi za Zambia na

> **Katika kipindi cha miaka mitatu ya Serikali ya Awamu ya Sita kumekuwa na ukuaji wa biashara kwa wadau wanaojihusisha na biashara ya kemikali, ambapo wadau wameongezeka kutoka wadau 2,125 mwaka 2021 hadi wadau 4,181 kufikia Desemba, 2023 sawa na ongezeko la asilimia 97 la wadau waliosajiliwa**

DR. Congo imeongezeka kutoka tani 135,445 Mwaka Fedha 2021/2022 hadi tani 319,889.5 kufikia Desemba, 2023 sawa na ongezeko la asilimia136.18.

ii.Kemikali ya Salfa ambayo hutumika hasa katika mchakato wa uchimbaji na uchenjuaji wa madini ya shaba nchi za Zambia na DR. Congo kupitia bandari ya Dar es Salaam imeongezeka kutoka tani 396,982 Mwaka Fedha 2021/2022 hadi tani 1,132,644 kufikia Desemba, 2023 sawa na ongezeko la asilimia185.31.

iii.Kemikali ya Sodium Cyanide ambayo hutumika katika uchenjuaji wa madini ya dhahabu nchini nanchi za Zambia na DR. Congo kupitia bandari ya Dar es Salaam zimeongezeka kutoka tani 41,461 Mwaka Fedha 2021/2022 na tani 37,331 kufikia Desemba, 2023 sawa na ongezeko la asilimia 156.47

Alisisitiza, sababu ambazo zimepelekea kuongezeka kwa uingizaji wa kemikali hizo kupitia Bandari ya Dar es Salaam ni kuwepo kwa maboresho ya miundombinu ya bandari na mahusiano mazuri kati ya Tannzania na nchi jirani yaliyowekwa na Serikali ya Awamu ya Sita.

Alisema vile vile, kupitia elimu kwa umma/wadau wa biashara ya kemikali kumekuwa na ongezeko kubwa la wadau wanaotimiza matakwa ya sheria za nchi ikiwemo sheria ya usimamizi na udhibiti wa kemikali.

**3.1 HUDUMA ZA MAMLAKA KUPITIA MATUMIZI YA TEHAMA**

Dk. Mafumiko alisema mamlaka imeendelea kutengeneza/kujenga na kusimika mifumo mbalimbali ya TEHAMA kupitia watalaam wake wa ndani.

"Mifumo hii imeimarisha na kuongeza matumizi ya TEHAMA ndani ya Mamlaka," alisema Dk. Mafumiko.

a)Mfumo wa Usajili na Utoaji Vibali kwa Wadau wa Kemikali (Customer Chemicals Management Portal - CCMP); (Kutoka siku saba hadi muda wa saa moja).

b)Mfumo wa Kuratibu taarifa za Maabara (Laboratory Management Information System) (Kuunganisha Mfumo wa Haki Jinai ili kubadilisha na taarifa za matokeo ya uchunguzi wa maabara na mifumo mingine ya Haki Jinai).

c)Mfumo wa kutoa ushahidi kwa ki-electroniki (Video conferencing and Virtual courts)–(Kupunguza gharama kwa serikali kwa wataalam kusafiri kwenda kutoa ushahidi mahakamani kwenye mnyororowa Haki Jinai).

d)Mfumo wa usimamizi wa taarifa za watoa ushahidi mahakani (Expert Witness Management System) –kuwezesha ofisi ya Taifa ya Mashtaka na Mahakama kupata taarifa za mwenendo wa kutoa ushahidi.

"Ujenzi na usimikaji wa mifumo hii umetumia wataalamu wa ndani wa Mamlaka kwa kushirikiana na wataalam wa Serikali Mtandao.

"Huduma za Kimaabara kwa Viwango vya Ubora wa Kimataifa, mamlaka imefanikiwa kuendelea kutoa huduma za uchunguzi wa Kimaabara kwa Viwango vya Ubora vya Kimataifa, viwango hivyo vya ubora vinatambulika kwa kupata Ithibati," alisema Dk. Mafumiko.

Alisema, Ithibati ya umahiri wa maabara ni moja ya mafanikio makubwa sana kwa Mamlaka na kwa Tanzania kwa ujumla, ambapo mamlaka inakuwa na uwezo wa kupokea na kufanya uchunguzi wa sampuli kutoka ndani na nje ya nchi na kutoa matokeo yanayokubalika duniani.

Vile vile aliongeza kuwa, mamlaka inatekeleza mifumo miwili ya ubora na umahiri ya kimataifa, ambayo ni Ithibati ya Mifumo ya Ubora (ISO 9001:2015) iliyohuishwa kwa mara tatu mfululizo, mifumo ya ubora ya uendeshaji wa mamlaka umekubalika Kimataifa na Ithibati katika umahiri wa uchunguzi wa kimaabara (ISO 17025:2027) katika maabara za kenne.

Aliongeza, matokeo ya uchunguzi wa kimaabara yanakubalika Kimataifa.



Jengo la Makao Makuu ya Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali lililopo eneo la Medeli Jijini - Dodoma

# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

## HOSPITALI YA RUFAA KANDA YA KUSINI MTWARA



Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan

# HOSPITALI YA RUFAA KANDA YA KUSINI MTWARA

## yajivunia mafanikio lukuki miaka mitatu ya Rais Mhe. Dk. Samia



Mkurugenzi wa Hospitali ya Rufaa Kanda ya Kusini-Mtwara Dk.Herbert Masigati.




Hospitali ya Rufaa ya Kanda ya Kusini Mtwara



Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan akikabidhi. funguo za Magari Matatu kwa Mkurugenzi wa Hospitali ya Rufaa Kanda ya Kusini



Mashine ya CT Scan- Hospitali ya Rufaa Kanda ya Kusini



Chumba cha Wagonjwa Mahututi (ICU)

HOSPITALI YA RUFAA MTWARA

# Hospitali ya Rufaa kanda ya kusini Mtwara yajivunia mafanikio lukuki miaka mitatu ya Rais Mhe. Dk. Samia



Mkurugenzi wa Hospitali ya Rufaa Kanda ya Kusini-Mtwara Dk.Herbert Masigati.



Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan akikabidhi. funguo za Magari Matatu kwa Mkurugenzi wa Hospitali ya Rufaa Kanda ya Kusini

**Na MWANDISHI WETU, MTWARA.**

HOSPITALI ya Rufani ya Kanda ya Kusini-Mtwara ipo katika Manispaa ya Mtwara-Mikindani, katika Mkoa wa Mtwara. Hospitali inakadiriwa kuhudumia wagonjwa 800-1,000 kwa siku, ikiwa na vitanda 1,000 vya kulaza wagonjwa pamoja na jumla ya watumishi 1,164 pindi itakapokamilika.

Hospitali ya Rufaa ya Kanda ya Kusini -Mtwara imeanza kutoa huduma Oktoba 1, mwaka 2021 na kufunguliwa rasmi tarehe Septemba 15,mwaka 2023 na Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan. Hospitali hii inahudumia wagonjwa kutoka katika mikoa ya Mtwara, Lindi, Ruvuma na pia nchi jirani za Msumbiji, Malawi na Visiwa vya Komoro.

Hivi karibuni Uhuru ya Kijani lilifanya mahojiano na Kaimu Mkurugenzi wa hospitali ya Rufani Kanda ya Kusini –Mtwara, Dk.Herbert Masigati, kuhusu miaka mitatu ya Rais Dk.Samia na uboreshaji wa sekta ya afya nchini.

Dk.Masigati alisema mradi wa ujenzi wa hospitali ya Rufani Kanda ya Kusini ulianza mwaka wa Fedha 2005/2006, kwa upimaji wa mipaka na mwinuko wa ardhi sambamba na uthaminishaji na ulipaji fidia kwa wananchi wakazi wa eneo la mradi.

Aliongeza mwaka 2010/2011 kazi ya ujenzi wa uzio wenye urefu wa kilometa 2.7 ilifanyika kwenye eneo lote la hospitali lenye ukubwa wa hekari 100. Aidha, ujenzi wa jengo la mapokezi na wagonjwa wa nje (Out Patient Department – OPD) ulianza kipindi cha mwaka 2013 hadi 2015.

**Jengo hili pia lilifanyiwa maboresho ili kuwezesha huduma zote za msingi, kuanza kutolewa na hospitali wakati majengo mengine yanasubiri kujengwa kadri ya upatikanaji wa fedha, hospitali hii kwa sasa ina jumla ya watumishi 177**

Kutokana na hali ya upatikanaji wa fedha, katika Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2019/2020, Wizara ya Afya, iliingia mkataba na Mkandarasi ambae ni Shirika la Nyumba la Taifa-NHC (Septemba 29, mwaka 2019) kuendeleza awamu ya pili ya ujenzi wa jengo la OPD kwa gharama ya shilingi 15,805,239,642.02.

"Jengo hili pia lilifanyiwa maboresho ili kuwezesha huduma zote za msingi, kuanza kutolewa na hospitali wakati majengo mengine yanasubiri kujengwa kadri ya upatikanaji wa fedha,hospitali hii kwa sasa ina jumla ya watumishi 174" alisema Dk.Masigati.

Kaimu Mkurugenzi huyo alizitaja huduma zinazotolewa kuwa huduma za kibingwa za mifupa, moyo, upasuaji, masikio, pua na koo pamoja, Magonjwa ya Wanawake na uzazi.

Nyingine ni huduma za kibingwa za uchunguzi wa magonjwa kama vile; Radiolojia, maabara, na uchunguzi wa maradhi ya Moyo (ECHO na ECG), kutokana na uwepo wa wataalamu na Vifaa Tiba vya Kisasa kama vile MRI, CT SCAN, Digital X-Ray, Vifaa vya Huduma za Dharula na Wagonjwa Mahututi.

Dk.Masigati alisema kwa mwaka wa fedha 2023/2024, hospitali ya Rufani ya Kanda ya Kusini Mtwara, kiasi cha sh.bilioni tatu, zimetengwa kwa ajili ya ujenzi wa miradi ya majengo mbalimbali hospitalini hapo ili kuongeza wigo wa huduma.

Aliyataja majengo hayo yanayotarajiwa kujengwa kuwa ni la mama na mtoto pamoja na vyumba upasuaji, ujenzi wa nyumba za watumishi, kichomea taka pamoja na jengo la kufulia na kwamba hatua za awali za kumpata Mshauri elekezi zimeishafanyika na ujenzi utaendelea kwa kadri ya upatikanaji wa fedha.

**MRADI WA UNUNUZI WA VIFAA VYA KISASA VYA TIBA NA UCHUNGUZI KUPITIA FEDHA ZA IMF-UVIKO 19.**

Dk.Masigati alisema hospitali ililetewa kiasi cha shilingi 7,482,680,088, kwa ajili ya ununuzi wa vifaa tiba vilivyowezesha kuanzishwa kwa huduma hospitalini hapo na kwamba manunuzi yaliishafanyika.



Hospitali ya Rufaa ya Kanda ya Kusini Mtwara



Mashine ya CT Scan- Hospitali ya Rufaa Kanda ya Kusini

HOSPITALI YA RUFAA MTWARA

# Hospitali ya Rufaa Kanda ya Kusini Mtwara yajivunia mafanikio lukuki miaka mitatu ya Rais Mhe. Dk. Samia



Kitengo cha Maabara



Chumba cha Wagonjwa Mahututi (ICU)

Kwa mujibu wa Dk.Masigati manunuzi hayo ni ununuzi na usimikaji wa mashine ya MRI kupitia Taasisi ya Saratani Ocean Road,mashine ya CT Scan, mashine za x ray na ultrasound pamoja na ununuzi na usimikaji wa vifaa vya wodi za wagonjwa mahututi.

Mengine ni ununuzi na usimikaji wa Mashine ya kutolea dawa ya usingizi na ganzi, ujenzi na ukarabati wa majengo yaliyotumika kwa ajili ya kusimika vifaa vya MRI na CT Scan na ununuzi na usimikaji wa mashine ya Apheresis.

**MAFANIKIO**

Kaimu Mkurugenzi wa hopitali ya Rufani ya Kanda ya Kusini Mtwara, Dk.Masigati alisema hospitali imefanikiwa kusimika vifaa tiba vya kisasa vya uchunguzi, na pia imefanikiwa kuanzisha vitengo na idara mbalimbali za kutolea huduma.

Aliyataja mafanikio mengine kuwa ni kusimika jenereta (standby), kwa ajili kupata umeme muda wote pindi umeme wa gridi ya Taifa unapokatika pamoja na kujenga kisima cha maji chenye uwezo wa kutunza lita 300,000.

Mengine ni hospitali hiyo kupokea magari mapya matatu aina ya 'Toyota Land cruiser' (mawili ya kubebea Wagonjwa na moja la Utawala), wakati wa ufunguzi wa hospitali uliofanyika Septemba 15, mwaka 2023.

"Hospitali ilipata kibali cha ajira za watumishi 140, wakiwemo madaktari bingwa watano wa fani mbalimbali mwaka 2023/2024,tulipata ufadhili wa masomo kwa madaktari bingwa na wataalamu wengine 25, katika mwaka wa fedha 2023/2024 kupitia Samia Suluhu Hassan Scholarship" alisema Dk.Masigati.



Mashine ya X Ray Mtwara Zonal 2

**Hospitali ilipata kibali cha ajira za watumishi 140, wakiwemo madaktari bingwa watano wa fani mbalimbali mwaka 2023/2024, tulipata ufadhili wa masomo kwa madaktari bingwa na wataalamu wengine 15, katika mwaka wa fedha 2023/2024 kupitia Samia Scholarship**

**MIKAKATI.**

Dk.Masigati aliongeza mikakati iliyopo sasa ni kuendeleza watumishi kitaaluma, katika kada mbalimbali ili hospitali iweze kutoa huduma za kibingwa na bingwa bobezi, na kuwa mwaka wa fedha 2023/2024 jumla ya watumishi 25, wamepata nafasi ya kwenda kujiendeleza wakiwepo Madaktari waliopata ufadhili wa Serikali.

Aliyataja mengine ni kutoa huduma bora kwa jamii,kuhakikisha upatikanaji wa bidhaa za afya katika hospitali, kuboresha na kuongeza wigo wa utoaji huduma,kutunza miundombinu, vifaa pamoja na vifaa tiba vilivyopo katika hospitali

**NENO LA SHUKRANI**

Dk.Masigati alisema uongozi wa hospitali ya Rufani ya Kanda ya Kusini-Mtwara, unatoa shukrani nyingi kwa serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, inayoongozwa na Rais Dk.Samia kwa kuendeleza hospitali hiyo, ambayo inatoa huduma za kibingwa kwa wananchi wa Kanda ya Kusini na kuwapunguzia adha ya kutafuta huduma hizi maeneo ya mbali.

"Aidha, tunaushukuru Viongozi wa Wizara ya Afya chini ya Waziri Ummy A.Mwalimu(Mb) na Katibu Mkuu Dkt.John Jingu kwa usimamizi wa Karibu wa hospitali pamoja na ushauri mbalimbali, katika kuleta ufanisi wa utoaji huduma kwa wananchi" alisema Dk.Masigati.



Chumba cha Wagonjwa Mahututi (ICU)



Dk. Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

# HOSPITALI YA RUFAA YA MKOA WA LINDI-SOKOINE ILIVYONUFAIKA KATIKA MIAKA MITATU YA RAIS SAMIA







Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Lindi-Sokoine

# Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Lindi-Sokoine ilivyonufaika katika miaka mitatu ya Rais Samia

**Na ELIZABETH JOHN**

HOSPITALI ya Rufaa ya Mkoa wa Lindi-Sokoine ni moja ya hospitali zinazojivunia uwepo wa miaka mitatu ya Rais Samia Suluhu Hassan madarakani kutokana na kufanikiwa katika idara mbalimbali.

Rais Samia leo anatimiza miaka mitatu katika uongozi wake tangu alipoanza majukumu hayo Machi 19, mwaka 2021.

Mganga mfawidhi wa Hospitali ya Rufaa Mkoa wa Lindi, Dk. Alexander Jeremia, anasema katika kipindi cha Rais Samia, wamefanya mengi katika hospitali hiyo ambayo wanajivunia nayo.

**MAFANIKIO MIAKA MITATU YA RAIS SAMIA**

Dk. Jeremia alisema katika kipindi hicho wameweza kufanya ununuzi, usimikwaji na kuanza matumizi kwa mashine ya CT Scan katika hospitali hiyo.

"Hii imepunguza gharama na usumbufu kwa wananchi wa mkoa wa Lindi ambao walikua wanasafiri umbali wa kilometa takribani 460 kufata huduma hii hospitali ya taifa Muhimbili Dar es salaam.

"Pia tumeweza kujenga jengo maalum lenye vifaa tiba vya kisasa la kuhudumia wagonjwa wa dharula (Emergency Medical Department) ambapo wagonjwa wanapata matibabu ya awali kuwaweka katika hali nzuri na salama kabla ya kulazwa wodini kwa matibabu zaidi," alisema.

Alisema pia wamejenga jengo maalum lenye vifaa tiba vya kisasa la kuhudumia wagonjwa mahututi (Intensive Care Unit-ICU)na kuokoa maisha ya wagonjwa hao kwa mazingira na huduma ya kisasa na rafiki.

Dk. Jeremia lisema katika kipindi hiki wameanza ujenzi wa hospitali mpya ya kisasa ya rufaa ya Mkoa wa Lindi ambao unaendelea.

"Ujenzi huu ulikuwa ni kilio cha muda mrefu cha wananchi wa mkoa wa Lindi kujengewa hospitali mpya ya rufaa ya mkoa kutokana na uchakavu wa majengo ya hospitali ya sasa na kuongezeka kwa mahitaji ya matibabu kwa wananchi," alisema.



Alisema pia serikali imewapa gari jipya la kisasa la kubeba wagonjwa (Advanced Ambulance) na gari jipya la uratibu na ufatiliaji wa huduma za afya kwa hospitali.

Mganga mfawidhi huyo alisema wameweza kununua vifaa tiba vya kisasa kwa idara zote za hospitali vya kiuchunguzi, ufatiliaji tiba na matibabu kwa wagonjwa.

**MIPANGO YA KUENDELEA KUFANYA VIZURI**

Dk. Jeremia alisema serikali ya awamu ya sita chini ya uongozi wa Rais Samia kupitia wizara ya afya

*Ujenzi huu ulikuwa ni kilio cha muda mrefu cha wananchi wa mkoa wa Lindi kujengewa hospitali mpya ya rufaa ya mkoa kutokana na uchakavu wa majengo ya hospitali ya sasa na kuongezeka kwa mahitaji ya matibabu kwa wananchi*



Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Lindi-Sokoine

# Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Lindi-Sokoine ilivyonufaika katika miaka mitatu ya Rais Samia



amefanya mapinduzi makubwa katika kuboresha hali ya utoaji huduma kwa wananchi, kuanzia miundombinu, vifaa, vifaatiba madawa na rasilimali watu.

"Mikakati yetu kama watoa huduma ni kupambana kuleta matokea chanya kwa wananchi tunaowahudumia ili waone matunda ya uwekezaji huu wa kihistoria katika nchi yetu uliofanywa katika kipindi kifupi na rais wetu mpendwa na msikivu Dk. Samia," alisema.

### JINSI WALIVYOJIPANGA KUSIMAMIA

Mganga mfawidhi huyo alisema wamejipanga vyema kuhakikisha wanasimamia miradi hiyo iweze kuwafikia wananchi kwa urahisi zaidi.

Alisema watafuata miongozo mbalimbali iliyowekwa katika kutoa huduma za afya.

"Tutasimamia matengenezo kinga ya vifaa, vifaatiba na miundombinu yote ya kutolea huduma za afya.

"Tutapambana kuhakikisha tunakuwa na upatikanaji endelevu wa dawa ili kuwanufaisha wananchi wetu na kupunguza sintofahamu," alisema.

*Watumishi tuna deni kubwa la kufanya kazi kwa bidii, nidhamu, weledi na kuhakikisha tunaleta matokeo bora yaliyokusudiwa kwa wananchi*

Alisema pia wamejipanga kuhakikisha wanasimamia maadili, miiko, viapo na nidhamu kazini kwa watumishi wote.

Alisisitiza kuwa watahakikisha wanaelimisha jamii kuhusu kinga, tiba na kutunza afya zao.

### SHUKRANI KWA RAIS SAMIA

Dk. Jeremia alisema watumishi wa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Lindi – Sokoine, wanatoa shukrani kubwa kwa Rais wa awamu ya sita Dk. Samia Suluhu Hassan kwa kuijali sekta ya afya, kuwekeza kimkakati katika sekta ya afya, Kuimarisha miundombinu, vifaa, vifaatiba, madawa, rasilimali watu na maslahi ya watumishi wa sekta ya afya.

"Watumishi tuna deni kubwa la kufanya kazi kwa bidii, nidhamu, weledi na kuhakikisha tunaleta matokeo bora yaliyokusudiwa kwa wananchi," alisema.

### WITO KWA JAMII

Daktari huyo alisema wanatoa wito kwa wakazi wote wa mkoa wa Lindi kuunga mkono juhudi kubwa za makusudi za Rais wa awamu ya sita Dk. Samia Suluhu Hassan kuboresha huduma za afya.

"Pia wananchi wanatakiwa kumpa Rais Samia nafasi zaidi ya kuendelea na mipango kabambe ya serikali yetu ya awamu ya sita kuinua zaidi ubora wa huduma za afya kwa wananchi.



# MIAKA MITATU YA RAIS DK. SAMIA NA UBORESHAJI SEKTA YA AFYA NCHINI



## MAONI YA WARATIBU WA GAZETI LA UHURU YA KIJANI TOLEO MAALUMU LA AFYA

"Kupitia Toleo hili la miaka mitatu ya Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, katika sekta ya afya kipekee kabisa ningependa kuipongeza serikali yake kwa mafanikio makubwa. Sekta ya afya imekuwa na maboresho ya hali ya juu hususan katika kupunguza vifo vya mama na mtoto, utoaji wa huduma bora kwa wananchi hasa kutokusafiri kwenda mikoa jirani na nchi nyingine kufuata huduma, kutoa huduma bure kwa watoto wenye umri wa chini ya miaka mitano pamoja na msamaha wa matibabu kwa wazee.

Kwa kufanya hivyo kumefanya uchumi wa nchi kuendelea kukua, kwa kuwa rasilimali watu ipo imara, ina nguvu na yenye afya bora .



**MADINA RAJABU**
**0789 226663**
**MRATIBU TOLEO LA AFYA GAZETI LA UHURU YA KIJANI**



"Kupitia Toleo hili maalumu la Miaka Mitatu ya Rais Mhe. Dk. Samia Suluhu Hassan na uboreshaji sekta ya afya tumeweza kuona na kushuhudia kwa macho namna huduma za afya zilivyoboreshwa, ikiwemo ujenzi wa hospitali, vituo vya afya, ununuzi wa vifaa tiba pamoja na kuongezeka kwa watumishi (ajira), Hakika napenda kuipongeza mno serikali hii ya awamu ya sita kwa kutambua umuhimu wa afya za Watanzania"

**ODRIANI NICOLAUS**
**MRATIBU WA TOLEO LA AFYA GAZETI LA UHURU YA KIJANI**
**SIMU:0756 635 658**

"Kupitia Toleo hili maalumu la Miaka Mitatu ya Rais Dk. Samia Suluhu Hassan na uboreshaji sekta ya afya. Nimeweza kujifunza na kuona namna gani Rais wetu anavyopambana kuhakikisha wananchi wanapata huduma bora za afya mjini na vijijini. Naipongeza serikali ya awamu ya sita kwa kutoa kipaumbele kwa afya za Watanzania"



**ANDASON MZIHWI**
**MSANIFU KURASA WA TOLEO HILI**
**SIMU:0654323064**



"Kupitia toleo hili la Mafanikio ya Miaka Mitatu ya Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan katika sekta ya afya hapa nchini. Hakika sekta hii imeimarika kwa viwango vikubwa na imezidi kupaa kimataifa hususan katika utoaji wa huduma za kibingwa na kwa kweli tumeona hospitali zimefanikiwa kujenga maabara za kisasa, wodi sambamba na upatikanaji wa vifaa tiba, huku upatikanaji wa dawa katika hospitali ukiwa ni wa uhakika. Hakika kupitia Dk. Samia tuna vingi vya kujifunza na kujivunia hasa wanawake tunaochipukia katika uongozi siku za usoni"

**GRACE LUBANZA**
**MRATIBU WA TOLEO LA AFYA GAZETI LA UHURU YA KIJANI**
**SIMU NA.0717 838 899**

UHURU
Jumanne Machi 19, 2024 MICHEZO



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA AFYA



**Ummy A. Mwalimu (Mb)**
**WAZIRI**



**Dkt. Godwin Mollel (Mb)**
**NAIBU WAZIRI**



**Dkt. John Jingu**
**KATIBU MKUU**



**Dkt. Grace Magembe**
**NAIBU KATIBU MKUU**

# ASANTENI

***Bodi na Menejimenti ya Uhuru Publications Ltd, inawashukuru na kuwapongeza kwa kufanikisha uandaaji wa toleo maalumu la miaka mitatu ya Rais Dkt. Samia katika sekta ya afya***

UHURU PUBLICATIONS LIMITED

KWA MAKALA, MATANGAZO YA BIASHARA WASILIANA NASI KWA SIMU NAMBA 0754-313-140, 0765-142-207, email uhuruadvert@gmail.com

Gazeti hili hutolewa na Uhuru Publications Limited, S.L.P. 9221 Dar es Salaam